

## BUNGE LA TANZANIA

---

### MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Arobaini – Tarehe 31 Mei, 2019

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

#### D U A

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendele na Mkutano wetu wa Kumi na Tano, na leo ni Kikao cha Arobaini. Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**MHE. KEMILEMBE J. LWOTA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara

ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 pamoja na Maoni ya Kamati hukusu Makadrio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kuhusu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. RAMADHAN ABDALLAH ISSA – KATIBU MEZANI:**  
Maswali.

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Maswali; swalii la kwanza linaanza na Mheshimiwa Esther Michael Mmasi, Mbunge wa Viti Maalum. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Mariam Ditopile.

Na. 330

**Mkakati wa Kulinda Ajira Zisizo Rasmi kwa Vijana**

**MHE. MARIAM D. MZUZURI (k.n.y. MHE. ESTHER M. MMASI)** aliuliza:-

Kutokana na kutimizwa kwa masharti na matakwa ya Kisheria ya kutangaza Mkoa wa Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi ni dhahiri imevutia wadau wengi wa uwekezaji katika nyanja mbalimbali za kiuchumi:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kulinda ajira zisizo rasmi kwa vijana wahitimu Tanzania hasa wa Mkoa wa Dodoma?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Anthony Mavunde, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. ANTONY PETER MAVUNDE) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Michael Mmasi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kutangazwa kwa Mkoa wa Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi, kumevutia uwekezaji katika nyanja mbalimbali za kiuchumi na za kijamii na hivyo kusababisha ongezeko la ajira rasmi na zisizo rasmi. Katika kulinda ajira za vijana wanaojishughulisha katika sekta isiyo rasmi, ikiwemo Mkoa wa Dodoma, Serikali inatekeleza mikakati ifuatayo:-

Kwanza, ni kuhamasisha vijana wakiwemo wahitimu kuunda makampuni katika Mkoa wa Dodoma, ambapo jumla ya makampuni 12 ya vijana yameundwa.

Pili, kuwezesha vijana kupata mikopo yenyе masharti nafuu kuititia Mfuko wa Maendeleo wa Vijana pamoja na mapato ya ndani ya Halamshauri, ambapo katika Mkoa wa Dodoma vijana kuititia vikundi na makampuni 978, wamewezeshwa mitaji yenyе thamani ya jumla ya shilingi 2,557,090,486/= kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya kuanzisha au kuendeleza biashara zao.

Tatu, kurasimisha ajira za vijana wanaojishughulisha katika sekta isiyo rasmi kwa kuwatambua na kuwapatia vitambulisho vya mjasiriamali ili kuwawezesha kufanya shughuli zao bila kubughudhiwa.

Nne, kutoa mafunzo ya ufundi stadi katika fani mbalimbali kwa jumla ya vijana 1,240 wa Mkoa wa Dodoma, kwa lengo la kuwawezesha kujajiri au kuajiriwa katika

shughuli za ujenzi na biashara hapa Dodoma kuitia programu mbalimbali.

Tano, kurasimisha ujuzi uliopoatikana nje ya mfumo rasmi wa mafunzo katika kada za ufundi mbalimbali kwa vijana 245 wa Mkoa wa Dodoma ili kuwawezesha kujajiri au kuajiriwa au kuendelea na mafunzo ya ngazi za juu.

Sita, kutoa mafunzo ya kilimo cha kisasa kwa kutumia teknolojia ya kitalu nyumba (*greenhouse*) kwa vijana 18,800 nchi nzima, ambapo vijana 800 wanatoka Halmashauri nane za Mkoa wa Dodoma.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam ameridhika. Uliza swalii lako Mheshimiwa Mariam Ditopile.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Mheshimiwa Spika, napenda kwanza kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ambayo yana tija kwa vijana wa Mkoa wa Dodoma; na kwa vile ye ye mwenyewe ni mtu sahihi, ni Waziri kijana, ni kijana na ni Mbunge anayetokana na Mkoa wa Dodoma, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swalii la kwanza, moja ya mazao ya biashara yaliyoonyesha kuwa na tija kwenye kilimo biashara Mkoa wa Dodoma ni pamoja na zao la zabibu, lakini mara baada ya Dodoma kutangazwa kuwa Makao Makuu ya Nchi, wageni wengi hususan kutoka katika nchi jirani za Afrika Mashariki, wameonekana kuvutiwa na uwekezaji kwenye zao la zabibu kama zao la biashara. Je, Serikali haioni umuhimu wa kutenga ardhi na pembejeo kwa vijana wa Mkoa wa Dodoma ili wawezeshiriki rasmi kwenye Sekta ya Kilimo cha Biashara kwenye zao la zabibu? (*Makof!*)

Swali la pili. Kwa kuwa kuna vijana tayari wamejajiri kwenye ujasiriamali wa mazao, hususan katika zao la biashara la ufuta, lakini hivi karibuni kumetokea sintofahamu kwa Mkoa wa Dodoma hasa kwenye Wilaya ya Kondoa kuwazuia vijana hawa wasinunue ufuta kutoka kwa

wakulima kwa kisingizio cha kuwa na stakabadhi ghalani, jambo ambalo halipo katika Mkoa wa Dodoma:-

Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu vijana hawa ambao wameamua kujajiri?

Mheshimiwa Spika, nashukuru. (*Makof!*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mawili, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Anthony Mavunde, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. ANTONY PETER MAVUNDE):** Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge Mariam Ditopile kwa namna ambavyo anawasimamia vijana wa nchi yetu ya Tanzania na hususan Vijana wa Mkoa wa Dodoma. Mwenyezi Mungu akubariki sana.

Mheshimiwa Spika, ni kweli, baada ya tangazo la Makao Makuu na pia baada ya Serikali ya Awamu ya Tano sikivu kufanya marekebisho katika ule mchuzi wa zabibu ili kuwavutia zaidi wakulima wa zabibu kuendelea kuilima zabibu, mwamko umekuwa mkubwa kwa vijana na kama Serikali mkakati wake katika eneo hili ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza, yalitoka maelekezo mwaka 2014 kutoka kwa aliyekuwa Waziri Mkuu wa wakati huo Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, ya kila Halmashauri nchi nzima kutenga maeneo maalumu kwa ajili ya shughuli za vijana kufanya kilimo. Kwa Mkoa wa Dodoma na hasa katika maeneo ambayo yanalima zabibu, tayari maelekezo yalishatoka na katika *master plan* ya Jiji la Dodoma, ambayo itakwenda kukamilika hivi karibuni, yametengwa maeneo maalumu ya kuhakikisha kwamba zao hili la zabibu halipotei.

Mheshimiwa Spika, hivyo, vijana pia watapata fursa ya kuweza kunufaika kuititia maeneo hayo ili nao waweze

kulima zabibu na kujiongezea fursa ya kuendeleza mitaji yao na biashara zao.

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi kuliko yote ni kwamba, Halmashauri ya Jiji la Dodoma katika maeneo yake ambayo wametenga kwa ajili ya shughuli za vijana, wameshapeleka wataalam kwenda *SUA* kukaa na wataalam wa *SUA* kwa ajili ya kuja na mpango mzuri endelevu wa kilimo cha zabibu ambacho kitakuwa kimefanyiwa utafiti ili vijana wengi zaidi waweze kunufaika.

Mheshimiwa Spika, siyo zabibu tu, kwa Dodoma hapa, vijana wengi hivi sasa wanafanya biashara za mazao, kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema; na hivi sasa tayari tunavyo viwanda ambavyo vimeanza kufanya kazi. Kwa mfano, Kiwanda cha Mazao Mchanganyiko ambacho kwa mwaka kitahitaji tani 12,000 za mahindi na tani 6,000 za alizeti. Kwa hiyo, tunachukua fursa hii pia kuwaalika vijana kushiriki katika kilimo hicho.

Mheshimiwa Spika, swali la pili la Mheshimiwa Mbunge, analijibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo ambaye ameandaliwa kwa ajili ya kulijibu swali hilo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Kwa kifupi, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo mwenyewe, kwa kifupi tafadhali.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nichukue nafasi hii kumpongeza Naibu Waziri kwa majibu mazuri ambayo ameyatoo. Ni kweli kabisa kumetokea sintofahamu katika zao la ufuta katika maeneo mengi hapa nchini na hasa katika mikoa ambayo inazalisha kwa kiwango kikubwa sana. Utaratibu ambao tumeweka kama Serikali, ni kwamba tunatumia ule utaratibu wa mwaka 2018 wa kuhakikisha, mtu ye yeyote anayetaka kununua ufuta, anaruhusiwa kwenda kununua maadam afuate taratibu zinazostahili; na wote wanaruhusiwa na hatujaweka masharti yoyote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kumetokea katika baadhi ya mikoa, wanasema kwamba tunatumia mfumo wa soko la bidhaa yaani *TMX* na kuna maeneo mengine wanalazimisha kwamba wanaoruhusiwa ni hawa, hatujaweka huo utaratibu. Kila mtu anaruhusiwa kwenda kushiriki na huo utaratibu wa soko la bidhaa utakapokamilika, tutatoa elimu ya kutosha kwa wananchi ili kuanza kutumia huo mfumo. Kwa mwaka huu kwa sababu mfumo hatujaukamilisha sawasawa, basi mfumo wa zamani unaendelea kutumika.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mtaona swali hili moja limechukua dakika 10 Waheshimiwa Wabunge. Tuendelee na Ofisi ya Mheshimiwa Rais TAMISEMI, swali la Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi, kwa niaba yake nimekuona Mheshimiwa Leah Komanya.

Na. 331

**Walimu wa Kike Katika Shule za Msingi na Sekondari**

**MHE. LEAH J. KOMANYA (k.n.y. MHE. MASHIMBA M. NDAKI)** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa kila shule ya msingi au ya sekondari kunakuwa na walimu wa kike kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi wa kike hasa katika masuala yanayohusiana na hedhi salama?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri, wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), naomba kujibu swali la

Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inao utaratibu kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha kuwa katika kila shule ya msingi na sekondari wanateuliwa walimu wa kike wa kuwasaidia wanafunzi wa kike hususan katika masuala yanayohusiana na ushauri nasaha na unasihi likiwemo suala hilo. Lengo la kuwa na walimu hawa shulenii ni kuhakikisha kuwa wanafunzi wa kike wanapatiwa elimu ya afya na usafi itakayowawezesha kutambua mabadiliko yanayotokana na kupevuka kwa miili yao na kuelimishwa njia bora na salama za kujistiri pale wanapopatwa na hali hiyo. Aidha, wanafunzi hawa wanahitaji mlezi wa kike wa kuweza kuwasaidia wanapokuwa na changamoto mbalimbali kuhusiana na masuala ya kike.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia mpango wa Lipa Kulingana na Matokeo (*Education Performance for Results - EP4R*) imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya kusawazisha ikama ya walimu wakiwemo walimo wa kike katika Halmashauri ili kukabiliana na tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Leah, umesimama, nimekuona.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Asilimia 10 ya *EP4R* inayotolewa kwa ajili ya msawazisho wa ikama, imekuwa siyo suluhi katika Mkoa wa Simiyu kwa kuwa walimu wengi sana wamekuwa wakihama. Walimu 60 wanahama kwa robo moja katika Wilaya ya Meatu na watano ndio wanahamia. Je, Serikali haioni haja ya kuwa na mkakati ili walimu wanaoajiriwa wakabaki kuitumikia Halmashauri angalau kwa miaka mitano kabla ya kuruhusiwa kuhamia?

Mheshimiwa Spika, ni dhahili kwamba, siyo wasichana wote hupata hisia (*pre-menstrual syndrome*) kabla ya kuanza

hedhi na wakati huo hakuna mwalimu yejote wa kike ambaye anaweza kutoa msaada. Je, Serikali haioni haja ya kuwapatia Waheshimiwa Madiwani wanawake elimu ya hedhi pamoja na afya ya uzazi angalau mara moja kwa mwaka ili kwa kushirikiana na Wabunge wanawake, angalau tuwe tunatoa elimu ya uzazi kwa watoto wetu wa kike? (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo. Ni kweli ziko shule hazina mwalimu wa kike hata mmoja.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wa Viti Maalum wote kwa kuzingatia mambo ya wanawake na hasa waschana katika shule zetu ili kuimarisha afya zao.

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza anapendekeza kwamba walimu ikiwezekana wakae miaka mitano ili waweze kuhudumia katika maeneo haya. Ndiyo maana Mheshimiwa Waziri Mkuu alishatoa maelekezo katika Ofisi ya Rais TAMISEMI kwamba walimu wote kwa ujumla pamoja na wahudumu wengine wa afya, tunaandaa mfumo wa kisayansi ambao utakuwa unaweza kuonyesha kama mwalimu anataka kuhama kutoka *point 'A'* kwenda *point 'B'* ikiwa tunaweza kuangalie ile ikama.

Mheshimiwa Spika, la pili, ni kwamba, tunavyozungumza hapa, mwezi huu mwanzoni, tumepeleka fedha za *EP4R*, motisha kila Halmashauri. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge wakafuatilie fedha zimeenda katika Halmashauri zao na kwenye majimbo yao, Halmashauri zote nchini zimepelekewa fedha hizi za ku-*balance* ikama, vilevile na fedha za kumalizia maboma ya shule za msingi. Naomba mkasimamie ili zifanye kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, nitasikitika sana kama kuna shule ambayo ina walimu katika Halmashauri yake, tumepeleka fedha za ku-*balance* ikama halafu bado iendelee kubaki shule

moja ambayo haina mwalimu wa kike, itakuwa ni bahati mbaya; na kwa kweli Mkurugenzi huyo, au Afisa Elimu wa Mkoa na viongozi wa mkoa huo watakuwa hawakuitendea haki Serikali. Maelekezo ni kwamba, fedha iliyopatikana wazingatie kuhamisha walimu wa kike, wahakikishe kila Halmashauri ina mwalimu wa kike. Kwa sababu unakuta Halmashauri mbalimbali zina walimu wengi katika maeneo mbalimbali. Tulipeleka fedha ili mwalimu akihamishwa asianze kulalamika. Hili nadhani lizingatiwe na lifanyiwe kazi. Waheshimiwa Wabunge, tusaidiane kufuatilia hili ili liweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, hoja ya miaka mitano kuelekeza, ziko taratibu mbalimbali za Utumishi wa Umma, hizo ndizo zinazingatiwa. Hata hili la kuzuia kwa muda, kimsingi tumezuia kwa sababu baada ya malalamiko mengi, kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema kwamba kuna maeneo walimu wanafika. Hata juzi tumeajiri walimu, walipaswa kuripoti tarehe 21 mwezi huu ndiyo ilikuwa waripoti kama ajira ndiyo tupange, lakini wameshaanza kuomba uhamisho. Hata kuripoti hajaripoti, hajapewa hata namna ya ajira, hajaanza kulipwa mshahara.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukizua ajira kunakuwa na malalamiko mengi sana kwamba watu wanaonewa, lakini kimsingi matatizo hayo ndiyo tunayazingatia. Kwa hiyo, tunaomba walimu waendelee kubaki maeneo yale na uhamisho umeendelea kusitishwa mpaka tutakopokamilisha mfumo ili tuweze kumhamisha mwalimu tukijua kwamba eneo analotoka au kwenda haliathiri sana utoaji wa elimu katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, anashauri kwamba Waheshimiwa Madiwani wa Viti Maalum wapewe semina hii ili waweze kusaidia na Waheshimiwa Wabunge. Hili jambo tunalipokea, lakini ukweli ni kwamba elimu hii ya uzazi inatolewa; ni elimu endelevu, inatolewa kwa wazazi wenyewe, kwa wanafunzi wenyewe, kwa walimu wa kike na wa kiume. Pia Mheshimiwa Waziri wa Afya alishauri juzi hapa; na hata akina mama katika nyumba zetu, unaweza

ukamlea mtoto vizuri zaidi, kwa sababu unakaa naye muda mwingu zaidi ili kusaidia kuboresha mambo haya. Tunaupokea ushauri huu, tutaona utakapofika wakati muafaka tuufanyie kazi. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza.

Na. 332

### **Shule za Watoto Wenyewe Mahitaji Maalum**

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA** aliuliza:-

Shule za watoto wenyewe mahitaji maalum hupokea wanafunzi wenyewe matatizo mbalimbali kama vile ulemavu wa viungo, viziwi, uoni hafifu na wenyewe ualbino; baadhi ya wazazi wamekuwa wakiwatekeleza wototo wao wakashawapeleka kwenye shule hizo:-

(a) Je, ni kwa nini Serikali haitoi fedha kwa shule hizo iliziweze kuhimili mahitaji ya watoto hao?

(b) Je, ni kwa nini Serikali inaziachia majukumu Halmashauri kuendesha shule hizo wakati zinapokea wanafunzi kutoka nje ya mkoa?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo muhimu sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza, Mbunge wa Viti Maalum, lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wanafunzi wenyewe mahitaji maalum wana haki sawa ya kupata elimu kama wanafunzi wengine wasio na mahitaji maalum. Kwa kutambua

changamoto wanazokutana nazo wanafunzi hawa, Serikali kuititia mpango wake wa elimu bila malipo, imekuwa ikigharimia huduma za chakula kwa wanafunzi wote wenye mahitaji maalum wanaosoma katika shule za bweni na za kutwa. Vilevile Serikali imekuwa ikinunua vifaa na visaidizi kwa kadri ya upatikanaji wa fedha kisha kuvigawa kwa wanafunzi husika.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha mwaka 2015/2016 hadi 2018/2019, Serikali imetumia jumla ya shilingi bilioni 3.87 kwa ajili ya chakula kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu shulenii. Changamoto kubwa kwenye utaratibu huu ni upatikanaji wa takwimu sahihi za wanafunzi wenye mahitaji maalum kutoka kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa na Serikali inaendelea kuimarisha mfumo wa upatikanaji na utoaji wa takwimu sahihi za wanafunzi wenye mahitaji maalum. Serikali itaendelea kusimamia utoaji bora wa elimu kwa wanafunzi wote wakiwemo wenye mahitaji maalum bila kujali mkoa au eneo ambalo anatoka.

Mhehimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Concestha, swali la nyongeza.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali yangu mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, watoto hawa wanapopelekwa kwenye shule wazazi wao wanawatelekeza, hawafuati watoto wao kuhakikisha kwamba wanapata mahitaji maalum hasa mavazi. Siyo hiyo tu, shule hizo zinakosa pesa za kulipia walinzi, kulipa, maji, kulipa mapato na *Matron* na wengine wanahitaji misaada maalum na hasa wale wenye uoni hafifu au wasiyoona.

Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu sasa kuwepo na mpango maalum wa kuhakikisha kwamba watoto hawa fedha hizo zinapelekwa kwa kuzingatia kwamba Halmashauri hazina mapato, zimezinyang'anywa

mapato yote, haziwezi kuhimili kumudu kusaidia shule hizo; Kuwepo na mkakati maalum wa kuhakikisha kwamba huduma kama hizo zinapatikana kwa watoto hawa.

Mheshimiwa Spika, shule ambazo mimi nimeuliza swali ni za Serikali, sikutegemea kwamba Serikali inaweza ikakosa takwimu maalum kwa ajili ya kuweza kutoa huduma.(*Makofii*)

Je, Serikali inataka kutuambia kwamba inafanya kazi bila kuwa na takwimu sahihi?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Swali lake la kwanza Mheshimiwa Conchesta amezungumza hoja ambayo kimsingi inatakiwa Watanzania wote tuichukue na kuifanyia kazi. Ni kweli kwamba wako wazazi ambao wametelekeza watoto wao, hata akimpeleka shulenii, anamwacha pale moja kwa moja, hawezi kumfuatilia.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli ni jambo hili ni jukumu la kijamii, haliwezi kuwa la Serikali peke yake, tulichukue na tuwashauri kwamba hawa ni watoto wenye haki sawa na watoto wengine, tuwapokee, tuwakubali, na tuwasaidie. Tukishikamana sisi Watanzania na jamii kwa ujumla na Serikali, jambo hili litakuwa jepesi sana.

Mheshimiwa Spika, vile vile Mheshimiwa Conchesta anapendekeza kwamba kama kuna uwezekano wa kipeleka fedha zaidi, tufanye hivyo. Ninachokizungumza hapa, tunapeleka huduma kwenye shule kulingana na idadi ya wanafunzi kulingana na taarifa tuliyopokea hapa. Hili swali naliyiblu kwa pamoja na swali lake la pili. Tunapozungumza kwamba taarifa hazipatikani, kama alivyosema mwenyewe ni kwamba kuna watoto wengine wanafichwa katika jamii,

kuna wengine kweli hawako kwenye mfumo rasmi, kuna wengine wapo mashulenii, lakini taarifa ya Serikali Kuu hapa TAMISEMI pamoja na Hazina ambao wanatuma fedha moja kwa moja kwenye mashule, tunapata taarifa kutoka kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika jambo hili natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge, Madiwani, Viongozi wa Vijiji na Mitaa, tupatiensi taarifa sahihi. Tukipata taarifa sahihi, tutapeleka fedha kwa kiwango kinachotosha katika eneo lile; na hiyo ndio ambayo inakosekana hapa. Kwa hiyo, jambo hili ni la kwetu wote, tunaendelea kufanya kazi. Inawezekana kuna upungufu katika maeneo mbalimbali, tumetembea katika shule mbalimbali, lakini kuna upungufu, lakini kadri Serikali inavyopata uwezo imekuwa ikiimarishe huduma hizi.

Mheshimiwa Spika, tumesema hakuna mtoto ambaye atakuwa katika shule hii au kupata shida kubwa bila kupata huduma. Cha muhimu tusaidiane, Mheshimiwa Mbunge kule wa Kagera ameona taarifa ipo, tuwasiliane, tutaipokea, tutalifanyia kazi. Lengo ni kuhakikisha kwamba watoto hawa wanapata elimu na ushahidi upo kwamba huko watoto waliachwa, walitelezewa, wamechukuliwa na Serikali na wasamaria wema, wameingia kwenye mfumo rasmi, sasa hiivi ni viongozi wakubwa katika nchi hii, wamejajiri na wanasaidia wenzao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mwalimu Mariamu Kisangi, uliza swali lako.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa katika Mkoa wa Dar es Salaam kumekuwa na ongezeko la watoto wenye mahitaji maalum; na kwa kuwa shule ambazo zinapokea watoto wenye mahitaji maalum kama Majimatitu Maalum, Mtoni Maalum, Salvation Army, Wailesi Maalum, Uhuru Mchanganyiko,

*Mgulani Inclusive* na Sinza Maalum zinakuwa hazitoshelezi mahitaji, watoto wale bado wanabaki majumbani:-

Je, Serikali haioni haja sasa ya kuongeza katika shule zote za msingi vitengo vya watoto wenye mahitaji maalum ili nao waweze kupata elimu katika maeneo yao wanayotoka? (*Makof!*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo muhimu sana, kuongeza huduma.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Mariam Kisangi kwa mawazo haya mazuri ya kuunga mkono Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Naomba nitoe taarifa kwamba sasa hivi baada ya kuona kwamba unapotenga shule maalum ni kama wale watoto unawatenga, wanakuwa *isolated* sana katika mazingira yao. Kwa hiyo, sasa hivi tumekuja na kitu kinaitwa Elimu Jumuishi. Ndiyo maana tumetoa maelekezo nchi nzima, tunapojenga miundombinu mipya, hata kama ni Kituo cha Afya izingatie mahitaji maalum, kama ni shule zetu za msingi na sekondari ziwe na mahitaji maalum.

Mheshimiwa Spika, ukienda kule Buhangizo utawakuta, Chaibushi utakuwata, Kilosa Sekondari utawakuta. Kwa hiyo, hiyo imeshaanza. Cha muhimu, ametoa *warning*, tuendelee kuzingatia. Tumeendelea kuwaeleza wanafunzi wa kawaida kwamba hawa watoto wenye mahitaji maalum ni wenzao, wawapokee, wawakubali, wawasadie na wasome kwa pamoja pale inapowezekana. Hilo kwa kweli linafanyika. Cha muhimu hapa tutaongeza nguvu zaidi na kwa maoni ya Mheshimiwa Mbunge tutayafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge. Kwa sababu ya muda, tunaendelea na swali linalofuata la Wizara

ya Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo, linaulizwa na Mheshimiwa Yussuf Haji Khamisi, Mbunge wa Nungwi.

Na. 333

### **Upimaji Afya kwa Wanamichezo**

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS** aliuliza:-

Upimaji wa Afya za Wanamichezo ni jambo muhimu kwa ajili ya kulinda na kuhakikisha afya zao kabla ya kushiriki michezoni kwani kumekuwa na matokeo mbalimbali ya Wanamichezo kupoteza maisha wakiwa uwanjani. Mathalani, Ismael Mirisho wa Timu ya Mbao FC, Marc Vivien Foe wa Cameroon na Cheikh Tiote wa Ivory Coast:-

Je, Serikali kupitilia Vyama vya Michezo vimeweka utaratibu gani kuhakikisha upimaji wa afya za wanamichezo ni jambo linalopewa kipaumbele?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, kuhusu afya ya wachezaji na upimaji wake.

### **NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri, wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mbunge wa Nungwi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia na kuwa na uelewa sahihi kuhusu umuhimu wa afya za wachezaji wetu wakiwa michezoni. Matukio ya wanamichezo kupata matatizo ya kiafya na hata wakati mwagine vifo kutokea uwanjani, yamekuwa yakinkeea mara kwa mara Tanzania na imeshuhudiwa matukio kama hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia ukweli huo, Wizara yangu kupitia kitengo chake cha Kinga na Tiba kwa kushirikiana na Chama cha Madaktari wa Michezo Nchini, imendelea kutoa elimu ya afya kwa wanamichezo na Viongozi wa Mashirikisho ya Vyama vya Michezo kwa lengo la kuwawezesha kuelewa umuhimu wa huduma za afya kwa wanamichezo muda wote wawapo viwanjani kwa mazoezini au katika mashindano.

Mheshimiwa Spika, kwa muktagha huo huo, vilabu vyote vya soka vya ligi kuu ya Tanzania kwa mfano, vimeelekezwa kuwa na Daktari mwenye sifa na ambaye muda wote atakuwa tayari kutoa huduma ya matibabu kwa wachezaji.

Mheshimiwa Spika, Kitengo cha Kinga na Tiba cha Wizara, mbali ya kutoa elimu ya afya kwa wanamichezo pia kina jukumu la upimaji wa afya na kutoa Huduma ya Kwanza kwa wanamichezo kila wanaposhiriki michezo au mashindano mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, suala la huduma za afya kwa wanamichezo ni suala la kisera. Sera ya Maendeleo ya Michezo ya Mwaka 1995 sehemu ya 10.1 imeelekeza kuwa ni lazima mchezaji achunguzwe afya yake na kuwekewa kumbukumbu zote za kiafya kwa kipindi chote awapo kambini na ahudumiwe na Daktari kwenye taaluma ya tiba kwa wanamichezo.

Aidha, utaratibu wa matibabu kwa wanamichezo ujumuishe mafunzo juu ya athari za kutumia madawa ya kuongeza nguvu kwa wanamichezo. Wizara yangu inashauri na kuelekeza Vyama na Mashirikisho yote ya Michezo Nchini kuwa na utaratibu wa mara kwa mara wa kutoa elimu ya afya kwa wadau wake pamoja na kutoa elimu kinga kwa wanamichezo ili kulinda afya zao. Wizara yangu iko tayari kutoa ushirikiano katika jitihada hizo kwa kutoa ushauri wa kitaalamu ili kuimarisha afya za wanamichezo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, nimekuona.

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba ruhusa yako kabla sijauliza maswali mawili ya nyongeza, niwapongeze *Simba Sports Club* kwa kuchukua ubingwa wa Tanzania mara mbili mfululizo. (*Makofi*)

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mnajuana eeh! (*Makofi*)

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Swali langu la kwanza, mimi nina wasiwasi kwamba agizo analolitoa Mheshimiwa Waziri kwamba linafanyiwa kazi na vilabu na hili tatizo ni kubwa linajitokeza mara kwa mara: Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kuleta sheria hapa Bungeni kuvibana vilabu angalau vile vya daraja la kwanza na vile vinavyocheza *Club Bingwa* ya Tanzania kupima kwa lazima? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, swali langu ya pili, hili suala la upimaji wa afya, basi Bunge tungekuwa mfano mzuri sana, kwa sababu tuna vilabu mbalimbali vya michezo hapa Bungeni, mfano *Club* ya Mpira wa Miguu Ndugai Boys na michezo hii inashirikisha Viongozi Mashuhuri. Mfano mzuri Waziri Mkuu amekuwa mchezaji, pia amekuwa Kocha ambaye ameleta ufanisi mkubwa katika timu ya Bunge hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nataka kujua, ni lini wamewahi kupima afya zao wakicheza michezo ya ndani? Au ile wanayotushirikisha katika Mabunge ya *East Africa*? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri; kupima afya ya wachezaji. Sijui ndiyo itasababisha baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wasiende uwanjani tena! Majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza

Mheshimiwa Mbunge kwa maswali yake mazuri. Nikianza na swalı lake la kwanza ambalo amezungumzia kwamba agizo hili huwa halifanyiwi kazi.

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii kusema kwamba suala la kupima afya kwa wachezaji ni agizo ambalo sisi kama Wizara tunalisimamia. Ukiacha kwamba ni suala la kisera, ukiangalia kwenye kanuni za *FIFA*, vilevile kwenye kanuni za *TFFimeelekeza* wazi kwamba vilabu vyote na mashiriko yote ya mpira wa miguu yahakikishe kwamba yanapima afya ya wachezaji wao, siyo tu kipindi ambacho vilabu vinajandaa kuingia kwenye mashindano, vilevile kabla ya usajili wowote kuweza kufanyika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hilo ni agizo, nasi kama Wizara tunalisimamia, lakini kwa ushauri ambao Mheshimiwa Mbunge ameutoa, kwamba sisi kama Wizara tulete sheria hapa Bungeni, niseme kwamba ushauri huo tumeupokea kwa sababu sisi Wabunge ndio ambao tunatunga sheria; na kama Mbunge ameona kwamba kuna haja ya kuwa na hiyo sheria, basi sisi kama Wizara tutakaa na kuangalia namna gani ambavyo tutaleta hiyo sheria ndani ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwenye swalı lake la pili amezungumzia kuhusiana na timu ya Wabunge. Ni kweli kwamba tunayo timu ya Wabunge na timu yetu imekuwa ikifanya vizuri sana katika mashindano mbalimbali ya *East Africa*. Kwa hiyo, kama ambavyo nimezungumza, suala la kupima afya kwa wachezaji siyo tu kwa timu ambazo zinashiriki mashindano mbalimbali, iwe ni timu ambazo zinashiriki ligi daraja la kwanza, daraja la pili, vilevile hata kwenye michezo ya UMISETA na UMITASHUMTA wanatakiwa kupima afya kwa wachezaji wao kabla ya kuanza kwa mashindano.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hata kwa sisi Wabunge, ni jukumu letu la kuhakikisha kwamba wanapima afya zao kabla ya kuweza kushiriki mashindano yoyote au kabla ya kwenda kushiriki kwenye mashindano ambayo huwa yanafanyika nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa kupima afya ya wachezaji ni jambo moja, lakini kama wachezaji wenyewe lishe ni mashakamashaka, mpaka utembeze bakuli ndiyo wachezaji wale, tutapima afya zao, unategema nini? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Katika mchezo wa ngumi, asilimia 99 ya wachezaji wanapata maumivu. Je, ni lini Serikali italazimisha ma-*promoterkuwakatia* bima hasa mabondoa wanawake hapa nchini Tanzania? Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Majibu kwa swali hilo muhimu, bima kwa mabondia na hasa wanawake.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza kwa sababu Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ni *promoterpekee* mwanamke ambaye anashiriki kwenye michezo ya ngumi. Nikija kwenye swali lake la msingi ambalo ametaka kujua kwamba ni lini sasa Serikali tutasimamia hawa wanaocheza michezo ya ngumi kuweza kukatiwa bima; nikiri kwamba imekuwa ni changamoto ya muda mrefu kwamba wachezaji wengi ambao wanacheza michezo ya ngumi wamekuwa wakifanya kazi kwenye mazingira magumu ikiwepo kutokuwa na Bima za Afya.

Mheshimiwa Spika, kwenye hivi vyama ambavyo vinashiriki mchezo huu ndondi kumekuwa kuna migogoro ya muda mrefu sana na ndiyo maana wachezaji hawa wakawa hawapati ile haki yao ya kuweza kupata Bima ya Afya. Kwa sasa hivi kama Wizara, tumeshaunda shirkisho la kuweza kusimamia mchezo huu wa ngumi nchini Tanzania. Lengo mojawapo kwenye vile vipengele ambavyo tumeviweka, ni kuhakikisha kwamba ni lazima kwa Ma-*promoterkuwakatia* Bima za Afya wachezaji wao.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Kilimo, swali litaulizwa na Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini.

Na. 334

**Serikali Kuja na Mbinu za Ziada Katika Kukabiliana na Tatizo la Ugonjwa wa Mnyauko wa Migomba**

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA** aliuliza:-

Ugonjwa wa Mnyauko wa Migomba umekuwa tatizo kubwa na la muda mrefu na limewaathiri Wakulima wa Migomba Mkoani Kagera:-

Je, ni kwa nini Serikali haichukui hatua za makusudi za kupambana na ugonjwa huo na kuutokomeza kabisa?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo muhimu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, swali la wananchi wa Bukoba, ugonjwa wa Migomba.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (INNOCENT L. BASHUNGWA)**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza Mbunge wa Bukoba Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mnyauko wa migomba kitaalamu unaitwa unyanjano wa migomba. Husababishwa na vimelea aina ya *bacteria* ambao hushambulia aina zote za migomba na jamii yake. Ugonjwa huu unasambazwa na ndege, nyuki, binadamu, ngedere na tumbili; miche iliyoathirika; vifaa vya shambani viliviyotumika kwenye migomba iliyoathirika na vifungashio vya kusafirisha ndizi.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2006 - 2014, Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Uongozi wa Mkoa wa Kagera tumekuwa tukitoa mafunzo ya kutokomeza ugonjwa huo kwa wakulima na Maafisa Ugani kwenye Wilaya zote zilizoathirika. Serikali imekuwa ikiendesha kampeni ya kung'oa migomba yote iliyoathirika, kukata Ua Dume na kuitekeleza. Halmashauri zote za Wilaya ya Mkoa wa Kagera ziliweka sheria ndogo ndogo za kuwataka wakulima kung'oa na kuchoma au kuzika migomba yote ailiyoathirika. Zoezi hilo lilipunguza ueneaji wa ugonjwa huo kwa asilimia 70.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kufanya tafiti za kuzalisha miche bora ambayo haina vimelea yya ugonjwa wa unyanjano kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (*TARI*) ikishirikiana na Shirika la *Belgium Technical Cooperation*. Hadi sasa miche bora milioni sita imezalishwa na kusambazwa kwa wakulima katika Mikoa ya Kagera na Kigoma.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatoa wito kwa wakulima kote nchini kutumia mbegu bora za migomba aina ya Shia 17, Shia 23, Nshakara, Nyoya na Kinohasha zinazozalishwa katika Taasisi za Utafiti Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine Mikocheni, Uyole, Kibaha, Maruku na Tengeru ili kuongeza tija katika uzalishaji na kutosafirisha ndizi zilizofungashwa na majani ya migomba kutoka mashamba yaliyoathirika.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Rweikiza swali la nyongeza kuhusu migomba kunyauka.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali na ni kweli ugonjwa huu umepungua kwa asilimia kubwa, lakini haujaisha. Sasa Serikali kwenye majibu inasema kwamba jitihada zimekoma 2014, lakini ukweli ni kwamba ugonjwa huu bado haujaisha kabisa, bado upo ingawa umepungua kwa kiasi kikubwa. Kwa hiyo, napenda kujua ni jitihada gani mahususi ambayo

Serikali inayo kutokomeza ugonjwa huu uishe kabisa kwa asilimia 100? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, sambamba na ugonjwa huo wa migomba kuna mnyauko pia wa mikahawa, kuna mnyanjanoo pia wa mihogo unaitwa batobato na yote haya yanalinwa Kagera haya. Napenda kujua ni jitihada gani zinachukuliwa na Serikali kuondoa magonjwa hayo mengine na mazao mengine kama kahawa, migomba, mihogo na mazao mengine?

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo, Mheshimiwa Innocent Lugh Bashungwa.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (INNOCENT L. BASHUNGWA):** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Jasson Rweikiza kwa jitihada nzuri za kuhakikisha kwamba tunatokomeza ugonjwa wa mnyauko wa ndizi pamoja mnyauko wa kahawa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Jasson Rweikiza ni mkulima mzuri wa ndizi, nilishawahi kutembelea shamba lake. Kwa hiyo, nakupongeza kwa kupambana na jitihada hizi huku nawe ukiwa mkulima kwa kuonesha mfano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, maswali mawili ya Mheshimiwa Jasson Rweikiza, swali la kwanza angependa kujua mikakati ya Serikali ya kutokomeza mnyauko wa migomba, ni kwamba Serikali kama nilliyosema kwenye swali nillilojibu wiki iliyopita, Mheshimiwa Rais wetu ametusaidia kupata mabillioni kutoka *IFAD*; shilingi bilioni 127.3 kwenda kwenye Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (*TARI* na *ASA*) kwenye kuzalisha mbegu pamoja na kupambana na mabadiliko ya tabianchi hasa hasa kwenye magonjwa kama haya ya mnyauko na magonjwa mengine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Rweikiza kwamba Serikali tayari ina jitihada

mahuususi za kuhakikisha tunapata fedha za kutosha kupambana na magonjwa haya. Vile vile nikuhakikishie katika bajeti ambayo itaenda *TAR/na ASA* tutahakikisha bajeti kwa ajili ya kupambana na magonjwa ya mnyauko wa kahawa na ndizi na yenye inazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi hii. (*Makof!*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Suzan nilikuona.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Tatizo la huu ugonjwa wa mnyauko katika migomba, linafanana kabisa kwa miaka mingi na mnyauko au ugonjwa wa manjano kwa kilimo cha mpunga ndani ya Wilaya ya Kilombero na mwaka huu athari hii imekuwa kubwa mno. Kila mara nilikuwa na fuatilia hapa kuuliza maswali Bungeni lakini hatujapata jibu kwamba tunafanyaje sisi wakulima wa mpunga kwani tunapata hasara kubwa?

Je, Serikali ina mpango gani wa kutupa majibu wakulima wa mpunga hususan wa Wilaya ya Kilombero, Ulanga, na Malinyi ambapo ndio walimaji wakubwa wa mpunga ili tuepukane na hizi harasa tunazopata kila mwaka? (*Makof!*)

**SPIKA:** Haya mnyauko umehamia kwenye mpunga sasa. Majibu Mheshimiwa Nibu Waziri Kilimo. Kazi ipo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye swali langu la msingi, Serikali inatambua kwamba kuna changamoto ya mabadiliko ya tabianchi na moja ya changamoto hizi ni magonjwa ambayo yanashambulia mazao yetu likiwemo zao la mpunga kama Mheshimiwa Susan alivyosema.

Mheshimiwa Spika, Serikali tunatambua mazao haya, ni lazima tuweke jitihada ya kuhakikisha tunaongeza uzalishaji wa wakulima wetu kwa sababu nchi zinazunguka Tanzania zina uhitaji mkubwa wa mchele na mazao mengine. Kwa

hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Susan kwamba Serikali inatambua changamoto zilizopo kwenye mabadiliko ya tabianchi. Kwa kupitia Taasisi zetu za *TAR/ha ASA*, tutaenda hata Jimboni kwake kuangalia changamoto alizozitaja ili tuweze kuzifanya kazi.

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii Waheshimiwa Wabunge, swali la Mheshimiwa Pascal Yohana Haonga, Mbunge wa Mbozi, uliza swali lako tafadhali.

Na. 335

**Vivutio vya Utalii Vilivyopo Katika Wilaya ya Mbozi**

**MHE. PASCAL Y. HAONGA** aliuliza:-

Wilaya ya Mbozi ina vivutio vingi sana vya utalii, baadhi yake ni Kimondo kilichopo Kijiji cha Ndolezi Kata ya Mlangali, Majimoto na Mapango ya Popo katika Kata ya Nanyara, lakini baadhi ya vivutio hivyo hasa Majimoto na Mapango ya Popo havitambuliwi na havipo hata kwenye orodha ya kumbukumbu za Serikali:-

- (a) Je, ni lini Serikali itavitambua rasmi vivutio hivyo?
- (b) Je, kivutio cha Kimondo kimeingiza shilingi ngapi kwenye Halmashauri ya Mbozi na Serikali Kuu tangu kigunduliwe?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Constatine John Kanyasu, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Pascal Yohana Haonga, Mbunge wa Mbozi lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inavitambua vivutio vilivyopo Mkoani Songwe ikiwemo vinavyopatikana Wilaya ya Mbozi vya Majimoto na Mapango ya Popo na tayari vimeorodheshwa katika kumbukumbu za Serikali. Vivutio hivyo vilitambuliwa rasmi katika maadhisho ya siku ya Kimondo Duniani yaliyofanyika katika Kituo cha Kimondo cha Mbozi kilichopo Kijiji cha Ndolezi, Kata ya Mlangali tarehe 28 - 30 Juni, 2018.

Mheshimiwa Spika, napenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali itaendelea kufanya utafiti wa kina kwa lengo la kukusanya taarifa sahihi na vivutio vilivyopo Mkoani Songwe kwa lengo la kuvitangaza katika gazeti la Serikali. Vivutio vitakavyokidhi vigezo kuwa urithi wa utamaduni wa Taifa tutavitumia kiatalii.

Mheshimiwa Spika, kuanzia Mwaka wa Fedha 2013/2014 hadi 2017/2018 Serikali imekusanya kiasi cha shilingi milioni 14,378,000/= kutoka katika kituo cha Mbozi kutokana na watalii waliokwenda kuona Kimondo. Kwa kutambua umuhimu wa kituo hicho, Serikali inaendelea kukiboresha kwa kujenga Kituo cha Kumbukumbu na Taarifa na kuandaa maadhisho ya Siku ya Kimondo Duniani. Aidha, jitihada za kuitangaza kituo hicho zitaongeza idadi ya watalii ndani na nje ya nchi na hatimaye kuongeza mapato ya Serikali.

Mhehsimiwa Spika, ahsante sana. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Haonga, swali la nyongeza.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; kwa kuwa fedha zote ambazo zinakusanya kutokana na utalii wa Kimondo Mbozi huwa zinachukuliwa na Serikali kuu na hakuna hata shilingi moja ambayo imewahi kurejeshwa kwa wananchi wa Kijiji husika cha Ndolezi na Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi: Je, Serikali

haioni kwamba huu ni ubaguzi kwa wananchi wa Wilaya ya Mbozi kwa sababu maeneo mengine yenye utalii, wananchi hurejeshewa sehemu kidogo ya fedha zilizotokana na utalii? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Vivutio vyta Utalii vyta Majimoto pamoja na Mapango ya Popo vimekuwepo kwa muda mrefu sana tangu uhuru. Je, Serikali kwa nini inaendelea kusuasua kutenga bajeti ya kuviendeleza vivutio hivi vyta utalii ambavyo vipo katika Kijiji cha Nanyala, Kata ya Nanyala, Wilaya ya Mbozi?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Kanyasu, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwanza katika swali lake la kwanza Mheshimiwa Mbunge ametaka kufahamu ni kwa nini Serikali imekuwa ikikusanya pesa hizi na kutokuzirudisha Halmashauri? Jambo hili siyo kweli.

Mheshimiwa Spika, unafahamu kwamba maduhuli yote yanayokusanya na Taasisi mbalimbali za Setikali yanachangia katika mfuko Mkuu wa Serikali na pesa hizo ndizo zinazorudi kwa ajili ya uendeshaji wa huduma mbalimbali za jamii zikiwemo hospitali, kulipa walimu pamoja na mambo mengine na ujenzi wa miundombinu. Kwa hiyo, makusanyo haya yanayofanyika katika Serikali siyo lazima yarudi kama *token* kwenye Halmashauri, bali yanarudi kwa *style* ambayo wananchi wote katika Mkoa wa Songwe wanapata.

Mheshimiwa Spika, nimkumbushe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kimsingi jukumu la kuleta watalii na kuongeza mapato kwenye Halmashauri yake linaweza pia kufanywa na yeye. Kama mnavyofahamu, pamoja na kwamba tunapata watalii milioni 1.5 Tanzania, sehemu kubwa ya watalii hawa wanaokuja Tanzania wanatafutwa na wadau wa utalii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhamasishe Mheshimiwa Mbunge kuihamasisha Halmashauri yake na yeye mwenyewe kikitangaza kivutio hiki cha utalii, lakini pia kuweka miundombinu kwa kushirikiana na Halmashauri ili kuweza kuingiza mapato mengi zaidi kwenye Wilaya yake.

Mheshimiwa Spika, katika swalii lake la pili amesema kwamba tumekuwa tukisuuasua katika kutangaza Majimoto. Hatujasuuasua, nimemweleza katika jibu langu la msingi Mheshimiwa Mbunge kwamba Majimoto haya na Pango la Popo tumeviingiza katika kumbukumbu za Serikali. Jukumu la kuvitangaza na kuvifanya vilette watalii linaweza kufanywa na mtu mmoja mmoja. Kama mnavyofahamu, ni kwamba sisi kama Serikali tunasimamia sera lakini jukumu la mtu mmoja mmoja linaweza kutangaza kituo kile na kuleta watalii na kuongezea Serikali mapato.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Twende kwa majirani wa Mbozi kule lleje. Nilikuona Mheshimiwa Janet Mbene uliza swalii lako.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Kwa kuwa suala la utalii limezingatia zaidi utalii wa mbuga za wanyama na fukwe, kuna utalii ambao umesahauliwa ambao nao pia ni mzuri na unawagusa wananchi moja kwa moja; utalii wa kitamaduni.

Mheshimiwa Spika, Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini hususan Songwe na hata Wilaya yangu ya lleje, tuna vivutio vingi ambavyo vingeendelezwa vingesaidia sana suala hili na wananchi wangenufaika. Tuna ngoma za jadi, tuna mila zetu na desturi, tuna aina zetu za nyumba na mavazi ambapo watalii wengi wangependa kuona, lakini tuna tatizo kubwa hatuna Maafisa Utalii katika Wilaya zetu. Tumekuwa tukiuliza mara nydingi tutafanyaje tupate Maafisa hao ili wawezeshe sasa kuboresha hii miundombinu ambayo tunaihitaji kwa ajili ya utalii wa utamaduni.

Mheshimiwa Spika, tunaomba sasa Serikali ituambie lini watatupa Maafisa Utalii ambao wamebobea katika masuala ya utalii ili watusaidie katika suala hilo?

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Wataalam wa Utalii Mikaoni na Wilayani watapatikana lini?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kama nchi, tumekuwa tukitangaza zaidi utalii wa asili kwa maana ya utalii wa safari (Mbuga za wanyama) lakini pia na utalii wa fukwe. Uko utalii wa aina nyingi sana na aina mbalimbali na labda nitumie fursa hii kuwaambia Waheshimiwa Wabunge kwamba, bado katika maeneo yote Tanzania tuna vivutio vya utalii ikiwemo ngoma za asili kama alivyosema lakini maisha yetu peke yake ni vivutio vya asili ambavyo wageni wangetamani kuona.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa kuwa na Maafisa Utalii katika kila Halmashauri, nimekuwa nikijibu swali hili hapa mara kwa mara kwamba Wakurugenzi wetu wanapowaomba Watumishi kwenye maombi yao kila mwaka, waingize maombi ya Maafisa Wanyamapori na Maafisa Utalii kwa sababu hawa ni watu ambao watakuja ku-*promote* utalii katika maeneo ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba tu nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumechukua ushauri wake, lakini niwakumbushe Wakurugenzi wote kwamba wanapoomba watumishi, waingize watumishi wenye taaluma ya utalii na wanyamapori ili kuweza kuzisaidia Halmashauri.

**SPIKA:** Tunahamia Viwanda na Biashara, swali la Mbunge wa Nachingwea, Mheshimiwa Hassan Elias Masala.

Na. 336

### **Kuwakwamua Wakulima wa Mbaazi Nchini**

**MHE. HASSAN E. MASALA** aliuliza:-

Kwa muda mrefu sasa soko la zao la mbaazi limekuwa likisuasua:-

Je, nini mpango wa Serikali katika kukwamua wakulima wa mbaazi nchini?

### **NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Elias Masala, Mbunge wa Nachingwea kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara imeandaa na kutekeleza mikakati ya muda mfupi na muda mrefu ili kutatua changamoto ya masoko ya zao la mbaazi na mazao mengine ya jamii ya mikunde. Mkakati wa muda mfupi ni pamoja na kutafuta masoko mbadala nchi za nje ambapo mbaazi ghafi zitauzwa. Jithada hizo zimeanza kuzaa matunda mwezi Machi, 2019 kufuatia ziara ya Serikali kutafuta masoko ya mazao ya kilimo ikiwemo mbaazi katika nchi jirani za Malawi, Burundi, *Congo DRC* na Zambia. Katika ziara hiyo, nchi ya Malawi kwa mwaka huu imeonyesha uhitaji wa tani 7000 na taratibu za kuhakikisha *order* hiyo inatekelezwa zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa muda mrefu ni kuhamasisha uwekezaji wa viwanda vya kukoboa na kuongeza thamani mbaazi na mazao mengine jamii ya mikunde nchini. Tayari Serikali imefanikiwa kushawishi wawekezaji kuja na kuwekeza katika viwanda vya kuchakata na kusindika mbaazi na mazao ya jamii ya mikunde. Kampuni ya *Mahashree Agro Processing Ltd* kutoka nchini India inajenga kiwanda Mkoani Morogoro ambapo

hadi kufikia mwezi Juni mwaka huu, yaani mwezi huu unaaoanza kesho, tunategemea kwamba kiwanda hicho kitaweza kuanza kazi.

Mheshimiwa Spika, kiwanda hicho kitakuwa kimeanza kufanya kazi na kitakuwa na uwezo wa kuchakata na kusindika tani 700,000 kwa mwaka. Aidha, viwanda vyta *Quality Pulse Exporters Limited* kilichopo Dar es Salaam - *SEZ (Agro Pulse Processing)* ambacho wawekezaji wake wanatoka India na Kenya sasa kinafanya kazi. Vilevile kuna kiwanda cha *Samson Agro Export Limited* nacho pia kinafanya kazi na wawekezaji wake ni kutoka India.

Mheshimiwa Spika, katika kukuza soko la ndani, naendelea kutoa wito na kuwakumbusha Watanzania kutumia mbaazi na mazao mengine jamii ya mikunde ikiwa ni moja ya mazao ambayo yana virutubisho muhimu kwa afya ya binadamu.

**SPIKA:** Jamani tumeambiwa tule mbaazi. Mbunge wa Nachingwea, Mheshimiwa Masala, swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. HASSAN E. MASALA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Naomba kufahamu, kwa sababu tumebakiza takribani mwezi mmoja ili tuweze kuvuna mbaazi na kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri anakiri kwamba ziko jitihada zimefanyika ikiwemo watu wa Malawi kuwashawishi waje wachukue mbaazi hizi; hebu atuambie mpaka sasa ndani ya mwezi huu mmoja ni maandalizi gani ambayo yamefanyika ili kuwahakikishia wakulima kupata uhakika wa masoko ya mbaazi ambazo wanakwenda kuvuna?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili ambalo nilikuwa naomba kuuliza, hebu watu wa Wizara watuambie pia, watu wa *SUA* sasa hivi wameanzisha *project* moja inaitwa *Vegi-Leg*. Hii *project* kuna baadhi ya maeneo wanaanza kufanya kazi ikiwemo ndani ya Wilaya ya Nachingwea, kuna Kijiji kinaitwa Mitumbati na Ruangwa wamechukua kijiji kimoja

kinaitwa Mibure. Kazi kubwa wanayokwenda kuiandaa ni kuweka utaratibu wa kusindika zao la mbaazi au mazao ya jamii ya mikunde. Hebu watuambie, wao kama Wizara wanashirikiana vipi na watu wa *SUA* kuhakikisha kazi hii inafanyika kwa wingi katika maeneo yote ambayo yanalima zao la mbaazi?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Kusindika Mbaazi, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:**

Mheshimiwa Spika, maandalizi yaliyofanyika kama ambavyo nimezungumza hapo awali, kwanza kwa kushirikiana na *TANTRADE* lakini na Wizara yenyewe tulifanya ziara ya kutafuta hayo masoko ili kuona kwamba mbaazi zinapokuwa tayari tuweze kujua ni wapi tunapeleka kwenda kuuza.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyo sema ni kwamba sisi wajibu wetu mwingine ni kuwahamasisha wadau mbalimbali na kuwafahamisha wapi wakulima wa mbaazi wapo na waeze kununua, lakini pia kulinda bei ya mkulima ili asionewe wakati wa kuza mbaazi zake.

Mheshimiwa Spika, kwa kupitia huu mpango ambao umeungumza unaotekelezwa na *SUA*, kimsingi Wizara yetu kama mratibu inashirikiana na Taasisi zote pamoja na Wizara nyingine katika masuala hayo yanayohisiana na lishe, lakini pia uongezaji thamani wa mazao hayo ya mbaazi pamoja na mazao mengine ili kuweka mazingira wezeshi ya wadau hao kuweza kushiriki kikamilifu na kuweza kuchakata au kuongeza thamani inayostahili.

**SPIKA:** Tunaendelea na swali la Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na litaulizwa na Mheshimiwa Amina Nassoro Malilagi.

Na. 337

### **Vifo vya Uzazi**

**MHE. AMINA N. MAKILAGI** aliuliza:-

Wanawake 24 hufariki kila siku wakati wa kujifungua nchini:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kunusuru vifo vya Wanawake wakati wa kujifungua?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA (k.n.y. WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Nassor Makilagi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tafiti zilizofanywa na Taasisi ya Takwimu ya Taifa ya Mwaka 2015 zinaonyesha vifo vitokanavyo na uzazi ni 556 kwa kila vizazi hai 100,000. Hii ni sawa na vifo 32 kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mikakati mbalimbali ya kupunguza vifo hivi ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kuboresha Vituo vya Afya kwa ajili ya kutoa huduma muhimu sa dharura kwa matatizo yatokanayo na uzazi na watoto wachanga. Pia kuendelea kuvipatia vituo vya kutolea huduma za afya vifaa tiba na vitendeakazi kwa ajili ya kuimarisha utoaji wa huduma za afya ya uzazi.

(ii) Kutoa mafunzo mbalimbali ya huduma muhimu za dhahrura kwa matatizo yatokanayo na uzazi na watoto wachanga kwa watoa huduma za afya ili waweze kutoa huduma zenye viwango kwa jamii. Aidha, mafunzo haya pia hutolewa kwa wahudumu wa afya ngazi ya jamii

kama njia ya kushirikisha jamii ili waweze kusaidia katika kupunguza vifo hivyo.

(iii) Kuhakikisha upatikanaji wa dawa muhimu kwa ajili ya uzazi salama ikiwemo dawa ya *oxytocin* kwa ajili ya kuzuia mama mjamzito kutokwa na damu nyingi wakati na baada ya kujifungua na dawa ya *magnesium sulphate* kwa ajili ya kuzuia kifafa cha mimba.

(iv) Kuimarishe huduma za rufaa kwa kuzambaza magari ya kubebea wagonjwa. Aidha, mwishoni mwa mwaka 2016 magari 67 yalitolewa kwa Halmashauri mbalimbali ili kusaidia kuimarishe huduma hizi.

(v) Wizara ilitoa mafunzo elekezi nchi nzima kwa watoa huduma wa afya ngazi za Mkoa na Halmashauri kuhusu upitajili na utoaji wa taarifa za vifo vitokanavyo na uzazi na watoto wachanga ili kutambua tatizo lillilotokea na kuweka mikakati ya kuzuia vifo hivyo visitokee tena.

(vi) Kushirikisha jamii kutambua kuwa inayo wajibu wa kutengeneza mikakati na Kanuni zitakazowawezesha kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na vifo vya watoto wachanga katika jamii husika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Amina Makilagi.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niipongeze Serikali kwa kazi nzuri inayofanya ya kuhakikisha inaboresha huduma za afya kwa ajili ya kupunguza vifo vya wanawake wanaojifungua. Pamoja na pongezi hizi nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza; moja ya sababu inayofanya wanawake wengi wanafariki kwa kujifungua ni kutokana na kutokwa damu nyingi wakati wakijifungua, lakini lipo tatizo kubwa sana la ile Benki ya Damu katika Hospitali za Mikoa. Kwa mfano, Kanda ya Ziwa Mikoa yote sita

tunategemea Bugando. Damu inatolewa Serengeti, Bunda, Simiyu, Geita, Kagera, Shinyanga mpaka Tabora na Kigoma lakini inatakiwa iletwe Bugando kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi.

Mheshimiwa Spika, wakati huo huo damu ikishatolewa kwenye mwili wa Mwanadamu inatakiwa ikae siku 30 baadaye ina-expire. Kwa hiyo, unakuta kutokana na tatizo na ule msongamano ulioko Bugando, damu inachelewa kurudi kule kwenye Vituo vya Afya na kwenye Hospitali za Mkoa na kwenye Hospitali za Wilaya. Ningependa kujua sasa, Serikali ina mkakati gani wa kujenga vituo vya Benki ya Damu katika Hospitali za Rufaa zote nchini pamoja na Hospitali za Wilaya na ikiwezekana hata Vituo vya Afya? Hilo swali la kwanza.

Mheshjimiwa Spika, swali la pili; moja ya sababu ya wanawake wanaofariki kwa kujifungua ni pamoja na kutoa mimba au mimba kutoka. Siku hizi humu mitaani kwenye maduka ya *pharmacy* kuna dawa zinaitwa *misoprostol*, Madakrati mtanisaidia kujua vizuri maana mimi siyo Daktari. Vijana wa kike na wanawake huko mtaani wanafundishana siku hizi ndio wanazotolea mimba na hasa zile mimba ambazo hazikutarajwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua, Serikali ina mkakati gani wa kudhibiti hali hiyo? Kwa sababu wanapokunywa zile dawa, mimba inatoka lakini wakati mwingine kile kiumbe kinabaki ndani kinasababisha maambukizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningependa kujua Serikali ina mkakati gani wa kudhibiti hali hiyo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, ultaka kusema kitu? Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara subiri kidogo. Mheshimiwa Nyongo nimekuona.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, naomba nimjibu Mheshimiwa Mama yangu...

**SPIKA:** Mheshimiwa Amina Makilagi.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI (K.n.y. WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO):**  
...Mheshimiwa Amina Makilagi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kwamba kweli akina mama wanapojifungua wakati mwingine damu nydingi hutoka na kuweza kupoteza maisha yao. Ushauri wangu tu ni kwamba akina mama wafuate masharti wanapokwenda kwenye kliniki wakati wa ujauzito, kuna elimu wanapewa wakati huo. Vilevile wakati wa kujifungua na hasa milmba ya kwanza ni kwamba akina mama ni vizuri wakajifungua kwenye Vituo vya Afya. Wakati mwingine wanapokuwa wanajifungua nje ya Vituo vya Afya au hospitalini hasa kwa ule ujauzito wa kwanza, inakuwa ni hatari sana, kwa sababu huwa wanafanyiwa kitu kinaitwa *Episiotomy* ambayo ni kuongeza njia wakati wa kujifungua. Sasa ile inafanya damu zinatoka nydingi, usipo-repair vizuri kwa wakati, mama huyu anaweza kupoteza maisha yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala la kuwa na *blood bank* ni kwamba huu ni mkakati ambao kila hospitali inatakiwa iwe na *blood bank* hata kama ni kiasi kidogo, wanahifadhi damu kwa ajili ya matumizi, pale inapotokea kuna dharura, basi waweze kumpa mgonjwa waweze kuokoa maisha yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vilevile kuhusiana na suala la hizi dawa ambazo ni *Misoprostol*, hizi dawa huwa zinatumika katika kuondoa au kutoa mimba. Dawa hizi huwa zinatakiwa zitolewe chini ya usimamizi wa daktari, yaani daktari ndiye anayetakiwa aandike dawa hiyo. Mgonjwa anapokwenda *pharmacy*, basi aende na cheti cha kuweza kupewa dawa hiyo. Hizi dawa huwa zina matumizi mengine.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna dawa hizo zimeanza kuzunguka ziko kwenye ma-*pharmacy* na dawa hizi ni za kazi maalum kwa kuzuia damu zisitoke, lakini wanazitumia vibaya kwa sababu *side effect*ya hiyo dawa ni kuweza kutoa mimba. Kwa hiyo, tunawashauri watu wote wenye *pharmacy* wasitoe dawa hizi bila *prescription*. Lazima dawa hii daktari athibitishe, aandike cheti, ampeleke kwenye *pharmacy* na mgonjwa aweze kupewa dawa hiyo. Kwa maana tunafahamu kabisa madaktari wanapotoa dawa hizo wanazitoa kwa sababu maalum.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana, tunashukuru sana kwa majibu mazuri Mheshimiwa Dkt. Haroon Nyongo. Sasa Mheshimiwa Ally Keissy, vifo vya akina mama.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Vifo vingine vya akina mama vinatokana na akina mama wenyewe. Juzi tu Kirando katika Jimbo langu la Nkasi Kaskazini, mama mmoja, tena zao lake la nane, kachelewa mwenyewe makusudi, Kirando kuna kituo kizuri cha afya kikubwa na kizuri kinafanya na operesheni, ni kizuri sana. Kajifanyia operesheni mwenyewe kwa kutumia nyembe na katoa mtoto. Hivi sasa yuko hospitali katika Kituo cha Afya cha Kirando, hali yake siyo nzuri, ila hali ya mtoto ni nzuri. Vifo vingine vinasababishwa na akina mama wenyewe kuchelewa kwenda kwenye Vituo vya Afya. (*Kicheko*)

**SPIKA:** Eeeh! Swali lake ni kwamba katika mazingira kama hayo, Serikali inasema nini? Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Haroon Nyongo, endelea na majibu. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MADINI (K.n.y. WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, naomba nijibu hoja ya Mheshimiwa Keissy kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kama nilivyozungumza katika majibu ya nyongeza ni kwamba akina mama wote nchini unapokuwa mjamzito, pale anapo jitambua tu kwamba sasa hivi amekuwa mjamzito ni vyema ukaenda kliniki kwa ajili ya kwanza unaenda kupimwa, wanaangalia *development* ya mtoto, lakini vilevile wanaangalia afya yako wewe mama kama inakwenda vizuri na kama kuna tatizo watakwambia na nini ufanye.

Mheshimiwa Spika, vilevile ni kwamba kwa kipindi hicho wanakupa elimu ya uzazi salama. Kwa hiyo, ni vizuri wakina mama wote wakati wa kujifungua hili suala usichukulie kama zamanii, tulikuwa na ma-tradition healers wale wanaitwa Wakunga wa Jadi, wasiende tena kule. Wengine pengine alivyosema Mheshimiwa Keissy, huyu mama ana uzao mwangi, kwa hiyo, ameshakuwa na *experience*, anaona kwamba kuzaa ni kitu rahisi, lakini kumbe kila kizazi ni *special*. Ni vizuri ukaenda kwenye Kituo cha aAya ukapewa huduma na Manesi ambao ni *professional*.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ehee! Kuna wengine kwa kweli wanafanya makusudi. Maana yake wewe mama umezeeka, unabeba mimba ya nini? Mheshimiwa Dkt. Sware. (*Kicheko*)

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi. Kwa kuwa vifo vingi vya wamama wakati wa kujifungua hutokana na kukosa huduma na ufuatiliaji katika hatua mbalimbali za ujauzito, sasa basi Serikali haioni ni wakati muafaka sasa kurasimisha hao *Community Health Workers* au watoa huduma katika jamii kwa mambo ya afya ili waweze kupewa mori, kuelimishwa na ili kuwawezesha wanajamii hususan akina mama wajawazito ili kupunguza vifo vya wamama wajawazito? (*Makofi*)

**SPIKA:** Tunaendelea, Mheshimiwa Haroon malizia.

**NAIBU WAZIRI MADINI (K.n.y. WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO):**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, naomba nijibu swalii la Mheshimiwa Dkt. Semesi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba *Community Health Workers* wanapewa elimu pana. Tumeanza kwenye masuala ya UKIMWI, lakini vilevile kwenye masuala ya afya ya uzazi na afya ya lishe kwa watoto. Hii elimu inatolewa kwa hawa *Community Health Workers* ili waweze kutoa elimu kwa wananchi, watoe elimu kwa wanavijiji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vilevile ni kwamba sasa hivi mkakati mkubwa ambao tunafanya katika Wizara hii ya Afya ni kuhakikisha kwamba hata wale ambao ni Waganga wa Jadi na wenyewe wanapewa elimu waelezwe vihatarishi, wapewe elimu kuweza kutambua hali ya hatari ambayo inaweza kusababisha mtu kupata kifo kutokana na uzembe fulani, kwa mfano, kupungukiwa na damu, masuala hayo ya ujauzito, wanapewa ile elimu ambayo ni kujua kabisa hali hatarishi kwamba katika hali kama hii mgonjwa huyu anatakiwa apewe huduma fulani, lakini hali fulani ikizidi, basi mgonjwa huyu apelekwe hospitali aweze kupata huduma zaidi. (*Makofii*)

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Haroon Nyongo kwa majibu haya.

Waheshimiwa Wabunge, mtaona tuko katika muda kabisa sasa, tuendelee. Leo ni Wizara muhimu ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambayo nina hakika Waheshimiwa Wabunge karibu wote mna cha kusema kuhusu Wizara hiyo. Kwa hiyo, tunataka kulinda muda wenu.

Katika wageni wa leo tunaanza na wageni wa Mheshimiwa Spika wanatoka Kongwa, ni Wanajumuiya wa Jumuiya inayoitwa Nazareti kutoka Kanisa la Anglikana pale St. Michaels Kongwa, wakiongozwa na Mwalimu Matajiri. Sijui wako upande gani? Naomba msimame, ahsanteni sana na karibuni sana. Tunawashukuruni sana kututembelea na

tunawashukuru sana kwa kutuombea kila wakati, tunaendelea kubarikiwa kwa dua zenu. Ahsanteni sana. (*Makof*)

Wengine ni wageni 139 wa Mheshimiwa Waziri William Lukuvi, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambaao ni pamoja na mke wa Mheshimiwa William Lukuvi, Ndugu Germina Lukuvi. Mama Lukuvi, ahsante sana shemeji yetu, karibu sana mjengoni. Sijakuona bado! Eeeh, karibu sana. Hajawahi kututembelea hata mwaka mmoja bwana. Safari hii ndiyo amekuja, eeeh, karibu sana mama. Tunafurahi sana kuwa pamoja nawe. (*Makof*)

Wengine ni wageni 117 wa Mheshimiwa Lukuvi, ni Watendaji wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Taasisi zake akiwemo Katibu Mkuu, Ndugu Dorothy Mwanyika. Katibu Mkuu, ahsante. Tumemwona Katibu Mkuu? Eeh, sawa sawa. Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Mathias Kabunduguru, karibu sana. Mwenyekiti wa Bodi ya *National Housing*, Dkt. Sophia Kongela, karibu. Mwenyekiti wa Bodi Tume ya Taifa ya Matumizi ya Ardhi, Ndugu Fidelis Mutakyamilwa. Mkurugenzi Mkuu *National Housing*, Dkt. Mulid Banyani, karibu sana. Mkurugenzi Mkuu Tume ya Taifa ya Matumizi ya Ardhi, Dkt. Stephen Nindi, karibu sana. Kaimu Mkurugenzi Mkuu Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi, Ndugu Dismas Minja, karibu. (*Makof*)

Wengine ni Mkuu wa Chuo cha Ardhi Tabora, Ndugu Biseko Musiba, karibu. Kaimu Mkuu wa Chuo cha Ardhi Morogoro Dkt. Adam Nyaruhuma, karibu. Kamishina wa Ardhi, Ndugu Mary Makondo, karibu sana Kamishna. Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu, Tutubi Mangazeni. Mkurugenzi wa Mipango Miji na Vijiji, Prof. John Lupala, karibu sana. Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani, Ndugu Hamdouny Mansour, karibu. Mthamini Mkuu wa Serikali, Ndugu Evelyn Mugashwa, ahsante sana. Mhasibu Mkuu, Ndugu Walter Lungu; Mkurugenzi Mkuu wa Ununuzi na Ugavi, Ndugu Ziada Msangi. Wizara hii ina akina mama wengi wenye madaraka makubwa sana. (*Makof*)

Pia wako wageni wengine 21 wa Mheshimiwa Waziri ambaao ni kutoka *Care International*, Mary Ndaro, karibu Mary. Mtendaji Mkoo wa *WHC* Fred Msemwa, karibu. Mkurugenzi Mkoo wa *WHC*, Ndugu Oscar Mgaya, karibu. *Chief of Party LTA* Sulivan Tressan; karibu sana Sulivan. Mtaalam Mshauri *LTA*, Malaki Msigwa karibu. Mtaalam *African Wildlife Foundation*, Ndugu Pastory Magingi, karibu. Mwakilishi wa Tanzania *Natural Resources Forum*, Ndugu Zakaria Faustine, karibu. Mratibu *Tanzania Land Alliance*, Ndugu Bernard Baha. (*Makofii*)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge ni wageni watano wa Mheshimiwa Angeline Mabula, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambaye ni mtoto wake, Dayana Vivian Mabula, karibu sana. Eeh, hee he! Maana yake kama mama vile. Dayana Waheshimiwa Wabunge wanasema hawajakuona, hebu simama tena. Eeh, safi kabisa; na nimeambiwa kabisa hajaolewa bado. kwa hiyo Wagogo wote mnakaribishwa kupita kupita hapo. (*Kicheko*)

Wageni wengine wanne wa Mheshimiwa Mabula ni Watendaji wa Sekta ya Ardhi kutoka Mkoa wa Mwanza wakiongozwa na Katibu Tawala Msaidizi wa Miundombinu Mkoa wa Mwanza, Ndugu Seif Hussein. Wale wa kutoka Mwanza, karibuni sana, kutoka Ilemela, Nyamagana, kote huko. (*Makofii*)

Wageni wa wanne wa Mheshimiwa Mwita Waitara, Naibu Waziri wa TAMISEMI ambaao ni wanafunzi wa *Excellent College* kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Sospeter Mosewe. *Excellent College* kutoka Dar es Salaam karibuni sana, wale pale. (*Makofii*)

Wageni 73 wa Mheshimiwa Antony Mavunde, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkoo, Kazi, Vijana, Ajira ambaao ni Wanachuo wa Chuo cha Utafiti na Maendeleo ya Jamii, wakiongozwa na Ndugu Gitinkwi Marwa. *Ooh*, karibuni sana kutoka Chuo cha Maendeleo ya Jamii hapa Dodoma. (*Makofii*)

Wageni wa watau wa Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate ambao ni wapiga kura wake kutoka Jimbo la Tunduru Kusini Mkoa wa Ruvuma. Wageni wa Mheshimiwa Mpakate wale pale, karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni tisa wa Mheshimiwa Fatma Toufiq ambao ni Wanahabari kutoka *TAMWA Tanzania Media Women Association* na ni Waandishi wa Usalama Barabarani kutoka Mikoa mbalimbali wakiongozwa na Ndugu Gladness Munuo. *TAMWA*, karibuni sana, tunashukuru kuwa nanyi. (*Makofi*)

Wageni 112 wa Mheshimiwa Joseph Haule ambao ni wanafunzi 100 na walimu 12 kutoka Shule ya Sekondari ya St. Peter Clever ya Mikumi Mkoani Morogoro. *Ooh*, karibuni sana watoto wetu kutoka Mikumi pamoja na Ma-sister karibuni sana. Karibuni sana watoto wetu, mtapokelewa baadaye mtapata maelezo ya kutosha kuhusiana na shughuli za Kibunge. Karibuni sana. Watoto wamependeza kweli kweli! Hongereni sana Sister. Sijui kati ya *Peter Cleverya Mikumi* na *Peter Cleverya* hapa Dodoma nani zaidi? (*Kicheko/Makofi*)

Wanafunzi 60 na walimu watatu kutoka Shule ya Msingi ya Fransalian ya Morogoro Mjini wakiongozwa na Sister Treesa Thomas. *Ooh*, hongereni sana. Sister Treesa karibuni sana. Watoto wanapendeza, shule za siku hizi bwana! Eeh! Ahsanteni sana na karibuni sana Bungeni. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, watoto wakija wametoka mbali, tuwapigie hata makofi kidogo. Asanteni sana. Nawashukuruni sana. Eeh, Mama Salma aliwahi kusema, mtoto wa mwenzio ni wako. Watoto ni upendo jamani. Tunashukuru sana tunapoona shule nzuri namna hii. (*Makofi/Kicheko*)

Miaka michache iliyopita ilikuwa lazima upeleke mtoto nchi jirani ndiyo apate shule kama hii. Sasa hivi nchi jirani wanatafuta namna ya kuleta watoto hapa Tanzania. Kabisa kabisa! Halafu nani anasema elimu ya Tanzania imeteremka, imeshuka? Nani huyo? Elimu imepanda sana. Ahsante sana.

Mwisho ni wanafunzi 25 kutoka Chuo Kikuu cha Mtakafitu John au Mtakatifu Yohana cha hapa Dodoma wakiongozwa na Ndugu Jerry Motela. wale wa St. John karibuni sana. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Edwin Ngonyani anatangaza kwamba siku ya Ijumaa iliyopita kama leo kwenye mashine zetu zile, miwani yake ilijichanganya na miwani ya Mheshimiwa Mbunge mwingine. Sasa amekuwa na hiyo miwani, japo hiyo ya mwenzake aliiacha pale kwa watu wa usalama, getini, anaomba kama ulichukua miwani ambayo unaona kama siyo yako, uende uchukue ile yako na umrudishie ile yake. Unaweza ukawahuisha hawa wahudumu wetu kuweza kurejesha ile miwani ya Mheshimiwa nawe ukapata yako. Nashukuru sana.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Naomba tu tuendelee kwa leo, wiki ijayo tutaangalia fursa. Katibu!

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

#### **HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa moja kwa moja namwita Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa William Lukvi ili aweze kutusomea hotuba yake na kutoa hoja yake mbele ya Bunge hili. Mheshimiwa Waziri, karibu sana. (*Makof!*)

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, mbele yako na Kiti chako, naomba kutoa hoja mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba baada ya kuzingatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni leo na Mwenyekiti wa Kamati

ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii inayohusu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, sasa Bunge likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Fungu 48 na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi Fungu Na. 3 kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Fungu 48 na Tume ya Taifa ya Matumizi Bora ya Ardhi Fungu Na. 3 kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Pamoja na hotuba hii, nawasilisha taarifa ya utekelezaji ya programu ya miradi iliyo simamiwa na Wizara na Taasisi na Majedwali mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kushiriki katika Bunge hili. Aidha, kufuatia kifo cha Mheshimiwa Steven Ngonyani aliyekuwa Mbunge wa Korogwe Vijijini kilichotokea mwezi Julai, 2018, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwako wewe binafsi, Bunge lako Tukufu, familia ya Marehemu, ndugu, wananchi wa Jimbo la Korogwe Vijijini, pamoja na wote walioguswa na msiba huo.

Mheshimiwa Spika, vilevile natoa pole kwa wananchi wote waliofiwa na walioathirika kutokana na majanga mbalimbali yaliyotokea katika maeneo mbalimbali nchini. Kipekee natoa pole kwa familia ya watumishi tisa wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi waliopoteza maisha katika ajali ya gari iliyotokea huko Kirombero tarehe 22 mwezi wa pili mwaka huu. Tumepoteza vijana ambaobado walikuwa wanategemewa na Taifa hili pamoja na familia zao. Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu wote mahali pema Peponi, Amina. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee, naomba pia nitumie fursa hii adimu kutambua na kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake

shupavu katika kusimamia rasilimali za Taifa, kupambana na rushwa na kuimarisha nidhamu ya uwajibikaji na utumishi wa Umma. Katika awamu hii tumeshuhudia maendeleo makubwa katika sekta zote hususan utoaji wa elimu bila malipo kwa shule za msingi na hadi sekondari, uimarishaji wa usalama wa milki za ardhi kwa wananchi hususan wananchi wanyonge, uboreshaji wa huduma za afya nchini, ujenzi wa viwanda, ufufuaji wa Shirika la Ndege la Tanzania, ujenzi wa reli ya kisasa, ujenzi wa mradi wa kufua umeme katika Mto Rufiji na pamoja na ujenzi wa bomba la mafuta.

Mheshimiwa Spika, mafanikio haya ni matokeo ya uongozi makini na thabiti katika masuala ya kiuchumi na kijamii, lakini tumeshuhudia hata kwenye Sekta ya Ardhi migogoro mbalimbali ikipungua katika awamu hii. Hakika uongozi wake umezidi kuijengea heshima kubwa nchi yetu na katika Bara la Afrika na Dunia kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza pia Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa jitihada zao za kuongoza, kusimamia, kuendeleza amani, utulivu na maendeleo ya nchi yetu. Nawashukuru pia kwa ushauri, maelekezo na ushirikiano wanaonipa ambao unaniwezesha kutekeleza majukumu niliyokabidhiwa ya kuongoza sekta hii muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu.

Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Dkt. Ali Mohammed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Balozi Seif Ali Idd, Mbunge, Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa mafanikio makubwa sana yanayoendelea kupatikana chini ya uongozi wao imara huko Tanzania Visiwani.

Mheshimiwa Spika, napenda sana kukupongeza wewe binafsi, Mheshimiwa Spika wetu kwa kazi kubwa kabisa

na weledi mkubwa wa kuongoza Bunge hili kwa kushirikiana na Naibu Spika Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu, Mbunge kwa ujumla, kwa kuongoza na kusimamia kwa ufanisi shughuli zetu za Bunge letu Tukufu. Hongera sana.

Mheshimiwa Spika, vilevile ninawapongeza Wenyeviti wote wa Bunge ambao kwa nyakati tofauti wamekuwa wakiongoza shughuli za Bunge kwa ufanisi. Mwenyezi Mungu aendelee kuwaongoza na kuwapa nguvu, afya njema na hekima.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kuwapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri walioteuliwa na Mheshimiwa Rais katika mabadiliko ya Baraza la Mawaziri aliyoyafanya kwa nyakati tofauti katika mwaka 2018 na 2019. Nawatachia wote kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Mwita Mwikwabwe Waitara, Mbunge wa Ukonga; Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul, Mbunge wa Babati Mjini; Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijijini; Mheshimiwa James Kinyasi Milly, Mbunge wa Simanjiro; Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer, Mbunge wa Monduli; Mheshimiwa Abdallah Ally Mtalea, Mbunge wa Temeke; Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe; Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha, Mbunge wa Serengeti; Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka, Mbunge wa Liwale; na Mheshimiwa John Pallangyo, Mbunge wa Arumeru Mashariki, kwa kuchaguliwa katika chaguzi ndogo zilizofanyika hivi karibuni. Nawatachia kila la heri katika kutekeleza majukumu yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake ambayo imeelezea utekelezaji wa malengo ya Serikali katika mwaka wa fedha 2018/2019 na mwelekeo wa kazi za Serikali zitakazotekelzwa kwa mwaka 2019/2020. Wizara

yangu itayafanya kazi maelekezo na maagizo yanayoihu  
Sekta ya Ardhi ili kuhakikisha kwamba malengo ya Serikali ya  
Awamu ya Tano yanafikiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee natoa shukrani zangu za dhati kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii chini ya Makamu Mwenyekiti shupavu, Mheshimiwa Kemirembe Rose Julius Lwota, Mbunge, kwa ushirikiano mkubwa na ushauri wao ambao umeiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, namshukuru aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati hii Mheshimiwa Nape Moses Nnauye, Mbunge, kwa kuiongoza Kamati katika kipindi chake kabla ya Mheshimiwa Kemirembe. Nawashukuru sana kwa uongozi wao.

Mheshimiwa Spika, pia, nawashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati kwa uchambuzi makini sana walioufanya na ushauri wanaoutoa kila mara wakati wa kupitia taarifa ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 48 na Na. 03, kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Pia, nawashukuru kwa maoni na ushauri waliota kwa Wizara wakati wa ziara mbalimbali za kukagua miradi ya maendeleo inayosimamiwa na Wizara na Taasisi zake. Napenda kulihakikisha Bunge lako Tukufu kwamba maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati hii yatazingatiwa kwa heshima kubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani na pongezi za dhati kwa wananchi wa Jimbo la Ismani kwa ushirikiano walilonipa na wanaoendelea kunipa katika kipindi chote cha kuwawakilisha hapa Bungeni na Serikalini. Aidha, nawapongeza kwa juhudni wanazofanya katika kujiletea maendeleo yao na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, mwisho, siyo kwa umuhimu, naishukuru sana familia yangu kule nyumbani ikiongozwa na mke wangu mpenda Germina Lukuvi ambaye leo ameshuhudiwa hapa na watoto wangu wote watatu;

Norbert, Brown na Anni kwa uvumilivu wao, lakini pia kwa kuniombea, kunishirikisha na kuniwezesha kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, sekta ya ardhi nchini imeendelea kuimarika na kuchangia katika maendeleo ya uchumi wa wananchi na Taifa kwa ujumla hususan katika kipindi hiki tunapojozatiti kujenga uchumi wa viwanda ili kuchochaea mageuzi ya uchumi na maendeleo ya watu. Pia sekta hii imeendelea kuwa kiungo wezeshi katika sekta mbalimbali nyingine za uzalishaji ikiwemo Viwanda, Kilimo, Mifugo, Ujenzi, Misitu, Maliasili, Miundombinu, Maendeleo ya Makazi na Miliki na hivyo kuongeza thamani ya uhitaji wa ardhi nchini.

Mheshimiwa Spika, ukuaji wa sekta ya ardhi nchini kwa mwaka 2018/2019 unaonesha kuendelea kuimarika ikillinganishwa na miaka iliyotangulia. Katika kuhakikisha Sekta ya Ardhi inaimarika, Wizara yangu imeendelea kujenga mifumo ya utawala na usimamizi wa ardhi, kukuza na kuhakikisha kuwepo kwa mifumo ya usalama wa milki nchini, kuhimiza matumizi bora ya ardhi, kurekebisha na kurahisisha mifumo ya upangaji, upimaji na usimamizi wa ardhi. Aidha, Wizara itaendelea kuboresha mahusiano ya wadau mbalimbali katika uendelezaji na utatuvi wa migogoro ya ardhi, kukuza uwezo na kutunza kumbukumbu, kutoa taarifa na elimu kwa Umma.

Mheshimiwa Spika, tunajua wote kwamba, takriban asilimia 75 ya wakazi mijini wanaishi katika maeneo yasiyopangwa na hawana miliki, hawana nyaraka za kisheria za kuthibitisha uhalali wa umiliki wa ardhi yao. Hali hii inawafanya wananchi kuendelea kuwa na mitaji ya ardhi iliyokufa (*dead capital*) na hivyo, kuwa mojawapo ya kikwazo cha kujlendeleza kiuchumi na kuwapa fursa za kujajiri. Pia inafanya ardhi isiwe na mchango mkubwa katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeongeza kasi ya kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kupanga, kupima na kumilikisha ardhi kisheria kwa kushirikiana na Mamlaka za

Upangaji. Aidha, Wizara inatekeleza mkakati maalum wa kurasimisha na kuboresha makazi yaliyoendelezwa kiholela na kutoa hati na leseni za makazi. Jumla ya makazi 610,655 katika Halmashauri mbalimbali nchini yamerasimishwa. Haya yalikuwa makazi holela, sasa ni makazi rasmi na wananchi wamepewa hati zao. Aidha, Hatimiliki 115,595 zimetolewa katika maeneo yaliyopangwa mapya kabisa na hatimiliki za kimila 308,549 zimeandaliwa na kusajiliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa makusanyo ya maduhuli ya Serikali, yameongezeka kutoka shilingi bilioni 74.71 mwaka 2015/2016 hadi bilioni 100 mwaka 2017/2018. Makusanyo hayo yameongezeka kutokana na juhudzi za Wizara katika kusimamia kupanga, kupima na kumilikisha ardhi. Vilevile, Serikali imesajili Vyeti vya Ardhi ya Vijiji vipatavyo 3,018 kati ya vijiji 12,545 kipindi cha mwaka 2015 hadi 2018, hilvyo, kufanya idadi ya vijiji vyenye Vyeti vya Ardhi vilivyotolewa na Kamishna wa Wizara yangu vilivyoasajiliwa nchini vimefikia sasa 11,153. Lengo ni kuhakikisha vijiji vyote nchini vinasajiliwa kabla ya kipindi cha kwanza cha awamu hii kukamilika.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia ilipunguza gharama ya umilikishaji wa ardhi na kuwa rafiki kwa wananchi. Kwa mfano, tozo ya mbele (*premium*) kwa mtu anayemiliki ardhi kwa mara ya kwanza, imepunguzwa kutoka 7% ya thamani ya ardhi iliyorasimishwa mijini katika mwaka wa fedha 2015/2016 hadi 1% kwa urasimishaji. Kwa sababu, tunaamini kwamba watu wanaorasimishiwa, waliojenga kiholea ni watu masikini. Kwa hiyo, kodi ya umilikishaji ya *premium* imepunguzwa kutoka 7.5% mpaka 1% na 2.5% kwa ardhi iliyopangwa kwa mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, gharama elekezi ya urasimishaji makazi imepunguzwa kutoka tulipoanza zoezi la urasimishaji mwaka 2015/2016 ilipokuwa shilingi 300,000/= mpaka sasa ni shilingi 150,000/= tu nchi nzima kwa mtu ye yeyote anayetaka kurasimisha ardhi yake. Tunaendelea kufanya utafiti ili angalau gharama hizi za 150,000/= ziendelee kupungua, watu waweze kumilikishwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha na kurahisisha utambuzi wa vipande vya ardhi mijini na kupata taarifa za wamiliki, Serikali imeandaa mfumo wa kielektroniki unaotumia simu za mkononi (simu janja) na kuwezesha kutoa leseni za makazi zinazotambulika kisheria. Mfumo huu umeanza kutekelezwa katika Jiji la Dar es Salaam na utaendelea kutumika nchi nzima. Hadi kufikia tarehe 15 mwezi huu, takriban vipande vya ardhi vya matumizi mbalimbali 150,000/= vimesajiliwa na wahusika wamepewa leseni za makazi ambazo zinatambulika na kibenki.

Mheshimiwa Spika, hatua hii itawapa wananchi uhakika wa miliki zao na kuwezesha ardhi yao kutumika kama mtaji wa kiuchumi. Zoezi hili linaendeshwa kwa ghamama nafuu sana tukijua hawa watu waliojenga kwenye *squater* ni masikini. Kwa hiyo, kila mtu anayepewa leseni ya makazi anachangia shillingi 5,000/= tu mpaka kupata leseni ya makazi.

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa wamiliki wote wa ardhi katika makazi yasiyopangwa, kutoa ushirikiano kwa wataalam watakaofika katika mitaa yao na kutoa taarifa sahihi za umiliki ili kufanikisha zoezi hili. Serikali itaendeleza kasi ya kufanya zoezi hili la utoaji wa leseni za makazi mwaka huu kwa nchi nzima, lakini pia itaongeza kasi ya utatuzi wa migogoro mbalimbali ya ardhi nchi nzima ambayo kwa sasa kila mmoja anaamini na anaona kwamba imepungua sana. Pia tutaendeleza jitihada za kukamilisha Sera ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Sera ya Makazi na Nyumba na kukamilisha Sheria ya *Real Estate Regulatory Authority* ambayo tumeshaanza kutayarisha, iko katika hatua ya mwisho. Sheria hii itawasaidia sana wapangaji, wenye nyumba, watoza kodi, pamoja na kuzuia uhalifu na utakatishaji wa fedha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016/2017 – 2020/2021, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015, Hotuba ya Rais wa Jamhuri

ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, katika Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge la Novemba, 2015; Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi wa 2013 – 2033; Agenda ya Dunia ya Malengo Endelevu ya Maendeleo ya mwaka 2030; Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995; Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 pamoja na sheria na miongozo mbalimbali iliyotolewa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia haya, mwelekeo wa Sekta ya Ardhi ambao Wizara itaendelea kuusimamia kwa dhati hadi mwaka 2025 ni kuleta mageuzi katika uandaaji na usimamizi wa upangaji, upimaji, uthaminishaji na umilikishaji wa ardhi nchini ili kuwawezesha wananchi na taasisi kuwa na uhakika wa miliki za ardhi.

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hiyo, mageuzi tunayotaka kuyafanya ni kuhakikisha Watanzania wanapata hati za kumiliki ardhi na kuzitumia kwa ajili ya kujiletea maendeleo kwa ustawi wa kiuchumi na kijamii. Malengo mengine ya mageuzi haya ni pamoja na kuboresha utendaji na utoaji huduma katika Sekta ya Ardhi ikiwemo kusimamia watumishi wa Sekta ya Ardhi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Pia kuratibu na kusimamia sera, sheria, kanuni na miongozo mbalimbali ya kisekta.

Mheshimiwa Spika, vileyile, Wizara itatumia teknolojia ya kisasa katika upangaji, upimaji, umilikishaji, uendelezaji wa miji na vijiji, utunzaji wa kumbukumbu za ardhi na ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali. Azma hii inalenga kuhakikisha huduma za Ardhi zinatolewa kwa ufanisi na kwa gharama nafuu. Tumeanza Dar es Salaam mifumo unganishi kwa kutumia elektroniki, lakini katika mwaka wa fedha huu na mwaka mwingine unaokuja, tutaanza programu hii katika mikoa yote nchini na tutaendelea nchi nzima kwa lengo la kuachana na analogia, tunataka tuingie tufanye shughuli kidijitali.

Mheshimiwa Spika, mageuzi haya pia yanalenga kupata ufumbuzi wa kudumu wa migogoro mbalimbali ya

matumizi ya ardhi nchini na kujenga uelewa kwa wananchi na wadau hususan kuhusu masuala mbalimbali ya ardhi. Aidha, Wizara itaendelea kuwajengea uwezo watumishi ili kuboresha huduma zinatolewa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, majukumu na hali ya Sekta ya Ardhi nchini, naomba sasa nielezee mapitio ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Fungu 48, pamoja na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi, Fungu Na. 03, kwa mwaka wa fedha 18/2019 na makadirio ya mapato na matumizi ya mafungu haya kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Takwimu za utekelezaji wa bajeti zilizomo katika hotuba hii zinaainishwa hadi tarehe 15 mwezi Mei, mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti wa mwaka 2018/2019 na malengo yake ya mwaka wa fedha ujao 2019/2020. Wizara imetekeliza majukumu yake kuitia mafungu mawili ya kibajeti. Mafungu hayo ni Fungu 48 ambalo ni la Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Fungu Na. 03 ambalo ni la Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, katika mapato na matumizi ya fedha, Fungu 48, mapato katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara ilipanga kukusanya shilingi bilioni 120 kutokana na vyanzo vya mapato ya kodi, ada na tozo mbalimbali za ardhi. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, mwaka huu 2019 Wizara imekusanya shilingi bilioni 75.73 sawa na asilimia 63.1 ya lengo. Nakisi ya makusanyo ya maduhuli yatokanayo na ardhi inachangiwa kwa sehemu kubwa na baadhi ya wamiliki kutolipa kodi ya pango la ardhi kwa wakati. Wizara inaendelea kufuatilia na kuhamasisha wamiliki wa ardhi kulipa kodi ya pango la ardhi kwa kutumia vyombo vya habari na kuwafikisha Mahakamani wadaiwa sugu na kuwafutia miliki zao.

Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii kuwapongeza wamiliki wa ardhi waloliipa kodi ya pango la ardhi kwa wakati. Aidha, natoa rai kwa wananchi pamoja na

Waheshimiwa Wabunge ambao wamepimiwa ardhi na kutambuliwa miliki zao na wale wote wanaodaiwa kodi ya pango la ardhi kulipa kwa wakati ili kuepuka hatua za kisheria. Vilevile, watu wote waliopimiwa au kurasimishiwa ardhi zao wamilikishwe ardhi husika na kupewa hatimiliiki kwa mujibu wa sheria na kulipia kodi ya pango la ardhi. Aidha, napenda sana kutumia fursa hii kuzipongeza Halmashauri zote ambazo zimevuka malengo na mikoa yote ya ukusanyaji wa kodi katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, mwisho wa mwezi wa Sita nitatangaza malengo ya makusanyo halisi ya kila Wilaya na Mkoa na asilimia ambayo kila mkoa umefikia katika makusanyo. Aidha, kwa leo napenda kuupongeza angalau mkoa uliosimamia vizuri ukusanyaji wa kodi ya ardhi ya mapato haya ya ardhi kwa mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 21 mwezi wa Tano, Mkoa ambao ulikuwa unaongoza kwa ukusanyaji wa kodi ya ardhi ni Mkoa wa Dodoma, ambao umekusanya kwa asilimia 173 ya lengo. Hii ni kwa sababu ya jitihada pekee za Manispaa ya Jiji la Dodoma kuendelea kupima viwanja vingi, ndio maana imepaisha. Kwa hiyo, Dodoma inaongoza, lakini Mkoa wa mwisho ni Katavi ambao wamekusanya asilimia 13.81 tu ya lengo. Wilaya na mikoa yote isimamie kuhakikisha wanafikia lengo kabla ya terehe 30 mwezi Juni.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara yangu inatarajia kukusanya shilingi bilioni 180 kutokana na kodi ya pango la ardhi, ada na tozo mbalimbali zinazohusiana na Sekta ya Ardhi. Lengo hili linafikiwa kwa kutekeleza mikakati ifuatayo:-

(1) Kuimarisha mifumo ya TEHAMA ya utunzaji wa kumbukumbu na kuboresha taarifa za ardhi;

(2) Kurahisisha ukadiriaji wa kodi ya pango la ardhi na tozo zitokanazo na sekta ya ardhi kwa kutumia vifaa elektroniki vinavyohamishika (*Point of Sales Machines – POS*);

(3) Kuendelea kushirikiana na Mamlaka za Upangaji pamoja na sekta binafsi katika zoezi la upangaji, upimaji, umilikishaji ardhi na kuongeza wigo wa mapato;

(4) Kutumia mfumo wa kielektroniki unaotumia simu ya mkononi (simu janja) na kuwezesha kutambua na kukusanya taarifa na kusajili vipande vya ardhi mijini na kutoa leseni za makazi zinazotambulika kisheria;

(5) Kuendelea kusimamia uendelezaji wa ardhi kulingana na matumizi yaliyopangwa na kuwatoza adhabu wakiukaji wa masharti kwa mujibu wa sheria;

(6) Kuhakikisha watu wote wa mijini wenye nyumba na ardhi isiyopimwa wanarasimishiwa, siyo kubomolewa; na kupewa hati na leseni za makazi;

(7) Kuendelea kusimamia na kuchukua hatua kali za kisheria kwa wamiliki wote wasiolipa kodi za ardhi kwa wakati;

(8) Kuhakikisha kuwa wamiliki wote wa ardhi waliopimiwa na kurasimishiwa maeneo yao, wanamilikishwa ili waweze kulipa kodi ya pango la ardhi kwa mujibu wa sheria;

(9) Kuhakikisha kuwa wamiliki wote wa ardhi waliopimiwa na kurasimishiwa maeneo yao wanamilikishwa ili waweze kulipa kodi ya pango la ardhi kwa mujibu wa sheria;

(10) Kuendelea kuboresha mfumo wa ulipaji maduhuli yatokanayo na ardhi kwa kutumia mitandao ya simu;

(11) Kuendelea kuhuishwa vigezo vinavyotumika kukadiria tozo mbalimbali za ardhi ili ziendane na wakati; na

(12) Kuendelea kutoa elimu kwa Umma kuhusu umuhimu wa wamiliki wa ardhi kulipa kodi kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara iliidhinishiwa shilingi bilioni 68.98 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 17.68 ni kwa ajili ya mishahara; shilingi bilioni 17.76 kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 30.54 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Baada ya uhakiki wa madeni uliofanywa na Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ilipewa shilingi bilioni 12.8 kwa ajili ya kulipa madeni ya wazabuni na hivyo kuifanya bajeti ya Wizara kuwa na jumla ya shilingi bilioni 78.8.

Mheshimiwa Spika, hadi tarehe 15 Mei, 2019, Wizara ilipokea shilingi bilioni 51.92 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo, sawa na asilimia 65.9 ya bajeti. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 12.9 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 22.2 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, shilingi bilioni 16.2 zilitolewa kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mapato na matumizi Fungu Na. 03. Kwa upande wa mapato, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Tume ilitarajia kupata kiasi cha shilingi milioni 700. Kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi milioni 680.15 kutoka kwa wadau wa kimkakati na kiasi cha shilingi milioni 19.85 kutokana na kodi ya pango la nyumba za Tabora na mauzo ya nyaraka mbalimbali za zabuni. Hadi tarehe 15 Mei, 2019, Tume ilipata shilingi milioni 998.16 sawa na asilimia 142.3 ya lengo kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Tume.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Tume iliidhinishiwa shilingi bilioni 7.08 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 1.10 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi milioni 979.8 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni tano ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2019, Tume ilipokea shilingi bilioni 3.37 fedha za matumizi ya kawaida na

maendeleo sawa na asilimia 47.59. Kati ya fedha hizo, shilingi milioni 737.6 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi milioni 633.7 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni mbili ni fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, huduma za utawala wa ardhi. Wizara yangu inasimamia huduma za utawala wa ardhi ikiwemo utoaji wa hatimilki na hati za hakimiliki za kimila, usajili wa hati, nyaraka na miamala ya ardhi, usuluhishi wa migogoro ya ardhi, uthamini wa mali, uendelezaji wa miliki, ukusanyaji wa maduhuli na utunzaji wa kumbukumbu za ardhi. Wizara yangu imeendelea kuboresha utoaji wa huduma hizi kwa kutumia mifumo ya kieletroniki.

Mheshimiwa Spika, Wizara ina jukumu la kusimamia watumishi wa Sekta ya Ardhi waliopo katika Halmashauri nchini kuwezesha kutekeleza majukumu. Katika utekelezaji wa jukumu hili, Wizara ilisaini Hati ya Makubaliano na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Zoezi la kuwatambua na kuwapanga watumishi hao kwa uwiano kulingana na mahitaji, limekamilika na ifikapo Julai Mosi, 2019 inatarajiwa kuwa watumishi wote watakuwa wamehamishiwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara kama nilivyosema hapa jana itawapanga upya watumishi wote kulingana na sifa, weledi na taarifa zao za kiutumishi. Wale watumishi wenyе tabia za hovyo, watachukuliwa hatua za kisheria na kuondolewa kwenye utumishi wa Umma kwa sababu tunawajua. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ina jumla ya kanda nane za utawala wa ardhi ambazo ni Dar es Salaam, Kati, Kusini, Nyanda za Juu Kusini, Kaskazini, Simiyu, Ziwa na Magharibi. Katika kuimarisha utoaji wa huduma za ardhi na kuzisogeza karibu na wananchi, Wizara yangu inaanizisha kanda maalum ya Morogoro. Kanda hii itahudumia mkoa wa Morogoro kutokana na ukubwa wake, sababu za kijiografia na uwepo na shughuli mbalimbali za kiuchumi zinazohitaji huduma za ardhi.

Mheshimiwa Spika, uandaaji na usajili wa hati na nyaraka mbalimbali za kisheria. Hadi tarehe 15 Mei, 2019, Wizara imeandaa na kusajili hati za hakimiliki 47,688 na pia kusajili nyaraka nyingine za kisheria 25,045. Vilevile, Wizara imesajili Vyeti vya Ardhi za Kijiji 341 na Hati za Hakimiliki ya Kimila 166,478. Natoa rai kwa wananchi waliopimiwa maeneo yao kuhakikisha wanamilikishwa. Wananchi wengi wamepimiwa na hawataki kuchukua hatimiliki, ni kosa.

Mheshimiwa Spika, ninawaagiza Maafisa wote wa ardhi kuanzia mwaka huu wawaapelekee bili ili walipe kodi watu wote ambao hawataki kuchukua hati makusudi ilhali ardhi zao zimepimwa na kujua gharama, lakini baada ya kujua gharama za malipo huwa hawaendi kulipa kutayarishiwa hati. Kwa hiyo, kuanzia mwaka huu watu wote ambao tayari tumeshawawekea vizingi kwenye viwanja na mashamba yao na wanajua kwamba yameplimwa, tutaanza kuwapelekea bili ya kodi waendelee kulipa kodi ya ardhi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara inakusudia kusajili nyaraka za kisheria 152,000. Napenda kutumia fursa hii kuhimiza wananchi kuona umuhimu wa kusajili nyaraka mbalimbali zinazotokana na miamala ya ardhi iliyosajiliwa. Mfano, mikataba ya uhamisho wa miliki, wosia, rehani za mikopo na kadhalika. Hii itasaidia kuwaepusha na wimbi la utapeli wa ardhi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara yangu kwa kushirikiana na Mamlaka ya Upangaji nchini, itaandaa na kusajili Vyeti vya Ardhi ya Kijiji 100, kati ya 1,392 ambavyo havijasajiliwa na Hati za Hakimiliki za Kimila 150,000 zitaandaliwa. Aidha, Wizara yangu imepanga kusajili nyaraka za kisheria zipatazo 53,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa rai kwa Mamlaka za Upangaji nchini kuhakikisha kuwa zinamilikisha viwanja vyote vilivyopimwa ili wananchi waweze kuwa na hatimiliki salama. Pia nawahimiza wamiliki wote wa ardhi kuchukua hati zao zilizokamilika kutoka Ofisi za Msajili wa Hati zilizopo

katika Ofisi za Ardhi za Kanda. Hivi sasa Kanda ya Dar es Salaam tu peke yake kuna hati zaidi ya 3,000 zimekamilika muda mrefu sana lakini watu hawataki kwenda kuchukua. Hawadaiwi chochote, lakini hawaendi kuchukua.

Mheshimiwa Spika, pia zipo hati mpya za elektroniki ambazo tunapaswa kuzichukua siku moja baada ya kuwasilisha nyaraka, nazo watu hawaendi kuchukua. Kwa hiyo, natoa wito kwa wananchi wote ambao wanajua kwamba walishawasilisha nyaraka kwenye Ofisi za Ardhi mahali popote, wafike kwenye ofisi zetu za Kanda Dar es salaam na kanda nyingine, wafuatilie hati zao zipo tayari, hawadaiwi chochote, wakazichukue hizo hati.

Mheshimiwa Spika, usuluhishi wa migogoro ya matumizi ya ardhi. Migogoro ya matumizi ya ardhi imekuwa na athari mbalimbali ikiwa ni pamoja na uharibifu wa mali, mifugo na mazao, uharibifu wa hifadhi za wanyamapori, uharibifu wa vyanzo vya maji na maeneo oevu, kupungua kwa vivutio vya utalii, kutoweka kwa wanyamapori, uharibifu wa mazingira ya bioanuai na kutoweka kwa amani katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika; katika mwaka wa fedha 2018/2019 Wizara iliahidi kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa migogoro mbalimbali ya matumizi ya ardhi na kuendelea kusikiliza kero za wananchi na kuzipatia majibu. Ili kupata ufumbuzi wa kudumu kuhusiana na migogoro na kero za matumizi ya ardhi, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za kisekta, Waheshimiwa Wabunge na Wakuu wa Mikoa imeratibu na kukamilisha taarifa yenye mapendekezo ya utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi. Hatua hii ni katika kutekeleza agizo la Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alilotoa tarehe 15 Januari, 2019 kwa Mawaziri wa Kisekta kuandaa mapendekezo ya ufumbuzi wa kudumu wa migogoro ya matumizi ya ardhi nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kushughulikia migogoro ya matumizi ya ardhi, Wizara za Kisekta zimezingatia maelekezo

yafuatayo yaliyotolewa na Mheshimiwa Rais, aliagiza; La kwanza, kutoviondoa vijiji na vitongoji vyote vilivymo ndani ya hifadhi; pili; kubainishwa kwa maeneo ya hifadhi ambayo yamepoteza sifa ili yaweze kugawiwa kwa wananchi kwa shughuli za ufugaji na kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tatu, kuhakiki na kurekebisha mipaka baina ya hifadhi za misitu, wanyama na makazi; nne; kumega baadhi ya hifadhi na kuwagawia wafugaji na wakulima. Haya ndiyo maelekezo ya Mheshimiwa Rais tuliyofafanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tano, kufanya mapitio ya sheria mbalimbali zinazohusiana na matumizi ya ardhi; sita, kupitia upya Sheria ya Vyanzo vya Maji inayozungumzia mita 60, maana nayo imekuwa ni kero kwa wananchi; saba, kuwasilisha mapendelekezo ya kufutwa mashamba yasiyoendelezwa na kugawa kwa wananchi kwa ajili ya uzalishaji wa mazao ya kilimo na mifugo; nane, kuendelea kulinda na kuhifadhi maeneo ya hifadhi za misitu, wanyamapori na vyanzo vya maji na zile mita 500 nyingine, nazo tulagiwa tuziangalie.

Mheshimiwa Spika, taarifa zilizochambuliwa na kuandalia mapendelekezo kwa kuzingatia maelekezo hayo zinahusu migogoro ya ardhi katika maeneo ya ufugaji, kilimo, hifadhi za misitu na wanyamapori, vyanzo vya maji, hifadhi za mazingira, ulinzi, mipaka ya kiutawala na fidia ya ardhi. Wizara zilizoshiriki katika utekelezaji wa agizo hilo ni Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambaye ndiye alikuwa Mwenyekiti; Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira); Maliasili na Utalii; Mifugo na Uvuvi; Kilimo; Maji; Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; na Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa naomba kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake imara na wenye weledi na huruma kwa kusimamia na kutatua migogoro ya matumizi ya ardhi iliyopo

nchini kupitia Mawaziri wa Kisekta walioteuliwa kufanya kazi hii muhimu kwa pamoja kwa ajili ya kuwatetea wananchi hususan wanyonge. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa yenyeye mapendekezo yote muhimu imekamilika na imewasilishwa rasmi Serikalini ili ipitiwe na Baraza la Mawaziri. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote ambao walitusaidia kutupa nyongeza ya taarifa hapa Bungeni na baada ya Bunge. Nataka kuwahakikishia taarifa zenu zote tumezipokea, tumezihakiki, tumezifuatilia na kuziingiza kwenye taarifa hiyo ya msingi.

Mheshimiwa Spika, hapa mbele yako nina *sample* tu ya kitabu cha taarifa kilichosheheni taarifa zote mlizotupatia Waheshimiwa Wabunge, hatukuacha hata kijiji kimoja ambacho kipo ndani ya hifadhi ambacho kinahitaji huruma hii ya Mheshimiwa Rais. Fikiria Mji wa Geita kwa mfano, wote upo kwenye hifadhi ya misitu. Fikiria wale wote ambao wapo kwenye *buffer zone*, akina Mheshimiwa Chenge na watu wa Serengeti, Tarime na wengine. Fikiria watu kama wa Kaliua wale ambao wanaishi kwenye hifadhi za misitu miaka yote.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, hii ndio sura ya taarifa ambayo imekamilika, hakuna hata mtu mmoja nikiangalia sura zenu ambaye hana taarifa inayomhusu humu ndani. Ni bahati mbaya tu kwamba taarifa hii hajapitiwa na kutolewa maamuzi, lakini ingekuwa imetolewa maamuzi, leo najua mngeamua kuahirisha huu mkutano wangu na kuondoka, kwa sababu mambo yenu yote yamo humu, hakuna jambo. Baada ya hapa mtaona hata *spirit* ya uchangiaji wenu bajeti ijayo itakavyokuwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka kuwahakikishia, mliandika, tumefuatilia, tumewaita Wakuu wa Mikoa, tumekwenda TAMISEMI tumepekuwa, tumezunguka kote, hata kule juzi uliposema kwenye *Ramsar* tumekwenda kule Kilombero kuangalia, tumekwenda mpaka Mbarali. Hakuna

jambo lilioshindikana; Umasaini tumekwenda na kila mahali. Kwa hiyo, aina yote ya migogoro ambayo tumekuwa tunawawakilisha wananchi miaka yote, yote unayoifikiri iko hapa.

Mheshimiwa Spika, nataka kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge, najua mtapenda mengi kuuliza baadaye katika kuchangia lakini majibu yako humu. Sitasema lakini yako humu; ila muamini tu kwamba kila mtu hamu yake ya mgogoro wake kwisha, hata migogoro ya vijiji na vijiji, mipaka ya Wilaya na Wilaya, kila kitu kipo humu ndani. Kwa hiyo, nataka kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge, kiu ya migogoro yenu sasa itamalizika chini ya mwelekeo na heshima aliyotupatia Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, najua hizi taarifa baada ya kukamilisha utaratibu utakaopitiwa na Baraza la Mawaziri, Wabunge mtapewa taarifa na wananchi watapewa taarifa ili waende kuishi kwa amani kwa sababu kuna maeneo ya wananchi wengine vijiji vyao vimesajiliwa miaka yote lakini wanaishi kwenye leseni au *GN*za misitu au *GN*za wanyama, lakini kuna watu ambao wilaya zao zimezungukwa na misitu, hawana hata maeneo ya ufugaji wala kilimo. Mheshimiwa Rais alitutuma tuangalie hao wananchi namna gani watapata hayo maeneo, maana misitu imewekwa kwa ajili ya wananchi vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, yote haya tumeyazingatia. Kwa hiyo, nataka muwe na imani, watu wote ambao vijiji vyenu vipo kwenye *GN* mnatishwa tishwa kila mara, vipo humu. Wilaya zenu zote zilizopo kwenye *GN* za misitu na wanyamaporu zipo humu; ninyi wote wenye *buffer zone* zimechukuliwa na wanyamaporu, zimo humu; watu wote mnaotishwa na mita 50/500 kama Bwawa la Mindu pale, mpo humu ndani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge nataka mjue kwamba pamoja na

kwamba taarifa hii sitaifichua maana bado haijawa rasmi, lakini kiu ya maswali yenu yote nikiwaona mnayotaka kuuliza majibu yao yamo humu ndani.

Mheshimiwa Spika, kupitia kauli mbiu ya Wizara yangu ya "Funguka na Waziri", Wizara imeendelea kusikiliza malalamiko ya wananchi katika Halmashauri mbalimbali nchini kupitia mikutano ya wananchi pamoja na ujazaji wa madodoso. Jumla ya kero na malalamiko 13,055 yalipokelewa ambapo 10,174 yamefanyiwa kazi na 2,719 yanaendelea kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea kusimamia na kuhudumia Mabaraza ya Ardhi na Nyumba yanayofanya kazi ya kusikiliza na kuamua mashauri yahusuyo migogoro ya ardhi. Katika mwaka wa fedha 2018/2019 Wizara yangu imefungua mabaraza mapya katika Wilaya za Mbulu na Ulanga na kufanya mabaraza kuwa 45. Kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Wizara iliahidi kushughulikia mashauri 24,600 yaliyobaki na yatakayofunguliwa. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2019, mashauri mapya 15,995 yalifunguliwa na kufanya jumla ya mashauri yote kuwa 40,595 ambapo kati ya hayo, mashauri 11,980 yameamuliwa. Katika mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara itaendelea kushughulikia mashauri 28,615 yaliyobaki na yatakayofunguliwa.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza kasi ya kusikiliza mashauri ya ardhi, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara yangu imeajiri Wenyeviti wapya mwezi wa nne mwaka huu 20 wa Mabaraza ya Ardhi na imeshawapanga ili kuongeza nguvu katika Mabaraza yenye mashauri mengi katika Wilaya za Ukerewe, Maswa, Mbanga, Mbulu, Kilosa, Kyela, Ulanga, Lushoto, Nzega, Lindi, Same, Iramba, Shinyanga, Bukoba, Morogoro, Musoma, Mwanza, Kigoma, Temeke na Kinondoni.

Mheshimiwa Spika, ni matarajio ya Wizara kuwa Wenyeviti hawa wataongeza kasi ya kusikiliza na kutoa uamuvi ya migogoro ya ardhi inayowakabili wananchi. Aidha, baadhi ya Wenyeviti nimewasimamisha kazi kupisha uchunguzi na wengine wamehamishwa vituo vyao kwa

sababu mbalimbali. Watumishi ambao nimewasimamisha ni wa Karagwe na Kibaha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mfumo Uunganishi wa Kuhifadhi Kumbukumbu za Ardhi (*Integrated Land Management Information System*) umeanzishwa kwa lengo la kuboresha utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka za ardhi kwa njia ya kielektroniki, kurahisisha utendaji kazi, kuharakisha mchakato wa utoaji hatimilki na hatimaye kuongeza mapato ya Serikali. Mfumo huu unatekelezwa katika Ofisi za Ardhi za Ubungo na Kinondoni.

Mheshimiwa Spika, kupitia mfumo huu, hati 4,461 zimeandaliwa, ambapo hati 1,218 zimekamilishwa na kusajiliwa. Kati ya hizo zilizosajiliwa, hati 870 zimechukuliwa lakini hati nyingi bado wenyewe hawajaja kuzichukua. Mpango wa Wizara yangu ni kukamilisha ufungaji wa mfumo huu mwaka huu kabla ya mwezi wa Nane, Mkoaa mzima wa Dar es Salaam ni lazima uingie kwenye *electronic*.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara imenunua vifaa vya kisasa vya upimaji ardhi, yaani *RTK* seti 29, *Total Stations* seti 41, *computers* na vifaa vingine vyote vimenunuliwa kwa fedha ya Serikali. Naomba Halmashuri zote ambazo zina matatizo ya upimaji, wachukue vifaa hivi bure kwenye kanda, wavitungie bila gharama yoyote; na hata kama wanachukua makampuni, wawasimamie wachukue hivi vifaa ili gharama za wananchi za upimaji ziweze kupungua. Tumetoa hivi vifaa bure, kwa hiyo, nataka Halmashauri zote zichukue, vifaa vipo vya kutosha kwenye kanda. Mwaka huu wa fedha, tunanunua vingine tena. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara iliahidi kuendelea na uimarishaji wa mpaka wa Kimataifa; Tanzania na Uganda, Tanzania na Zambia, Tanzania na Burundi, Tanzania na Kenya na kuimarisha mipaka ya nchi ndani wa Ziwa Tanganyika na nchi za Jamhuri

ya Kidemokrasi ya Kongo, Burundi na Zambia. Lengo ni kuhakikisha ifikapo mwaka 2022 kazi ya uimarishaji wa mpaka huu iwe imekamilika.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba upande wa mpaka kati ya Tanzania na Uganda wa nchi kavu wenyе urefu wa kilometa 149 majadiliano kwa ajili ya kuimarisha mpaka huu yamefanyika sawia na ukaguzi wa alama za mpaka na upimaji wa malundo 15 ya alama za mpaka umefanyika. Vilevile, ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa alama katika mpaka umefanyika. Aidha, mpaka ndani ya maji katika Ziwa Victoria kati ya Tanzania na Uganda wenyе urefu wa kilomita 246 haujaanza kuimarishwa, lakini pia vikao mbalimbali vya ujirani mwema juu ya kusimamia uwekaji wa mipaka vinaendelea.

Mheshimiwa Spika, upande wa Tanzania na Kenya, mpaka wenyе urefu wa kilomita 819.7, kati ya hizo kilomita 760 za nchi kavu na 59.7 ziko ndani ya maji. Uimarishaji wa mpaka huo unajumuisha utengenezaji wa ramani za msingi, kupima kipande cha mpaka na kusimika alama za ardhini. Jumla ya kilomita 172 kati ya 760 za nchi kavu zimeirishwa kufikia Juni, 2018 za mpaka kati ya Tanzania na Kenya. Kwa mwaka wa fedha 2018/2019, kufikia tarehe 15 Mei, jumla ya kilomita 128 kutoka Ziwa Natron hadi Namanga zimekaguliwa kufikia tarehe 15 mwezi Mei ili kubaini mahitaji halisi.

Mheshimiwa Spika, urefu wa mpaka kati ya Tanzania na Zambia ni kilometa 345 ambapo sehemu ya nchi kavu ina urefu wa kilometa 289 na ndani ya maji ina urefu wa kilometa 56. Kazi hii ya uimarishaji wa wa Zambia na Tanzania tunataka tuienze mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, upimaji wa viwanja na mashamba; katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara yangu iliahidi kuidhinisha ramani za upimaji zenye viwanja 200,000 na mashamba 400 pamoja na kufufua mipaka ya viwanja na mashamba 500 yenye migogoro ya mipaka. Hadi Mei, 2019, jumla ya viwanja 261,387 na mashamba 3,291

yamepimwa na kuidhinishwa katika halmashauri mbalimbali. Aidha, jumla ya viwanja 70 vyenye migogoro vimefufuliwa mipaka. Mwaka wa Fedha 2019/2020 Wizara yangu imepanga kuidhinisha ramani za upimaji wa viwanja na mashamba 200,000 pamoja na kutatua migogoro 50 ya mipaka ya vijiji, hifadhi na wilaya.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Wizara iliahidi kusimika na kupima alama za msingi za upimaji (*control points*) 500. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2019, Wizara yangu imesimika na kupima alama za msingi 150 kwa kutumia mfumo mpya wa upimaji ardhi unaojulikana kama *TAREF11* katika Mikoa ya Mwanza (Wilaya za Illemela, Nyamagana, Sengerema, Buchosa, Magu), Geita (Nyang'wale, Chato, Bukombe, Mbogwe), Kagera (Biharamulo, Muleba, Bukoba Mjini, Bukoba Vijiji, Misenyi, Karagwe, Kyerwa, Ngara), Shinyanga (Kahama Mjini, Msalala, Ushetu, Shinyanga Vijiji na Shinyanga Mjini), Dodoma (Dodoma Jiji), Morogoro (Manispaa), Kilimanjaro (Manispaa ya Moshi) na Arusha (Arusha Jiji). Katika mwaka wa fedha ujao, Wizara inatarajia kusimika na kupima alama za msingi za upimaji 150 za nyongeza.

Mheshimiwa Spika, upangaji na uendelezaji wa miji na makazi; upangaji na uendelezaji wa miji na makazi unalenga kuwa na makazi yaliyopangwa, kuhifadhi mazingira, kupunguza ukinzani wa matumizi ya ardhi na kutoa uhakika wa uwekezaji katika ardhi. Majukumu hayo yamekuwa yakitekelezwa kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo mbalimbali ya uendelezaji wa miji na vijiji nchini.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji imetangaza jumla ya maeneo 455 kuwa maeneo ya mipango miji; kwenye viambatanisho mtano vijiji ambavyo vimepandishwa hadhi na kutangazwa kama maeneo ya kupanga kimji katika wilaya mbalimbali kwenye mikoa yenu. Aidha, maeneo hayo yamepandishwa kutoka hadhi ya vijiji na kuwa maeneo ya mipango miji na wananchi wanapaswa kumilikishwa kwa hati. Kutangazwa

kwa maeneo hayo kunaziwezesha Mamlaka za Upangaji ambazo ni Halmashauri, Manispaa, Miji na Wilaya kuyapanga kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za Mipango Miji na hivyo, kudhibiti ujenzi holela.

Mheshimiwa Spika, Mipango Kabambe ya Uendelezaji Miji; katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara iliahidi kushirikiana na halmashauri mbalimbali nchini kukamilisha Mipango Kabambe 12 ifikapo Juni, 2019. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Mipango Kabambe 11 imekamilika; Mipango hiyo ni ya Miji ya Songea, Tunduma, Bariadi, Tabora, Babati, Morogoro, Sumbawanga, Kigoma/Ujiji, Geita, Njombe na Dodoma. Mwezi ujao tunakwenda kuzindua Mpango Kabambe wa Tunduma na Songea na wilaya nyingine.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha, Wizara yangu imekuwa ikisimamia kwa karibu mapitio ya Mpango Kabambe wa Jiji la Dodoma kama Makao Makuu ya Serikali na utayarishaji wa mpango kina wa mji wa Serikali. Hadi Kufikia Novemba, 2018 Mpango kina wa Mji wa Serikali ulikuwa umekamilika na kuwezesha ujenzi na uhamiaji wa Ofisi za Serikali katika eneo la Mtumba.

Mheshimiwa Spika, rasimu ya kwanza ya mapitio ya Mpango Kabambe ilikamilika mwezi Januari, 2019 na kupitiwa na vikao mbalimbali vyta Serikali na wadau. Aidha, rasimu ya pili imekamilika mwezi Aprili, 2019 kwa ajili ya kupitishwa kwenye Mamlaka ya Upangaji hatimaye ambayo ni Jiji la Dodoma na kuidhinishwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa mipango kabambe iliyodhinishwa, shughuli mbalimbali zimefanyika ikiwemo pamoja na urasimishaji wa makazi, uandaaji wa mipango kina, ujenzi wa huduma muhimu za kijamii na kiuchumi na utengaji wa maeneo kwa ajili ya viwanda na matumizi mengine. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2019 jumla ya ekari 280,654.55 zilitengwa kwenye miji 24 ambayo imeandaliwa mipango kabambe (*master plans*) kwa ajili ya

maendeleo ya viwanda. Kwenye jedwali mtaona maeneo gani yametengwa kila mkoa kwa ajili ya maendeleo ya viwanda.

Mheshimiwa Spika, usanifu na uendelezaji miji; katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara iliahidi kupokea, kukagua na kuidhinisha michoro ya mipangomiji 2,000. Michoro 1,942 ya Mipango miji ilipokelewa na kukaguliwa. Kati ya hiyo, michoro 1,722 yenye jumla ya viwanja 620,720 iliihdhinishwa na michoro 220 ilirudishwa kwenye Mamlaka za Upangaji kwa ajili ya kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Spika, kuitia Mipango Kabambe, Wizara imewezesha utayarishaji wa mipango saba ya uendelezaji upya wa Maeneo ya Kati ya Manispaa za Kigoma/Ujiji, Songea, Morogoro, Tabora, na Shinyanga na Miji ya Geita na Bariadi. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Manispaa ya llala imekamilisha mapitio ya mipango ya uendelezaji upya wa maeneo mawili ya Katikati ya Jiji (*Central Business District – CBD*) na eneo la Upanga. Katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Wizara yangu itafuatilia na kutathmini utekelezaji wa Mipango Kabambe na Mipango Kina katika kanda tatu za Kaskazini, Ziwa na Nyanda za Juu Kusini. Aidha, kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji, Wizara itakamilisha Mipango Kabambe sita ya Moshi, Mbeya, Bukoba, Mafinga, Kahama na Handeni.

Mheshimiwa Spika, urasimishaji makazi mijini; katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara kwa kushirikiana na mamlaka za upangaji iliahidi kurasimisha makazi mijini kwa halmashauri mbalimbali. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba hadi tarehe 15 Mei, 2019, urasimishaji makazi wenye jumla ya viwanja 626,920 ulitekelezwa katika halmashauri mbalimbali. Mkoa wa Mwanza bado unaongoza kwa wilaya mbili kuwa na viwanja vingi zaidi na hati nyingi zaidi za urasimishaji, jedwali linaonesha. Mwaka 2019/2020 Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji itaendelea na zoezi hili la urasimishaji ambapo tunakadiria hati 600,000 zitatambuliwa.

Mheshimiwa Spika, upangaji wa makazi vijijini; miji inapopanuka au mipaka yake kupanuliwa, humeza vijiji vya pembezoni mwa miji hiyo. Upanuzi wa miji hiyo hupelekeea kuzaliwa kwa makazi yasiyo rasmi au yasiyopangwa iwapo vijiji vinavyomezwa havikupangwa. Kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 Wizara iliahidi kuwezesha mamlaka za upangaji ili ziweze kuandaa mipangokina ya makazi vijijini pamoja na vitovu vya biashara. Katika kutekeleza hilo Wizara imezijengea uwezo timu za kitalaam za usimamizi wa matumizi ya ardhi za Wilaya za Kilwa, Lindi, Masasi, Nanyumbu, Muheza, Kilindi, Chamwino, Bahi, Morogoro na Rufiji.

Mheshimiwa Spika, aidha, mipango kina ya matumizi ya ardhi ya makazi katika vijiji 90 katika Wilaya za Kilombero, Malinyi na Ulanga Mkoani Morogoro na Wilaya ya Iringa Mkoani Iringa imekamillka ambapo jumla ya viwanja 121,810 vimepangwa. Katika mwaka wa fedha ujao Wizara itaendelea kuandaa mipangokina ya makazi vijijini katika halmashauri mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, huduma ya mikopo ya nyumba; Wizara inaendelea kufuatilia utekelezaji wa Sheria ya Mikopo ya Nyumba ambayo iliwezesha upatikanaji wa mitaji na kuongezeka kwa mabenki na taasisi za fedha zinazotoa mikopo ya nyumba. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa jumla ya mabenki na taasisi za fedha 32 nchini zimetoa mikopo ya nyumba kwa wananchi 4,989 yenye thamani ya shilingi bilioni 421.09.

Mheshimiwa Spika, aidha, masharti ya mikopo ya nyumba yameendelea kulegezwa kwa kuwa viwango vya riba vimepungua kutoka asilimia 21 ya zamani kwa mwaka 2017 hadi sasa wananchi wanakopeshwa kati ya asilimia 13 na 18 kwa mwaka 2019 na ukopaji umekuwa ni wa muda mrefu. Wizara yangu inaendelea kufanya mazungumzo na Benki Kuu ya Tanzania, Benki za Biashara na Taasisi za Fedha ili kushusha viwango hivyo zaidi na kuwezesha wananchi kumiliki nyumba hizo chini ya taasisi zinazosimamia mpango huu, *TMRC*.

Mheshimiwa Spika, kupitia Mfuko wa Mikopo Midogomidogo ya Nyumba (*Housing Microfinance Fund*), taasisi sita zimetoa mikopo midogomidogo ya nyumba yenye thamani ya shilingi bilioni 17.87 kwa wananchi 1,467 wa kipato cha chini. Kwenye jedwali mtakuta taasisi hizo ni zipi. Natoa wito kwa wananchi hususan wa kipato cha chini kutumia fursa hii ya kukopa kwenye taasisi hizo ili waweze kujenga nyumba na kuboresha makazi yao ambayo sasa wanaweza kukopa kwa muda mrefu, lakini pia riba imepungua.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru pia viongozi wa Mabenki ya *CRDB* na *NBC* ambao kila mara wamekuwa wanatuwezesha Wabunge kwa kuhifadhi nyaraka zetu kama leo mlivyoona, huu ni mwendelezo wa ushirikiano katika shughuli hizi tunazoshirikiana nao zinazohusiana na mikopo ya nyumba. Nawashukuru sana *CRDB* na *NBC*.

Mheshimiwa Spika, miradi ya Wizara; katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara ilipanga kutekeleza miradi mbalimbali ambapo hadi tarehe 15 Mei, 2019, ilitekeleza mradi wa upangaji, upimaji na umilikishaji aidha kwa kutumia jumla ya shilingi bilioni 8. Kati ya fedha hizo, shilingi milioni 694.9 zimetumika kuandaa Mpango Kabambe wa Jiji la Dodoma, shilingi bilioni 7.3 zimetumika kwa ajili ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi katika halmashauri mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, kati ya fedha hizo, Wizara imeshatoa shilingi bilioni 6.29 na wilaya ambazo zimekopesha, zimepewa hizo fedha zimeorodheshwa kwenye majedwali mbalimbali kwa halmashauri 24 zilizokidhi vigezo kwa ajili ya kupanga, kupima na kumilikisha vipande vyatya ardhi 40,241. Wizara itaendelea kuzipatia halmashauri nyingine kwa kadri maombi yao yanatakavyokuwa yamekuja kwetu na kupitiwa ili kuweza kupanga na kupima vipande mbalimbali vyatya ardhi kwenye wilaya zao.

Mheshimiwa Spika, pia Wizara iliendelea kutekeleza Programu ya Kuwezesha Umilikishaji wa Ardhi (*Land Tenure*

Support Programme) katika vijiji vya Wilaya za Kilombero, Ulanga na Malinyi Mkoani Morogoro ambayo muda wa utekelezaji unaisha mwezi Septemba, 2019. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2019 Wizara ilipima vipande vya ardhi na kuandaa Hati za Hakimiliki ya Kimila katika vijiji 109 vya Wilaya za Kilombero (56), Ulanga (37) na Malinyi (16). Jumla ya vipande vya ardhi 178,980 vimehakikiwa na kupimwa kwa ajili ya kuandaa Hati za Hakimiliki ya Kimila sawa na asilimia 224 ya lengo.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo itatekeleza kazi zilizobaki za Programu ya Kuwezesha Umilikishaji Ardhi Mkoani Morogoro ikiwemo kuhakiki vipande vya ardhi na kuandaa Hati za Hakimiliki ya Kimila 60,000 kwa wilaya hizo tatu na kuandaa Mpango Kabambe ya Ifakara, Mahenge na Malinyi. Aidha, kwa kuzingatia mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa mradi huu, Wizara inaandaa sasa programu ya utekelezaji katika maeneo mengine nchini ambayo tunatarajia pengine mwaka ujao, ule mwingine, siyo huu lakini sasa hivi tunakamilisha maandalizi, lakini baada ya mwaka huu wa fedha mwaka mwingine tutakuja na mpango kabambe wa kupanga na kupima kila kipande cha ardhi cha nchi hii kutokana na uzoefu tulipata wa wilaya hizi tatu.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa kutembelea mradi huu mara kadhaa na kututia moyo, nawashukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Programu ya Kuimarisha Milki za Ardhi; kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, Serikali ilipanga kukamilisha uandaaji wa Programu ya Kuimarisha Milki za Ardhi (*Land Tenure Improvement Project*) chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia. Kazi ya mradi huu inaendelea kufanyika na itaonekana katika bajeti itakayofuata. Lakini pia Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa Korea, *Exim Bank* ya Korea inaandaa mradi wa kuboresha miundombinu

ya upangaji na ramani ya msingi kwa njia za kidigitali. Tunakamilisha mazungumzo lakini mwaka huu wa fedha unaoanza mwezi Julai pengine tutaanza mpango huu ambao utakuwa ni wa nchi nzima ambao utarahisisha kazi ya upangaji na upimaji wa ardhi katika nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, miradi ya kitaifa; katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara yangu iliahidi kushiriki katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya ujenzi wa miundombinu ya kitaifa hususan Ufuaji wa Umeme katika mto Rufiji (*Rufiji Hydropower Project*), Bomba la Mafuta (*East African Crude Oil Pipeline*) kutoka Hoima Nchini Uganda hadi Chongoleani – Tanga na Reli ya Kisasa (*Standard Gauge Railway*). Katika Mradi wa Ufuaji Umeme wa Mto Rufiji, Wizara imeshiriki katika upangaji wa eneo la kujenga mtambo wa kuzalisha umeme lenye ukubwa wa hekta 1,402, eneo litakalotumika kwa ujenzi wa karakana lenye ukubwa wa hekta 4,711, eneo litakalokinga sehemu ya Mto Rufiji na Ruaha inayoingia katika eneo la kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Spika, lakini pia katika uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi kwa ajili ya uendelezaji wa eneo la ukanda wa Reli ya Kisasa kuanzia Dar es Salaam hadi Isaka, Shinyanga na eneo la ukanda wa Bomba la Mafuta kutoka Mtukula hadi Chongoleani – Tanga Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi imeunda timu shirikishi za uandaaji wa Mipango ya Ukanda wa Reli ya Kisasa na Bomba la Mafuta. Aidha, mipango miwili ya kila timu imefanyika kwa ajili ya maandalizi ya kazi hizo na rasimu za awali za mipango ya matumizi ya ardhi kwa ajili ya uendelezaji wa maeneo ya kanda maalum ya uwekezaji kando ya *SGR*, yaani Reli ya Kisasa na Bomba la Mafuta, zimeandaliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mradi wa Reli ya Kisasa Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Reli Tanzania imefanya zoezi la uthamini katika njia ya Reli kutoka Mvomero Mkoani Morogoro hadi Makutupora, Manyoni Mkoani Singida. Wizara pia inaandaa *Corridor Development Plan*

ya Bomba la Mafuta na Reli ya Kisasa kutoka Dar es Salaam hadi Kituo cha Makutupora Singida ili kuainisha fursa mbalimbali za uwekezaji kandokando ya hii miradi miwili. Mpango huo utaainisha matumizi ya ardhi katika miji na vijiji vitakavyopitiwa na miradi hii mikubwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara imeendelea kushiriki katika shughuli mbalimbali za ujenzi wa Bomba la Mafuta Afrika Mashariki na pia katika shughuli mbalimbali za kitaifa. Wizara imekamilisha taratibu za utwaaji wa maeneo 17 ya kipaumbele kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu wezeshi ya mradi wa bomba la mafuta. Maeneo hayo yapo katika Wilaya za Nzega, Igunga, Kiteto, Misenyi, Muleba, Chato, Bukombe, Singida, Kondoa, Kilindi, Handeni na Muheza. Wizara pia imetwaa eneo lote litakalojenga bomba la mafuta na kulipanga na litakabidhi hati kwa Shirika la Mafuta la *TPDC*.

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa taasisi zilizo chini ya Wizara, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi; Serikali ilianzisha Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi kwa Sheria ya Bunge Na. 3 ya Mwaka 1984. Kazi zake ni pamoja na kuainisha matumizi mbalimbali ya ardhi kuweza kuwezesha ardhi kutumika kwa ufanisi na tija kupunguza migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara yangu kupitia Tume ilipanga kufanya mapitio ya Programu za Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi. Tayari Tume imeanza kukusanya taarifa za kisekta juu ya kukamilisha programu hiyo.

Mheshimiwa Spika, mipango ya matumizi ya ardhi ya wilaya na vijiji; katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Tume ilipanga kuratibu tathmini ya uharibifu wa mazingira katika Wilaya tatu za Mlele, Urambo (Ulyankulu) na Tanganyika zilizokuwa na makambi ya wakimbizi katika ukanda wa magharibi mwa nchi, kutoa mafunzo kwa timu za usimamizi wa wilaya sita na pia kuwezesha upangaji wa matumizi ya

ardhi katika Wilaya sita za Geita, Nyang'hwale, Misenyi, Urambo (Ulyankulu), Misenyi na Tanganyika na vijiji 250.

Mheshimiwa Spika, Tume kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira imeendelea kujenga uwezo kwa timu za usimamizi wa matumizi ya ardhi za wilaya mbalimbali na kuwezesha upangaji wa matumizi ya ardhi ya vijiji 14 katika Wilaya tatu za Kondoa, Nzega na Mkalama ambazo zinapitiwa na Mradi wa Bomba la Mafuta.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 15 Mei 2019, Tume kwa kushirikiana na Wakala wa Taifa wa Huduma za Misitu (*TFS*) imewezesha upangaji wa matumizi ya ardhi kwa vijiji 37 kati ya 95 vinavyopakana na hifadhi za misitu katika Wilaya za Lindi, Kilwa, Nanyumbu, Muheza, Kilindi, Bahi, Chamwino, Mbeya Vijiji, Mbarali na Masasi. Katika mwaka wa fedha ujao, jumla ya vijiji 58 vilivyoabaki vitaandaliliwa mipango hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuanzia Mwaka wa Fedha 2018/2019 uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi kwa ngazi za vijiji tayari umeanza kuzingatia utengaji wa maeneo kwa ajili ya ujenzi na uendelezaji wa viwanda. Katika vijiji 258 vilivyoandaliliwa mipango ya matumizi ya ardhi katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, jumla ya hekta 282,805.45 zimetengwa kwa ajili ya kilimo na hekta 201,091.60 kwa ajili ya malisho ya mifugo, hekta 35,262.65 kwa ajili ya misitu, hekta 26,136.01 zimetengwa kwa ajili ya hifadhi, hekta 30,721.92 kwa ajili ya hifadhi ya vyanzo vya maji na hekta 43,848.65 kwa ajili ya maeneo ya usimamizi wa wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Nyumba la Taifa; shirika hili ambalo sasa limepata bodi thabitii kamili imeundwa na Wizara iliahidi kuendelea katika awamu ya pili ya ujenzi wa nyumba katika eneo la lyumbu na kukamilisha taratibu za kupata ardhi ya kujenga nyumba Jijini Dodoma. Napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, shirika linaendelea na ujenzi wa nyumba 149 pamoja na maduka mawili makubwa ya kisasa liilopo katika hatua mbalimbali za ujenzi katika eneo la lyumbu.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliahidi kuendelea na ukamilishaji wa miradi iliyopo katika mikoa mbalimbali pamoja na kujenga nyumba za gharama nafuu. Kwa sasa shirika lina miradi 66 ambapo imeongezeka kutoka miradi 57 mwaka 2017/2018. Miradi 9 ilioongezeka ni ya ujenzi wa ofisi mbalimbali katika miji na sehemu mbalimbali. Pia imojiandaa katika kujenga nyumba za gharama nafuu katika maeneo mbalimbali ikiwepo hapa katika Mji wa Dodoma ambapo tunakusudia kujenga nyumba zisizopungua 1,000 kwa ajili ya gharama nafuu lakini na nyumba za kupangisha ambazo zitakuwa za maghorofa kama hizi tulizojenga hapa.

Mheshimiwa Spika, Vyuo vya Ardhi vya Tabora na Morogoro vinaendelea kutoa mafunzo, na kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 vilidahili wanafunzi 706 lakini mwaka huu 2018/2019 imefikia 1,220; hicho ni Chuo cha Tabora. Lakini Chuo cha Morogoro kimeongeza udahili kutoka 271 hadi sasa 1,011.

Mheshimiwa Spika, utawala na rasilimali watu; kama nilivyosema, na kwenye jedwali mtaona na jana uliniuliza, katika kusimamia majukumu ya Sekta ya Ardhi kwa ufanisi Wizara inahitaji watumishi 1,692 wa kada mbalimbali ikilinganishwa na watumishi 945 waliopo kwa hiyo, kuwa na upungufu wa watumishi 745. Mahitaji makubwa yako katika mabaraza ya ardhi, lakini ukiangalia kwenye jedwali utaona jinsi watumishi waliopo na walivyopangwa lakini ukiona utaona kabisa kuna wengine wako wengi, wengine wachache, kwa hiyo, ndiyo maana jana nilisema tunataka kuwapanga upya ili kila wilaya iwe na watumishi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, utoaji wa huduma kwa wateja umeimarika kituo cha Dar es Salaam peke yake kimeongeza kuhudumia wateja kutoka 88,960 ilivyokuwa kwa wastani lakini leo tunahudumia wateja 2,360 kwa wiki katika kituo kimoja cha Dar es Salaam lakini huduma hizi zinaendelea kila mahali lakini pia Serikali kuititia Wizara yangu imetoa namba ya simu yenye namba 222121107 na simu nyingine ya

mkononi ya *TTCL* yeny namba 0736777777 ukipiga utakuta inaonyesha jina la Waziri lakini hiyo ni simu ambayo nimeichukua kwa ajili ya wananchi wote ambaowanashida ya kutaka kumsikia Waziri anatatua kero yao kwa njia ya simu watumie namba 0736777777 wakipiga ni bure na sisi tukipokea ni bure. Wakituma meseji ni bure wakituma *whatsap* ni bure wakituma fax ni bure 0737777777 hii ni simu yangu lakini nimeitoa maalum kwa ajili ya kusikiliza kero za wananchi nchi kwa hiyo wapige simu hii bure. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, shukrani naomba kwa niaba ya Wizara yangu, naomba kumalizia hotuba yangu kwa kuwashukuru kwa dhati Mawaziri na Makatibu Wakuu wa kisekta tulioshirikiana kufanya uchambuzi wa taarifa za migogoro mbalimbali ya ardhi lakini nirudie kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt John Pombe Joseph Magufuli kwa msukumo wake na dira yake ya huruma kwa wananchi hawa kwa kutupa nguvu ya kufanya kazi hii ambayo itakwenda kukamilika hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, pia napenda niwashukuru wadau mbalimbali MKURABITA, Benki ya Dunia, wahisani kama Uingereza, Denmark, Sweden, Japan, Ujeruman, Jamhuri wa Watu wa Korea na Marekani kwa mchango mkubwa katika shughuli mbalimbali za upangaji wa ardhi nchini. Wizara yangu inatambua kwa kuthamini mchango yao iliyotolewa na wadau hao.

Mheshimiwa Spika, pia niwatambue wadau wengine wa Asasi za Kiraia kama SOLIDARIDAD, Taasisi ya Hakiardhi, Shirika la *CORDS, Care International Tanzania*, Taasisi ya STEP, Elephant Program, *Ujamaa Community Resource Team*, Taasisi ya Kuwezesha Mazingira, WWF, AWF na taasisi zote ambazo zimeshirikiana na sisi wajue nawatambua rasmi.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kumshukuru sana Naibu wangu Mheshimiwa Dkt. Angelina Sylvester Lubala Mabula kwa kunisiaidia sana katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha, napenda kutoa shukrani

za dhati kwa Katibu Mkuu Bibi Dorothy Stanley Mwanyika, Naibu Katibu Mkuu Bw. Mathias Kabunduguru, Dkt. Stephen Nindi Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi bora ya Ardhi, Dkt. Maulid Baniani Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba la Taifa, Dismas Minja na watendaji na viongozi wote wa Wizara na taasisi mbalimbali ambao kwa namna moja au nyine wametoa mchango huu ambao mnauona sasa Tanzania kumbe bila migogoro ya ardhi inawezekana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hitimisho katika hotuba yangu nimeainisha mafanikio yaliyopatikana lakini pia nataka niwashukuru vile vile viongozi wangu wa Kanda Makamishna mbalimbali na watendaji wa wilaya zote wa ardhi ambao wamesaidia katika kuwezesha shughuli mbalimbali zinazoendelea hivi sasa tutaendelea kushirikiana ili angalau kazi zote ziweze kukamilika kwa ufanisi mkubwa lakini kazi kubwa ya kupambana na migogoro Wabunge wote ni mashahidi spidi mlikuwa mnasema zamani migogoro na sasa imekuwa chini kidogo kwa kweli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana Mheshimiwa Dkt John Pombe Magufuli ame-seti nidhamu ya pekee kwa watumishi wa Serikali ni wale wale lakini nidhamu mpya lakini kwa ushirikiano wenu pia na baada ya taarifa hii kukamilika mtapumua sana tutakapoingia kwenye uchaguzi wa mwaka 2020 ripoti hii itawaongeza kura wote Waheshimiwa Wabunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka 2019/2020 katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara inatarajia kukusanya jumla ya shilingi bilioni 180 kutokana na kodi, tozo na ada mbalimbali zinazotokana na shughuli za sekta ya ardhi kutekeleza mikakati ambayo imeainishwa katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya matumizi, ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yaliyotekeliza katika hotuba hii kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020, sasa naomba

kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lijadili na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Fungu 48 Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Fungu 03, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, naomba univumilie nataka kusoma kwenye kitabu badala ya hotuba yangu wasije wakawa wamenichapia tofauti. Fungu 48 Maendeleo ya Makazi mapato ya Serikali 180,000,000,000, Matumizi ya Mishahara bilioni 17.3, Matumizi Mengineyo bilioni 15.7, Jumla ndogo bilioni 33.155, matumizi mengine fedha za ndani 18,000,000,000, fedha za nje bilioni 6.2, jumla ndogo bilioni 24.2. Jumla ni shilingi 57,439,991,387. Fungu 03 Tume ya Matumizi bora ya ardhi 5,245,072,000. Jumla ya fedha yote zinazoombwba na Wizara kwa mafungu yote mawili ni 62,685,063,687.

Mheshimiwa Spika, mwisho natoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza pamoja na hotuba hii nimeambatanisha viambatanisho vingi sana mkiangalia kwenye vitabu vyenu mtakuwa majedwali mbalimbali ambayo mngependa kuona taarifa zake naomba myapitie hayo majedwali lakini tupo hapa wote mtu yejote ambaye atashindwa kuchangia au anafikiri anataka kumuona Waziri moja kwa moja. Niko hapa tumepewa chumba namba 11 hapa tuonane yale ambayo unafikiri ni marefu yanahitaji kuonana na mimi peke yake hutaki ukumbi huu ujue tuonane kuanzia kesho nitakuwa chumba namba 11 tuelezane na hata kama una kundi la wananchi wenye shinda kutoka Jimboni kwako walete nitakuwa hapa wiki nzima natoa hiyo huduma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**HOTUBA YA WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI, MHESHIMIWA WILLIAM V. LUKUVI (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20**

**1.0 UTANGULIZI**

**1.** *Mheshimiwa Spika;* naomba kutoa hoja mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba baada ya kuzingatia taarifa iliowasilishwa hapa Bungeni leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii inayohusu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, sasa Bunge likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo (Fungu 48) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03) kwa mwaka wa fedha 2018/19. Aldha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupidisha Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu 48) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03) kwa mwaka wa fedha 2019/20. Pamoja na hotuba hii nawasilisha taarifa ya utekelezaji wa programu na miradi inayosimamiwa na Wizara na Taasisi zake.

**2.** *Mheshimiwa Spika;* awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kushiriki katika Bunge hili. Aldha, kufuatia kifo cha Mhe. Stephen Ngonyani aliyekuwa Mbunge wa Korogwe Vijiji, kilichotokea mwezi Julai, 2018, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwako wewe binafsi, Bunge lako Tukufu, familia ya marehemu, ndugu, wananchi wa Jimbo la Korogwe Vijiji pamoja na wote walioguswa na msiba huo. Vilevile, natoa pole kwa wananchi wote waliofiwa na walioathirika kutohana na majanga mbalimbali yaliyotokea katika maeneo mbalimbali nchini. Kipekee natoa pole kwa familia za watumishi tisa (**09**) wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi waliopoteza maisha katika ajali ya gari iliyotheke huko Kilombero tarehe 23 Februari, 2019. Tumewapoteza vijana ambaao bado walikuwa wanategemewa na Taifa hili

pamoja na familia zao. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu wote mahali pema peponi, Amina.

**3. *Mheshimiwa Spika***; kwa namna ya kipekee, naomba pia nitumie fursa hii adimu kutambua na kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake shupavu katika kusimamia rasilimali za Taifa, kupambana na rushwa na kuimarisha nidhamu na uwajibikaji katika utumishi wa umma. Katika awamu hii tumeshuhudia maendeleo makubwa katika sekta zote hususan utoaji wa Elimu bila malipo kwa shule za msingi hadi sekondari, uimarishaji wa usalama wa milki za ardhi kwa wananchi hususan wananchi wanyonge, uboreshaji wa huduma za Afya nchini, ujenzi wa viwanda, ufufuaji wa Shirika la Ndege Tanzania, ujenzi wa reli ya kisasa, ujenzi wa mradi wa kufua umeme katika mto Rufiji na mradi wa pamoja wa ujenzi wa bomba la mafuta. Mafanikio haya ni matokeo ya uongozi makini na thabiti katika masuala ya kiuchumi na kijamii. Hakika uongozi wake umezidi kuijengea heshima kubwa nchi yetu katika Bara la Afrika na Dunia nzima kwa ujumla.

**4. *Mheshimiwa Spika***; nawapongeza pia Mhe. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada zao za kuongoza, kusimamia na kuendeleza amani, utulivu na maendeleo ya nchi yetu. Nawashukuru pia kwa ushauri, maelekezo na ushirikiano wanaonipa ambao unaniwezesha kutekeleza majukumu niliyokabidhiwa ya kuongoza sekta hii muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu. Aidha, nawapongeza Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mhe. Balozi Seif Ali Idd (Mb.), Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa mafanikio makubwa yanayoendelea kupatikana chini ya uongozi wao imara huko Tanzania Visiwani.

**5. *Mheshimiwa Spika***; napenda kukupongeza wewe na Naibu Spika Mhe. Dkt. Tulia Ackson Mwansasu (Mb.) kwa

kuongoza na kusimamia kwa ufanisi shughuli za Bunge letu Tukufu. Vilevile ninawapongeza Wenyeviti wote wa Bunge ambaao kwa nyakati tofauti wamekuwa wakiongoza shughuli za Bunge kwa ufanisi. Mwenyezi Mungu aendelee kuwaongoza na kuwapa nguvu, afya njema na hekima.

**6. *Mheshimiwa Spika*:** napenda pia kutumia fursa hii kuwapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri walioteuliwa na Mheshimiwa Rais katika mabadiliko ya Baraza la Mawaziri aliyoyafanya kwa nyakati tofauti katika mwaka 2018 na 2019. Nawatachia wote kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

**7. *Mheshimiwa Spika*:** napenda kuwapongeza Mhe. Mwita Mwikabwe Waitara, Mbunge wa Ukonga, Mhe. Pauline Philipo Gekul, Mbunge wa Babati Mjini, Mhe. Timotheo Paul Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijiji, Mhe. James Kinyasi Ole-Millya, Mbunge wa Simanjiro, Mhe. Julius Kalanga Laizer, Mbunge wa Monduli, Mhe. Abdallah Ally Mtalea, Mbunge wa Temeke, Mhe. Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe, Mhe. Marwa Ryoba Chacha, Mbunge wa Serengeti na Mhe. Zuberi Mohamedi Kuchauka, Mbunge wa Liwale na Mhe. John D. Pallangyo Mbunge wa Arumeru Mashariki kwa kuchaguliwa katika chaguzi ndogo zilizofanyika hivi karibuni. Ninawatachia kila la heri katika kutekeleza majukumu yao.

**8. *Mheshimiwa Spika*:** naomba kutumia fursa hii kumpongeza Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake ambayo imeelezea utekelezaji wa malengo ya Serikali katika mwaka wa fedha 2018/19 na mwelekeo wa kazi za Serikali zitakazotekelawa katika mwaka wa fedha 2019/20. Wizara yangu itayafanya kazi maelekezo na maagizo yanayoihusu sekta ya ardhi ili kuhakikisha kwamba malengo ya Serikali ya Awamu ya Tano yanafikiwa.

**9. *Mheshimiwa Spika*:** kwa namna ya kipekee natoa shukranizangu za dhati kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii chini ya Makamu Mwenyezekiti Mhe. Kemirembe Rose Julius Lwota (Mb.), kwa

ushirikiano mkubwa na ushauri wao ambao unaiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, namshukuru aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati hii Mhe. Nape Moses Nnauye (Mb.) kwa kuiongoza Kamati katika kipindi chake. Pia, nawashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati kwa uchambuzi makini walioufanya na ushauri walioutoa wakati wa kupitia taarifa ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka wa fedha 2018/19 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu **48**, na Fungu **03**, kwa mwaka wa fedha 2019/20. Pia, ninawashukuru kwa maoni na ushauri waliota kwa Wizara wakati wa ziara za kukagua miradi ya maendeleo inayosimamiwa na Wizara na Taasisi zake. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa yamezingatiwa katika bajeti hii.

**10.** *Mheshimiwa Spika*; natoa shukrani na pongezi za dhati kwa Wananchi wa Jimbo la Ismani kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa katika kipindi chote cha kuwawakilisha hapa Bungeni. Aidha, nawapongeza kwa juhudhi wanazofanya katika kujiletea maendeleo yao na Taifa kwa ujumla.

## **2.0 MAJUKUMU YA WIZARA**

**11.** *Mheshimiwa Spika*; Wizara yangu inatekeleza majukumu yafuatayo:-

- i) Kuratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995;
- ii) Kuratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000;
- iii) Kusimamia utawala wa ardhi;
- iv) Kusimamia upangaji na uendelezaji wa miji na vijiji;
- v) Kusimamia na kuwezesha upimaji wa ardhi na kutayarisha ramani;

- vi) Kumilikisha ardhi na kuwezesha utoaji wa hatimiliki za kimila;
- vii) Kusajili hatimiliki za ardhi, kuimarisha usalama wa milki na nyaraka za kisheria;
- viii) Kusimamia uthamini wa mali nchini;
- ix) Kuhamasisha na kuwezesha ujenzi wa nyumba bora;
- x) Kusimamia uendelezaji milki;
- xi) Kusimamia Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya;
- xii) Kusimamia utunzaji wa kumbukumbu za ardhi;
- xiii) Kusimamia ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na huduma za sekta ya ardhi;
- xiv) Kuwezesha uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi na kufuatilia utekelezaji wake;
- xv) Kusimamia taasisi zilizo chini ya Wizara ambazo ni Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi; Shirika la Nyumba la Taifa; Vyuo vya Ardhi vya Tabora na Morogoro na Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba na Vifaa vya Ujenzi;
- xvi) Kusimamia maslahi na utendaji kazi wa watumishi wa Wizara; na
- xvii) Kusimamia maendeleo ya watumishi wa sekta ya ardhi nchini.

**12. *Mheshimiwa Spika***; kwa kuzingatia majukumu haya, Wizara imeendelea kuandaa na kusimamia mipango mbalimbali ya uendelezaji wa sekta ya ardhi na kuzaa matunda chanya.

### 3.0 HALI YA SEKTA YA ARDHI NCHINI

13. ***Mheshimiwa Spika;*** sekta ya ardhi nchini imeendelea kuimarika na kuchangia katika maendeleo ya uchumi wa wananchi na Taifa kwa ujumla hususan katika kipindi hiki tunapojozititi kujenga uchumi wa viwanda ili kuchochea mageuzi ya uchumi na maendeleo ya watu. Pia sekta hii imeendelea kuwa kiungo wezeshi katika sekta nyingine za uzalishaji ikiwemo Viwanda, Kilimo, Mifugo, Ujenzi, Misitu, Maliasili, Miundombinu, Maendeleo ya Makazi na Miliki na hivyo kuongeza thamani na uhitaji wa ardhi nchini.

14. ***Mheshimiwa Spika;*** ukuaji wa sekta ya ardhi nchini kwa mwaka 2018/19 unaonesha kuendelea kuimarika ikilinganishwa na miaka iliyotangulia. Katika kuhakikisha sekta ya ardhi inaimarika zaidi, Wizara inaendelea kujenga mifumo ya utawala na usimamizi wa ardhi, kukuza na kuhakikisha kuwepo kwa mifumo ya usalama wa milki nchini, kuhimiza matumizi bora ya ardhi, kurekebisha na kurahisisha mifumo ya upangaji, upimaji na usimamizi wa ardhi. Aidha, Wizara itaendelea kuboresha mahusiano na wadau mbalimbali katika uendelezaji na utatuzi wa migogoro ya ardhi, kukuza uwezo wa kutunza kumbukumbu, kutoa taarifa na elimu kwa umma.

15. ***Mheshimiwa Spika;*** takriban asilimia **75** ya wakazi mijini wanaishi katika maeneo yasiyopangwa na hawana nyaraka za kisheria za kuthibitisha uhalali wa umiliki wa ardhi yao. Hali hii inawafanya wananchi kuendelea kuwa na mitaji ya ardhi iliyokufa (dead capital) na hivyo, kuwa mojawapo ya kikwazo cha kuijendezea kiuchumi na kupata fursa za kujajiri. Pia inafanya ardhi isiwe na mchango mkubwa katika pato la Taifa.

16. Mheshimiwa Spika; Wizara imeongeza kasi ya kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kupanga, kupima na kumilikisha ardhi kisheria kwa kushirikiana na mamlaka za upangaji. Aidha, Wizara inatekeleza mkakati maalum wa kurasimisha na kuboresha makazi yaliyoendelezwa kiholela na kutoa hati na leseni za makazi. Jumla ya makazi **610,655**

katika halmashauri mbalimbali nchini yamerasimishwa kuanzia mwaka 2015 hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2019. Aidha, katika kipindi hicho jumla ya hatimiliki **115,593** na hatimiliki za kimila **308,549** ziliandaliwa na kusajiliwa. Kwa upande wa makusanyo ya maduhuli ya Serikali, yameongezeka kutoka shilingi bilioni **74.71** mwaka 2015/16 hadi shilingi bilioni **100** mwaka 2017/18. Makusanyo hayo yameongezeka kutokana na juhudzi za Wizara katika kusimamia kupanga, kupima na kumilikisha ardhi. Aidha, Serikali imesajili vyeti nya ardhi ya kijiji vипатавyo **3,018** kati ya vijiji **12,545** katika kipindi cha mwaka 2015 hadi 2018 hivyo kufanya idadi ya vijiji vyenye vyeti nya ardhi vilivyosajiliwa nchini kufika **11,153**. Lengo ni kuhakikisha vijiji vyote nchini vinasajiliwa na kupewa vyeti nya umiliki wa ardhi.

**17. *Mheshimiwa Spika:*** Serikali pia ilipunguza gharama za umilikishaji ardhi na kuwa rafiki kwa wananchi. Kwa mfano, tozo ya mbele (premium) imepunguzwa kutoka asilimia **7.5** ya thamani ya ardhi inayorasimishwa mijini katika mwaka wa fedha 2015/16 hadi asilimia moja (**1**) na asilimia **2.5** kwa ardhi iliyopangwa kwa mwaka 2018/19, gharama elekezi ya urasimishaji makazi imepunguzwa kutoka shilingi **300,000/=** kwa mwaka 2015/16 hadi shilingi **150,000/=** mwaka 2018/19.

**18. *Mheshimiwa Spika:*** ili kuwezesha na kurahisisha utambuzi wa vipande nya ardhi mijini na taarifa za wamiliki, Serikali imeandaa mfumo wa kielektroniki unaotumia simu ya mkononi (simu janja) na kuwezesha kutoa leseni za makazi zinazotambulika kisheria. Mfumo huu umeanza kutekelezwa katika Jiji la Dar es Salaam na utaendelea kutumika nchi nzima. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2019 takriban vipande nya ardhi nya matumizi mbalimbali **150,000** vimesajiliwa. Hatua hii itawapa wananchi uhakika wa milki zao na kuwezesha ardhi yao kutumika kama mtaji kiuchumi. **Ninatoa wito kwa wamiliki wote wa ardhi katika makazi yasiyopangwa kutoa ushirikiano kwa wataalam watakaofika katika mitaa yao na kutoa taarifa sahihi za umiliki ili kufanikisha zoezi hili.**

#### **4.0 MWELEKEO NA MALENGO YA KUENDELEZA SEKTA YA ARDHI NCHINI**

**19.** *Mheshimiwa Spika*; Wizara yangu inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 - 2020/21); Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015; Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, katika Mkutano wa 11 wa Bunge wa Novemba 2015; Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi (2013-2033); Agenda ya Dunia ya Malengo Endelevu ya Maendeleo ya mwaka 2030; Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995; Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 pamoja na sheria na miongozo mbalimbali inayotolewa na Serikali.

**20.** *Mheshimiwa Spika*; kwa kuzingatia haya, mwelekeo wa sekta ya ardhi ambao Wizara itaendelea kuusimamia kwa dhati hadi mwaka 2025 ni kuleta mageuzi katika uandaaji na usimamizi wa upangaji, upimaji, uthaminishaji na umilikishaji wa ardhi nchini ili kuwawezesha wananchi na taasisi kuwa na uhakika wa miliki ya ardhi.

**21.** *Mheshimiwa Spika*; kwa mantiki hiyo, mageuzi tunayotaka kuyafanya ni kuhakikisha Watanzania wanapata hati za kumiliki ardhi na kuzitumia kwa ajili ya kujiletea maendeleo kwa ustawi wa kiuchumi na kijamii. Malengo mengine ya mageuzi haya ni pamoja na kuboresha utendaji na utoaji huduma katika sekta ya ardhi ikiwemo kusimamia watumishi wa Sekta ya Ardhi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Pia kuratibu na kusimamia Sera, Sheria, kanuni na miongozo mbalimbali ya sekta. Vilevile, Wizara itatumia teknolojia ya kisasa katika upangaji, upimaji umilikishaji, uendelezaji wa miji na vijiji, utunzaji wa kumbukumbu za ardhi na ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali. Azma hii inalenga kuhakikisha huduma za ardhi zinatolewa kwa ufanisi na kwa gharama nafuu.

**22.** *Mheshimiwa Spika*; mageuzi haya pia yanalenga kupata ufumbuzi wa kudumu wa migogoro mbalimbali ya matumizi ya ardhi nchini na kujenga uelewa kwa wananchi na wadau kuhusu masuala mbalimbali ya ardhi. Aidha, Wizara itaendelea kuwajengea uwezo watumishi ili kuboresha huduma zinatolewa kwa wananchi.

**23.** *Mheshimiwa Spika*; baada ya maelezo hayo ya utangulizi, majukumu na hali ya sekta ya ardhi nchini, naomba sasa nieleze mapitio ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara (Fungu 48), pamoja na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03) kwa mwaka wa fedha 2018/19 na makadirio ya mapato na matumizi ya mafungu haya kwa mwaka wa fedha 2019/20. Takwimu za utekelezaji wa bajeti zilizopo katika hotuba hii zinaishia tarehe 15 Mei, 2019.

#### **5.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2018/19 NA MALENGO YA MWAKA WA FEDHA 2019/20**

**24.** *Mheshimiwa Spika*; Wizara imetekeleza majukumu yake kuititia mafungu mawili ya kibajeti. Mafungu hayo ni Fungu 48-Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Fungu 03-Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi.

##### ***Mapato na Matumizi ya Fedha: Fungu 48***

###### **Mapato**

**25.** *Mheshimiwa Spika*; katika mwaka wa fedha 2018/19, Wizara ilipanga kukusanya shilingi bilioni **120** kutokana na vyanzo vya mapato ya kodi, ada na tozo mbalimbali za ardhi. Hadi tarehe 15 Mei, 2019, Wizara imekusanya shilingi bilioni **75.73** sawa na asilimia **63.1** ya lengo (**Jedwali Na. 1**).

**26.** *Mheshimiwa Spika*, nakisi ya makusanyo ya maduhuli yatokanayo na ardhi inachangiwa kwa sehemu kubwa na baadhi ya wamiliki kutolipa kodi ya pango la ardhi kwa wakati. Wizara inaendelea kufuatilia na kuhamasisha

wamiliki wa ardhi kulipa kodi ya pango la ardhi kwa kutumia vyombo vya habari, kuwafikisha mahakamani wadaiwa sugu na kuwafutia miliki. **Natumia fursa hii kuwapongeza wamiliki wa ardhi waloliwa kodi ya pango la ardhi kwa wakati.** Aidha, natoa rai kwa wananchi walioopimiwa ardhi na kutambuliwa milki zao na wale wote wanaodaiwa kodi ya pango la ardhi kulipa kwa wakati ili kuepuka hatua za kisheria. Vilevile, watu wote walioopimiwa au kurasimishiwa ardhi lazima wamilikishwe ardhi husika na kupewa hatimiliki kwa mujibu wa sheria na kulipia kodi ya pango la ardhi.

**27. *Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara yangu inatarajia kukusanya shilingi bilioni **180** kutokana na kodi ya pango la ardhi, ada na tozo mbalimbali zinazohusiana na sekta ya ardhi. Lengo hili litafikiwa kwa kutekeleza mikakati ifuatayo:-

- i) Kuimarisha mifumo ya TEHAMA ya utunzaji wa kumbukumbu na kuboresha taarifa za ardhi;
- ii) Kurahisisha ukadiriaji wa kodi ya pango la ardhi na tozo zitokanazo na sekta ya ardhi kwa kutumia vifaa vya kielektroniki vinavyohamishika (Point of Sales Machines-POS);
- iii) Kuendelea kushirikiana na Mamlaka za Upangaji pamoja na sekta binafsi katika zoezi la upangaji, upimaji na umilikishaji ardhi ili kuongeza wigo wa mapato;
- iv) Kutumia mfumo wa kielektroniki unaotumia simu ya mkononi (simu janja) na kuwezesha kutambua na kusajili vipande vya ardhi mijini na kutoa leseni za makazi zinazotambulika kisheria;
- v) Kuendelea kusimamia uendelezaji wa ardhi kulingana na matumizi yaliyopangwa na kuwatoza adhabu wakiukaji wa masharti kwa mujibu wa sheria;

- vi) Kuhakikisha watu wote wa mijini wenye nyumba na ardhi isiyopimwa wanarasimishiwa na kupewa hati na leseni za makazi;
- vii) Kuendelea kusimamia na kuchukuwa hatua kali za kisheria kwa wamiliki wote wasiolipa kodi za ardhi kwa wakati;
- viii) Kuhakikisha kuwa wamiliki wote wa ardhi waliopimiwa na kurasimishiwa maeneo yao wanamilikishwa ili waweze kulipa kodi ya pango la ardhi kwa mujibu wa sheria;
- ix) Kuendelea kuboresha mfumo wa ulipaji maduhuli yatokanayo na ardhi kwa kutumia mitando ya simu;
- x) Kuendelea kuhuisha vigezo vinavyotumika kukadiria tozo mbalimbali za ardhi ili ziendane na wakati; na
- xi) Kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa wamiliki wa ardhi kulipa kodi kwa wakati.

### **Matumizi**

**28. *Mheshimiwa Spika***; katika mwaka wa fedha 2018/19, Wizara ilidhinishiwa shilingi bilioni **65.98** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni **17.68** ni kwa ajili ya mishahara; shilingi bilioni **17.76** kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni **30.54** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Baada ya uhakiki wa madeni uliofanywa na Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ilipewa shilingi bilioni **12.8** kwa ajili ya kulipa madeni ya wazabuni na hivyo kuifanya bajeti ya Wizara kuwa jumla ya shilingi bilioni **78.8 (Jedwali Na. 2)**. Hadi tarehe 15 Mei, 2019, Wizara ilipokea shilingi bilioni **51.92** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo, sawa na asilimia **65.9** ya bajeti. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni **12.9** ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni **22.2** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, shilingi bilioni **16.2** zilitolewa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

## *Mapato na Matumizi ya Fedha: Fungu 03*

### **Mapato**

**29.** *Mheshimiwa Spika*; katika mwaka wa fedha 2018/19, Tume ilitarajia kupata kiasi cha shilingi milioni **700**. Kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi milioni **680.15** kutoka kwa wadau wa kimkakati na kiasi cha shilingi milioni **19.85** kutokana na kodi ya pango la nyumba za Tabora na mauzo ya nyaraka mbalimbali za zabuni. Hadi tarehe 15 Mei, 2019, Tume ilipata shilingi milioni **998.16** sawa na asilimia **142.3** ya lengo. Kati ya fedha hizo, shilingi milioni **966.23** sawa na asilimia **142.1** ni fedha kutoka kwa wadau wa kimkakati na shilingi milioni **31.93** sawa na asilimia **160.9** ni mapato ya ndani.

### **Matumizi**

**30.** *Mheshimiwa Spika*; katika mwaka wa fedha 2018/19, Tume iliidhinishiwa shilingi bilioni **7.08** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni **1.10** ni kwa ajili ya mishahara, shilingi milioni **979.8** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni **5.0** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2019, Tume ilipokea shilingi bilioni **3.37** fedha za matumizi ya kawaida na maendeleo sawa na asilimia **47.59**. Kati ya fedha hizo, shilingi milioni **737.6** ni kwa ajili ya mishahara, shilingi milioni **633.7** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni **2** ni fedha za maendeleo.

### **5.1      HUDUMA ZA UTAWALA WA ARDHI**

**31.** *Mheshimiwa Spika*; Wizara yangu inasimamia huduma za utawala wa ardhi ikiwemo utoaji wa hati milki na hati za hakimiliki za kimila, usajili wa hati, nyaraka na miamala ya ardhi, usuluhishi wa migogoro ya ardhi, uthamini wa mali, uendelezaji wa milki, ukusanyaji wa maduhuli na utunzaji wa kumbukumbu za ardhi. Wizara yangu imeendelea kuboresha utoaji wa huduma hizi kwa kutumia mifumo ya kieletroniki.

**32. *Mheshimiwa Spika***; Wizara ina jukumu la kusimamia watumishi wa sekta ya ardhi walioko katika halmashauri nchini. Katika utekelezaji wa jukumu hili, Wizara ilisaini Hati ya Makubaliano na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Zoezi la kuwatambua na kuwapanga watumishi hao kwa uwiano kulingana na mahitaji limekamilika, na ifikapo Julai 2019 inatarajiwa kuwa watumishi wote watakuwa wamehamishiwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Aidha, Wizara itawapanga upya watumishi wote kulingana na sifa na weledi na taarifa zao za kiutumishi. Wale watumishi wenye tabia za hovyo, watachukuliwa hatua za kisheria na kuondolewa kwenye utumishi wa umma.

**33. *Mheshimiwa Spika***; Wizara yangu ina jumla ya kanda nane (8) za utawala wa ardhi ambazo ni Dar es Salaam, Kati, Kusini, Nyanda za Juu Kusini, Kaskazini, Simiyu, Ziwa na Magharibi. Katika kuimarisha utoaji wa huduma za ardhi na kuzisogezza karibu na wananchi, Wizara yangu inaaniszha kanda maalum ya Morogoro. Kanda hii itahudumia mkoa wa Morogoro kutokana na ukubwa wake, sababu za kijiografia na uwepo na shughuli mbalimbali za kiuchumi zinazohitaji huduma ya ardhi.

#### **Uandaaji na Usajili wa Hati na Nyaraka za Kisheria**

**34. *Mheshimiwa Spika***; katika kutekeleza sera na sheria za ardhi, Wizara inaratibu utoaji wa vyeti vya ardhi ya vijiji, hati za hakimiliki za kimila na hatimiliki za ardhi. Azma hii inalenga kuimarisha usalama wa milki za ardhi kwa wananchi.

**35. *Mheshimiwa Spika***; hadi tarehe 15 Mei, 2019, Wizara imeandaa na kusajili hati za hakimiliki **47,688 (Jedwali Na. 3)** na pia kusajili nyaraka nyingine za kisheria **25,045** chini ya Sheria ya Usajili wa Ardhi (Sura 334) (**Jedwali 4 A**). Kati ya hizo, Hati za Umiliki wa Sehemu ya Jengo ni **460** ambazo zimesajiliwa chini ya sheria ya Umiliki wa Sehemu ya Jengo (Sura 416). Aidha, Nyaraka za Kisheria zipatazo **14,604 (Jedwali 4 B)** zimesajiliwa chini ya Sheria ya Usajiliwa Nyaraka (Sura

117) na Nyaraka **1,796 (Jedwali 4 C)** zimesajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Rehani ya Mali Zinazohamishika (Sura 210). Vilevile, Wizara imesajili Vyeti vya Ardhi ya Kijiji **341** na Hati za Hakimiliki ya Kimila **166,478 (Jedwali Na. 5)**. Natoa rai kwa wananchi waliopimiwa maeneo yao kuhakikisha wanamilikishwa.

**36. *Mheshimiwa Spika***; katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara inakusudia kusajili Hatimiliki na Nyaraka za kisheria **152,000**. Kati hizi, hati za kumiliki ardhi ni **100,000**, hati za kumiliki sehemu ya jengo/eneo **2,000** na Nyaraka za Kisheria **50,000**. Napenda kutumia fursa hii kuhimiza wananchi kuona umuhimu wa kusajili nyaraka mbalimbali zinazotokana na miamala ya ardhi iliyosajiliwa, mfano mikataba ya uhamisho wa milki, wosia, rehani za mikopo n.k. Hii itasaidia kuwaepusha na wimbi la utapeli wa ardhi.

**37. *Mheshimiwa Spika***; katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara yangu kwa kushirikiana na mamlaka za upangaji nchini itaandaa na kusajili Vyeti vya Ardhi ya Kijiji **100** kati ya **1,392** ambavyo havijasajiliwa na Hati za Hakimiliki za Kimila **150,000** zitaandaliwa. Aidha, Wizara yangu imepanga kusajili nyaraka za kisheria zipatazo **53,000**. Natoa rai kwa Mamlaka za Upangaji nchini kuhakikisha kuwa zinamilikisha viwanja vyote vilivyopimwa ili wananchi waweze kuwa na milki salama. Pia nawahimiza wamiliki wote wa ardhi kuchukua hati zao zilizokamilika kutoka Ofisi za Msajili wa Hati zilizopo katika ofisi za ardhi za kanda.

### **Usimamizi wa Masharti ya Umiliki**

**38. *Mheshimiwa Spika***; Wizara yangu ilipanga kukagua utekelezaji wa masharti ya umiliki wa mashamba **6,000**. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2019 Wizara yangu imekagua mashamba yasiyoendelezwa **1,425**. Katika mwaka wa fedha 2019/20 Wizara itaendelea kufanya utambuzi na ukaguzi wa mashamba makubwa yasiyozingatia masharti ya umiliki nchini na kuchukua hatua za kisheria. Aidha, ardhi ya mashamba ambayo milki zake zitabatilishwa itakuwa sehemu ya hazina ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji na

kuwapatia wananchi wenye mahitaji kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji baada ya kupangwa na kupimwa upya.

### **Uthamini wa Mali na Fidia**

**39.** *Mheshimiwa Spika*; katika mwaka wa fedha 2018/19 Wizara iliahidi kuhuisha viwango vya bei ya ardhi katika soko kwa nchi nzima. Pia, Wizara iliahidi kuandaa na kuidhinisha taarifa **35,000** za uthamini. Wizara imekamilisha uandaaji wa jedwali la viwango vya thamani ya mazao kwa nchi nzima na inaendelea kuandaa jedwali la viwango vya thamani ya ardhi mijini. Aidha, taarifa **33,160** za uthamini zimeidhinishwa ambapo kati ya hizo, taarifa zenye idadi ya wafidiwa ni **23,926** na **9,234** ni za uthamini wa kawaida.

**40.** *Mheshimiwa Spika*; katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara inatarajia kuidhinisha taarifa **29,000**, ambapo kati ya hizo taarifa **10,000** ni za uthamini wa kawaida na taarifa za uthamini wa fidia kwa wafidiwa **19,000**, kushughulikia malalamiko ya migogoro **120** iliyopo kutokana na uthamini uliyofanyika na kuimarisha kumbukumbu za uthamini ikiwemo kukamilisha uhuishaji wa viwango vya bei ya soko la ardhi katika mikoa **26**.

### **Usuluhishi wa Migogoro ya Matumizi ya Ardhi**

**41.** *Mheshimiwa Spika*; migogoro ya matumizi ya ardhi imekuwa na athari mbalimbali ikiwa ni pamoja na uharibifu wa mali, mifugo na mazao; uharibifu wa hifadhi za wanyamapor; uharibifu wa vyanzo vya maji na maeneo oevu; kupungua kwa vivutio vya utalii; kutoweka kwa wanyamapor; uharibifu wa mazingira ya bioanuai; na kutoweka kwa amani katika maeneo husika.

**42.** *Mheshimiwa Spika*; katika mwaka wa fedha 2018/19 Wizara iliahidi kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa migogoro mbalimbali ya matumizi ya ardhi na kuendelea kusikiliza kero za wananchi na kuzipatia majibu. Ili kupata ufumbuzi wa kudumu kuhusiana na migogoro na kero mbalimbali za

matumizi ya ardhi, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za kisekta, Waheshimiwa Wabunge na Wakuu wa Mikoa imeratibu na kukamilisha taarifa yenyе mapendekezo ya utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi. Hatua hii ni katika kutekeleza agizo la Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alilotoa tarehe 15 Januari, 2019 kwa Mawaziri wa Kisekta kuandaa mapendekezo ya ufumbuzi wa kudumu wa migogoro ya matumizi ya ardhi nchini.

**43. *Mheshimiwa Spika***; katika kushughulikia migogoro ya matumizi ya ardhi, Wizara za Kisekta zilizingatia maelekezo yafuatayo katika kuandaa mapendekezo:-

- i) Kutoviondoa vijiji na vitongoji **366** vilivymo ndani ya hifadhi;
- ii) Kubainisha maeneo ya hifadhi ambayo yamepoteza sifa ili yaweze kugawiwa kwa wananchi kwa shughuli za ufugaji na kilimo;
- iii) Kuhakiki na kurekebisha mipaka baina ya hifadhi za misitu, wanyama na makazi;
- iv) Kumega baadhi ya hifadhi na kuwagawia wafugaji na wakulima;
- v) Kufanya mapitio ya sheria mbalimbali zinazohusiana na matumizi ya ardhi;
- vi) Kupitia upya Sheria ya Vyanzo vy'a Maji inayozungumzia mita 60;
- vii) Kuwasilisha mapendekezo ya kufutwa mashamba yasiyoendelezwa na kugawa kwa wananchi kwa ajili ya uzalishaji wa mazao ya kilimo na mifugo; na
- viii) Kuendelea kulinda na kuhifadhi maeneo ya hifadhi za misitu, wanyamaporii na vyanzo vy'a maji.

**44. *Mheshimiwa Spika***; taarifa zilizochambuliwa na kuandaliwa mapendekezo kwa kuzingatia maelekezo hayo zinahusu migogoro ya matumizi ya ardhi katika maeneo ya ufügaji, kilimo, hifadhi za misitu na wanyamapori, vyanzo vya maji, hifadhi za mazingira, ulinzi, mipaka ya kiutawala na fidia ya ardhi. Wizara zilizoshiriki katika utekelezaji wa agizo hilo ni Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira);Maliasili na Utalii; Mifugo na Uvuvi; Kilimo; Maji; Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; na Fedha na Mipango. Kwa heshima kubwa naomba kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake imara na wenge weledi katika kusimamia na kutatua migogoro ya matumizi ya ardhi iliyopo nchini kupitia Mawaziri wa Kisekta walioteuliwa kufanya kazi hii muhimu kwa pamoja kwa ajilli ya kuwatetea wananchi hususan wanyonge. Taarifa yenye mapendekezo yote muhimu imewasilishwa rasmi Serikalini ili ipitiwe na Baraza la Mawaziri. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa taarifa mlizotoa ambazo zimezingatiwa ipasavyo.

**45. *Mheshimiwa Spika***; napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara itaendelea kushirikisha sekta zinazohusiana na ardhi kutatua migogoro mtambuka ikijumuisha ile ya mipaka ya vijiji, wakulima na wafugaji, wanavijiji na hifadhi na mapori ya akiba. Katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara yangu imepanga kutatua migogoro ya matumizi ya ardhi kiutawala na kushughulikia mashauri **500** yaliyopo na yatakayofikishwa mahakamani.

**46. *Mheshimiwa Spika***; kupitia kauli mbiu ya Wizara yangu ya “**Funguka na Waziri**”, Wizara imeendelea kusikiliza malalamiko ya wananchi katika halmashauri mbalimbali nchini kupitia mikutano na wananchi pamoja na ujazaji wa madodoso. Jumla ya kero na malalamiko **13,055** yalipokelewa ambapo **10,174** yamefanyiwa kazi na **2,719** yanaendelea kufanyiwa kazi (**Jedwali Na. 6**).

## Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya

47. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara yangu imeendelea kusimamia na kuhudumia Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya yanayofanya kazi ya kusikiliza na kuamua mashauri yahusuyo migogoro ya ardhi. Katika mwaka wa fedha 2018/19 Wizara yangu imefungua Mabaraza mapya katika Wilaya za Mbulu na Ulanga na kufanya mabaraza kuwa **55** (Jedwali Na. 7). Katika mwaka wa fedha 2018/19 Wizara iliahidi kushughulikia mashauri **24,600** yaliyobaki na yatakayofunguliwa. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2019 mashauri mapya **15,995** yalifunguliwa na kufanya jumla ya mashauri yote kuwa **40,595** ambapo kati ya hayo, mashauri **11,980** yaliamuliwa. Katika mwaka wa fedha 2019/20 Wizara itaendelea kushughulikia mashauri **28,615** yaliyobaki na yatakayofunguliwa.

48. ***Mheshimiwa Spika;*** ili kuongeza kasi ya kusikiliza mashauri ya ardhi, katika mwaka wa fedha 2018/19, Wizara yangu imeajiri Wenyeviti wapya **20** wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kwa ajili ya kuongeza nguvu katika Mabaraza yenye mashauri mengi katika Wilaya za Ukerewe, Maswa, Mbinga, Mbulu, Kilosa, Kyela, Ulanga, Lushoto, Nzega, Lindi, Same, Iramba, Shinyanga, Bukoba, Morogoro, Musoma, Mwanza, Kigoma, Temeke na Kinondoni. Ni matarajio ya Wizara kuwa Wenyeviti hawa wataongeza kasi ya kusikiliza na kutoa maamuzi ya migogoro ya ardhi inayowakabili wananchi. Aidha, baadhi ya wenyeviti wamesimamishwa kazi kupisha uchunguzi na wengine wamehamishwa vituo vyao veya kazi.

## Kamati ya Taifa ya Ugawaji Ardhi

49. ***Mheshimiwa Spika;*** Kamati ya Taifa ya Ugawaji Ardhi pamoja na majukumu mengine, ina jukumu la kuidhinisha maombi ya umilikishaji ardhi yanayohusiana na uwekezaji, maeneo ya fukwe, pamoja na maeneo yote ya kimkakati ya uwekezaji yenye manufaa kwa Taifa. Kuanzia mwaka 2015 hadi tarehe 15 Mei, 2019 Kamati ilipokea maombi **421**. Kati ya hayo, maombi ya uwekezaji na viwanja nya fukwe ni **354**

na maombi **67** ni viwanja vya kibalozi na mashirika ya kimataifa Jijini Dodoma. Katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara itaendelea kuwezesha vikao vya Kamati ya Kitaifa ya Ugawaji wa Ardhi kadiri ya mahitaji na kwa wakati.

### **Baraza la Taifa la Ushauri wa Ardhi**

**50.** *Mheshimiwa Spika*; katika kutekeleza na kusimamaia utawala wa ardhi nchini, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba Wizara imekamilisha uundaji wa Baraza la Taifa la Ushauri wa Ardhi ambalo lilizinduliwa rasmi mwezi Julai, 2018. Baraza hili ni chombo muhimu kilichoundwa kisheria kwa ajili ya kuishauri Wizara kuhusu masuala ya kisera, sheria na muundo wa kitaasisi wa Wizara na taasisi zinazosimamia sekta ya ardhi nchini. Katika mwaka wa fedha 2018/19 Wizara imeweza vikao vya Baraza la Taifa la Ushauri wa Ardhi kujadili na kutoa mapendekezo ya maboresho ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995.

### **Bodi za Usajili wa Wataalam wa Fani za Ardhi**

**51.** *Mheshimiwa Spika*; katika kuimarisha utawala wa ardhi, Wizara yangu imeendelea kushirkiana na Bodi ya Usajili wa Wataalam wa Mipangomiji na Bodi ya Usajili wa Wathamini. Jukumu la Bodi hizi ni kusajili, kusimamia weledi na kutoa adhabu stahiki pale inapotokea ukiukwaji wa maadili ya kitaaluma.

**52.** *Mheshimiwa Spika*; katika mwaka wa fedha 2018/19 Bodi ya Wataalam ya Mipangomiji imesajili Wataalam **46** na hivyo kufikia jumla ya wataalam **364**. Aidha, imesajili kampuni **11** na kufikisha kampuni **60 (Jedwali Na.8)**. Vilevile Bodi ya Wataalamu ya Upimaji Ardhi imesajili jumla ya kampuni **84** za upimaji (**Jedwali Na.9**). Katika kusimamia maadili ya taaluma, wataalamu wawili (**02**) wamechukuliwa hatua za kinidhamu kwa kupewa onyo, kampuni moja (**01**) imesimamishwa na kampuni tano (**05**) zilifunguliwa mashtaka na mashauri bado yanaendelea mahakamani.

## Utunzaji wa Kumbukumbu za Ardhi

**53. Mheshimiwa Spika;** Mfumo Uganishi wa Kuhifadhi Kumbukumbu za Ardhi (Integrated Land Management Information System-ILMIS) umeanzishwa kwa lengo la kuboresha utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka za ardhi kwa njia ya kielektroniki, kurahisisha utendaji kazi, kuharakisha mchakato wa utoaji hatimilki ya ardhi na hatimaye kuongeza mapato ya Serikali. Mfumo wa ILMIS unatekelezwa katika Ofisi za Ardhi za Manispaa za Ubungo na Kinondoni. Kupitia mfumo huu jumla ya hati **4,461** zimeandaliwa, ambapo hati **1,218** zimekamilishwa na kusajiliwa. Kati ya hati zilizosajiliwa, hati **870** zimechukuliwa na wamiliki. Mpango wa Wizara yangu ni kukamilisha ufungaji wa mfumo kwenye halmashauri zote za Manispaa za mkoa wa Dar es Salaam ifikapo mwezi Julai 2019. Kuanzia mwezi Agosti, 2019 mkoa wote wa Dar es Salaam utaanza kutoa hati za kielektroniki.

**54. Mheshimiwa Spika;** katika mwaka wa fedha 2018/19, Wizara iliahidi kuendelea kuboresha na kuimarisha mifumo ya kielektroniki ya utoaji wa huduma za ardhi hususan mfumo wa makusanyo ya maduhuli yatokanayo na ardhi. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2019 jumla ya mashine za kielektroniki (Point of Sales Machine-PoS) **238** zimenunuliwa na kusambazwa kwenye ofisi za ardhi zilizoko katika Halmashauri **184** na Mabaraza **53** ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya. Mashine hizo zinalenga kurahisisha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali na zimeunganishwa na Mfumo wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali (GePG). Katika mwaka wa fedha 2019/20 Wizara imedhamiria kuendelea kuunganisha mfumo wa ILMIS na utunzaji wa kumbukumbu za ardhi kidigitali katika halmashauri zilizobaki nchini kwa awamu.

**55. Mheshimiwa Spika;** sanjari na utunzaji wa kumbukumbu za ardhi kwa njia ya kidijitali, Wizara pia inaendelea na juhudi za ujenzi wa masjala za ardhi katika halmashauri na vijiji. Hivi sasa ujenzi unaendelea katika halmashauri za wilaya za Kilombero, Ulanga na Malinyi. Lengo ni kuhakikisha kuwa kila halmashauri inakuwa na masjala yake ya kutunza kumbukumbu za ardhi.

## 5.2 UPIMAJI ARDHI NA UTAYARISHAJI WA RAMANI

### Huduma za Ramani

56. ***Mheshimiwa Spika***; katika mwaka wa fedha 2018/19, Wizara yangu iliahidi kuhuisha ramani za msingi za uwiano wa chini kwa miji **100** katika wilaya mbalimbali nchini. Ramani hizi hutumika katika kuandaa michoro ya mipango ya matumizi ya ardhi, ramani zinazoonesha mipaka ya viwanja na mashamba, kuwezesha usanifu wa miradi ya ujenzi wa miundombinu, mfano barabara, reli, mabomba ya mafuta na gesi pamoja na njia kuu za kusafirisha umeme. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Wizara imehuisha ramani **30** za uwiano wa 1:50,000 katika miji ya mkoa wa Dodoma na Ruvuma. Katika mwaka wa fedha, 2019/20 Wizara yangu itaendelea kuhuisha ramani za msingi **68** pamoja na ramani zingine katika wilaya mbalimbali.

57. ***Mheshimiwa Spika***; katika mwaka wa fedha 2018/19, Wizara imenunua vifaa vya kisasa vya upimaji ardhi (*RTK seti 29, Total Stations seti 41, desktop computers 93, printers 66 na laptops 68*). Vifaa hivyo vimegawanywa katika kanda zote za ardhi na vyuo vya ardhi Tabora na Morogoro. Aidha, ili kuwa na matumizi bora na kuhakikisha usalama wa vifaa hivi wakati wa kuvitumia, Wizara imetoa mafunzo kwa Maafisa Ardhi waliopo katika Halmashauri na Ofisi za Kanda. Dhamira ya Wizara ni kuendelea kuimarisha huduma zake katika ngazi za Mikoa na Halmashauri zote nchini. **Natoa rai kwa Halmashauri zote nchini kutumia vifaa vya upimaji vilivyonunuliwa kwa shughuli za upimaji badala ya kukodi vifaa hivyo kutoka sekta binafsi.** Lengo ni kupunguza gharama za umilikishaji ardhi.

### Mipaka ya Ndani ya Nchi

58. ***Mheshimiwa Spika***; katika mwaka wa fedha 2018/19 Wizara yangu iliahidi kuhakiki mipaka sita (**06**) ya Wilaya za Babati na Monduli, Manyoni na Sikonge, Gairo na Kilosa, Kisarawe na Kibaha, Njombe na Mufindi na Mbarali na

Mufindi. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi tarehe 15 Mei 2019 kazi za uhakiki wa mipaka sita ya Wilaya tajwa imefanyika kwa hatua za uwandani na sasa zipo katika hatua za utekelezaji. Katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara itaendelea kutatua migogoro ya mipaka ya ndani ya nchi kwa kadiri itakavyokuwa inajitokeza. **Natoa rai kwa wakuu wa Mikoa na Wilaya kuendelea kubaini na kutatua migogoro ya mipaka baina ya vijiji na wilaya kabla ya uchaguzi ujao wa Serikali za Mitaa.**

### **Mipaka ya Kimataifa**

**59.** *Mheshimiwa Spika*; katika mwaka wa fedha 2018/19, Wizara iliahidi kuendelea na uimarishaji wa mpaka wa Tanzania na Uganda, Tanzania na Zambia, Tanzania na Burundi, Tanzania na Kenya na kuimarisha mipaka ya nchi ndani ya Ziwa Tanganyika na nchi za Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo, Burundi na Zambia. Lengo ni kuhakikisha ifikapo mwaka 2022 kazi ya uimarishaji wa mpaka huu iwe imekamilika.

**60.** *Mheshimiwa Spika*; napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba upande wa mpaka kati ya Tanzania na Uganda wa nchi kavu wenyе urefu wa kilometa **149** majadiliano kwa ajili ya kuimarisha mpaka huu yamefanyika sawia na ukaguzi wa alama za mpaka na upimaji wa malundo **15** ya alama za mpaka umefanyika. Vilevile, ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa alama za katikati za mpaka umefanyika. Maandalizi ya kuweka alama za mpaka yamefanyika kuititia kikao cha Makatibu Wakuu wanaohusika na mipaka ya Tanzania na Uganda kilichofanyika tarehe 27-30 Aprili, 2019 mjini Bukoba. Aidha, mpaka ndani ya maji katika Ziwa Victoria kati ya Tanzania na Uganda wenyе urefu wa kilomita **246** haujaanza kuimarishwa.

**61.** *Mheshimiwa Spika*; upande wa mpaka wa Tanzania na Kenya wenyе urefu wa kilomita **819.7** kati ya hizo kilomita **760** za nchi kavu na **59.7** ziko ndani ya maji. Uimarishaji wa mpaka huo unajumuisha utengenezaji wa ramani za msingi,

kupima kipande cha mpaka na kusimika alama za ardhini. Jumla ya kilomita **172** kati ya **760** za nchi kavu ziliimarishwa kufikia Juni 2018. Kwa mwaka wa fedha 2018/19, kufikia tarehe 15 Mei, 2019 jumla ya kilomita **128** kutoka Ziwa Natron hadi Namanga zimekaguliwa kufikia tarehe 15 Mei, 2019 ili kubaini mahitaji halisi.

**62. *Mheshimiwa Spika;*** urefu wa mpaka kati ya Tanzania na Zambia ni kilometra **345** ambapo sehemu ya nchi kavu ina urefu wa kilometra **289** na ndani ya maji ina urefu wa kilometra **56**. Maandalizi yanaendelea kwa ajili ya uimarishaji wa mpaka huu kwa makubaliano na Serikali ya Zambia ifikapo Juni 2019. Aidha, Serikali ya Tanzania inaendelea kuwasiliana na Serikali za nchi za Zambia, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo namna ya kuimarisha mpaka ndani ya Ziwa Tanganyika.

### **Upimaji wa Viwanja na Mashamba**

**63. *Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2018/19, Wizara yangu iliahidi kuidhinisha ramani za upimaji zenye viwanja **200,000** na mashamba **400** pamoja na kufufua mipaka ya viwanja na mashamba **500** yenye migogoro ya mipaka. Hadi tarehe 15 Mei, 2019, jumla ya viwanja **261,387** na mashamba **3,291** yamepimwa na kuidhinishwa katika halmashauri mbalimbali. Aidha, jumla ya viwanja **70** vyenye migogoro vimefuliwa mipaka. Katika mwaka wa fedha 2019/20 Wizara yangu imepanga kuidhinisha ramani za upimaji wa viwanja na mashamba **200,000** pamoja na kutatua migogoro **50** ya mipaka ya vijiji, hifadhi na wilaya.

**64. *Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2018/19 Wizara yangu iliahidi kusimika na kupima alama za msingi za upimaji (*control points*) **500**. Hadi tarehe 15 Mei, 2019, Wizara yangu imesimika na kupima alama za msingi **150** kwa kutumia mfumo mpya wa upimaji ardhi nchini unaojulikana kama TAREF11 katika mikoa ya Mwanza (Ilemela, Nyamagana, Sengerema, Buchosa, Magu), Geita (Nyang'wale, Chato, Bukombe, Mbogwe), Kagera

(Biharamulo, Muleba, Bukoba Mjini, Bukoba Vijijiini, Misenyi, Karagwe, Kyerwa, Ngara), Shinyanga (Kahama mjini, Msalala, Ushetu, Shinyanga Vijijiini na Shinyanga mjini), Dodoma (Dodoma Jiji), Morogoro (Manispaa), Kilimanjaro (Manispaa ya Moshi) na Arusha (Arusha Jiji) (**Ramani Na.1**). Katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara inatarajia kusimika na kupima alama za msingi za upimaji **150** za nyongeza.

### **Upimaji wa Ardhi Chini ya Maji**

**65.** *Mheshimiwa Spika*; katika mwaka wa fedha 2018/19 Wizara yangu iliahidi kukamilisha uandaji wa ramani elekezi (navigation charts) za upimaji uliofanyika katika bandari za Wete na Pemba. Hadi tarehe 15 Mei 2019, ramani za Wete na Pemba zimeandaliwa na zinasubiri kukamilishwa katika taratibu za kisheria. Aidha, maandalizi ya kupima bandari ya Mtwara yanaendelea.

### **5.3 UPANGAJI NA UENDELEZAJI WA MIJI NA MAKAZI**

**66.** *Mheshimiwa Spika*; upangaji na uendelezaji wa miji na makazi unalenga kuwa na makazi yaliyopangwa, kuhifadhi mazingira, kupunguza ukinzani wa matumizi ya ardhi na kutoa uhakika wa uwekezaji katika ardhi. Majukumu hayo yamekuwa yakitekelezwa kwa mujibu wa sera, sheria, kanuni na miongozo mbalimbali ya uendelezaji wa miji na vijiji nchini.

**67.** *Mheshimiwa Spika*; Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji imetangaza jumla ya maeneo **455** kuwa maeneo ya mipangomiji. Aidha, maeneo hayo yamepandishwa kutoka hadhi ya vijiji na kuwa maeneo ya mipangomiji. Kutangazwa kwa maeneo hayo kunaziwezesha Mamlaka za Upangaji ambazo ni Halmashauri za Majiji, Manispaa, Miji na Wilaya kuyapanga kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za Mipango Miji na hivyo, kudhibiti ujenzi holela. Aidha, maeneo hayo ya mijini yanatakiwa kupangwa kwa makini kuwezesha wananchi kumilikishwa ardhi na kupatiwa hati miliki.

## Mipango Kabambe ya Uendelezaji Miji

**68.** *Mheshimiwa Spika*; katika mwaka wa fedha 2018/19, Wizara iliahidi kushirikiana na Halmashauri mbalimbali nchini kukamilisha Mipango Kabambe **12** ifikapo mwezi Juni 2019. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Mipango Kabambe **11** imekamilika. Mipango hiyo ni ya miji ya Songea, Tunduma, Bariadi, Tabora, Babati, Morogoro, Sumbawanga, Kigoma/Ujiji, Geita, Njombe na Dodoma (**Jedwali Na. 10**).

**69.** *Mheshimiwa Spika*; Katika mwaka wa fedha 2018/19, Wizara yangu imekuwa ikisimamia kwa karibu mapitio ya Mpango Kababmbe wa Jiji la Dodoma kama makao makuu ya Serikali na utayarishaji wa mpango kina wa mji wa Serikali. Hadi Kufikia Novemba 2018 Mpango kina wa Mji wa Serikali ulikuwa umekamilika na kuwezesha ujenzi na uhamiaji wa Ofisi za Serikali katika eneo la Mtumba. Rasimu ya kwanza ya mapitio ya Mpango Kambbambe ilikamilika mwezi Januari 2019 na kupitiwa na vikao mbalimbali vya Serikali na wadau. Aidha rasimu ya pili imekamilika mwezi Aprili 2019 kwa ajili ya kupitishwa kwenye Mamlaka ya Upangaji na hatimaye kuidhinishwa na Serikali.

**70.** *Mheshimiwa Spika*; katika utekelezaji wa Mipango Kabambe iliyoidhinishwa, shughuli mbalimbali zimefanyika ikiwemo urasimishaji wa makazi, uandaaji wa mipangokina, ujenzi wa huduma muhimu za kijamii na kiuchumi na utengaji wa maeneo kwa ajili ya viwanda na matumizi mengine. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2019 jumla ya ekari **280,654.55** zilitengwa kwenye miji **24** inayoandalisha mipango kabambe kwa ajili ya ujenzi wa viwanda (**Jedwali Na.11**). **Naendelea kutoa wito kwa mamlaka zote za upangaji nchini kulipatia kipaumbele suala la uandaaji wa mipango kabambe kwa kutenga fedha katika bajeti zao ili kuwezesha uandaaji.** Aidha, Mamlaka za Upangaji zizingatie mwongozo uliotolewa na Wizara wa kutenga maeneo kwa ajili ya uwekezaji na ujenzi wa viwanda.

## **Usanifu na Uendelezaji Miji**

**71.** *Mheshimiwa Spika*; katika mwaka wa fedha wa 2018/19, Wizara iliahidi kupokea, kukagua na kuidhinisha michoro ya mipangomiji **2,000** kutoka Mamlaka za Upangaji nchini. Hadi kufikia tarehe 15 Mei 2019, michoro **1,942** ya Mipangomiji ilipokelewa na kukaguliwa. Kati ya hiyo, michoro **1,722** yenye jumla ya viwanja **620,720** iliidhinishwa na michoro **220** ilirudishwa kwenye Mamlaka za Upangaji kwa ajili ya kufanyiwa marekebisho. Katika mwaka wa fedha 2019/20 Wizara yangu inatarajia kukagua na kuidhinisha michoro ya mipangomiji **2,000** kutoka kanda nane (**08**).

**72.** *Mheshimiwa Spika*; kuititia Mipango Kabambe, Wizara imewezesha utayarishaji wa mipango saba (**07**) ya uendelezaji upya wa Maeneo ya Kati ya Manispaa za Kigoma/Ujiji, Songea, Morogoro, Tabora, na Shinyanga na miji ya Geita na Bariadi. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Manispaa ya llala imekamilisha mapitio ya mipango ya uendelezaji upya wa maeneo mawili (**02**) ya Katikati ya Jiji la Dar es Salaam (*Central Business District - CBD*) na eneo la Upanga. Katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara yangu itafuatilia na kutathmini utekelezaji wa Mipango Kabambe na Mipango Kina katika kanda tatu (**03**) za Kaskazini, Ziwa na Nyanda za Juu Kusini. Aidha, kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji, Wizara itakamilisha Mipango Kabambe sita (**06**) ya Moshi, Mbeya, Bukoba, Mafinga, Kahama na Handeni.

**Jedwali Na.**

## **Urasimishaji Makazi Mijini**

**73.** *Mheshimiwa Spika*; katika mwaka wa fedha 2018/19, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji iliahidi kurasimisha makazi mijini katika halmashauri mbalimbali. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2019, urasimishaji makazi wenyе jumla ya viwanja **626,920** ulitekelezwa katika halmashauri mbalimbali (**Jedwali Na. 12**). Aidha, kwa mwaka 2019/20 Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji itaendelea na zoezi la urasimishaji katika halmashauri katika kanda zote tisa (**9**)

ambapo takriban viwanja **600,000** vitatambuliwa na kurasimishwa katika halmashauri mbalimbali nchini.

### **Usimamizi na Udhibiti wa Uendelezaji Miji**

**74.** *Mheshimiwa Spika*; katika mwaka wa fedha 2018/19 Wizara iliahidi kukagua na kuidhinisha maombi **300** ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi kutoka Kanda nane (8). Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2019, Wizara ilipokea jumla ya maombi **374** ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi na kati ya hayo maombi **271** yaliidhinishwa na maombi **103** yalikataliwa kutokana na kutokidhi vigezo na yalirejeshwa kwa mamlaka husika. Katika mwaka wa fedha 2019/20 Wizara itaendelea kuratibu uidhinishaji wa maombi **300** ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi.

### **Upangaji wa Makazi Vijijini**

**75.** *Mheshimiwa Spika*; katika mwaka wa fedha 2018/19 Wizara iliahidi kuwezesha Mamlaka za Upangaji ili ziweze kuandaa mipangokina ya makazi vijijini pamoja na vitovu vya biashara. Katika kutekeleza hilo Wizara imezijenega uwezo Timu za kitalaam za usimamizi wa matumizi ya ardhi za Wilaya za Kilwa, Lindi, Masasi, Nanyumbu, Muheza, Kilindi, Chamwino, Bahi, Morogoro na Rufiji. Aidha, mipangokina ya matumizi ya ardhi ya makazi katika vijiji **90** katika Wilaya za Kilombero, Malinyi na Ulanga mkoani Morogoro na Wilaya ya Iringa mkoani Iringa imekamilika ambapo jumla ya viwanja **121,810** vimepangwa. Katika mwaka wa fedha 2019/20 Wizara itaendelea kuandaa mipangokina ya makazi vijijini katika halmashauri mbalimbali nchini.

### **Uratibu Ujenzi wa Nyumba Bora**

**76.** *Mheshimiwa Spika*; Wizara imeendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji kwa kurahisisha upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya upatikanaji wa mikopo ya nyumba kwa kushirikiana na mamlaka zingine ikiwemo Benki Kuu ya Tanzania. Aidha, Wizara yangu imeendelea kuhimiza Shirika la Nyumba la Taifa, Taasisi za Serikali, Sekta binafsi na wadau

wengine kuongeza kasi ya uwekezaji katika sekta ya nyumba ili kupunguza uhaba wa nyumba za gharama nafuu.

**77. *Mheshimiwa Spika***; katika mwaka wa fedha 2018/19, Wizara yangu iliahidi kuendelea kukusanya taarifa za waendelezaji milki na kujenga kanzidata ya Waendelezaji Milki nchini. Hadi kufikia tarehe 15 Mei 2019, taarifa za waendelezaji na wasimamiaji milki **138** ambao wamejenga jumla ya nyumba **26,408** zimeingizwa katika kanzidata. Aidha, Vyama vya Ushirika wa Nyumba **34** vilivyo hai vimejenga nyumba **1,056** katika Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Morogoro, Iringa, Kagera, Mwanza, Mara na Shinyanga. Katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara yangu itaendelea kuboresha taarifa za nyumba katika kanzidata ya nyumba ikiwa ni pamoja na kuhamasisha uundwaji zaidi wa vyama vya ushirika wa nyumba kwa kuwa kuna fursa nyingi za teknolojia rahisi na upatikanaji mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu.

### **Huduma ya Mikopo ya Nyumba**

**78. *Mheshimiwa Spika***; Wizara yangu inaendelea kufuatilia utekelezaji wa Sheria ya Mikopo ya Nyumba ambayo iliwezesha upatikanaji wa mitaji na kuongezeka kwa Mabenki na Taasisi za fedha zinazotoa mikopo ya nyumba. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa jumla ya mabenki na taasisi za fedha **32** nchini zimetoa mikopo ya nyumba kwa wananchi **4,989** yenye thamani ya shilingi bilioni **421.09 (Jedwali Na. 13A)**. Aidha, masharti ya mikopo ya nyumba yameendelea kulegezwa kwa kuwa viwango vya riba vimepungua kutoka asilimia **21** kwa mwaka 2017 hadi asilimia **13** mpaka **18** kwa mwaka 2019. Wizara yangu inaendelea kufanya mazungumzo na Benki Kuu ya Tanzania, Benki za Biashara na Taasisi za Fedha ili kushusha viwango hivyo zaidi na kuwezesha wananchi kumiliki nyumba.

**79. *Mheshimiwa Spika***; kupitia Mfuko wa Mikopo Midogomidogo ya Nyumba (*Housing Microfinance Fund*) jumla ya Taasisi sita **(06)** zimetoa mikopo midogomidogo ya nyumba yenye thamani ya shilingi bilioni **17.87** kwa wananchi

**1,467** wa kipato cha chini (**Jedwali Na. 13B**). Taasisi zilizotoa mikopo hiyo ni DCB Commercial Bank shilingi bilioni **3**, Yetu Microfinance Bank Plc shilingi bilioni **3.5**, EFC Tanzania Microfinance shilingi bilioni **4**, MUCOBA Bank Plc shilingi bilioni **2** na Mkombozi Commercial Bank shilingi bilioni **2.37** na Maendeleo Bank shilingi bilioni **3**. Kiwango cha riba inayotozwa kwa mikopo hii kimeshuka kutoka asilimia **10** hadi asilimia saba nukta tano (**7.5%**) na pia muda wa kurejesha mikopo hiyo umeongezeka kutoka miaka mitano (5) hadi miaka kumi (10). **Natoa wito kwa wananchi hususan wa kipato cha chini kutumia fursa hii ya kukopa toka kwenye taasisi hizi ili waweze kujenga au kuboresha makazi yao.**

#### **Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa Watumishi wa Serikali**

**80.** *Mheshimiwa Spika*; katika mwaka wa fedha 2018/19, Wizara yangu iliahidi kuendelea kusimamia mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa Watumishi wa Serikali ikiwa ni pamoa na kupokea na kushughulikia maombi mapya na kukusanya marejesho kulingana na taratibu za mfuko. Hadi tarehe 15 Mei, 2019 Wizara yangu ilipokea na kuchambua maombi mapya ya mikopo ya nyumba ya Watumishi **106** ambayo yatahitaji shilingi bilioni **1.74**. Aidha, marejesho ya mikopo kiasi cha shilingi milioni **309.73** yalikusanywa hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2019 na hivyo, kufanya mfuko kuwa na jumla ya shilingi bilioni **4.57**. Katika mwaka wa fedha 2019/20 Serikali itaimarisha Mfuko huu na kuangalia uwezekano wa kuongeza kiasi cha mkopo kinachotolewa sasa cha shilingi milioni **20** hadi shilingi milioni **40** ili kiasi hiki kiweze kukidhi ongezeko la gharama za ujenzi wa nyumba kwa sasa na pia kufikisha huduma ya mikopo kwa watumishi wengi zaidi.

#### **Ushirikiano na Taasisi Mbalimbali Katika Uendelezaji wa Makazi**

**81.** *Mheshimiwa Spika*; Wizara yangu imeendelea kuratibu ushirikiano na taasisi za kimataifa katika masuala ya makazi. Katika mwaka wa fedha 2018/19 Wizara iliratibu

na kushiriki katika maadhimisho ya siku ya makazi duniani iliyofanyika Dodoma. Pia ilishiriki katika mukutano mkuu wa 37 wa *Shelter Afrique* uliofanyika Jijini Nairobi Kenya ambapo Tanzania iliteuliwa kuwa Mwenyekiti wa taasisi hiyo. Aidha, Tanzania ilishiriki katika Mkutano Mkuu wa Pili wa Mawaziri wenye dhamana ya Nyumba na Makazi uliofanyika Dakar, Senegal Oktoba, 2018 ambapo uliweka mkakati wa nchi za Afrika kukabiliana na ukosefu wa nyumba bora ikiwa ni utekelezaji wa Agenda mpya ya Makazi duniani. Katika mwaka wa fedha 2019/20 Wizara itaendelea kusimamia na kuratibu ushirikiano huu.

### *Malengo Endelevu ya Milenia 2030*

**82. *Mheshimiwa Spika:*** Malengo Endelevu ya Milenia 2030 (SDGs) pamoja na mambo mengine, lengo Na. **11** (SDG 11) linalenga kuwa na miji na makazi ya binadamu ambayo ni jumuishi, salama, fanisi na endelevu ifikapo mwaka 2030. Aidha, tathmini iliyofanyika Mei, 2018 kuhusiana na utekelezaji wa malengo hayo inaonesha kuwepo mafanikio kadhaa pamoja na changamoto zake katika nchi mbalimbali. Kwa upande wa Tanzania, tathmini inaonesha kuwepo mafanikio katika nyanja za uimarishaji wa miundombinu mijini ikiwemo barabara, umeme, maji na huduma zingine ili miji yetu iwe endelevu na kuimariika kwa ustawi wa watu. Pia inaonesha kuwa miji inaendelea kuboreshwa kwa kupanga, kupima na kurasimisha makazi na hatimaye kutoa hatimilliki kwa wamiliki wa ardhi.

## **5.4 MIRADI YA MAENDELEO**

### **Miradi ya Wizara**

**83. *Mheshimiwa Spika:*** katika mwaka wa fedha 2018/19, Wizara ilipanga kutekeleza miradi mbalimbali ambapo hadi kufikia 15 Mei, 2019, ilitekeleza mradi wa Upangaji, Upimaji na Umilikishaji Ardhi kwa kutumia jumla ya shilingi bilioni **8**. Kati ya fedha hizo, shilingi milioni **694.9** zimetumika kuandaa mpango kabambe wa Jiji la Dodoma, shilingi bilioni **7.3** zimetumika kwa ajili ya kupanga, kupima na

kumilikisha ardhi katika halmashauri mbalimbali nchini. Kati ya fedha hizo, Wizara imeshataoa shilingi bilioni **6.29** kwa halmashauri **24** zilizokidhi vigezo (**Jedwali Na.14**) kwa ajili ya kupanga, kupima na kumilikishaa vipande vya ardhi **40,241**. Wizara itaendelea kuzipatia halmashauri zingine fedha kadri zitakavyopatikana na kwa kukidhi vigezo.

**84. *Mheshimiwa Spika***; katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara itaendelea kutekeleza mradi wa upangaji, upimaji na umilikishaji ardhi ikiwemo kuimarisha Mfuko wa Fidia; kuhuisha ramani za msingi katika Jiji la Dodoma; kupima na kuidhinisha viwanja na mashamba; na uandaaji wa mpango wa maendeleo wa ukanda wa Reli ya *Standard Gauge* na Bomba la Mafuta la Afrika Mashariki.

**85. *Mheshimiwa Spika***; Wizara illiendelea kutekeleza Programu ya Kuwezesha Umilikishaji wa Ardhi (*Land Tenure Support Programme*) katika vijiji vya wilaya za Kilombero, Ulanga na Malinyi mkoani Morogoro ambayo muda wa utekelezaji unaisha mwezi Septemba 2019. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2019 Wizara ilipima vipande vya ardhi na kuandaa Hati za Hakimiliki ya Kimila (CCROs) katika vijiji **109** vya Wilaya za Kilombero (**56**), Ulanga (**37**) na Malinyi (**16**). Jumla ya vipande vya ardhi **178,980** vimehakikiwa na kupimwa kwa ajili ya kuandaa Hati za Hakimiliki ya Kimila sawa na asilimia **224** ya lengo katika Wilaya za Kilombero (**61,530**), Ulanga (**65,143**) na Malinyi (**52,307**). Aidha, jumla ya Hati za Hakimiliki ya Kimila **118,534** zimeandaliwa katika Wilaya za Kilombero (**56,680**), Ulanga (**37,353**) na Malinyi (**24,501**). Vilevile, jumla ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji **79** imeandaliwa sawa na asilimia **214** ya lengo katika Wilaya ya Kilombero (**41**), Ulanga (**23**) na Malinyi (**15**) na pia jumla ya Mipango Kina ya Makazi ya Vijiji **66** imeandaliwa katika Wilaya ya Kilombero (**28**), Ulanga (**20**) na Malinyi (**18**). Halikadhalika, Wizara inaendelea na ujenzi wa ofisi za ardhi za Wilaya za Kilombero, Ulanga na Malinyi ambapo ujenzi umekamilika kwa takriban asilimia **50** na vijiji **44** vimewezeshwa kukamilisha ujenzi wa masjala za ardhi katika Wilaya za Kilombero (**18**), Ulanga (**14**) na Malinyi (**12**).

**86.** *Mheshimiwa Spika*; katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo itatekeleza kazi zilizobaki za Programu ya Kuwezesha Umilikishaji Ardhi mkoani Morogoro ikiwemo kuhakiki vipande vyta ardhi na kuandaa Hati za Hakimiliki ya Kimila (CCROs) **60,000** katika wilaya za Kilombero, Ulanga na Malinyi na kuandaa Mipango Kabambe ya Miji ya Ifakara, Mahenge na Malinyi. Aidha, kwa kuzingatia mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa mradi huu, Wizara inaandaa programu ya utekelezaji katika maeneo mengine nchini. Nawashukuru wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa kutembelea na kutupa moyo kwenye mradi huu.

#### *Programu ya Kuimarisha Milki za Ardhi*

**87.** *Mheshimiwa Spika*; katika mwaka wa fedha 2018/19, Serikali ilipanga kukamilisha uandaaji wa Programu ya Kuimarisha Milki za Ardhi (Land Tenure Improvement Project) chini ya ufadhilli wa Benki ya Dunia. Ukamilishaji wa makubaliano ya utekelezaji wa Programu hii yapo katika hatua za mwisho. Ni matumaini kuwa utekelezaji wa programu hii utakuwa ni nyenzo muhimu katika kuleta mageuzi katika sekta ya ardhi ikiwemo kuondoa na kudhibiti migogoro ya matumizi ya ardhi mionganoni mwa watumiaji, kutumia ardhi kama mtaji hai, kuchochaea uwekezaji, kupanua wigo wa mapato ya Serikali na kuhakikisha kuwa ardhi inatumika kwa tija. Maandalizi ya mpango huu yatakamilishwa mwaka ujao wa fedha 2019/20 na utekelezaji unatarajiwu kuanza kwa bajeti ya mwaka 2020/21.

#### **Mradi wa Kuboresha Miundombinu ya Upimaji na Ramani**

**88.** *Mheshimiwa Spika*; Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa Korea kuititia *Exim* Benki ya Korea inaandaa mradi wa kuboresha miundombinu ya upimaji na ramani za msingi kwa njia ya kidigitali. Mradi huu utahusisha utayarishaji wa ramani za msingi pamoja na kujenga vituo vyta kuwezesha upimaji ardhi katika baadhi ya miji nchini.

## Miradi ya Kitaifa

89. ***Mheshimiwa Spika***; katika mwaka wa fedha 2018/19, Wizara yangu iliahidi kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya ujenzi wa miundombinu ya kitaifa hususan Ufuaji wa Umeme katika mto Rufiji (*Rufiji Hydropower Project*), Bomba la Mafuta (*East African Crude Oil Pipeline*) kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani-Tanga na Reli ya Kisasa (*Standard Gauge Railway*). Katika mradi wa ufuaji umeme katika mto Rufiji, Wizara imeshiriki katika upimaji wa eneo la kujenga mtambo wa kuzalisha umeme lenye ukubwa wa hekta **1,402** (ekari **3,464.4**), eneo litakalotumika kwa ujenzi wa karakana lenye ukubwa wa hekta **4,711** (ekari **11,641.1**) eneo linalokinga sehemu ya mito Rufiji na Ruaha inayoingia katika eneo la kuzalisha umeme lenye ukubwa wa takriban hekta **298,000** (ekari **736,374.04**).

90. ***Mheshimiwa Spika***; katika uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi kwa ajili ya uendelezaji wa eneo la ukanda wa Reli ya Kisasa kuanzia Dar-es-Salaam hadi Isaka, Shinyanga na eneo la ukanda wa Bomba la Mafuta kutoka Mtukula hadi Chongoleani- Tanga Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi imeunda timu shirikishi za uandaaji wa Mipango ya Ukanda wa Reli ya Kisasa na Bomba la Mafuta. Aidha, mikutano miwili (**02**) ya kila timu imefanyika kwa ajili ya maandalizi ya kazi hizo na rasimu za awali za mipango ya matumizi ya ardhi kwa ajili ya uendelezaji wa maeneo ya kanda za Reli ya Kisasa na Bomba la Mafuta zimeandaliwa.

91. ***Mheshimiwa Spika***; kwa upande wa mradi wa Reli ya kisasa Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Reli Tanzania inafanya zoezi la uthamini katika njia ya Reli kutoka Mvomero mkoani Morogoro hadi Makutupora, Manyoni mkoani Singida yenye urefu wa kilometra **336** kwa ajili ya ulipaji wa fidia. Pamoja na hayo, Wizara pia inaandaa *Corridor Development Plan* ya Bomba la Mafuta na Reli ya Kisasa kutoka Dar es Salaam hadi Kituo cha Makutupora Singida. Mpango huo utaainisha matumizi ya ardhi katika miji na vijiji vitakavyopitiwa na mradi huu. Aidha, Wizara imeandaa

rasimu ya awali ya mpango wa matumizi ya ardhi kwa ajili ya uendelezaji wa eneo la ukanda wa Reli ya Kisasa kutoka Dar-es-Salaam hadi Isaka, Shinyanga.

**92. *Mheshimiwa Spika***; katika mwaka wa fedha 2018/19, Wizara imeendelea kushiriki katika shughuli za mradi wa ujenzi wa Bomba la Mafuta Afrika Mashariki kutoka Hoima, Uganda mpaka Chongoleani-Tanga. Wizara imekamilisha taratibu za utwaaji wa maeneo **17** ya kipaumbele kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu wezeshi ya mradi. Maeneo hayo yapo katika Wilaya ya Nzega, Igunga, Kiteto, Misenyi, Muleba, Chato, Bukombe, Singida, Kondoa, Kilindi, Handeni na Muheza. Aidha, Wizara imeshiriki katika upangaji, upimaji na usimamizi wa uthamini kwa ajili ya utwaaji wa maeneo ya vipaumbele ambayo yanategemea kumilikishwa kwa Shirika la Maendeleo ya Petroli. Baada ya kukamilisha ulipaji wa fidia katika maeneo ya kipaumbele, Wizara itaendelea na taratibu za upangaji, upimaji na uthamini wa maeneo ya mkuza. Mpango wa matumizi ya ardhi kwenye vijiji vinavyopitiwa na bomba la mafuta umezinduliwa rasmi tarehe 25 Mei, 2019. Katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara itazinduwa mpango kama huo kwenye vijiji na wilaya zinazopitiwa na reli (SGR).

**93. *Mheshimiwa Spika***; Wizara inashauriana na wamiliki wa Bomba la Mafuta na Shirika la Reli Tanzania kuhusu mpango wa kupima njia ya Bomba la Mafuta na Reli ya Kisasa. Vilevile, Wizara imeshiriki katika utafiti wa udongo ili kujua mahali sahihi pa kuitisha bomba hilo kulingana na uimara wa udongo kwa kuzingatia mahitaji ya mradi na pia kuangalia njia sahihi ya kuitisha bomba hilo.

## **5.5 USIMAMIZI WA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA**

**94. *Mheshimiwa Spika***; Wizara yangu inaratibu na kusimamia shughuli za taasisi za: Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi; Shirika la Nyumba la Taifa; Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba na Vifaa vya Ujenzi na Vyuo vya Ardhi vya Tabora na Morogoro.

## **Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi**

**95.** *Mheshimiwa Spika*; Serikali ilianzisha Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi kwa Sheria ya Bunge Na. 3 ya Mwaka 1984 na baadaye kurejewa na Sheria ya Upangaji wa Matumizi ya Ardhi Na. 6 ya mwaka 2007 kwa madhumuni ya kuandaa Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi na kuratibu utekelezaji wake. Mipango ya matumizi bora ya ardhi nchini inasaidia: kuainisha matumizi mbalimbali ya ardhi; kuwezesha ardhi kutumika kwa ufanisi na tija; kupunguza migogoro ya matumizi ya ardhi; na kutoa mwelekeo kwa mamlaka za upangaji katika kuandaa, kutekeleza na kusimamia mipango ya matumizi ya ardhi.

**96.** *Mheshimiwa Spika*; katika mwaka wa fedha 2018/19, Wizara yangu kuititia Tume ilipanga kufanya mapitio ya Programu za Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi (2013 – 2033). Tayari Tume imeanza kukusanya taarifa za kisekta kwa ajili ya kuhuisha Programu za Utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi. Kwa mwaka 2019/20, Wizara yangu kuititia Tume itaendelea kukamilisha mapitio ya Mpango huo.

## ***Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Wilaya na Vijiji***

**97.** *Mheshimiwa Spika*; katika mwaka wa fedha 2018/19, Tume ilipanga kuratibu tathmini ya uharibifu wa mazingira katika wilaya tatu (3) za Mlele, Urambo (Ulyankulu) na Tanganyika zilizokuwa na makambi ya wakimbizi katika ukanda wa magharibi mwa nchi, kutoa mafunzo kwa Timu za Usimamizi wa Matumizi ya Ardhi katika wilaya sita (6) na pia kuwezesha upangaji wa matumizi ya ardhi katika wilaya sita (6) za Geita, Nyang'hwale, Misenyi, Urambo (Ulyankulu), Misenyi na Tanganyika na vijiji **250** katika ukanda wa njia ya Bomba la Mafuta kwa upande wa Tanzania.

**98.** *Mheshimiwa Spika*; tathmini ya hali ya uharibifu wa mazingira katika Kanda ya Magharibi zilipokuwepo kambi za wakimbizi imeanza kufanyika mwezi Aprili, 2019 katika Wilaya za Mlele, Urambo (Ulyankulu) na Tanganyika. Kazi hii inatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2019.

**99.** *Mheshimiwa Spika*; Tume kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira imeendelea kujenga uwezo kwa Timu za Usimamizi wa Matumizi ya Ardhi za Wilaya (*PLUM Teams*) na Vijiji (*VLUM Teams*) na kuwezesha upangaji wa matumizi ya ardhi ya vijiji **14** katika Wilaya tatu (**3**) za Kondoaa, Nzega na Mkalama ambazo zinapitiwa na Mradi wa Bomba la Mafuta (EACOP). Katika kwa mwaka wa fedha 2019/20 Tume itaendelea kuwezesha uandaaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji katika Wilaya na vijiji vinavyopitiwa na Mradi wa Bomba la Mafuta ambapo jumla ya vijiji **236** vinatarajiwa kuandaliwa mipango hiyo.

**100.** *Mheshimiwa Spika*; hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2019, Tume ilitoa elimu kwa umma kuhusu sheria, miongozo na upangaji wa matumizi ya ardhi nchini kupitia mikutano ya vijiji katika vijiji **135**; warsha katika Chuo Kikuu Ardhi na Chuo cha Ardhi Morogoro; vipindi vya luninga (vipindi **3**) na radio (vipindi 3); na machapisho **76** kupitia tovuti ya Tume ([www.nlupc.go.tz](http://www.nlupc.go.tz)), magazeti na mitando ya kijamii.

**101.** *Mheshimiwa Spika*; vilevile katika mwaka wa fedha 2018/19, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi iliypanga kuwezesha upangaji wa matumizi ya ardhi ya vijiji **392** vinavyopakana na Hifadhi za Taifa kote nchini. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2019, Tume imewezesha upangaji wa matumizi ya ardhi ya vijiji **43** katika Wilaya za Bariadi, Bunda, Karatu, Kondoaa na Simanjiro kwa kushirikiana na Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (TANAPA). Uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi katika maeneo kuzunguka Hifadhi za Taifa utaendelea kwa mwaka wa fedha 2019/20 ambapo jumla ya vijiji **95** kati ya **349** vilivyobaki vinatarajiwa kuandaliwa mipango hiyo.

**102.** *Mheshimiwa Spika*; hadi kufikia tarehe 15 Mei 2019, Tume kwa kushirikiana na Wakala wa Taifa wa Huduma za Misitu (TFS) iliwezesha upangaji wa matumizi ya ardhi katika vijiji **37** kati ya **95** vinavyopakana na hifadhi za misitu katika Wilaya za Lindi, Kilwa, Nanyumbu, Muheza, Kilindi, Bahi, Chamwino, Mbeya Vijiji, Mbarali na Masasi. Katika mwaka

wa fedha 2019/20 jumla ya vijiji **58** vilivyobaki vitaandaliwa mipango hiyo.

**103.** *Mheshimiwa Spika*; vilevile Tume kwa kushirikiana na wadau wengine kama vile Asasi za Kiraia na Mashirika yasiyo ya Kiserikali imewezesha upangaji wa matumizi ya ardhi ya vijiji **52** katika Wilaya **11** za Ngorongoro, Makete, Ludewa, Mbinga, Nyasa, Mkinga, Korogwe, Mufindi, Kondoa, Uvinza na Kyela.

**104.** *Mheshimiwa Spika*; kuanzia mwaka wa fedha 2018/19 uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi katika ngazi za vijiji tayari umeanza kuzingatia utengaji wa maeneo kwa ajili ya ujenzi na uendelezaji wa viwanda nchini. Katika vijiji **258** vilivyoandalila mipango ya matumizi ya ardhi (**Jedwali Na. 15**) katika mwaka wa fedha 2018/19, jumla ya hekta **282,805.45** zimetengwa kwa ajili ya kilimo, hekta **201,091.60** kwa ajili ya malisho ya mifugo, hekta **35,262.65** kwa ajili ya misitu ya vijiji, hekta **26,136.01** kwa ajili ya hifadhi za misitu, hekta **30,721.92** kwa ajili ya hifadhi ya vyanzo vya maji, hekta **43,848.65** kwa ajili ya maeneo ya usimamizi wa wanyamapori.

### **Shirika la Nyumba la Taifa**

**105.** *Mheshimiwa Spika*, Shirika la Nyumba la Taifa lilianzishwa kwa Sheria Na. 2 ya mwaka 1990 kama ilivyorekebishwa mwaka 2005. Jukumu la msingi la ni ujenzi wa nyumba za kuuza na kupangisha ikijumuisha nyumba za gharama nafuu.

**106.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2018/19, Wizara iliahidi kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa nyumba katika eneo la Iyumbu na kukamilisha taratibu za kupata ardhi ya kujenga nyumba Jijini Dodoma. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba, Shirika linaendelea na ujenzi wa nyumba **149** pamoja na maduka **2** makubwa ya kibiashara (zilizoko katika hatua mbalimbali za ujenzi) katika eneo la Iyumbu. Katika mwaka wa fedha 2017/18, Shirika likamilisha ujenzi wa awamu ya kwanza ya nyumba **151** kat

ya nyumba **300**. Mauzo ya nyumba hizi yanaendelea kwa wananchi wa kawaida na watumishi wa Serikali. Sambamba na utekelezaji huu, Shirika linafanya maandalizi ya kuanza upimaji wa eneo lililobaki lenye ukubwa wa ekari **188**. Shirika linaendelea na taratibu za kupata ardhi zaidi kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za makazi na maeneo ya biashara Jijini Dodoma. Aidha, katika mwaka wa fedha 2019/20, Shirika limepanga kuanza ujenzi wa nyumba **1,000** za gharama nafuu katika eneo la lyumbu na sehemu nyingine Jijini Dodoma.

**107.** *Mheshimiwa Spika*, vilevile, Wizara iliahidi kuendelea na ukamilishaji wa miradi iliyopo katika mikoa mbalimbali pamoja na kujenga nyumba za gharama nafuu. Kwa sasa, Shirika lina miradi **66** ambayo imeongezeka kutoka miradi **57** mwaka 2017/18. Miradi **9** ilioongezeka ni ya ujenzi wa ofisi mbalimbali za wizara kwenye Mji wa Serikali, Mtumba jijini Dodoma. Kati ya miradi **66**, ujenzi wa miradi **46** umekamilika ambayo ni ya nyumba za gharama nafuu, gharama ya katni na juu, majengo ya biashara na majengo ya matumizi mchanganyiko na ina jumla ya nyumba **2,709**. Kati ya miradi hiyo iliyokamilika miradi **23** ni ya nyumba za gharama nafuu yenye jumla ya nyumba **806**. Miradi **12** ni ya nyumba za makazi ya bei ya katni na juu na ina nyumba **1,112**. Miradi **9** ni ya nyumba za biashara yenye jumla ya nyumba **336** na miradi **2** ni ya nyumba za matumizi mchanganyiko yenye jumla ya nyumba **455**. Aidha, miradi **20** ipo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Shirika linaendelea na jitihada za kutafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali ili kukamilisha ujenzi wa miradi mikubwa Jijini Dar es Salaam.

**108.** *Mheshimiwa Spika*, hadi tarehe 15 Mei, 2019, Shirika limefanikiwa kuuza nyumba za makazi **152** kwa wateja wapya katika miradi ya nyumba za makazi iliyoko katika maeneo mbalimbali nchini. Hii ni sehemu ya nyumba za makazi **1,284** za kuuza ambazo zinajumuisha nyumba zilizokamilika na zinazoendelea kujengwa. Walengwa katika ujenzi huu ni wananchi pamoja na halmashauri za wilaya. Kwa upande wa maeneo ya biashara na ofisi, Shirika limefanikiwa kuuza mita za mraba **2,144** katika miradi

mbalimbali yenyé maeneo maalum ya ofisi na biashara yenyé jumla ya mita za mraba **21,495**.

**109.** *Mheshimiwa Spika*; Shirika linaendelea na mikakati endelevu ya muda mfupi na mrefu ya kuuza nyumba za makazi zilizokamilika na zinazoendelea kujengwa. Mikakati hii inajumuisha mfumo wa “**Mpangaji Mnunuzi**” (**Tenant Purchase Scheme – TP**) ili kuwawezesha wananchi wa kada mbalimbali kumiliki nyumba za makazi. Shirika linashirikiana na benki za biashara **16** ambazo zimesaini makubaliano ya kutoa Mikopo ya Mnunuzi wa Nyumba za Makazi (Mortgage Financing) kwa wananchi.

**110.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2018/19, Shirika liliahidi kuandaa mipango kabambe ya Songwe, Ruvu, Mafuru (Morogoro), Pemba Mnazi, Chato na Kibondo. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2019, Shirika limeandaa mipango kabambe ya Pemba Mnazi na Rubambangwe (Chato). Aidha, Shirika linaendelea kuandaa Mpango Kabambe wa Kwala (Ruvu) na pia kuandaa Mpango Kabambe wa mradi wa mji mpya wa Kisarawe.

**111.** *Mheshimiwa Spika*, Shirika lilipanga kukusanya shilingi bilioni **93.1** kutokana na kodi ya pango la nyumba. Hadi tarehe 15 Mei, 2019, Shirika limekusanya jumla ya shilingi bilioni **68** sawa na asilimia **73** ya lengo. Aidha, shilingi bilioni **12.6** zimekusanywa kutokana na mauzo ya nyumba na shilingi bilioni **1.1** zikiwa ni mauzo ya viwanja. Katika mwaka wa fedha 2019/20 Shirika limepanga kukusanya kodi ya pango kiasi cha shilingi bilioni **97**.

#### **Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba na Vifaa vya Ujenzi**

**112.** *Mheshimiwa Spika*; katika mwaka wa fedha 2018/19 Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba na Vifaa vya Ujenzi uliendelea kufanya tafiti mbalimbali. Mionganî mwa tafiti zilizokamilika ni pamoja na utengenezaji wa fremu za milango kwa kutumia zege, matumizi ya chokaa badala ya saruji katika ujenzi na matumizi ya vigae vya udongo vya

kuchoma kwa ajili ya kuezekea. Malighafi ya kutengeneza vifaa hivi inapatikana katika maeneo mbalimbali nchini.

**113. *Mheshimiwa Spika***; ili kuwezesha matumizi ya teknolojia ya tofali za kufungamana, Wakala umeendelea kuunda mashine ya injini yenye uwezo wa kuzalisha matofali mawili na nyingine ya kawaida inayotumia mkono. Hadi tarehe 15 Mei, 2019 Wakala imeunda jumla ya mashine **52** ambapo mashine **2** ni za kutumia injini na mashine **50** ni za kutumia mkono. Wakala imefyatua tofali za mfano zipatazo **7,000** kwa kutumia mashine hizo zilizopo Mwenge Jijini Dar es Salaam.

**114. *Mheshimiwa Spika***; katika mwaka wa fedha 2019/20 Wakala utaendelea kufanya tafiti zaidi na kutangaza matokeo ya tafiti zake kupitia redio, luninga, magazeti, semina na maonesho ya kitaifa. Aldha, Wakala utashirikiana na halmashauri nchini kuunda vikundi vya vijana ambavyo vitapatiwa mafunzo ya kutumia mashine za kutengeneza tofali na kalibu za kutengeneza vigae vya kuezeka ili wananchi wengi zaidi waweze kutumia vifaa hivyo kupunguza gharama za ujenzi na kupata nyumba bora.

**115. *Mheshimiwa Spika***; kwa kuzingatia majukumu ya Wakala na yale ya Chuo Kikuu Ardhi, Wizara imeanza taratibu za kuuhamisha Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba na Vifaa vya Ujenzi kuwa chini ya Chuo Kikuu Ardhi. Hatua hii inalenga kuongeza ufanisi na tija katika kufanya tafiti mbalimbali zinazohusiana na vifaa vya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu.

#### *Vyuo vya Ardhi Tabora na Morogoro*

**116. *Mheshimiwa Spika***; Wizara inasimamia vyuo viwili vya Ardhi vilivyopo Tabora na Morogoro ambavyo vinatoa mafunzo ya fani mbalimbali za ardhi katika ngazi ya cheti na stashahada. Fani zinazotolewa ni upangaji wa mijii na vijiji, upimaji wa ardhi, usimamizi wa ardhi, uthamini na usajili, urasimu ramani na sanaa, ubunifu na uchapishaji. Wizara imeendelea kuviimarisha vyuo hivi ili viweze kudahili

wanachuo wengi zaidi na kutoa ujuzi unaokidhi viwango vya taaluma zao. Idadi ya wanachuo waliodahiliwa imeongezeka kutoka **706** mwaka 2017/18 hadi kufikia wanachuo **1,282** mwaka 2018/19. Kati ya hao, Chuo cha Morogoro ni **271** na Tabora **1,011**.

**117.** *Mheshimiwa Spika*; katika mwaka wa fedha 2019/20 Wizara yangu itaendelea kuboresha miundombini ya vyuo hivi ili kuviwezesha kuongeza udahili wa wanachuo na kujenga mazingira wezeshi kwa wakufunzi katika kutoa mafunzo yanayokidhi viwango. Ili kukidhi mahitaji ya fani mbalimbali za ardhi, vyuo vinakamilisha mapitio ya mitaala ya mafunzo yanayotolewa katika ngazi ya cheti na stashahada za upangaji wa miji na vijiji, upimaji wa ardhi, usimamizi wa ardhi, uthamini na usajili, urasimu ramani, ubunifu na uchapishaji. Aidha, katika mapitio hayo vyuo vitaandaa mitaala kwa ajili ya kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa watendaji wa vijiji na mitaa nchini katika upangaji na usimamizi wa makazi.

**118.** *Mheshimiwa Spika*; Wizara kwa kushirikiana na vyuo itaandaa mwongozo wa upangaji wa makazi vijijini utakaowezesha utoaji wa mafunzo. Lengo la kutoa mafunzo hayo ni kuvijengea uwezo vijiji ili viweze kusimamia matumizi ya ardhi kwa ufanisi kwa kuzingatia sera, sheria na kanuni zilizopo. Mafunzo hayo yatawawezesha watendaji wa vijiji na mitaa kuwa na ujuzi na uwezo wa kutatua changamoto mbalimbali zinazotokana na matumizi ya ardhi vijijini ikiwemo migogoro ya wakulima na wafugaji. Mafunzo hayo yatakuwa ya muda mfupi yatakayowawezesha kupata ujuzi wa namna ya kuandaa na kusimamia utekelezaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji. **Natoa wito kwa Wakurugenzi wa Halmashauri zote nchini kutoa kipaumbele katika mafunzo haya kwa kutenga fedha katika bajeti zao kuwezesha watendaji wote wa vijiji kupata mafunzo hayo.**

## **5.6 UTAWALA NA RASILIMALI WATU**

**119.** *Mheshimiwa Spika*; katika kutekeleza tamko la Serikali la kuhamia Dodoma tarehe 23 Julai, 2016, Wizara

imekamilisha ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Makao Makuu ya Wizara lililoko katika Mji wa Serikali Kata ya Mtumba Jijini Dodoma na kuhamia rasmi tarehe 15 Aprili, 2019. Kwa sasa huduma za utawala na usimamizi wa ardhi zinapatikana katika ofisi hiyo.

**120. *Mheshimiwa Spika***; katika kusimamia majukumu ya sekta ya ardhi kwa ufanisi, Wizara inahitaji watumishi **1,692** wa kada mbalimbali ikilinganishwa na watumishi **945** waliopo na hivyo, kuwa na upungufu wa watumishi **747**. Mahitaji makubwa yapo katika Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya ambapo kwa sasa kuna watumishi **173** kati ya **844** wanaohitajika hivyo kuwa na upungufu wa watumishi **671**.

**121. *Mheshimiwa Spika***; katika kuimarisha Ofisi za Kanda, hadi Juni, 2018 jumla ya wataalam **56** wa kada za ardhi katika fani za upangaji, upimaji, uthamini, usimamizi ardhi na usajili wa hati walikuwa wamehamishiwa katika ofisi nane (**8**) za Kanda. Aidha, kufikia tarehe 15 Mei, 2019 jumla ya wataalam **122** wamehamishiwa kwenye ofisi za ardhi za Kanda ili kuongeza ufanisi katika utoaji huduma.

**122. *Mheshimiwa Spika***; katika utekelezaji wa Agizo la Mhe. Rais la kuwahamishia watumishi wote wa sekta ya ardhi waliopo katika Sekretarieti za Mikoa na halmashauri zote kuwa chini ya Wizara, uhakiki wa watumishi umefanyika na kubaini kuwepo watumishi **1,546 (Jedwali Na. 16)** kati ya watumishi **2,957** wanaohitajika na hivyo, kuwa na upungufu wa watumishi **1,411**. Hata hivyo, watumishi waliopo hawajapangwa kwa uwiano unaohitajika kwa kuzingatia majukumu halisi ya halmashauri husika. Katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara yangu itawapanga upya watumishi hao kwa uwiano.

### **Utawala Bora na Uwajibikaji**

**123. *Mheshimiwa Spika***; katika kuimarisha utawala bora kuhusu utoaji huduma za ardhi, Wizara yangu imeboresha utoaji huduma kwa mteja. Maboresho hayo yanalenga

kupunguza muda wa kuandaa na kutoa hati kutoka miezi mitatu (siku **90**) hadi mwezi mmoja (siku **30**) na muda wa upekuzi wa nyaraka za ardhi (official search) kutoka siku **14** hadi siku saba (**7**). Katika mwaka fedha, 2019/20 Wizara yangu itahuisha Mkataba wa Huduma kwa Wateja ili kuongeza kasi ya utoaji wa huduma kwa ufanisi sawia na maboresho ya mifumo yanayofanyika katika sekta ya ardhi.

**124. *Mheshimiwa Spika***; kuhusu maadili ya watumishi na mapambano dhidi ya rushwa, Wizara inazo Kamati za Kudhibiti Uadilifu na Kusimamia Utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu (2017-2022). Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2019, jumla ya watumishi sita (**6**) walichukuliwa hatua mbalimbali za kinidhamu na watumishi **12** walituhumiwa kwa rushwa na taarifa zao kuwasilishwa kwa mamlaka husika. Katika mwaka wa fedha 2019/20 Wizara yangu itaendelea kutekeleza mkakati wa kupambana na viashiria vya rushwa kwenye sekta ya ardhi.

**125. *Mheshimiwa Spika***; katika mwaka wa fedha 2018/19 Wizara iliahidi kuajiri watumishi kwa kadri vibali vya ajira vitakavyotolewa. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2019, Wizara imeajiri watumishi **30** wakiwemo maafisa TEHAMA **10** na Wenyeviti wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya **20**. Katika mwaka wa fedha 2019/20 Wizara inatarajia kuajiri watumishi **56** kadri vibali vitakavyokuwa vinatolewa.

### **Mafunzo kwa Watumishi**

**126. *Mheshimiwa Spika***; kuhusu mafunzo, katika mwaka wa fedha 2018/19 Wizara yangu iliahidi kuwapatia mafunzo watumishi **70**. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2019 Wizara ilitoa mafunzo mbalimbali kwa watumishi **84**. Ongezeko hili linatokana na baadhi ya watumishi kupata ufadhili kutoka nje ya nchi ikiwemo China na India kuhusu masuala ya TEHAMA, upimaji na upangaji wa ardhi. Katika mwaka wa fedha 2019/20 Wizara yangu itatoa mafunzo kwa watumishi **90** kwa kuzingatia mahitaji ya mafunzo.

## Utoaji wa Huduma kwa Wateja

**127. *Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi kupitia kituo cha huduma kwa wateja kilichopo katika Kanda ya Dar es Salaam. Kituo kimeweza kuwahudumia jumla ya wananchi **88,960** ambao ni sawa na wastani wa wateja **2,360** kwa wiki na takribani wateja **472** kwa siku mwaka 2018/19 ikilinganishwa na wastani wa wateja **442** kwa siku mwaka 2017/18. Huduma zinazotolewa na kituo hicho ni upimaji na ramani, ardhi, mipangomiji, uthamini, na usajili wa hati na nyaraka mbalimbali. Wizara yangu imeanzisha pia chumba maalum kwenye kituo hicho kwa ajili ya huduma za miamala ya kielektroniki inayotokana na mfumo wa ILMIS ambao umeanza kufanya kazi katika Manispaa za Ubungo na Kinondoni. Aidha, Wizara imetoa namba za simu **+255222121107** na **+255736777777** za huduma kwa wateja illi kuwezesha wananchi kutoa malalamiko au kero zao kuhusiana na huduma za ardhi. Dhamira ya Wizara ni kuwa na vituo vya huduma kwa wateja kwa kila ofisi ya kanda na halmashauri nchini.

## Habari na Elimu kwa Umma

**128. *Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2018/19 Wizara yangu iliahidi kuendelea kuelimisha umma kuhusu sera, sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia sekta ya ardhi. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara iliandaa na kusambaza nakala **3,000** za jarida lenye taarifa za shughuli za Wizara, nakala **2,500** za jarida kuhusu urasimishaji wa makazi, nakala **6,000** za vipeperushi (*flers*) kuhusu ulipaji kodi ya pango la ardhi na **2,207** za machapisho mengine kuhusu shughuli za sekta ya ardhi. Aidha, vipindi **85** vya televisheni na redio kuhusu shughuli za Wizara viliandaliwa na kurushwa na vituo mbalimbali. Pia elimu ilitolewa kupitia mtandao wa Wizara na mitandao ya kijamii ikiwemo *facebook, instagram, youtube* na *twitter*. Katika mwaka wa fedha 2019/20 Wizara itaendelea na utaratibu wa upashanaji habari na elimu kwa umma kuhusu masuala ya sekta ya ardhi.

## **6.0 SHUKRANI**

**129.** *Mheshimiwa Spika*; kwa niaba ya Wizara yangu, naomba kumalizia hotuba yangu kwa kuwashukuru kwa dhati Mawaziri na Makatibu Wakuu wa kisekta tulioshirikiana kufanya uchambuzi wa taarifa mbalimbali za migogoro ya matumizi ya ardhi na kuandaa mapendekezo kama alivyoagiza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt John Pombe Joseph Magufuli. Aidha, nawashukuru Wabunge na Wakuu wa Mikoa kwa ushiriki wao katika kufanikisha zoezi hili.

**130.** *Mheshimiwa Spika*; vilevile napenda kuwashukuru MKURABITA pamoja na wadau wote wa sekta ya ardhi ikiwa ni pamoja na Mamlaka za Upangaji, na wadau mbalimbali wa ndani na nje wa maendeleo ikiwemo Benki ya Dunia na nchi wahisani zikilwemo Uingereza, Denmark, Sweden, Japan, Ujeruman, Jamhuri wa Watu wa Korea na Marekani. Wizara yangu inatambua na kuthamini michango inayotolewa na wadau hawa katika kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

**131.** *Mheshimiwa Spika*; natumia fursa hii pia kuzipongeza Asasi za Kiraia na Mashirika Binafsi ikiwemo Shirika la SOLIDARIDAD, Taasisi ya Hakiardhi, Shirika la CORDS, Care International Tanzania, Taasisi ya STEP (Southern Tanzania Elephant Program), *Ujamaa Community Resource Team* (UCRT), Taasisi ya Kuwezesha Mazingira ya Uwekezaji (Local Investment Climate - LIC), Eco-Agriculture Partners, WWF, Shirika la Uhifadhi wa Wanyamapori (*African Wilflife Foundation – AWF*) na Chuo Kikuu Michigan –Idara ya Mazingira na Uendelevu kwa kushirikiana na Wizara katika kutekeleza majukumu ya sekta ya ardhi.

**132.** *Mheshimiwa Spika*; napenda kutumia fursa hii kumshukuru Naibu Waziri, Mhe. Dkt. Angelina Sylvester Lubala Mabula (Mb) kwa kunisaidia katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Katibu Mkuu Bibi Dorothy Stanley Mwanyika, Naibu Katibu Mkuu Bw. Mathias Kabunduguru, Dkt. Stephen Nindi Mkurugenzi wa

Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Dkt. Maulid Banyani Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba la Taifa na Bw. Dismas Minja Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba na Vifaa vya Ujenzi kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Vilevile, napenda kuwashukuru watendaji wa Wizara, Wakuu wa Vyuo vya Ardhi vya Tabora na Morogoro, Wakuu wa Vitengo na Wafanyakazi wote wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi katika kutekeleza majukumu ya Wizara.

## **7.0 HITIMISHO**

**133. *Mheshimiwa Spika***; katika hotuba yangu nimeainisha mafanikio yaliyopatikana katika kuwawezesha wananchi hususan wanyonge kumiliki ardhi kama nguzo kuu ya uchumi na kupunguza umaskini. Aidha, katika kukabiliana na changamoto mbalimbali, Wizara yangu itaendelea kuimarisha ofisi za ardhi za kanda kwa kuajiri wataalam na kuweka uwiano wa wataalam wa kutosha katika halmashauri. Halikadhalika, itaendelea kupeleka vifaa na vitendea kazi vingine katika ofisi zote za kanda na halmashauri ili kuwezesha kazi ya upangaji, upimaji na umilikishaji ardhi kufanyika kwa kasi. Wizara itaendelea kuishirikisha sekta binafsi katika utekelezaji wa majukumu haya.

**134. *Mheshimiwa Spika***; ili kuondokana na kero ya ucheleweshaji wa malipo ya fidia unaofanywa na taasisi na wadau wanaotwaa ardhi kwa ajili ya matumizi mbalimbali, Wizara yangu imeunda Bodi ya Mfuko wa Fidia kwa ajili ya kuratibu shughuli za ulipaji wa fidia. Kuhusu utunzaji wa kumbukumbu Wizara inakamilisha programu ya kuimarisha milki za ardhi na ujenzi wa miundombinu ya utunzaji wa kumbukumbu za ardhi.

**135. *Mheshimiwa Spika***; katika kudhibiti migogoro ya matumizi ya ardhi ambayo ni mtambuka nchini, Serikali imeunda Kamati ya Kitaifa ya kuchunguza na kushauri

namna bora ya kutatua migogoro ya matumizi ya ardhi iliyopo nchini. Vilevile, Wizara yangu itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu sheria, kanuni, taratibu na miongozo inayotawala sekta ya ardhi.

**136. *Mheshimiwa Spika***; napenda sasa kuhitimisha kwa kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara yangu imedhamiria kufanya mageuzi kwa kutumia teknolojia katika utoaji wa huduma za ardhi utakaohakikisha usalama wa milki, uwezeshaji wa wananchi kiuchumi, na kuongeza thamani ya ardhi na pato la Taifa. Natoa rai kwa mamlaka za upangaji, washirika wa maendeleo na wadau wote wa sekta ya ardhi kuendelea kushirikiana na Wizara yangu katika kutekeleza mageuzi haya katika bajeti ya mwaka wa fedha 2019/20. Mwelekeo huu utasaidia kutekeleza sera ya kujenga uchumi wa viwanda hatimaye kulifkisha Taifa katika uchumi wa kipato cha katii ifikapo 2025.

## **8.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2019/20**

### **Makadirio ya Mapato**

**137. *Mheshimiwa Spika***; katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara inatarajia kukusanya jumla ya shilingi bilioni **180** kutohuna na kodi, tozo na ada mbalimbali zinazotokana na shughuli za sekta ya ardhi kwa kutekeleza mikakati ambayo imeainishwa katika hotuba yangu.

### **Makadirio ya Matumizi**

**138. *Mheshimiwa Spika***; ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu niliyoyaeleza katika hotuba hii kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lijadili na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Fungu **48**: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Fungu **03**: Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi kama ifuatavyo:-

**Fungu 48: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi;**

AINA	MAPATO	SHILINGI
A	Mapato ya Serikali	180,000,000,000.00
	<b>AINA YA MATUMIZI</b>	<b>FEDHA ZINAZOOMBWA</b>
B	Matumizi ya Kawaida:	
	Matumizi ya Mishahara	17,393,124,000.0
	Matumizi Mengineyo	15,762,363,000.0
	<b>Jumla Ndogo</b>	<b>33,155,487,000.0</b>
C	Matumizi ya Maendeleo:	
	Fedha za Ndani	18,000,000,000.0
	Fedha za Nje	6,284,504,387.0
	<b>Jumla Ndogo</b>	<b>24,284,504,387.0</b>
	<b>JUMLA KUU (B+C)</b>	<b>57,439,991,387.0</b>

Jumla ya matumizi ya kawaida na maendeleo ni shilingi  
**57,439,991,387/=.**

**Fungu 03: Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi;**

AINA	AINA YA MATUMIZI	FEDHA ZINAZOOMBWA
A	Matumizi ya Mishahara	1,265,250,000.0
B	Matumizi Mengineyo	979,822,000.0
C	Matumizi ya Maendeleo	3,000,000,000.0
	<b>Jumla</b>	<b>5,245,072,000.0</b>

Jumla ya matumizi ya kawaida na maendeleo ni shilingi  
**5,245,072,000/=.**

**139.** *Mheshimiwa Spika*, jumla kuu ya fedha zote zinazoombwwa kwa Wizara (Fungu 48 na Fungu 03) ili muweze kujadili na kuidhinisha ni shilingi **62,685,063,387/=.**

**140.** *Mheshimiwa Spika*, mwisho natoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Pamoja na hotuba hii ipo taarifa ya utekelezaji miradi na majedwali ambayo yanafafanua kwa kina shughuli zilizotekelzwa na Wizara. Hotuba hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Wizara ambayo ni ***www.lands.go.tz***.

141. *Mheshimiwa Spika*, naomba kutoa hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana hoja imetolewa na imeungwa mkono, tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa William Lukuvi. Ahsante sana kwa kuwasilisha hotuba yako kwa umahiri mkubwa, umetufafanulia mambo mengi sana, tunakushukuru sana.

Sasa moja kwa moja nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii, ahsante sana karibu sana. Mheshimiwa una nusu saa na si zaidi

**MHE. SHABAN O. SHEKILINDI - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji

**SPIKA:** Mheshimiwa Rwakatare hairuhusiwi kugeuza kitu na kumpa mgongo Spika, nilikuwa nanyoosha mambo kidogo. Waheshimiwa huwa hairuhusiwi kugeuza hicho kitu kiasi kwamba sasa Spika unampa mgongo hapana, endelea Mheshimiwa kusoma hotuba yako.

**MHE. SHABAN O. SHEKILINDI – (K.n.y. MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA KUDUMU YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka 2018/2019 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ardhi kwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, naanza na utangulizi, kwa mujibu wa kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Fungu – 48 na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi

ya Ardhi Fungu 03 kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa majukumu yaliyotekelizwa mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ukusanyaji wa maduhuri kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Katika mwaka wa fedha 2018/2019 Wizara Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ili kadiria kukusanya maduhuli ya jumla ya bilioni 120 kutoka katika vyanzo mbalimbali vya mapato vinavyohusiana na shughuli za sekta ya ardhi. Hadi kufikia Februari, 2019 jumla ya Shilingi bilioni 60.27 zilikusanya. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 50.2% ya maoteo kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa upande wa fungu 03 Tume ya Taifa ya Mpango ya Matumizi ya Ardhi ilikadiria kukusanya Jumla ya shillingi 700, 000,000 kutoka katika kodi ya pango la nyumba Tabora, mauzo ya vitabu vya mpango ya matumizi ya ardhi na wadau wa maendeleo ya ardhi (*strategic Partners*). Hadi kufikia Februari 2019, Tume ilikusanya kiasi cha shilingi milioni 996.1 kiasi hiki ni sawa na asilimia 142% ya lengo lililokusudiwa. Mchanganuo wa mapato yatokanayo na vyanzo mbalimbali vya Sekta ya Ardhi pamoja na wadau wa kimkakati unaonekana katika Jedwali Na.1

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua taarifa ya makusanyo kwa kulinganisha makadirio yaliyokusudiwa na makusanyo halisi yaliyofikiwa hadi mwezi Februari 2019 na kubaini kuwa mwenendo wa makusanyo kwa fungu 48 na fungu dogo la 03 ni ya kuridhisha, Kamati inaipongeza Wizara kwa kukusanya zaidi ya asilimia 50 ya lengo lililokusudiwa katika Mwaka wa Fedha 2018/19. Aidha kamati inaisisitiza Wizara isimamie mikakati ya makusanyo iliyojewekea ili kufikia malengo ya makusanyo kwa mwaka ifikapo Juni, 2019.

Mheshimiwa Spika, Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina Fungu 48 Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya makazi, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Wizara iliidhinishiwa na Bunge jumla ya shillingi bilioni 65.989 na

kupewa ongezeko la shilingi bilioni 12.155 kwa ajili ya kulipa madeni yaliyohakikiwa na kupelekea bajeti ya Wizara kuwa shilingi bilioni 78.1 katì ya fedha hizo shilingi Billioni 29.26 ni za matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 46.1 ni kwa ajili ya miradi ya Maendeleo. Hadi kufika Februari, 2019 Wizara ilipokea jumla ya Shilingi Billioni 46.1 sawa na asilimia 59 ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, mchanganuo ni kama ifuatavyo:- bilioni 18.9 kwa ajili ya matumizi mengineyo, Billioni 10.3 Mishahara, Bilioni 16.8 fedha za maendeleo ambapo katì ya hizo bilioni 8.3 fedha za ndani na bilioni 8.5 fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, Fungu 03 Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi kwa upande wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi - fungu 03 Bunge liliidhinisha jumla ya shilingi bilioni 2.081 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Katika fedha hizo shilingi bilioni 1.102 ziliidhinishwa kwa ajili ya mishahara na Shilingi milioni 979.82 ziliidhinishwa kwa ajili ya Matumizi mengineyo. Hata hivyo, uchambuzi wa bajeti unaonyesha kuwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Tume iliidhinishwa shilingi 5,000,000,000 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2019 Tume ilipokea jumla ya shilingi bilioni 1.09 sawa na asilimi 47.2 ya fedha iliyoidhinishwa.

Jedwali Na. 2 linaonyesha Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo Kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi hadi Februari, 2019.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa bajeti unaonyesha kuwa mwenendo wa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina ni wa kuridhisha kwa mafungu yote mawili. Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuziwezesha halmashauri kusimamia sekta ya Ardhi ipasavyo ili kupunguza migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, Ukaguzi wa Baadhi ya Miradi ya Maendeleo, Kamati ilifanya ziara kukagua miradi ya

maendeleo iliyo chini ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Katika ziara hiyo Kamati ilitembelea mpaka wa Tanzania na Kenya katika kijiji cha Jasin na eneo la Horohoro Mkoani Tanga. Mpaka huu uko katika hatua za kuboreshwa na kuimariswa kutokana na ongezeko la watu, muingiliano wa shughuli za kiuchumi katika maeneo ya mpakani.

Mheshimiwa Spika, Kamati hairidhishwi na kasi ya uimarishaji wa alama za mpakani. Aidha, Kamati imebaini kutokuwepo kwa eneo la wazi *no mans Land* hali inayosababisha wananchi wa pande mbili kuingilia maeneo ya nchi nyingine na kujenga makazi na kufanya shughuli nyingine za kiuchumi. Zipo nyumba za watanzania zimejengwa ndani ya Kenya au katikati ya mpaka nusu Kenya nusu Tanzania. Vile vile kutokuwepo kwa alama hasa katika mpaka wa majini kunasababisha usumbufo kwa wavuvi hali ilinayopelekea wavuvi wetu kukamatwa kwa madai ya kuvua katika eneo la Kenya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri serikali kuwepo vipaumbele katika kuimariswa alama za mipakani ili kuwaondolea wananchi wetu usumbufo unaojitokeza na kutowepo kwa alama madhubuti zinazobainisha mipaka yetu. Aidha, Kamati inaishauri kuwa Serikali ihakikishe mipaka yote ya majini inaimarishwa kwa kuweka alama madhubuti.

Mheshimiwa Spika, Katika muendelezo wa ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati ilipata fursa ya kutembelea mradi wa ujenzi wa nyumba za gharama nafuu unaotekelawa na Shirika la Nyumba la Taifa katika Halmashauri ya Wilaya ya Muheza eneo la Chatur. Kamati haikuridhishwa na ukubwa wa nyumba hizo kwani vyumba ni vidogo sana na haviendani na hali halisi ya maisha ya sasa. Kamati inalishauri Shirika kuwashirikisha wadau/wateja wakati wa kuandaa michoro ili wakubaliane kuhusu ukubwa wa nyumba kulingana na mahitaji ya mteja. Aidha, Kamati inaishauri Shirika kuhakikisha kuwa linaingia mikataba ya ujenzi wa nyumba za halmashauri baada ya kuhakikisha kuwepo

kwa fedha za mradi. Hii itaongeza kasi ya ujenzi kuliko ilivyo sasa ambapo shirika hulazimika kusimamisha mradi au kutumia fedha vyanzo vyake vingine vya mapato kukamilisha mradi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata fursa ya kukagua mradi wa upimaji na umilikishaji ardhi unaotekelizwa kwa majaribio katika Wilaya za Kilombero, Malinyi na Ulanga. Mradi huu ulipangwa kutekelezwa kwa miaka mitatu kuanzia Januari, 2016 hadi Juni, 2019. Fedha zilizotengwa kwa ajili ya mradi huu ni shilingi billioni 28,000,000,000 fedha za nje na shilingi bilioni 7,000,000,000 Fedha za ndani. Hadi wakati Kamati inafanya ziara jumla ya shilingi bilioni 25.127 fedha za nje sawa na asilimia 90% na shilingi milioni 710,000,000 Fedha za ndani sawa na asilimia 10% zilikuwa zimetolewa Kwa kuangalia mwenendo wa utoaji wa fedha za ndani ni dhahiri kuwa serikali haiwezi kufikia malengo ya kuhakikisha kila kipande cha ardhi ya nchi yetu kimepimwa hasa baada ya wafadhili kuondoka.

Mheshimiwa Spika, Programu hii ina manufaa mengi kwa wananchi kwani siyo tu imechangia kupunguza migogoro ya ardhi bali pia inawezesha wananchi kiuchumi kwani hati za haki milki za kimila wanazopewa zinaweza kutumika kama dhamana ya kukopa katika taasisi za fedha. Kamati inaishauri Serikali kuweka mkakati maalum wa kutenga fedha za kutosha zitakazowezesha kupima na kumilikisha ardhi yote ya nchi yetu. Hali hiyo itaiongezea Serikali mapato hasa katika ardhi za jumla kwani itakuwa rahisi kukusanya kodi za ardhi.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Maoni ya Kamati, wakati wa kuchambua bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, Kwa Fungu 03 na Fungu 48 Kamati ilitoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa kazi za Wizara hii. Napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa maoni na ushauri wa kamati ulifanyiwa kazi, aidha maoni mengine yaliendelea kufanyiwa kazi, lakini yapo maoni ambayo hayakufanyiwa

kazi kikamilifu kutokana na changamoto ya uhaba wa rasilimali fedha.

Mheshimiwa Spika, Mwaka jana Kamati ilikagua mpaka wa Tanzania na Uganda na moja ya changamoto ilikuwa kutokuwepo kwa barabara hali iliyotulazimu kuingia nchini Uganda kwa ajili ya kukagua alama za mpaka. Mwezi Machi mwaka huu 2019 Kamati ilikagua mpaka wa Tanzania na Kenya katika kijiji cha Jasin na eneo la Horohoro na kukutana na changamoto ile ile ya kutokuwepo kwa barabara ya kuwesheha kufika katika alama za mipaka. Sambamba na barabara hakuna alama madhubuti hasa katika mpaka wa majini hali inayosababisha wavuvi wetu kupata usumbufo kutoka kwa askari wa nchi jirani. Kamati hairidhishwi na kasi ya Serikali katika kuimarisha mipaka ya nchi yetu Kamati inaishauri Serikali kuimarisha mipaka kwa kuweka alama madhubuti.

Mheshimiwa Spika, Kamati hairidhishwi na utaratibu wa Serikali kupunguza bajeti hususan fedha za maendeleo. Bajeti ya maendeleo imeshuka kutoka shilingi bilioni 30.5 mwaka 2018/2019 hadi shilingi bilioni 24.3 mwaka 2019/2020. Huu sio mwenendo mzuri kama Serikali imedhamiria kuleta mageuzi katika Sekta ya ardhi hususani katika kupima na kupanga matumizi ya ardhi. Ni matarajio ya Kamati kuwa Serikali iendelee kuongeza bajeti kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza Serikali kwa kuanzisha Mabaraza 97 ya Ardhi na Nyumba. Hata hivyo Kamati inashauri Serikali kutimiza lengo lake la kuwa na Mabaraza ya aina hiyo kwa kila Wilaya hususani kwa kuzingatia vigezo vya umbali, jiografia husika, na wingi wa migogoro. Kamati inapongeza Serikali kwa kuajiri wenyeviti 20 wa mabaraza ya ardhi na nyumba kati ya 44 waliokuwa wanahitajika. Ni matarajio ya Kamati kwamba Serikali itaendelea kuajiri watumishi wa kutosha kuhudumia mabaraza sambamba na kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya uendeshaji wa mabaraza hayo.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 umeainisha kutekeleza shughuli mbalimbali. Baadhi ya shughuli hizo ni kama zifuatazo:-

- (a) Kuimarisha usalama wa milki za ardhi;
- (b) Kuboresha takwimu za kijigrafia nchini;
- (c) Kuendeleza utafiti wa vifaa vyta ujenzi wa nyumba bora na zenye gharama nafuu kwa ajili ya uendelezaji makazi;
- (d) Kuboresha Sera, Sheria, Kanuni na miongozo inayohusu sekta ya ardhi;
- (e) Kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi katika miji kadhaa hapa nchini;
- (f) Kusimamia upangaji na uendelezaji wa miji nchini;
- (g) Kusimamia ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na sekta ya ardhi; na
- (h) Kuhamasisha na kuwezesha wananchi kuwa na nyumba bora.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliridhishwa na vipaumbele viliyowekwa na Wizara kwakuwa vipaumbele hivi vinaendana na Mpango wa Taifa wa Mwaka 2019/2020 na vinalenga dira, dhima na madhumuni ya Wizara hususani katika kuimarisha usalama wa miliki za ardhi, kuboresha sera, sheria, kanuni na miongozo inayohusu sekta ya ardhi pamoja na kuboresha utendaji kazi na utoaji huduma katika sekta ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Uchambuzi wa Makisio ya Makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Fungu 48 inatarajia kukusanya maduhuli ya shilingi 180,000,000,000/= kutohana na vyanzo mbalimbali vya mapato katika sekta ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, kiasi hiki ni ongezeko la takribani shilingi billioni 60 sawa na ongezeko la 50% ikilinganishwa na shilingi 120,000,000,000 zilizokadiriwa kukusanya katika Mwaka wa Fedha 2018/2019. Ongezeko hili linatokana na kuongezeka kwa kasi ya urasimishaji makazi mijini pamoja na punguzo la ada ya mbele kutoka 2.5% hadi 1% ya thamani ya ardhi katika maeneo ya urasimishaji makazi mijini. Zoezi hili lina lengo la kuwawezesha wamiliki wengi wa ardhi hususani mijini kumudu gharama za kumilikishwa ardhi na hivyo kuiwezesha Serikali kumilikisha ardhi zaidi na kuongeza makusanyo.

Mheshimiwa Spika, kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kwa ujumla bajeti inayoombwa imepungua kwa shilingi bilioni 20.7 Ukilinganishwa na bajeti ya Mwaka wa Fedha 2018/2019 ambapo punguzo hilo ni sawa na asilimia 26%. Kamati inaona kwamba punguzo hilo linaweza kupelekea Wizara kushindwa kufikia malengo iliyojiwekea.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa upande wa bajeti ya maendeleo bajeti imepungua kwa shilingi bilioni 6.253 sawa na asilimia bilioni 20.2 ikilinganishwa na shilingi bilioni 30.537 iliyoidhinishwa na Bunge katika mwaka wa fedha 2018/2019. Kupungua kwa bajeti kutazorotesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Fungu namba 3 katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Wizara iliomba Bunge iidhinishe jumla ya shilingi bilioni 5.9 ili ziweze kutumika kutekeleza mpango na bajeti ya Tume. Kati ya bajeti hiyo, shilingi bilioni 2.2 ni za Matumizi ya kawaida, na shilingi bilioni 3 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Mchanganuo wa bajeti unaonyesha kuwa bajeti inayoombwa imepungua kwa kiasi cha shilingi bilioni 1.8 ukilinganishwa na bajeti ya Mwaka 2018/

2019 ya shilingi bilioni 7.7. Upungufu huu unatokana na kupunguzwa kwa bajeti ya maendeleo kutoka shilingi bilioni 5 mwaka 2018/2019 hadi shilingi bilioni 3. Hali hii itazorotesha shughuli za upimaji na upangaji wa matumizi ya ardhi nchini.

Mheshimiwa Spika, masuala mengine muhimu yaliyojitokeza wakati wa kuchambua na Kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Wakati wa kujadili bajeti ya Wizara hii masuala mbalimbali yaliyjitekeza na kuhitaji kujadiliwa kwa kina ili kuweza kuleta uelewa wa pamoja na kuweza kuishauri Serikali ipasavyo. Masuala haya ni kama yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na taarifa kwamba Shirika la nyumba la Taifa (*NHC*) linaelekea kufilisika kutokana na kuwa na madeni makubwa kuliko mali zake. Kumekuwa na taarifa kwamba kuna mwingiliano wa majukumu ya Tume ya Taifa ya mipango ya matumizi ya Ardhi na Halmashauri za Miji, Manispaa na Majiji.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na changamoto ya ugawaji wa mashamba makubwa yaliyobatilishiwa milki hali inayosababisha wananchi kuyavamia na hivyo kuleta migogoro. Kumekuwa na changamoto ya uwepo wa migogoro ya ardhi baina ya watumiaji mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hizo kamati iliagiza Wizara kuleta mbele ya Kamati Taarifa nne zifuatazo:-

(a) Taarifa kuhusu hali halisi ya Maendeleo na Utendaji wa Shirika la Nyumba la Taifa;

(b) Taarifa kuhusu utendaji wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya ardhi;

(c) Taarifa kuhusu maendelezo ya mashamba makubwa na hatua zinazochukuliwa na Serikali kwa mashamba yasioendelezwa; na

(d) Taarifa kuhusu hali ya migogoro ya ardhi nchini.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliwasilisha taarifa hizo mbele ya Kamati na zikajadiliwa kwa kina. Kutokana na taarifa zilizowasilishwa Kamati imebaini yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Shirika la Nyumba la Taifa kamati inaipongeza Serikali kwa kuteua Bodi mpya ya Shirika pamoja na kuweka Menejimenti mpya. Ni matarajio ya Kamati kwamba sasa kasi ya utekelezaji wa majukumu itarejea kama ilivyo kuwa mwanzo. Aidha, kamati imeridhishwa na taarifa ya Shirika iliyotoa taswira ya hali halisi ya shirika kuliko taarifa zilizokuwa zimesambaa katika vyombo mbalimbali vyta habari kwamba Shirika liko katika hali mbaya kinyume na ukweli. Kamati inaishauri Serikali kutekeleza yafuatayo ili kuliwezesha shirika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

(a) Serikali ikamilishe utaratibu wa kulipa Shirika idhini ya kukopa ili liweze kukamilisha ujenzi wa miradi mikubwa ambayo kwa sasa imesimama. Hii itasaidia kuliepusha Shirika kupata hasara inayoweza kutokea kwa kutoikamilisha miradi hiyo kwa wakati.

(b) Shirika liboreshe zaidi hali ya ukwasi ili kuwa na fedha za kutosha kuijendesha, kulipa mikopo yake na kubaki na ziada kwa ajili ya uendelezaji wa miradi mingine bila kutegemea mikopo muda wote. Serikali iharakishe mchakato wa kukamilisha Sera ya nyumba itakayotoa mwongozo na kusimamia sekta ya nyumba nchini.

(c) Serikali ihakikishe kwamba taasisi zinazohusika zifakishe huduma za miundombinu kama maji, umeme na barabara katika maeneo ya miradi ya ujenzi wa nyumba za Shirika hasa zile za gharama nafuu ili kuwapa nafuu wanunuzi waliookusudiwa. Vilevile Serikali ione uwezekano wa kuliondolea Shirika Kodi ya Ongezeko la thamani kwenye vifaa vyta ujenzi. Hali hii itasaidia kupunguza gharama za nyumba kuliko ilivyo sasa ambapo shirika hugharamia uwekaji wa miundombinu hiyo na kusababisha bei ya

nyumba kuwa juu. Aidha, Kamati inalipongeza Shirika kwa kubuni mradi wa kujenga nyumba elfu moja kwa ajili ya makazi katika jiji la Dodoma ambayo ni Makao Makuu ya nchi. Ni ushauri wa Kamati kwamba nyumba zinazojengwa ziwe ni zile zenye hadhi ya jiji.

(d) Utendaji Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ina majukumu makubwa kitaifa ambayo yanalenga kuhakikisha kuwa ardhi na rasilimali zake zinatumika kwa tija na uendelevu. Pamoja na majukumu haya makubwa na Tume kujitahidi kufanya kazi kwa juhud, muundo na uwezo mdogo wa Tume umeifanya isiweze kutimiza majukumu yake ya kuratibu, kushauri, kuandaa, kukagua na kusimamia utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi. Kamati imebaini kuwepo kwa majukumu makubwa kwa Tume ikillinganishwa na bajeti iliyotengwa kwa ajili ya kupima na kupanga matumizi ya ardhi katika vijiji, miji, wilaya, Manispaa na Majiji.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya Tume. Aidha, Serikali ipitie upya Sheria iliyoanzisha Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya ardhi kwa lengo la kuiboresha na kuipandisha hadhi Tume kuwa Mamlaka ili kuipa nguvu zaidi za kisheria kusimamia upimaji, upangaji na utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi. Mabadiliko haya pia yatasaidia kuimarissha usimamizi wa matumizi bora ya ardhi nchini, kuongeza uzalishaji, kuondokana na migogoro ya matumizi ya ardhi, uharibfu wa mazingira na rasilimali ardhi hasa katika kipindi hiki ambapo Taifa letu linaelekea kwenye uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutenga fedha kupitia Tume ya Mipango ya Matumizi ya ardhi kwa ajili ya mradi wa kupima na kupanga matumizi ya ardhi katika vijiji vyote vinavyopitiwa na Bomba la Mafuta. Wilaya na vijiji vyote vya mipakani na Wilaya na vijiji vilivyokuwa na makambi ya wakimbizi. Mradi huu siyo tu utasaidia kuibua

fursa za kiuchumi katika maeneo husika bali pia utaimarisha utawala bora wa ardhi na hivyo kuondoa uwezekano wa kutokea migogoro ya ardhi wakati wa ujenzi wa bomba la mafuta kama ilivyokuwa katika ujenzi wa bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam. (*Makofii*)

(e) Maendelezo ya Mashamba makubwa na hatua zinazochukuliwa na Serikali kwa mashamba yaliyotelekezwa. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua inazochukua za kubatilisha milki za mashamba makubwa yasiyoendelezw. Ili kuondoa malalamiko kuhusu utaratibu unaotumika kugawa mashamba makubwa yaliyofutiwa milki zake, Kamati inaishauri Serikali ihakikishe kwamba halmashauri zinazohusika na mashamba yaliyobatilishiwa milki zake, ziandae mapendekezo ya mpango wa matumizi ya mashamba hayo haraka na kuyawasilisha katika ngazi za juu kwa uamuzi kuliko kuchelewa kuyapangia matumizi na hivyo kusababisha yavamiwe na wananchi na hivyo kusababisha migogoro.

(f) Hali ya migogoro ya ardhi nchini kwa muda mrefu sana kumekuwa na migogoro mingi ya ardhi baina ya watumiaji mbalimbali hali inayochangiwa kwa kiasi kikubwa na sehemu kubwa ya ardhi yetu kutopimwa na kupangiwa matumizi na kukosa Mamlaka ya kusimamia matumizi ya ardhi. Tunaipongeza Serikali kwa kubuni mradi wa kupima, kupanga matumizi na kumilikisha ardhi unaotekelizwa kwa majaribio katika Wilaya za Kilombero, Malinyi na Ulanga ambayo umeonyesha mafanikio makubwa. Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha za kutosha ili mradi huu utekelezwe nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, kipekeeee, Kamati inampongeza Mheshimiwa Rais Dkt John Pombe Joseph Magufuli, kwa hatua yake ya hivi karibuni kuteua Kamati ya Mawaziri wanane kushughulikia migogoro ya ardhi katika maeneo yote ya hifadhi nchini. Hatua hii inalenga kumaliza kabisa migogoro ya ardhi baina ya wananchi na Mamlaka za uhifadhi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, ni matarajio ya Kamati kwamba ripoti itakayoandaliwa na Kamati hii inakwenda siyo kupunguza tu bali kumaliza kabisa migogoro ya ardhi katika maeneo ya hifadhi hapa nchini. Aidha ni matarajio ya Kamati kwamba Serikali itahakikisha inaweka mkakati wa kushughulikia migogoro ya ardhi katika maeneo mengine. Hali hiyo itawapa wananchi fursa ya kufanya shughuli zao za kiuchumi kwa amani na hivyo kuongeza tija na kukuza uchumi wa Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa jumla, Sekta ya Ardhi inakabiliwa na changamoto kubwa ya kuongezeka kwa migogoro ya ardhi, ujenzi holela, na kukosekana kwa mipango ya matumizi bora ya ardhi. Kamati inaishauri Serikali kutekeleza yafuatayo ili kunusuru sekta hii muhimu.

(a) Kuendelea kuzisimamia na kutekeleza kikamilifu sheria zote za ardhi ili kuongeza ufanisi katika kutoa huduma za ardhi. Aidha, sheria zilizopitwa na wakati ziletwe Bungeni kwa ajili ya kufanyiwa marekebisho;

(b) Kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu sheria mbali mbali za ardhi ili kupunguza migogoro;

(c) Kuyaimarisha Mabaraza ya Ardhi yaliyopo kwa kuyapatia vitendea kazi sambamba na kuajiri wafanyakazi wa kutosha kwa ajili ya kuendeleza mabaraza ya ardhi. Aidha, Serikali ihakikishe kuwa Watendaji wa Mabaraza haya wanafanya kazi kwa uadilifu mkubwa na kuondoa malalamiko yaliyopo sasa kwamba Mabaraza hayo yamegubikwa na vitendo nya rushwa;

(d) Kuandaa mkakati wa kitaifa utaohakikisha kuwa Serikali inatenga fedha za kutosha kwa ajili ya kupima na kupanga matumizi ya kila kipande cha ardhi ya nchi yetu;

(e) Kuwashirikisha kikamilifu wananchi katika kupanga matumizi na kusimamia ugawaji wa ardhi ya mashamba yaliyofutiwa milki;

(f) Kuhakikisha kuwa fidia stahiki kwa ajili ya ardhi iliyotwaliwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo inalipwa ipasavyo;

(g) Kupitia upya sheria iliyoanzisha Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ili kuipa nguvu ya kusimamia upimaji, upangaji na utekelezaji wa matumizi ya ardhi; na

(h) Kushirikisha wananchi katika zoezi la urasimishajji makazi holela mijini ili kupunguza malalamiko yanayoweza kutokea. Aidha, Serikali ipunguze gharama za upimaji sambamba na kuweka utaratibu wa wananchi kulipia gharama za upimaji kwa awamu na kutoa elimu kwa wananchi juu ya kuwepo kwa fursa za kupata mkopo kutoka katika taasisi za fedha zinazokopeshwa na Tanzania *Mortgage Refinance Company* kwa masharti nafuu ili kuwawezesha wananchi kuitumia fursa hiyo kujenga nyumba za kisasa hasa wale wanaoishi vijijini.

Mheshimiwa Spika, hitimisho napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa hii. Kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ambao Maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina ya wajumbe yaingie kwenye Hansard. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kumshukuru Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. William Lukuvi, (Mb), Naibu Waziri, Mhe.Dkt Angeline L. Mabula, (Mb), Katibu Mkuu na Wataalam wote wa Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa ushirikiano waliotha kwa kamati wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge wakiongozwa na Ndugu Stephen Kagaigai Katibu wa Bunge, ndugu Athuman Hussein Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, ndugu Dickson Bisile Mkurugenzi Msaidizi, Makatibu wa Kamati hii, Ndugu

Haika Mtui, Gerald Magili, na Msaidizi wa Kamati Ndugu Mwimbe John kwa kuihudumia vyema Kamati pamoja na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kama yalivyowasilishwa na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI,  
MALIASILI NA UTALII KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA  
WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI KWA  
MWAKA WA FEDHA 2018/2019; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI  
KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA  
KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 KAMA ILIVYOWASILISHWA  
MEZANI**

---

## **SEHEMU YA KWANZA**

## **MAJUKUMU YA KAMATI NA MUUNDO WA TAARIFA**

## **UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Fungu - 48 na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi Fungu-03 kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika**, Fasili ya 7 (1) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 inabainisha majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuwa ni :-

- (a) Kushughulikia Bajeti ya Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi;
- (b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya wizara hiyo;
- (c) Kushughulikia Taarifa za utendaji za kila mwaka za wizara hiyo; pamoja na
- (d) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hiyo

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na majukumu mengine yaliyoorodheshwa hapo juu, Kanuni ya 98(1),(2) na Nyongeza ya Nane iliyo chini ya kanuni ya 118, fasili ya 7 (1) (a) ya kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 zimeweka sharti la Kamati za Kisekta, ikiwemo Kamati hii, kufanya ukaguzi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha uliotangulia sambamba na kufanya uchambuzi wa bajeti ya wizara inazosimamia.

Naomba kutoa taarifa kuwa tarehe 18 hadi 21 Machi, 2019 Kamati ilifanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha chini ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Aidha kati ya tarehe 23 hadi 26 Machi, 2019 Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na kufanya uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kwa mafungu yaliyo chini ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, yaani **Fungu 03** – Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi na **Fungu 48** – Wizara ya Ardhi,Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa hii inafafanua mambo makubwa manne (4) yafuatayo:-

(a) Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ikijumuisha;:-

(i) Makusanyo ya Mapato 2018/19;

(ii) Upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019;

(iii) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019;

(iv) Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

(b) Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020; ukijumuisha;:-

(i) Makisio ya Makadirio ya Makusanyo ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020;

(ii) Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020;

(iii) Mambo mengine muhimu yaliyojitokeza wakati wa kuchambua na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

(c) Maoni na Ushauri wa Kamati; na

(d) Hitimisho.

**Mheshimiwa Spika**, mpangilio huu unakusudia kuliwezesha Bunge kupata taswira ya hali ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na kulinganisha na makadirio ya fedha za matumizi yaliyowasilishwa na mtoa

hoja ili Bunge liweze kuamua kuhusu maombi ya fedha ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

## **SEHEMU YA PILI**

### **UCHAMBUZI WA MAJUKUMU YALIYOTEKELEZWA**

#### **1.0. Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika** katika uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii, Kamati ilijikita katika kulinganisha kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge mnamo mwezi Mei, 2018 na kiwango ambacho kimepokelewa hadi kufikia Machi 2019 katika Robo ya Tatu ya Mwaka wa fedha 2018/2019. Kamati pia ilitazama kiasi cha fedha kilichoidhinishwa katika miradi ya maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na kiasi cha fedha kilichopokelewa hadi kufikia Mwezi Machi 2019. Lengo la kufanya tathmini ya namna hii ni kufahamu Mwelekeo wa Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Serikali katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 ili kujua hali halisi iliyopo Serikalini katika kutekeleza bajeti inayoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kuwaleta wananchi maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile Kamati ilijielekeza katika eneo la ukusanyaji wa maduhuli kwa kulinganisha kiasi kilichokusanywa hadi kufikia mwezi Machi 2019 ikilinganishwa na lengo la ukusanyaji liliowekwa wakati wa kupitisha bajeti Mwezi Mei 2018. Lengo la kufanya ulinganisho wa namna hii ni kuiwezesha Kamati kupima juhudzi za Serikali na umakini wa mipango yake katika kukusanya Maduhuli ipasavyo. Taarifa zilizotumiwa na Kamati zilitokana na vyanzo mbalimbali hususan Taarifa zilizowasilishwa na Wizara mbele ya Kamati kwa kipindi cha Februari na Machi 2019, mahojiano na majadiliano na wadau mbalimbali yaliyofanyika kwa pamoja yalichangia upatikanaji wa taarifa muhimu wakati wa vikao vyta Kamati.

## 2.0. **Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ilikadiria kukusanya Maduhuli ya jumla ya Shilingi Bilioni **120** kutoka katika vyanzo mbalimbali vya mapato vinavyohusiana na shughuli za sekta ya ardhi. Hadi kufikia Februari, 2019 jumla ya Shilingi **60.27** zilikusanya. Kiasi hiki ni sawa na asilimia **50.2%** ya maoteo kwa mwaka. Aidha kwa upande wa **fungu 03**-Tume ya Taifa ya Mpango ya Matumizi ya Ardhi ilikadiria kukusanya Jumla ya shillingi **700, 000,000** kutoka katika kodi ya pango la nyumba Tabora, mauzo ya vitabu vya mipango ya matumizi ya ardhi na wadau wa maendeleo ya ardhi (*strategic Partners*).

Hadi kufikia Februari 2019, Tume ilikusanya kiasi cha shilingi **996,133,445**. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 142% ya lengo lilokusudiwa. Mchanganuo wa mapato yatokanayo na vyanzo mbalimbali vya Sekta ya Ardhi pamoja na wadau wa kimkakati unaonekana katika Jedwali **Na.1** hapa chini:-

### **Jedwali: 1 Mchanganuo wa Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

FUNGU	MAKADIRIO	MAKUSANYO	% YA JUMLA YA MAKUSANYO
48- Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi	120,000,000,000	60,270,000,000.15	50.2%
03- Tume ya Taifa ya Mpango ya Matumizi ya Ardhi	700,000,000	996,133,445	142%

**Chanzo: Taarifa ya Utekelezaji ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika** Kamati ilichambua taarifa ya makusanyo kwa kulinganisha makadirio yaliyokusudiwa na

makusanyo halisi yaliyofikiwa hadi mwezi Februari 2019 na kubaini kuwa mwenendo wa makusanyo kwa fungu **48** na fungu **03** ni wa kuridhisha, Kamati inaipongeza Wizara kwa kukusanya zaidi ya asilimia 50 ya lengo liliokusudiwa katika Mwaka wa Fedha 2018/19. **Aidha kamati inaisisitiza Wizara isimamie mikakati ya makusanyo iliyojiwekea ili kufikia malengo ya makusanyo kwa mwaka ifikapo Juni, 2019.**

### 3.0. Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina

#### 1.3.1 Fungu 48-Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya makazi

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Wizara iliidhinishiwa na Bunge jumla ya shilingi **65,989,347,638/=** na kupewa ongezeko la shilingi bilioni **12,155,724,516** kwa ajili ya kulipa madeni yaliyohakikila na kupelekea bajeti ya Wizara kuwa shilingi **78,145,072,154**. Kati ya fedha hizo shilingi **Bilioni 29.26** ni za matumizi ya kawaida na shilingi **Bilioni 46.1** ni kwa ajili ya miradi ya Maendeleo. Hadi kufika Februari, 2019 Wizara ilipokea jumla ya Shilingi Billioni 46.1 sawa na asilimia **59** ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Mchanganuo ni kama ifuatavyo:- **bilioni 18.9** kwa ajili ya matumizi mengineyo, **Billioni 10.3** Mishahara, **Bilioni 16.8** fedha za maendeleo ambapo kati ya **hizo bilioni 8.3** fedha za ndani na **bilioni 8.5** fedha za nje.

#### 1.3.2 Fungu 03-Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi

**Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi- **fungu 03** Bunge liliidhinisha jumla ya **shilingi 2, 081, 926,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo **shilingi 1, 102, 104,000** ziliidhinishwa kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 979, 822,000** ziliidhinishwa kwa ajili ya Matumizi mengineyo. Hatahivyo, uchambuzi wa bajeti unaonyesha kuwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Tume iliidhinishiwa shilingi **5, 000,000,000** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Hadi kufikia

Machi,2019 Tume ilipokea jumla ya shilingi 1,098,873,302 sawa na asilimi **47.2** ya fedha iliyoidhinishwa.

**Jedwali Na.2** linaonyesha Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo Kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi hadi Februari, 2019

### **Jedwali Na, 02-Upaikanaji wa Fedha kutoka Hazina hadi Februari 2019**

Fedha zilizoidhinishwa 2018/19			Fedha zilizotolewa hadi kufikia Februari 2019		
Mishahara na Matumizi Mengineyo	Fedha za Ndani za Miradi ya Maendeleo	Fedha za Nje za Miradi ya Maendeleo	Mishahara na Matumizi Mengineyo	Fedha za Ndani za Miradi ya Maendeleo	Fedha za Nje za Miradi ya Maendeleo
47,607,470,154	2,000,000,000	10,537,602,000	29,260,868,778	8,310,000,000	8,548,308,152

### **Chanzo: Taarifa ya Utekelezaji ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa bajeti unaonyesha kuwa mwenendo wa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina ni wa kuridhisha kwa mafungu yote mawili. **Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuziwezesha Halmashauri kusimamia sekta ya Ardhi ipasavyo ili kupunguza migogoro ya ardhi.**

#### **4.0. Ukaguzi wa Baadhi ya Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ziara kukagua miradi ya maendeleo ilijo chini ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Katika ziara hiyo Kamati ilitembelea mpaka wa Tanzania na Kenya katika kijiji cha Jasin na eneo la Horohoro Mkoani Tanga. Mpaka huu uko katika hatua za kuboreshwa na kuimarishwa kutokana na ongezeko la watu, muingilio wa shughuli za kiuchumi katika maeneo ya mpakani.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati hairidhishwi na kasi ya uimarishaji wa alama za mpakani. Aidha Kamati imebaini kutokuwepo kwa eneo la wazi ( No mans Land) hali inayosababisha wananchi wa pande mbili kuingilia maeneo ya nchi nyingine na kujenga makazi na kufanya shughuli

nyingine za kiuchumi. Zipo nyumba za watanzania zimejengwa ndani ya Kenya au kati kati ya mpaka nusu Kenya nusu Tanzania. Vile vile kutokuwepo kwa alama hasa katika mpaka wa majini kunasababisha usumbufu kwa wavuvi hali iliyopelekea wavuvi wetu kukamatwa kwa madai ya kuvua katika eneo la Kenya. **Kamati inaishauri serikali kuweka kipaumbele katika kuimarisha alama za mipakani ili kuwaondolea wananchi wetu usumbufu unaotokana na kutokuwepo kwa alama madhubuti zinazobainisha mipaka yetu.** Aidha, Kamati inaishauri kuwa Serikali ihakikishe mipaka yote ya majini inaimarishwa kwa kuweka alama madhubuti.

**Mheshimiwa Spika,** Katika muendelezo wa ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati ilipata fursa ya kutembelea mradi wa ujenzi wa nyumba za gharama nafuu unaotekelizwa na Shirika la Nyumba la Taifa katika Halmashauri ya Wilaya ya Muheza eneo la Chatur. Kamati haikuridhishwa na ukubwa wa nyumba hizo kwani vyumba ni vidogo sana na haviendani na hali halisi ya maisha ya sasa. **Kamati inaishauri Shirika kuwashirikisha wadau/wateja wakati wa kuandaa michoro ili wakubaliane kuhusu ukubwa wa nyumba kulingana na mahitaji ya mteja.** Aidha, Kamati inaishauri Shirika kuhakikisha kuwa linaingia mikataba ya ujenzi wa nyumba za Halmashauri baada ya kuhakikishiwa kuwepo kwa fedha za mradi. Hii itaongeza kasi ya ujenzi kuliko ilivyo sasa ambapo shirika hulazimika kusimamisha mradi au kutumia vyanzo vyake vingine vya mapato kukamilisha mradi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata fursa ya kukagua mradi wa upimaji na umilikishaji wa ardhi unaotekelizwa kwa majoribio katika Wilaya za Kilombero, Malinyi na Ulanga. Mradi huu ulipangwa kutekelezwa kwa miaka mitatu kuanzia Januari, 2016 hadi juni, 2019. Fedha zilizotengwa kwa ajili ya mradi huu ni shilingi billion **28,000,000,000** fedha za nje na shilingi bilioni **7,000,000,000** Fedha za ndani. Hadi wakati Kamati inafanya ziara jumla ya shilingi bilioni **25,127,902,152** fedha za nje sawa na asilimia 90% na shilingi milioni **710,000,000** Fedha za ndani sawa na asilimia 10% zilitikuwa zimetolewa.

Kwa kuangalia mwenendo wa utoaji wa fedha za ndani ni dhahiri kuwa serikali haiwezi kufikia malengo ya kuhakikisha kila kipande cha ardhi ya nchi yetu kimepimwa hasa baada ya wafadhili kuondoka.

**Mheshimiwa Spika**, Programu hii ina manufaa mengi kwa wananchi kwani siyo tu imechangia kupunguza migogoro ya ardhi bali pia inawezesha wananchi kiuchumi kwani hati za haki milki za kimila wanazopewa zinaweza kutumika kama dhamana ya kukopa katika taasisi za fedha. **Kamati inaishauri Serikali kuweka mkakati maalum wa kutenga fedha za kutosha zitakazowezesha kupima na kumilikisha ardhi yote ya nchi yetu. Hali hiyo itaiongezea Serikali mapato hasa katika ardhi za jumla kwani itakuwa rahisi kukusanya kodi za ardhi.**

#### **5.0. Utekelezaji wa Maoni ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kuchambua bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, Kwa Fungu 03 na Fungu 48 Kamati ilitoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa kazi za Wizara hii. Napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa maoni na ushauri wa kamati ulifanyiwa kazi, aidha maoni mengine yanaendelea kufanyiwa kazi, lakini yapo maoni ambayo hayakufanyiwa kazi kikamilifu kutokana na changamoto ya uhaba wa rasilimali fedha.

**Mheshimiwa Spika**,. Mwaka jana Kamati ilikagua mpaka wa Tanzania na Uganda na moja ya changamoto ilikuwa kutokuwepo kwa barabara hali iliyotulazimu kuingia nchini Uganda kwa ajili ya kukagua alama ya mpaka. Mwezi Machi mwaka huu 2019 Kamati ilikagua mpaka wa Tanzania na Kenya katika kijiji cha Jasin na eneo la Horohoro na kukutana na changamoto ile ile ya kutokuwepo kwa barabara ya kuwezesha kufika katika alama za mipaka. Sambamba na barabara hakuna alama madhubuti hasa katika mpaka wa majini hali inayosababisha wavuvi wetu kupata usumbufu kutoka kwa askari wa nchi jirani. Kamati hairidhishwi na kasi ya Serikali katika kuimarisha mipaka ya

nchi yetu Kamati inaishauri Serikali kuimarisha mipaka kwa kuweka alama madhubuti.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati hairidhishwi na utaratibu wa Serikali kupunguza bajeti hususan fedha za maendeleo. Bajeti ya maendeleo imeshuka kutoka shilingi bilioni 30.5 mwaka 2018/19 hadi shilingi bilioni 24.3 mwaka 2019/20. Huu sio mwenendo mzuri kama Serikali imedhamiria kuleta mageuzi katika Sekta ya ardhi hususan katika kupima na kupanga matumizi ya ardhi. Ni matarajio ya Kamati kuwa Serikali itaendelea kuongeza bajeti kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanzisha Mabaraza 97 ya Ardhi na Nyumba. Hata hivyo Kamati inashauri Serikali kutimiza lengo lake la kuwa na Mabaraza ya aina hiyo kwa kila Wilaya hususan kwa kuzingatia vigezo vya umbali, jiografia husika, na wingi wa migogoro. **Kamati inapongeza Serikali kwa kuajiri wenye viti 20 wa mabaraza ya ardhi na nyumba kati ya 44 waliokuwa wanahitajika.** Ni matarajio ya Kamati kwamba Serikali itaendelea kuajiri watumishi wa kutosha kuhudumia mabaraza sambamba na kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya uendeshaji wa mabaraza hayo.

#### **Mpango wa Utekelezaji wa Kazi za Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020**

**Mheshimiwa Spika**, Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 umeainisha kutekeleza shughuli mbalimbali. Baadhi ya shughuli hizo ni kama zifuatazo:-

- a) Kuimarisha usalama wa milki za ardhi;
- b) Kuboresha takwimu za kijiografia nchini;
- c) Kuendeleza utafiti wa vifaa vya ujenzi wa nyumba bora na zenye gharama nafuu kwa ajili ya uendelezaji makazi;

- d) Kuboresha Sera, Sheria, Kanuni na miongozo inayohusu sekta ya ardhi;
- e) Kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi katika miji kadhaa hapa nchini;
- f) Kusimamia upangaji na uendelezaji wa miji nchini;
- g) Kusimamia ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na sekta ya ardhi; na
- h) Kuhamasisha na kuwezesha wananchi kuwa na nyumba bora

**Mheshimiwa Spika**, Kamati iliridhishwa na vipaumbele villyowekwa na Wizara kwakuwa vipaumbele hivi vinaendana na Mpango wa Taifa wa Mwaka 2019/2020 na vinalenga dira, dhima na madhumuni ya Wizara hususani katika kuimariswa usalama wa milki za ardhi, kuboresha sera, sheria, kanuni na miongozo inayohusu sekta ya ardhi pamoja na kuboresha utendaji kazi na utoaji huduma katika sekta ya ardhi.

### **SEHEMU YA TATU**

#### **MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020**

#### **Uchambuzi wa Makisio ya Makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020**

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Fungu 48 inatarajia kukusanya maduhuli ya **shilingi 180,000,000,000/** = kutokana na vyanzo mbalimbali vya mapato katika sekta ya ardhi. Kiasi hiki ni ongezeko la takribani **shilingi Billioni 60** sawa na ongezeko la asilimia 50% ikilinganishwa na **shilingi 120,000,000,000** zilizokadiriwa kukusanywa katika Mwaka wa Fedha 2018/2019. Ongezeko hili linatokana na kuongezeka

kwa kasi ya urasimishaji makazi mijini pamoja na punguzo la ada ya mbele (Premium) kutoka **asilimia 2.5** hadi **asilimia 1** ya thamani ya ardhi katika maeneo ya urasimishaji makazi mijini. Zoezi hili lina lengo la kuwawezesha wamiliki wengi wa ardhi hususan mijini kumudu gharama za kumilikishwa ardhi na hivyo kuiwezesha Serikali kumilikisha ardhi zaidi na kuongeza makusanyo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa **Fungu 03** Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi inatarajia kukusanya jumla ya shilingi **706,000,000** kutokana na vyanzo mbalimbali vya mapato hususani makusanyo ya kodi ya nyumba Tabora, Uuzaji wa vitabu vya miongozo ya upangaji wa matumizi ya ardhi, uuzaji wa nyaraka za zabuni na kutoka kwa wadau wa kimkakati. **Ni mapendekezo ya Kamati kwamba Serikali ihakikishe inasimamia mikakati ya makusanyo iliyojiwekea ipasavyo ili kuweza kufikia malengo ya makusanyo ifikapo Juni 2020, na kuongeza pato la Taifa kwa mwaka.**

#### **Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Mwaka wa fedha 2019/2020**

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Wizara ya Ardhi, Nyumba na maendeleo ya Makazi (**Fungu 48**) inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi **57,439,991,387** Kati ya fedha hizo shilingi **33,155,487,000/-** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi **24,284,504,387/-** = kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kwa ujumla bajeti inayoombwua imepungua kwa shilingi **20,705,180,767** ikilinganishwa na bajeti ya Mwaka wa Fedha 2018/2019 ambapo punguzo hilo ni sawa na asilimia **26%**. Kamati inaona kwamba punguzo hilo linawenza kupelekeea Wizara kushindwa kufikia malengo iliyojiwekea .

Aidha kwa upande wa bajeti ya maendeleo bajeti imepungua kwa shilingi **6,253,097,613** sawa **na asilimia 20.2** ikilinganishwa na shilingi **30,537,602,000** iliyoidhinishwa na Bunge katika mwaka wa fedha 2018/19. Kupungua kwa bajeti kutazorotesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2019/20.

**Mheshimiwa Spika** Kwa upande wa Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, (**Fungu 03**) katika Mwaka wa Fedha **2019/2020** Wizara inaliomba Bunge liidhinishe jumla ya shilingi **5,951,072,000/=** ili ziweze kutumika kutekeleza mpango na bajeti ya Tume. Kati ya bajeti hiyo, shilingi **2,245,072,000/=** ni za Matumizi ya kawaida, na shilingi **3,000,000,000** kwa ajili ya kutekekeleza miradi ya maendeleo. Mchanganuo wa bajeti unaonyesha kuwa bajeti inayoombwa imepungua kwa kiasi cha shilingi **1,830,854,000** ikilinganishwa na bajeti ya Mwaka 2018/19 ya shilingi **7,781,926,000**. Upungufu huu unatokana na kupunguzwa kwa bajeti ya maendeleo kutoka shilingi bilioni **5,000,000,000** mwaka 2018/2019 hadi shilingi bilioni **3,000,000,000**. Hali hii itazorotesha shughuli za upimaji na upangaji wa matumizi ya ardhi nchini.

**Masuala mengine Muhimu yaliyojitokeza wakati wa Kuchambua na Kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kujadili bajeti ya Wizara hii masuala mbalimbali yalijitokeza na kuhitaji kujadiliwa kwa kina ili kuweza kuleta uelewa wa pamoja na kuweza kuishauri Serikali ipasavyo. Maswala haya ni kama yafuatayo:-

- Kumekuwa na taarifa kwamba Shirika la nyumba la Taifa (NHC) linaelekea kufilisika kutockana na kuwa na madeni makubwa kuliko mali zake.
- Kumekuwa na tarifa kwamba kuna mwingiliano wa majukumu ya Tume ya Taifa ya mipango ya matumizi ya Ardhi na Halmashauri za miji, Manispaa na Majiji.
- Kumekuwa na changamoto ya ugawaji wa mashamba makubwa yaliyobatilishiwa milki hali inayosababisha wananchi kuyavamia na hivyo kuleta migogoro.
- Kumekuwa na changamoto ya uwepo wa migogoro ya ardhi baina ya watumiaji mbali mbali

Kutokana na changamoto hizo kamati iliagiza Wizara kuleta mbele ya Kamati Taarifa nne zifuatazo:-

- (a) Taarifa kuhusu hali halisi ya Maendeleo na Utendaji wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC)
- (b) Taarifa kuhusu utendaji wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya ardhi
- (c) Taarifa kuhusu maendelezo ya mashamba makubwa na hatua zinazochukuliwa na Serikali kwa mashamba yasioendelezwa
- (d) Taarifa kuhusu hali ya migogoro ya ardhi nchini

**Mheshimiwa Spika**, Wizara iliyasilisha Taarifa hizo mbele ya Kamati na zikajadiliwa kwa kina. Kutokana na taarifa zilizowasilishwa Kamati imebaini yafuatayo:-

(a) **Shirika la Nyumba la Taifa (NHC)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuteua Bodi mpya ya Shirika pamoja na kuweka Menejimenti mpya. Ni matarajio ya Kamati kwamba sasa kasi ya utekelezaji wa majukumu itarejea kama ilivyokuwa mwanzo. Aidha Kamati imeridhishwa na taarifa ya Shirika iliyotoa taswira ya hali halisi ya shirika kuliko tarifa zilizokuwa zimesambaa katika vyombo mbali mbali vya habari kwamba Shirika liko katika hali mbaya kinyume na ukweli. Kamati inaishauri serikali kutekeleza yafuatayo ili kuliwezesha shirika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi:-

- (i) Serikali ikamilishe utaratibu wa kulipa Shirika idhini ya kukopa ili liweze kukamilisha ujenzi wa miradi mikubwa ambayo kwa sasa imesimama. Hii itasaidia kuliepusha Shirika kupata hasara inayoweza kutokea kwa kutoikamilisha miradi hiyo kwa wakati;
- (ii) Shirika liboreshe zaidi hali ya ukwasi (liquidity) ili kuwa na fedha za kutosha kujiendesha, kulipia mikopo yake

na kubaki na ziada kwa ajili ya uendelezaji wa miradi mingine bila kutegemea mikopo muda wote;

- (iii) Serikali iharakishe mchakato wa kukamilisha Sera ya nyumba itakayotoa mwongozo na kusimamia sekta ya nyumba nchini.
- (iv) Serikali ihakikishe kwamba taasisi zinazohusika zifakishe huduma za miundombinu kama maji, umeme na barabara katika maeneo ya miradi ya ujenzi wa nyumba za Shirika hasa zile za gharama nafuu ili kuwapa nafuu wanunuzi waliokusudiwa. Viled vile Serikali ione uwezekano wa kuliondolea Shirika Kodi ya Ongezeko la thamani kwenye vifaa vya ujenzi. Hali hii itasaidia kupunguza gharama za nyumba kuliko ilivyo sasa ambapo shirika hugharamia uwekaji wa miundombinu hiyo na kusababisha bei ya nyumba kuwa juu. **Aidha Kamati inalipongeza Shirika kwa kubuni mradi wa kujenga nyumba elfu moja kwa ajili ya makazi katika jiji la Dodoma ambayo ni makao makuu ya nchi. Ni ushauri wa Kamati kwamba nyumba zinazojengwa ziwe ni zile zenye hadhi ya jiji.**
- (v) **Utendaji wa Tume ya Taifa ya Mipango ya matumizi ya ardhi**

**Mheshimiwa Spika**, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ina majukumu makubwa kitaifa ambayo yanalenga kuhakikisha kuwa ardhi na raslimali zake zinatumika kwa tija na uendelevu. Pamoja na majukumu haya makubwa na Tume kujitahidi kufanya kazi kwa juhudhi, muundo na uwezo mdogo wa Tume umeifanya isiweze kutimiza majukumu yake ya kuratibu, kushauri, kuandaa, kukagua na kusimamia utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi. Aidha Kamati imebaini kuwepo kwa majukumu makubwa kwa Tume ikilinganishwa na bajeti inayotengwa kwa ajili ya kupima na

kupanga matumizi ya ardhi katika vijiji, miji, wilaya, Manispaa na Majiji. **Kamati inaishauri Serikali** itenye bajeti ya kutosha kwa ajili ya Tume. Aidha Serikali ipitie upya Sheria iliyoanzisha Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya ardhi kwa lengo la kuiboresha na kuipandisha hadhi Tume kuwa Mamlaka ili kuipa nguvu zaidi za kisheria kusimamia upimaji, upangaji na utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi. Mabadiliko haya pia yatasaidia kuimarisha usimamizi wa matumizi bora ya ardhi nchini, kuongeza uzalishaji, kuondokana na migogoro ya matumizi ya ardhi, uharibifu wa mazingira na raslimali ardhi hasa katika kipindi hiki ambapo Taifa letu linanaelekea kwenye uchumi wa viwanda.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutenga fedha kuititia Tume ya Mipango ya Matumizi ya ardhi kwa ajili ya mradi wa kupima na kupanga matumizi ya ardhi katika vijiji vyote vinavyopitiwa na Bomba la Mafuta, Wilaya na vijiji vyote vya mipakani na Wilaya na vijiji vilivyokuwa na makambi ya wakimbizi. Mradi huu siyo tu utasaidia kuibua fursa za kiuchumi katika maeneo husika bali pia utaimarisha utawala bora wa ardhi na hivyo kuondoa uwezekano wa kutokea migogoro ya ardhi wakati wa ujenzi wa bomba la mafuta kama ilivyokuwa katika ujenzi wa bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Dar Es Salaam.

(vi) **Maendelezo ya Mashamba makubwa na hatua zinazochukuliwa na Serikali kwa mashamba yaliyotelekezwa**

Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua inazochukua za kubatilisha milki za mashamba makubwa yasiyoendelezwa. Ili kuondoa malalamiko kuhusu utaratibu unaotumika kugawa mashamba makubwa yaliyofutiwa milki zake, **Kamati inaishauri**

Serikali ihakikishe kwamba Halmashauri zinazohusika na mashamba yaliyobatilishiwa milki zake, ziandae mapendekezo ya mpango wa matumizi ya mashamba hayo haraka na kuyawasilisha katika ngazi za juu kwa uamuzi kuliko kuchelewa kuyapangia matumizi na hivyo kusababisha yavamiwe na wananchi na hivyo kusababisha migogoro.

**(vii) Hali ya migogoro ya ardhi nchini**

Kwa muda mrefu sana kumekuwa na migogoro mingi ya ardhi baina ya watumiaji mbali mbali hali inayochangiwa kwa kiasi kikubwa na sehemu kubwa ya ardhi yetu kutopimwa na kupangiwa matumizi na kukosa Mamlaka ya kusimamia matumizi ya ardhi. Tunaipongeza Serikali kwa kubuni mradi wa kupima, kupanga matumizi na kumilikisha ardhi unaotekelizwa kwa majoribio katika Wilaya za Kilombero, Malinyi na Ulanga ambao umeonyesha mafanikio makubwa. Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha za kutosha ili mradi huu utekelezwe nchi nzima. Kipekeeee, Kamati inampongeza Mheshimiwa Rais Dkt John Pombe Joseph Magufuli, kwa hatua yake ya hivi karibuni kuteua Kamati ya Mawaziri wanane kushughulikia migogoro ya ardhi katika maeneo yote ya hifadhi nchini. Hatua hii inalenga kumaliza kabisa migogoro ya ardhi baina ya wananchi na Mamlaka za uhifadhi hapa nchini. Ni matarajio ya Kamati kwamba ripoti itakayoandaliwa na Kamati hii inakwenda siyo kupunguza tu bali kumaliza kabisa migogoro ya ardhi katika maeneo ya hifadhi hapa nchini. Aidha ni matarajio ya Kamati kwamba Serikali itahakikisha inaweka mkakati wa kushughulikia migogoro ya ardhi katika maeneo mengine. Hali hiyo itawapa wananchi fursa ya kufanya shughuli zao za kiuchumi kwa amani na hivyo kuongeza tija na kukuza uchumi wa Taifa.

## **SEHEMU YA NNE**

### **MAONI NA USHAURI WA JUMLA**

**Mheshimiwa Spika**, Sekta ya Ardhi inakabiliwa na changamoto kubwa ya kuongezeka kwa migogoro ya ardhi, ujenzi holela, na kukosekana kwa mipango ya matumizi bora ya ardhi. Kamati inaishauri Serikali kutekeleza yafuatayo ili kunusuru sekta hii muhimu;:-

- (a) Kuendelea kuzisimamia na kutekeleza kikamilifu Sheria zote za ardhi ili kuongeza ufanisi katika kutoa huduma za ardhi. Aidha, sheria zilizopitwa na wakati ziletwe Bungeni kwa ajili ya kufanyiwa marekebisho;
- (b) Kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu sheria mbali mbali za ardhi ili kupunguza migogoro;
- (c) kuyaimarisha Mabaraza ya Ardhi yaliyopo kwa kuyapatia vitendea kazi sambamba na kuajiri wafanyakazi wa kutosha kwa ajili ya kuendeleza mabaraza ya ardhi. Aidha Serikali ihakikishe kuwa Watendaji wa Mabaraza haya wanafanya kazi kwa uadilifu mkubwa na kuondoa malalamiko yaliyopo sasa kwamba Mabaraza hayo yamegubikwa na vitendo vya rushwa;
- (d) Kuandaa mkakati wa kitaifa utaohakikisha kuwa Serikali inatenga fedha za kutosha kwa ajili ya kupima na kupanga matumizi ya kila kipande cha ardhi ya nchi yetu;
- (e) Kuwashirikisha kikamilifu wananchi katika kupanga matumizi na kusimamia ugawaji wa ardhi ya mashamba yaliyofutiwa milki;
- (f) Kuhakikisha kuwa fidia stahiki kwa ajili ya ardhi iliyotwaliwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo inalipwa ipasavyo;

- (g) Kupitia upya sheria ilioanzisha Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ili kuipa nguvu ya kusimamia upimaji, upangaji na utekelezaji wa matumizi ya ardhi;
- (h) Kushirikisha wananchi katika zoezi la urasimishaji makazi holela mijini ili kupunguza malalamiko yanayoweza kutokea. Aidha Serikali ipunguze gharama za upimaji sambamba na kuweka utaratibu wa wananchi kulipia gharama za upimaji kwa awamu; na
- (i) Kutoa elimu kwa wananchi juu ya kuwepo kwa fursa za kupata mkopo kutoka katika taasisi za fedha zinazokopeshwa na Tanzania Mortgage Refinance Company kwa masharti nafuu ili kuwawezesha wananchi kuitumia fursa hiyo kujenga nyumba za kisasa hasa wale wanaoishi vijijini.

## **HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa hii. Kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ambaao Maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Kemirembe Julius Lwota, Mb-M/ Mwenyekiti - Mjumbe
2. Mhe. Nape Mosses Nnauye, Mb - Mjumbe
3. Mhe. Grace Sindato Kiwelu, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Magdalena Hamis Sakaya, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Pauline Philip Gekul, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Halima Abdallah Bulembo, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Khalifa Salum Suleiman, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Lucy Fidelis Owenya, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Lucy Thomas Mayenga, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Timotheo Paul Mnzava, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Salim Abdallah Turky, Mb - Mjumbe

- |     |                                     |          |
|-----|-------------------------------------|----------|
| 12. | Mhe. Boniface Mwita Getere, Mb      | - Mjumbe |
| 13. | Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb        | - Mjumbe |
| 14. | Mhe. Shabani Omari Shekilindi, Mb   | - Mjumbe |
| 15. | Mhe. Neema William Mgaya, Mb        | - Mjumbe |
| 16. | Mhe. Mch. Peter Simon Msigwa, Mb    | - Mjumbe |
| 17. | Mhe. Flatei Gregory Massay, Mb      | - Mjumbe |
| 18. | Mhe. Risala Saidi kabongo, Mb       | - Mjumbe |
| 19. | Mhe. Dkt Jasmine Tiisekwa Bunga, Mb | - Mjumbe |
| 20. | Mhe. Dkt Stephen Lemomo Kiruswa, Mb | - Mjumbe |
| 21. | Mhe. Yussuf Haji Khamis, Mb         | - Mjumbe |
| 22. | Mhe. Yussuf Salim Hussein, Mb       | - Mjumbe |
| 23. | Mhe. Zainab Nuhu Mwamwindi, Mb      | - Mjumbe |
| 24. | Mhe. Mbarouk Salim Ali, Mb          | - Mjumbe |
| 25. | Mhe. Salim Abdallah Turky, Mb       | - Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kumshukuru Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi **Mhe. William V. Lukuvi, (Mb)** Naibu Waziri, **Mhe.Dkt Angeline L. Mabula, (Mb)**, Katibu Mkuu na Wataalam wote wa Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa ushirikiano waliota kwa Kamati wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge wakiongozwa na **Ndg. Stephen Kagaigai** Katibu wa Bunge, Ndg. **Athuman Hussein** Mkurugenzi wa Idara ya Kamatiza Bunge, **Ndg. Dickson Bisile** Mkurugenzi Msaidizi, Makatibu wa Kamati hii, Ndg. **Haika Mtui, Gerald Magili**, na Msaidizi wa Kamati Ndg. **Mwimbe John** kwa kuihudumia vyema Kamati pamoja na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kama yalivyowasilishwa na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Kemirembe Julius Lwota, Mb.

**M/MWENYEKITI,**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI,**

**MALIASILI NA UTALII,**

Mei, 2019

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Shaban Shekilindi Mjumbe wa Kamati ya Ardhi Maliasili na Utalii tunakushukuru sana kwa kutusomea taarifa ya kamati vizuri sana mwanzo mwisho.

Sasa Waheshimiwa Wabunge ni hatua ambayo sasa inabidi nimuute Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara hii ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mheshimiwa Wilfred Lwakatare na kwa sababu ni nia yangu usome hotuba yako mwanzo mwisho bila kuleta shida yoyote nikwambie tu kwamba ukurasa wa 30 lile fungu (m) lenye vifungu vidogo 101 hadi 104, kuhusiana na ubaguzi. Hii ni *claim* nzito sana inahitaji kujengewa hoja katika utaratibu mwingine wa Kikanuni kwa leo nimeona kwamba hebu, hii usiwasilishe, mengine yote wewe soma tu, uiache hiyo ya ubaguzi ya M basi, maana hatupendi kusisitiza masuala ya ubaguzi katika nchi yetu ndiyo maana, endelea Mheshimiwa dakika zako nazilinda. (*Makofii*)

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE – MSEMADI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na nguvu ili kuweza kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2019/2020, na kutokana na muda na ukubwa na urefu wa hotuba yenyewe nitaomba taarifa nzima na maoni yetu ya Kambi ya Upinzani yaingizwe yote katika Hansard. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru wanachama na wananchi wote wa Bukoba *Town* kwa ushirikiano wanaonipatia katika kuhakikisha tunamaliza au kupunguza kero zinazowakabili wakazi wa mji wetu. Niwape pole kwa madhira ya mafuriko waliyoyapata ikiwemo kifo cha mtoto na uharibifu wa nyumba zaidi ya 75. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na kwa kuwa tayari Manispaa ya Bukoba kuitia Mkandarasi *CRM* wametayarisha rasimu ya mwisho ya *Master Plan* 2018 - 2038, bila shaka suala la namna ya kuepukana na hali ya mafuriko yanayoukumba mji mzima wa Bukoba utapatiwa majibu na taarifa hiyo.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze waheshimiwa na viongozi wa chama wenye kesi mbalimbali za kisiasa ambazo zimekuwa zinawaweka mahabusu, jela na kuwekwa katika sokomoko la kila siku, lakini kwa uzoefu nillionao wa kukaa ndani zaidi ya siku 118. Nafikiri, wasife moyo kwa sababu huo ni moshi mweupe kuelekea kwenye ushindi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini sio kwa umuhimu nitoe shukrani sana kwa familia yangu mke wangu Angel na watoto wangu Frank, Lovelet, Doreen na Vick, kwa Kunivumilia katika harakati za siasa kwa kipindi chote ambacho hulazimika kuwa mbali na familia.

Mheshimiwa Spika, haki za makazi unaposema Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, jambo la kwanza kwa mtanzania wa kawaida ni haki ya kupata ardhi kwa ajili ya kuishi yeye na familia yake, makubaliano ya mwaka 1996 nchini Uturuki yaliyojulikana kama, *Instanbul Agreement and Habitat Agenda*. Haki za Makazi ni suala na Haki za Kibinadamu, na pia hili liko kwenye Ibara ya 25 ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Binadamu, yaani *Universal Declaration of Human Rights*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, Ibara ya 11 ya mkataba wa *International Covenant on Economic, Social and Cultural Rights* inatoa uhakika kwamba haki ya makazi ni kama haki ya kiwango cha maisha timilifu.

Mheshimiwa Spika, haki ya makazi ni pamoja na haki ya kutoingiliwa bila sababu kwenye mambo binafsi ya familia au nyumbani; haki ya usalama ikiwa ni pamoja na uhakika wa kisheria wa upangaji; kulindwa kisheria na kufidiwa na mahakama kwa ukiukwaji wa haki za makazi.

Mheshimiwa Spika, pia haki ya kulindwa kutokana na *forced evictions*, kubomolewa au/na kuharibiwa kwa makazi ikiwa ni pamoja na kukaliwa kijeshi, vita vyta kimataifa na vita vyta wenye kwa wenye kwa wenye kuanzishwa kwa makazi mapya ya wageni, kuhamisha wakazi na miradi ya maendeleo. Hii yote inatakiwa kusimamiwa vyema na Wizara hii ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, changamoto zilizopo hadi sasa za Haki za kupata Makazi ni pamoja na; Umiliki wa Makazi Upatikanaji wa Viwanja Ujenzi wa Makazi Upatikanaji wa Fedha za Ujenzi Vipato duni vyta Wananchi Bei kubwa ya kuuza Viwanja, Idadi ndogo ya viwanja vinavyopimwa. Kukosekana kwa Miundombinu yaani umeme, maji, simu, mfumo wa majitaka katika maeneo yanayopimwa, lakini pia, Serikali kushindwa kuandaa mpango kabambe kuzuia ukuaji wa makazi holela pembezoni mwa miji yake.

Mheshimiwa Spika, Anguko la Sekta ya Nyumba Nchini, kwa sasa sekta ya nyumba hasa majengo makubwa ya biashara inapitia katika changamoto kubwa sana kutokana na kuyumba kwa uchumi na biashara nyingi kufungwa, inakadiriwa kuwa kwa sasa kuna mita za mraba 300,000 ambazo ziko wazi hazina wapangaji. Wapangaji wengi wameshindwa kuhimili bei za majengo makubwa ambazo zilikuwa zinatozwa kwa dola.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuporomoka na kuyumba kwa uchumi, inakadiriwa kuwa kwa sasa ni 35% hadi 45% ya majengo makubwa ya kibashara na maduka hayana wapangaji. Hii sio ishara njema, maana yake tafsiri pana ya anguko hili ni kuwa Serikali itakosa mapato kwa sababu biashara zinafungwa na pia kutakuwa na ongezeko la mikopo ya nyumba isiyolipika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza Bunge kuchukua hatua za haraka ikiwa ni pamoja na kuunda Kamati teule ya kuchunguza na kuishauri Serikali ili kuokoa sekta ya majengo nchini ambapo imefikia hata Jijini Dar es Salaam watu wengine na Makampuni na Taasisi nyingine wameamua kuhamishia shughuli zao na biashara katika mitandao na katika maeneo ya makazi ambapo gharama za kupangisha ni ndogo ukilinganisha na gharama za majengo makubwa katikati ya Jiji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wakati wa Bunge la Kumi mwaka 2011 tulipendekeza na kuishauri Serikali kuleta Bungeni Muswada wa kuanzisha mamlaka ya kusimamia sekta ya majengo makubwa ambapo leo ni miaka saba tangu tutoe ushauri huo, lakini Serikali iliahidi kuleta muswada lakini bado hilo halijafanyika.

Mheshimiwa Spika, katika Randama ya Wizara Serikali imesema kuwa muswada kwa ajili ya kuanzisha Mamlaka ya Majengo Nchini upo katika hatua za mwisho, hata hivyo tunaomba huo Muswada basi ukamilishwe na kuletwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, tunataka kauli ya Waziri kuhusu hatua ambazo Serikali itazichukua kuokoa sekta ya nyumba nchini kwa sababu kuyumba kwa sekta hii muhimu kunaenda sambamba na kuathiri sekta ya fedha na uchumi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi, (*NHBRA*) Wakala huu ulianzishwa mwaka 2001 chini ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa lengo la kutoa huduma na kupunguza gharama kwa vifaa vya ujenzi kwa makazi bora. Taasisi hiyo pia imekuwa ikijihuisha na mafunzo teknolojia ya ujenzi wa nyumba za bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, kuna uhitaji mkubwa wa tafiti ambazo zitawezesha Watanzania kupata makazi bora ya kudumu. Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza Wakala huyu

amejii marisha kwa kiwango gani? Ukweli ni kuwa Wakala huyu amekuwa *dormant*.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa sasa hivi linalozua Watanzania wengi kuwa na makazi bora ni kutokana na gharama kubwa ya vifaa vya ujenzi, ambavyo ni nguzo kubwa katika ujenzi. Vifaa hivyo vyenye gharama kubwa ni pamoja na vifaa vinavyofanyiwa utafiti na Wakala huyu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mnamo Mei tarehe 6 mwaka 2014 aliye kuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi alishauri kupunguzwa au kuondolewa kwa kodi katika vifaa vya ujenzi ili watanzania wengi waweze kujenga nyumba bora.

Mheshimiwa Spika, hata Septemba 5, 2018 Mheshimiwa Rais akiwa mjini Mwanza kushuhudia utiaji saini wa mikataba minne ya ujenzi wa meli kubwa chelezo na ukarabati wa meli za MV Butiama na MV Victoria, Rais Dkt. John Pombe Magufuli alitoa maelekezo kwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi na wa Waziri wa Fedha na Mipango, Dkt. Philip Mpango kukutana haraka ili kumaliza kilio cha kodi kwenye vifaa vya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kupata ufanuzi kuhusu utekelezaji wa maelekezo ya Mheshimiwa Rais kuhusu kupunguza kodi kwenye vifaa vya ujenzi?

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kabisa kama alivyoshauri Mheshimiwa Prof. Anna Tibajuka wakati ule kwamba iwapo kodi kwenye vifaa vya ujenzi itapungua Watanzania wengi watamu du kumiliki makazi bora zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Nchi ya Rwanda imefanikiwa kusimamia programu ya kuondosha nyumba za kuezekwa kwa nyasi, inakuwaje kwetu sisi nchi yenye rasilimali kibao tunashindwa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa ya Mipango na Matumizi ya Ardhi, ardhi ni mali; ardhi ni mojawapo ya kisababishi kikubwa cha migogoro ya wenyewe kwa wenyewe kwa nchi za Kiafrika, na ili kutimiza lengo hilo la kuondoa migogoro, ndio sababu kubwa ya uwepo wa Tume ya Taifa ya mipango na matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa Tanzania ina tatizo kubwa la upangaji na utumiaji wa ardhi ili makundi yote ya kijamii kuweza kushiriki katika shughuli zake za kiuchumi na kijamii bila ya kuwepo wa migogoro yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Taarifa ya Tume ya *National Land use Framework Plan* ya 2013 - 2033 iliyotolewa mwaka 2014, inaeleza changamoto nyingi zinazoikabili sekta ya ardhi, lakini changamoto zote hizo zimetengwa katika makundi makuu mawili ambayo ni matumizi na upangaji wa ardhi, lakini pamoja na masuala ya Kitaasisi.

Mheshimiwa Spika, Ukitanya rejea ya taarifa ya Tume ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka 2018/2019 inaonesha kuwa tume ina changamoto ya uhaba wa watumishi kwa asilimia 63.8, ina magari matatu tu na magari manne yameharibika vibaya, Tume ina upungufu wa vifaa vyaa upimaji *computers*, mashine za uchapishaji nakadhalika. Aidha kuna uhaba mkubwa wa rasilimali fedha ambazo unasababisha kasi ndogo ya uandaaji wa mipango mahsusii ya matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, tarehe 7 Februari 2019 Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mheshimiwa William Lukuvi aliongoza kikao cha Mawaziri wenzake sita kujadili changamoto mbalimbali za matumizi ya sekta ya ardhi. Mawaziri walioshiriki kikao hicho ni pamoja na Waziri wa Maliasili na Utalii, Wizara ya Kilimo, Uvuvi na Mifugo, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Maji, Wizara ya Ulinzi, na Wizara ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, vikao hivi hata vikikaa kila siku au kila mwezi haviwezi kutatua changamoto tajwa ambazo zinajulikana, suluhu yake ni uwepo wa rasilimali watu, fedha, vitendea kazi, kwani mkakati wa utatuzi upo tayari, vikao vingi nya kisiasa ni kuongeza matumizi yasiyo na sababu? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, taarifa ya utekelezaji inaonesha kuwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Tume ilitengewa jumla ya shilingi 7,081,926,000.00 kati ya hizo fedha, fedha za maendeleo zilikuwa ni shilingi 5,000,000,000.00. Katika fedha hizo zilizotengwa kwa miradi ya maendeleo hadi Januari 2019 hakuna hata shilingi moja ambayo ilitolewaw toka Hazina. Japokuwa wanasema tengeo la 2018/19 liliongezeka kwa asilimia 234 kulinganisha la lile la shilingi 2.1 lakini, kama tengeo liliongezeka lakini hiyo pesa haikutolewa hata shilingi katika utendaji kazi wa Tume haina maana yoyote? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Kama Serikali inasema kuwa kila mwezi inakusanya kiasi ya shilingi trilioni 1.3 inakuwaje inashindwa kutoa fedha ambazo zinakuwa zimetengwa na kuidhinishwa na Bunge? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Mwezi Februari 2019 Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Shirika la Kilimo *FAO* walizindua Mradi wa Msada wa Kitaalamu wa Kukuza Uwezo wa Wadau katika Kuratibu Mfumo wa Utawala wa Ardhi hapa nchini. *FAO* iliandaa mipango hii kwa muktadha wa usalama wa chakula.

Mheshimiwa Spika, Uzinduzi rasmi wa mradi huu ulifanyika Wilaya ya Mvomero, mkoani Morogoro mbali ya Wilaya ya Mvomero, mradi huu pia utatekelezwa katika Wilaya za Kilombero, Malinyi, Kilosa na Ulanga ambayo ni maeneo yanayofahamika kwa migogoro ya ardhi hususan baina ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kufahamu ni kwa vipi mradi huu wa *FAO* unashirikisha Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi?

Kwani majukumu ya mradi huo ndiyo madhumuni na majukumu ya Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, Milki za Mashamba Nchini, hadi Oktoba, 2018 takribani mashamba 1,926 yalikuwa yamehakikiwa kwa lengo la kujua hali halisi ya maendelezo yake. Jumla ya mashamba 114 yamebatilishwa umiliki katika kutetea uamuzi huu wa Serikali, taarifa hiyo imenkuu Sheria ya Ardhi Sura 113, kifungu cha 45(2) kinachompatia mamlaka Mheshimiwa Rais kubatilisha milki zote.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani haina tatizo na uamuzi huo wa Kisheria kusitisha milki za mashamba hayo, hoja yetu ya msingi ni je, utaratibu gani unatumika hadi Mheshimiwa Rais anafuta milki za awali na pia utaratibu gani unatumika kufanya *re-allocation* kwa milki zilizofutwa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Hapa kuna tatizo kubwa kwani baadhi ya milki inasemekana zimefutwa kwa sababu za kisiasa au sababu za kibinagsi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ieleze ni utaratibu gani wa wazi unaotumika kufuta na kugawa upya mashamba yaliyotaifishwa?

Mheshimiwa Spika, Mashamba yaliyofutiwa milki mwaka 1997 na kukabidhiwa kwa wananchi ni pamoja na Kilimanjaro *Sisal Estate* Mkundi B; Kihonda *Sisal Estate* Mkundi A; Tungi *Sisal Estate* Mkundi C, lakini wananchi walikuwa wanatumia ardhi hiyo toka mwaka 1984. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mwaka 2017 alipoingia Mkuu wa Mkoa kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya wamekuwa wakitumia vyombo vyaya dola kutaka kuwaondoa wananchi hao kwa nguvu ilhali wakifahamu kuwa eneo hilo tayari wananchi walikwisha kabidhiwa na aliyekuwa analimiliki.

Mheshimiwa Spika, Tunashauri, Mheshimiwa Waziri aingilie kati mgogoro huo wenye sura ya maslahi binafsi na rushwa kwani kisingizio kikubwa ni kuleta wanasesma ni kuleta mwekezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Pia, pamekuwepo na mgogoro wa miaka mingi kati ya Mkoa wa Dar Es Salaam na Mkoa wa Pwani wa mipaka katika Mitaa ya Kisopwa na Mloganzila. Wananchi wa mitaa hiyo huduma zote muhimu wanazipata Manispaa ya Kinondoni, walikuwa wanazipata Manispaa ya Kinondoni na sasa wanazipata Manispaa ya Ubungo. Ikiwemo na suala la upigaji kura. Wilaya ya Kisarawe imekuwa ikidai kwamba mitaa hiyo ipo katika Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe kauli mitaa hiyo ipo katika Mkoa upi kati ya Dar Es Salaam na Pwani? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Mgogoro Mpya wa Kiwanda cha Twiga na Wakazi wa Chasimba kumbukumbu zinaonesha kuwa Mheshimiwa Waziri Lukuvi akiwa na timu yake yote ya utendaji mnamo tarehe 13 Juni, 2015 walifanikiwa kumaliza mgogoro uliokuwepo baina ya Kiwanda cha Simenti cha Twiga na Wakazi wa Chasimba, na suala hilo liko katika muhtasari ambao pia umeambatanishwa na taarifa yangu hii.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lukuvi katika kikao hicho kilitoa maazimo saba, ambayo pia yanapatikana katika muhtasari huo nilioutaja lakini pia katika kitabu changu cha taarifa.

Mheshimiwa Spika, Maazimio hayo yalisainiwa tarehe 30 Juni, 2015, katika hali ya kushangaza ni kuwa uongozi mpya wa Kiwanda cha Twiga umekuja na mambo mengine mbali na makubaliano yaliyoongozwa na Mheshimiwa Waziri Lukuvi na hivyo kuanzisha mtafaruku mpya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Hii ni kutokana na barua ambayo tarehe 31 Januari, 2019 iliandikwa kwenda kwa Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Kawe. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Ni ukweli kuwa, Mheshimiwa Waziri Lukuvi amekuwa jasiri na kinara katika kutoa suluhu

ya migogoro mingi ya ardhi nchini na mgogoro huo wa Chasimba alikwisha upatia suluhi mwaka 2015. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Sasa, Kambi inataka kujua kulikoni Chasimba? Kwa Wizara kushindwa kutekeleza maazimio ya makubaliano yaliyosimamiwa na mwenyewe Waziri Lukuvi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Udhafifu katika Mpango miji na usimamizi wa ardhi, tafiti zinaonyesha kuwa 62.5% ya wakazi wote wa miji wanaishi kwenye makazi yasiyokuwa rasmi na 37.5% pekee ndiyo wanaishi kwenye makazi katika maeneo ambayo yamepimwa.

Mheshimiwa Spika, mpaka Juni mwaka 2015, takwimu zilikuwa zinaonyesha kuwa ardhi ya jumla (*General land*) mbayo illikuwa imepimwa illikuwa na jumla viwanja milioni 1.6 na mashamba ambayo yalisajiliwa kwa hati yalikuwa 23,000 pekee na pia leseni za makazi zilikuwa ni jumla ya 379,000. Kwa maana hiyo inakisiwa kuwa 10% pekee ya ardhi ndiyo imepimwa. Kwa tafsiri ya moja kwa moja ni kuwa katika nchi yetu takribani 90% ya ardhi ya jumla haijapimwa na hivyo haijatolewa kisheria kumilikishwa kwa wananchi. Pamoja na ukweli kuwa ardhi ya jumla haijapimwa kwa 90% Wizara katika randama wanaonesha kuwa wanatekeleza mradi wa kupima ardhi za vijiji katika Wilaya za Ulanga na Malinyi. Hili ni jambo jema lakini vema Serikali ikaja na mkakati wenyewe mashiko na wenyewe kasi stahiki wa kuhakikisha kuwa ardhi ya jumla inapimwa na kumilikishwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Jiji la Dar es Salaam limekuwa likikumbwa na mafuriko mara kwa mara na Serikali haijaweka wazi kuhusu uwepo au kutokuwepo kwa mpango mkuu (*master plan*) wa matumizi na uendelezaji wa ardhi katika Jiji. Jambo ambalo linasababisha watu kuendelea kujenga na kuanzisha miji mingine nje ya Jiji ambayo haijapangwa. Aidha Serikali imekuwa na maamuzi ya kisiasa zaidi kuliko kutegemea ushauri. Mathalani, Serikali iliwhamisha kwa nguvu wakazi wa Mkwajuni na Jangwani

na kwa kubomoa makazi yao lakini ni Serikali hiyo hiyo ambayo imewaruhusu Kampuni ya mabasi yanayokwenda kasi kujenga kituo cha maegesho Jangwani huku wakijua ile ni sehemu ambayo maji ya Bonde la Msimbazi hukusanyaika pale kuelekea baharini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kwa Bunge kuitia Kamati yake ya Miundombinu au kuundwa kwa Kamati Teule ya Bunge ili kuhakikisha kuwa Bunge linakuwa sehemu ya kusimamia Jiji la Dar es Salaam kuepukana na majanga yanayojirudia na kuhakikisha kunakuwa na *master plan* ya Jiji ambayo haiwaumizi wananchi. Aidha, tunamtaka Waziri katika hili la Dar es Salaam la mafuriko ya mara kwa mara atoe maelezo hapa Bungeni kuhusu mamlaka na maafisa waliohusika kutoa kibali kwa kampuni *UDART* kuruhusiwa kujenga kituo cha maegesho katika eneo la Jangwani huku wananchi wakihamishwa kwa madai kuwa ni eneo hatari kwa makazi. Juzi mmeona kasheshe iliyotokea hapo hapo katika bonde hilo na hasa katika makao ya *UDART* ambao walikaa kwenye kisiwa na wakatoka humo kwenye ofisi kwa kuogelea.

Mheshimiwa Spika, Serikali kushindwa kutatua changamoto za uuzaji na ugawaji wa ardhi nchini. Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Fedha za Serikali ya ufanisi katika ugawaji wa viwanja nchini, (*CAG Performance Audit Report on the Management of Plots Allocation*) imedhihirisha kuwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeshindwa kusimamia na kutatua changamoto za umilikishaji wa ardhi kwa wananchi. *CAGameeleza* pia kuwa bei za maeneo ambayo yalitangazwa kuuzwa zilikuwa kubwa kiasi cha watu wengi kushindwa kugharamia na kukidhi vigezo ili wamilikishwe viwanja. Hivyo watu hao huamua kutafuta maeneo ya mashamba au yale ambayo siyo rasmi na kuamua kujenga makazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani ingetegemea kuwa Serikali ambayo inaona mbali ingeanza

kupima miji ya pembezoni mwa Jiji (*Peri-Urban*) ili kuepuka changamoto za makazi holela za maeneo hayo na kuhakikisha kuwa miji ya pembezoni inayochipukia inapimwa na kuwekewa miundombinu pamoja na huduma mbalimbali za kijamii. Kwa kuwa ulipaji kodi wa viwanja ambavyo humilikishwa huwa ni jambo la muda mrefu, Kambi Rasmi ya Upinzani haioni sababu ya ulipaji malipo ya awali kuwa makubwa.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya CAG inaonesha pia kuwa Wizara imeshindwa kusimamia na kutoa maelekezo kuhusu miradi mbalimbali inayotekelawa na Wizara yenye au halmashauri. Tofauti na jinsi ilivyokuwa inategemewa, Wizara imejikita kukusanya kodi ya pango la ardhi pekee kuliko kusimamia ugawaji na umilikaji wa ardhi kwa ufanisi ili pia kodi wanayoipigia kelele iweze kukusanywa na kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ambazo zimekuwa zikitekeleza miradi imeonekana kuwa hazina vifaa vya kitaalamu vya kufanya kazi hii. CAG alisema vifaa hivi vinahitaji siyo chini ya milioni 50 sasa Kambi ya Upinzani inashauri, kwa kuwa suala hili ni muhimu na nilakuongezea Serikali fedha, ingefaa hata ile milioni 50 ilioyahidiwa kwa kila kijij basi ingeelekezwa katika kununua vifaa hivi kama alivyoshauri CAG. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Urasimishaji makazi; Serikali kwa kushirikiana na kampuni binafsi za mipangomiji na upimaji, inatekeleza programu ya miaka 10 ya urasimishaji makazi na kuzuia ujenzi holela mijini.

Mheshimiwa Spika, ili kutatua changamoto hizo Kambi ya Upinzani tunashauri Serikali ifanye yafuatavyo; Wizara itoe tamko kwa halmashauri kusaidia katika suala la urasimishaji inayofanywa na makampuni mbalimbali yaliyojitokeza, lakini pia baadhi ya halmashauri zisiziachie kampuni zifanye kila kitu hata katika kuhamasisha zoezi hili; Wizara ikataze halmashauri zinazotaka kupunguza tozo

ambayo wananchi wanalipa kwa ajili ya urasimishaji na kuweka katika mfuko wa jumla wa halmashauri kama *own source*.

Mheshimiwa Spika, Mpango kabambe wa Jiji la Dar es Salaam; Kambi Rasmi ya Upinzani imetathmini baadhi ya mijadala kusikiliza *draft* ya *master plan* ya Dar es Salaam inayoratibiwa na Wakurugenzi wa Manispa ya Jiji la Dar es Salaam na imegundulika kuna udhaifu mkubwa. Kwa uzito wa Jiji la Dar es Salaam, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri Serikali kuwasilisha Bungeni rasimu ya mpango kabambe wa Jiji la Dar es Salaam kwa ajili ya Wabunge kama wadau wakuu wa maendeleo ya Jiji kushiriki katika mchakato na kuwasilisha maoni na mapendekezo yao.

Mheshimiwa Spika, Migogoro kati ya mamlaka za hifadhi na wananchi; Kambi Rasmi ya Upinzani inaunga mkono kabisa kabisa mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Ardhi. Ni mapendekezo mazuri na ifike mahali ambako Serikali iweze kufanya utekelezaji wa mambo mbalimbali ambayo ameyazungumza Waziri katika hotuba yake. Kambi Rasmi ya Upinzani inalitaka Bunge pia kuingilia kati ili kuja na suluhisho la kudumu kuhusu migogoro ya ardhi ambayo imekuwa inajitokeza mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, kodi ya majengo na malalamiko ya wananchi kuhusu thamani ya majengo. Kambi Rasmi ya Upinzani kwa miaka mitatu mfululizo imepinga uamuzi wa Serikali kupoka halmashauri chanzo cha mapato kinachotokana na kodi ya majengo. Hivi sasa limeibuka sakata lingine la utaratibu mbovu wa kufanya tathmini za nyumba za wananchi kwa kuongeza thamani ya nyumba ili waweze kulipa kodi kubwa ya majengo. Jambo hili linalalamikiwa sana na wananchi kwa sababu halmashauri nyingi ambazo zimefanya kinachoitwa tathmini ya nyumba hawajawashirikisha wananchi ambao ndio wamiliki wa majengo hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka maelezo ya Waziri wa Ardhi ya sababu zinazopelekea Serikali

kufumbia macho utaratibu wa kufanya tathimini ya nyumba za wananchi bila kuzingatia utaratibu uliowekwa kwa mujibu wa sheria ambao umefanywa kwa kuwavizia wananchi. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali imuelekeze Mthamini Mkuu kufuta tathmini zilizofanywa katika halmashauri mbalimbali nchini ikiwemo Manispaa ya Bukoba Mjini ambapo tathmini ilifanyika bila kuzingatia taratibu.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Taifa la Nyumba; Kambi ya Upinzani inataku kujua hatma ya miradi ya *National Housing Corporation* iliyokwama tangu 2017 tena mingine ilikuwa imekopa fedha benki *TIB*, hatma yake ni nini na mkwamo huo utatoka lini?

Mheshimiwa Spika, yatokanayo na hotuba ya Upinzani kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Ni ukweli usiopingika ukiangalia bajeti ya 2017/2018, 2018/2019, bajeti ambayo imepitishwa na Bunge lako tukufu imekuwa inapitishwa lakini kile kinachokwenda katika Wizara hii ni kiasi kidogo kweli kweli. Kiujumla inaonekana Bunge limekuwa likipitisha fedha lakini kuna usugu wa Serikali kutotoa fedha hizo. Hata leo Kambi ya Upinzani inaona huenda mchezo ukawa huo huo kwa fedha iliyoombwa. Kwa hiyo, tunaomba hiki kilichotolewa, basi ni bora sasa kitolewe hiki kilichoombwa lakini sasa tuje tupambane katika kusimamiana baada ya kuwapa watu hawa fedha kuliko kuzipitisha lakini hawakabidhiwi fedha hizo.

**SPIKA:** Kengele ya pili Mheshimiwa.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, hitimisho; ardhi kama tulivyosema ni rasilimali muhimu sana katika ukuaji wa uchumi wetu na kama tunataka kuondoa migogoro ya ardhi basi ni vema bajeti ikatolewa ili Wizara hii ipambane na changamoto ambazo zinarudisha nyuma wananchi katika maeneo yao kwa kutokupimwa kila kipande cha ardhi, ili kila kipande cha ardhi kipate matumizi sawia. Kambi Rasmi ya Upinzani tunaamini katika mfumo wa umiliki wa ardhi ambapo kila mwananchi atamiliki ardhi na

kila kipande cha ardhi kilichopo juu ya ardhi na ndani ya ardhi, itakuwa ni suluhisho la migogoro ya mara kwa mara.

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

**HOTUBA YA MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI,  
WILFRED MUGANYIZI LWAKATARE (MB), KUHUSU MAKADIRIO  
YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA ARDHI, NYUMBA  
NA MAENDELEO YA MAKAZI KWA MWAKA WA 2019/2020  
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

(Inatolewa chini ya kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka 2016)

---

#### A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na nguvu katika kipindi hiki kigumu sana katika ufanyaji wa siasa hasa kwa upande shindani na Chama Tawala na kuweza kusimama mbele ya hadhira hii ili kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2019/2020.
2. **Mheshimiwa Spika**, kwa heshima kubwa napenda kuwashukuru wanachama na wananchi wote wa Bukoba Town kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia mimi pamoja na viongozi wote wa chama na halmashauri yetu ya Bukoba Town katika kuhakikisha tunamaliza au kupunguza kero nyingi zilizokwu zinawakabili wakazi wa mji wetu. Niwape pole kwa madhira ya mafuriko waliyoyapata ikiwemo kifo cha mtoto na uharibifu wa nyumba zaidi ya 75.

3. **Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa tayari Manispaa ya Bukoba kupitia Mkandarasi CRM wametayarisha rasimu ya mwisho ya Master Plan 2018-2038, bila shaka suala la namna ya kuepukana na hali ya mafuriko yanayoukumba mji mzima wa Bukoba utapatiwa majibu.
4. **Mheshimiwa Spika**, nitoe neno la kuwapongeza waheshimiwa wote pamoja na viongozi wa chama wenyewe kesi mbalimbali za kisiasa kwamba kukaa rumande, kufukuzwa Bungeni ni uzoefu mkubwa katika kukuonesha ni kwa jinsi gani demokrasia ya kweli inavyopiganiwa au inavyotafutwa. Hivyo kesi, mahabusu au jela ni moshi mweupe kuelekea kwenye ushindi. Tusife moyo au kukata tamaa kwa yote tunayofanyiwa!!!
5. **Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu ni kwa familia yangu mke wangu Angel na watoto Frank, Lovelet, Doreen na Vick, kwa kunivumilia katika harakati za siasa kwa kipindi chote ambacho hulazimika kuwa mbali na familia.

## B. HAKI ZA MAKAZI

6. **Mheshimiwa Spika**, unaposema Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, jambo la kwanza kwa mtanzania wa kawaida ni haki ya kupata ardhi kwa ajili ya kuishi yeye na familia yake, baadae ndiyo matumizi ya ardhi kwa ajili ya maendeleo binafsi.
7. **Mheshimiwa Spika**, Aya ya 61 ya makubaliano ya mwaka 1996 nchini Uturuki - Istanbul yaliyojulikana kama, "Instanbul Agreement and Habitat Agenda". Hatua zinazostahili kuchukuliwa na Serikali katika kukuza, kulinda na kuhakikisha kukamilika na kuendelea kwa haki za makazi kamili (adequate housing). Haki za Makazi ni suala na Haki za Kibinadamu, hili liko kwenye Ibara ya 25 ya Mkataba

wa Kimataifa wa Haki za Binadamu, "Universal Declaration of Human Rights" inatambua kwamba haki ya makazi ni haki ya kibinadamu.

8. **Mheshimiwa Spika**, aidha, Ibara ya 11 ya mkataba wa "International Covenant on Economic, Social and Cultural Rights" inatoa uhakika kwamba haki ya makazi ni kama haki ya kiwango cha maisha timilifu.
9. **Mheshimiwa Spika**, haki ya makazi si kuwa na makazi peke yake, bali ni pamoja na; haki ya kibinadamu ya kutoingiliwa bila sababu kwenye mambo binafsi ya familia au nyumbani; haki ya kibinadamu ya usalama ikiwa ni pamoja na uhakika wa kisheria wa upangaji; haki ya kibinadamu ya usawa wa kulindwa kisheria na kufidiwa na mahakama kwa ukiukwaji wa haki za makazi.
10. **Mheshimiwa Spika**, pia haki ya kulindwa kutokana na "forced evictions", kubomolewa au/na kuharibiwa kwa makazi ikiwa ni pamoja na kukaliwa kijeshi, vita vya kimataifa na vita vya wenyewe kwa wenyewe, kuanzishwa kwa makazi mapya ya wageni, kuhamisha wakazi na miradi ya maendeleo. Hii yote inatakiwa kusimamiwa vyema na Wizara hii ya Ardhi.
11. **Mheshimiwa Spika**, changamoto za Haki za Makazi ni pamoja na:
  - ü Umiliki wa Makazi
  - ü Upatikanaji wa Viwanja
  - ü Ujenzi wa (Nyumba) Makazi
  - ü Upatikanaji wa Fedha za Ujenzi/ Kununua nyumba
  - ü Vipato vya Wananchi

- ü Bei ya Serikali kuuza viwanja tupu ipo juu (kwa mfano; kwa mwaka 2012 Kigamboni ilikuwa ni Sh. 7,000 –10,000 kwa kila mita ya mraba, Tegeta ni Sh. 15,000 – 19,000 (ni sehemu ndogo ya Watanzania wenyewe vipato vya kuwawezesha kununua viwanja rasmi vinavyopimwa na Serikali katika maeneo mbalimbali).
- ü Idadi ndogo ya viwanja vinavyopimwa na usimamizi mdogo wa uendelezaji viwanja hivyo unasababisha kuwepo na “speculation”. Speculation inasababisha kuhodhi kwa ardhi na kupanda kwa bei.
- ü Kukosekana kwa Miundombinu (umeme, maji, simu, mfumo wa majitaka n.k.) Pamoja na Serikali kuuza viwanja kwa bei za juu, Serikali haiweki miundombinu yoyote kuyafanya maeneo hayo yawe na gharama zilizojificha.
- ü Serikali imeshindwa kuandaa mpango kabambe kuzuia ukuaji wa makazi holela pembezoni mwa miji. Wananchi wanajitwalia jukumu la kupanga makazi na hivyo wananchi kujenga maeneo holela na hatarishi<sup>1</sup>.

### **C. ANGUKO LA SEKTA YA NYUMBA NCHINI**

- 12. Mheshimiwa Spika**, Kumekuwa na ongezeko kubwa la watu katika miji mikubwa nchini hasa kwa Jiji la Dar es Salaam ambapo ongezeko hilo linaenda sambamba na mahitaji makubwa ya nyumba za kuishi, ofisi za biashara mbalimbali, maduka

---

<sup>1</sup> Haki za ardhi - Mada: Changamoto ya Haki ya Makazi na namna Shirika la Nyumba linavyoikabili- 27<sup>th</sup> Jan. 2012

makubwa pamoja na hoteli. Taarifa zinaonyesha kuwa kwa nchi nzima kuna mahitaji ya nyumba 200,000.

13. **Mheshimiwa Spika**, kwa sasa sekta ya nyumba hasa majengo makubwa ya biashara inapitia katika changamoto kubwa sana kutokana kuyumba kwa uchumi na biashara nyingi kufungwa, inakadiriwa kuwa kwa sasa kuna mita za mraba 300,000 ambazo ziko wazi hazina wapangaji. Wapangaji wengi wameshindwa kuhimili bei za majengo makubwa ambazo zilikuwa zinatozwa kwa dola<sup>2</sup>.
14. **Mheshimiwa Spika**, kutokana na kuporomoka na kuyumba kwa uchumi, inakadiriwa kuwa kwa sasa ni 35% hadi 45% ya majengo makubwa ya kibiashara na maduka yana wapangaji. Hii sio ishara njema kwa sekta ambayo imekua kwa mfululizo kwa miaka saba iliyopita. Tafsiri pana ya anguko hili ni kuwa Serikali itakosa mapato kwa sababu biashara zinafungwa na pia kutakuwa na ongezeko la mikopo ya nyumba isiyolipika (mikopo chechefu) jambo ambalo litaathiri pia sekta ya fedha kwa ujumla wake.
15. **Mheshimiwa Spika**, mwaka 2009 sekta ya majengo ilikadiriwa kuwa na thamani ya dola bilioni moja ambapo mpaka mwaka 2014 sekta hiyo ilikuwa mpaka dola bilioni 1.8 sawa na 3.7% ya pato la taifa ambapo ni ongezeko la 63%.
16. **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza Bunge kuchukua hatua za haraka kuokoa sekta ya majengo nchini ambapo imefikia hatua waliokuwa wanaendesha biashara zao katika maeneo ya katikati ya Jiji la Dar es Salaam wameamua kuhamishia shughuli zao katika maeneo

---

<sup>2</sup> <http://www.thecitizen.co.tz/News/Business/works/Real-estate-business-has-come-a-long-way/3956094-4258346-3fusvo/index.html>

ya makazi ambapo gharama za kupangisha ni ndogo ukilinganisha na gharama za majengo makubwa katikati ya Jiji.

17. **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wakati wa Bunge la Kumi mwaka 2011 tulipendekeza na kuishauri Serikali kuleta Bungeni muswada wa kuanzisha mamlaka ya kusimamia sekta ya majengo makubwa (The Real Estate Regulatory Authority Bill) ambapo leo ni miaka saba toka ushauri huo utolewe na Serikali kuahidi kuleta muswada lakini bado hoja hiyo hajatekelezwa.
18. **Mheshimiwa Spika**, katika Randama ya Wizara Serikali imesema kuwa muswada kwa ajili ya kuanzisha Mamlaka ya Majengo Nchini upo katika hatua za mwisho na umekabidhiwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali jambo ambalo ni kinyume na ahadi ya Serikali katika Randama za Wizara kwa mwaka 2016/2017 ambapo Serikali ilisema kuwa muswada huo umekamilika.
19. **Mheshimiwa Spika**, ni vema sekta ya nyumba ikasimamiwa kwa sababu pamoja na tatizo la anguko la uchumi bado sekta hiyo ilikuwa inakabiliwa na kupandisha hovyo kwa bei ya kupangisha kwenye majengo makubwa pamoja na matumizi ya dola jambo ambalo limeendelea kuathiri shilingi yetu.
20. **Mheshimiwa Spika**, tunataka kauli ya Waziri kuhusu hatua ambazo Serikali itazichukua kuokoa sekta ya nyumba nchini kwa sababu kuyumba kwa sekta hii muhimu kunaenda sambamba na kuathiri sekta ya fedha na uchumi kwa ujumla. Aidha, kwa sababu Serikali haioni umuhimu wa kutafuta suluhisho la jambo hili ni vema Bunge likaingilia kati kwa kuunda Kamati Teule kufanya uchunguzi na kulishauri Bunge hatua ambazo Serikali itatakiwa kutekeleza.

**D. WAKALA WA TAIFA WA UTAFITI WA NYUMBA BORA NA VIFAA VYA UJENZI**

21. Mheshimiwa Spika, Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi (NHBRA) ulianzishwa mwaka 2001 chini ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa lengo la kutoa huduma na kupunguza gharama kwa vifaa vya ujenzi kwa makazi bora. Taasisi hiyo pia imekuwa ikijihusisha na mafunzo teknolojia ya ujenzi wa nyumba za bei nafuu kwa vikundi mbalimbali nchini ikiwa ni pamoja na kuwafundisha juu ya utengenezaji wa matofali, vigae vya kuezekea nyumba pamoja na ujenzi wa nyumba zenyewe ambapo taasisi na wananchi mbalimbali wanaweza kufaidika na mpango huo nchini.
22. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa wakala ni kuwa kuna uhitaji mkubwa wa tafiti ambazo zitakazowezesha watanzania kupata makazi bora na ya kudumu, kwani katika vifaa na huduma zinazopatikana zinajikita zaidi katika usanifu majengo pamoja na matumizi ya vifaa, kwa hiyo tafiti hizi ni muhimu kwa wananchi wenye mahitaji ya makazi bora, jambo hilo ni jema sana lakini Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza wakala huyo amejiimarisha kwa kiwango gani katika kuhakikisha watanzania wote wanapata makazi bora? Ukweli ni kuwa wakala huyu amekuwa dormant.
23. Mheshimiwa Spika, tafiti mbalimbali zinazoendelea kufanywa na NHBRA zina lengo la kupunguza gharama za ujenzi wa makazi na majengo mengine ya biashara, baadhi ya tafiti hizo ni utafiti wa kutengeneza fremu za milango kwa kutumia zege, utafiti kuhusu matofali yanayofungamana na kuchoma pamoja na vigae vya kuchoma vya kuezekea n.k.

24. **Mheshimiwa Spika**, tatizo kubwa sasa hivi linalozua watanzania wengi kuwa na makazi bora ni kutokana na gharama kubwa ya vifaa vya ujenzi ambavyo ni nguzo kubwa katika ujenzi. Vifaa hivyo vyenye gharama kubwa ni pamoja na vifaa vinavyofanyiwa utafiti na wakala huyu.
25. **Mheshimiwa Spika**, mfano wa hivi karibuni ni ule uliotolewa na mmoja wa maofisa wa kiwanda kimoja cha uzalishaji saruji katika mkutano uliokuwa umeitishwa na Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara ambaye alieleza juu ya kodi kubwa wanayotozwa pale wanapoingiza malighafi zinazotumika kutengeneza saruji kutoka nje, jambo ambalo husababisha uzalishaji kuwa na gharama kubwa. Pia baadhi ya mawakala wa vifaa vya ujenzi wamekuwa wakilalamika kupanda kwa bei ya vifaa vya ujenzi kutokana na kupanda kwa bei hizo kutoka viwandani na nje ya nchi, hivyo kusababisha wateja kuwa wachache.
26. **Mheshimiwa Spika**, ni kutokana na hali hiyo, bei ya bidhaa na vifaa mbalimbali vinavyotumika kwa ajili ya ujenzi vinaendelea kupanda bei na hivyo kuathirii azma ya Serikali ya ujenzi wa makazi bora na ya kudumu. Mei 6, 2014 aliyekuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi alishauri kupunguzwa au kuondolewa kwa kodi katika vifaa vya ujenzi ili watanzania wengi waweze kujenga nyumba bora.
27. **Mheshimiwa Spika**, Septemba 5, 2018 akiwa mjini Mwanza kushuhudia utiaji saini wa mikataba minne ya ujenzi wa meli kubwa ya abiria na mizigo ya Serikali, chelezo na ukarabati wa meli za MV Butiama na MV Victoria, Rais John Magufuli alizungumza mambo mengi na kutoa maelekezo kwa watendaji wa Serikali. Miiongoni mwa maelekezo aliyoyatua ni pamoja na kuwaagiza Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano,

Isack Kamwelwe na wa Fedha na Mipango, Dkt. Phillip Mpango kukutana haraka ili kumaliza kilio cha kodi kwenye vifaa nya ujenzi.

28. **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kupata ufanuzi kuhusu utekelezaji wa maelekezo ya Rais kuhusu kupunguza kodi kwenye vifaa nya ujenzi na punguzo hilo limekuwa ni kwenye kodi gani, mionganoni mwa kodi hizo?
29. **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kabisa kama alivyoshauri Mheshimiwa Prof. Anna Tibajuka wakati ule kwamba iwapo kodi kwenye vifaa nya ujenzi itapunguzwa katika vifaa nya ujenzi, Watanzania wengi watamudu kumiliki makazi bora zaidi na hivyo itakuwa ni sifa ya ziada kwa Taifa letu kuwa lenye watu wengi wanaoishi kwenye makazi bora. Nchi ya Rwanda imefanikiwa kusimamia programu ya kuondosha nyumba za nyasi, inakuwaje kwetu sisi nchi yenye rasilimali kibao tunashindwa?

#### **E. TUME YA TAIFA YA MIPANGO NA MATUMIZI YA ARDHI**

##### **1.5.1.1.1 (FUNGU 03)**

30. **Mheshimiwa Spika**, ardhi ni mali; ardhi ni mojawapo ya kisababishi kikubwa cha migogoro ya wenyewe kwa wenyewe kwa nchi nyingi za Afrika, hivyo ardhi ni usalama wa nchi pia ardhi ni siasa, hivyo basi ili hayo yote yawepo katika hali ya kustahimilika ni muhimu na ni lazima kuwepo na mipango ya matumizi endelevu ya ardhi katika nchi yetu. Katika kutimiza lengo hilo ndio sababu kubwa ya uwepo wa Tume ya Taifa ya mipango na matumizi ya ardhi.
31. **Mheshimiwa Spika**, Ukweli ni kuwa ardhi ya Tanzania haiongezeki lakini matumizi yake na watumiaji wa ardhi wanaongezeka kila siku. Tanzania ina eneo la ardhi la kilometra za mraba zipatazo 945,087 na idadi ya watu wapatao milioni 54.2 lakini ni ukweli pia kuwa

hadi sasa Tanzania ina tatizo kubwa la upangaji na utumiaji wa ardhi ili makundi yote ya kijamii kuweza kushiriki katika shughuli zake za kiuchumi na kijamii bila ya uwepo wa migogoro yoyote.

32. **Mheshimiwa Spika**, katika matumizi ya ardhi hapa nchini kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2012 ni kwamba; eneo la uhifadhi (protected areas) linachukua 28.7% ikifuatiwa na kilimo, uchimbajii madini na makazi inayochukua eneo la 17.1%, vijiji mtawanyiko na kilimo inachukua eneo la 21.1%, mashamba ya miti na misitu 16.3%, eneo la malisho, uwindaji na uvunaji wa misituni 10.3% na mwisho eneo la maji (water bodies) 6.7%.
33. **Mheshimiwa Spika**, hali ya matumizi ilivyo kuanzia mwaka 2013 hadi 2033 ni kuwa; eneo la hifadhi sawa na 29.7% sawa na kilometa za mraba 281,357.0; eneo la makazi mijini, kilimo na malisho ni 17.5% sawa kilometa za mrada 165,605.0; Vijiji mtawanyiko, kilimo na malisho ni 18.7% sawa na kilometa za mraba 176,747.0; Eneo la malisho uwindaji na uhifadhi (Ranchi) ni 13.1% sawa na kilometa za mraba 123,460.0; maeneo ya maji ni 6.7% au kilometa za mraba 63,172.0; Matumizi ya ardhi kwa makundi hayo tajwa yanakumbwa na migogoro na sintofahamu kubwa.
34. **Mheshimiwa Spika**, takwimu hizo za kufikia mwaka 2012 na zile za kuanzia 2013 hadi 2033 zinaonesha kuongezeka kwa eneo linalohifadhiwa (reserved and protected area kutoka asilimia 28.7 hadi 29.7 na eneo la kilimo kikubwa (*large scale commercial crop cultivation and ranching*) ni dhahiri kuwa punguzo la ardhi hasa kwa matumizi ya kundi kubwa katika jamii la wakulima na wafugaji na ardhi hiyo kuwa katika ardhi ya hifadhi, migogoro na mtafaruku ni wazi kutokea.

- 35. Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa taarifa ya Tume ya "National Land Use Framework Plan 2013-2033" iliyotolewa mwaka 2014, inaeleza changamoto nyingi zinazoikabili sekta ya ardhi, lakini changamoto zote hizo zimetengwa katika makundi makuu mawili ambayo ni:
- i. Matumizi na upangaji wa ardhi ili kukabiliana na mgawanyo usio na usawia wa rasilimali zetu.
  - ii. Masuala ya kitaasisi.
- 36. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa changamoto za kundi la kwanza zinaweza kutatuliwa vizuri kama tukiweza kutatua changamoto za kitaasisi ambazo zimegawanyika katika maeneo matano, la kwanza likiwa ni uwezo mdogo wa taasisi wa rasilimali kulinganisha na ukubwa wa ardhi na makundi ya watumiaji waliopo (Rasilimali hizo ni watu, vifaa, teknolojia na fedha).
- 37. Mheshimiwa Spika**, ukifanya rejea ya taarifa ya Tume ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka 2018/2019 inaonesha kuwa tume ina changamoto ya uhaba wa watumishi kwa asilimia 63.8, ina magari matatu tu na magari manne yameharibika vibaya, Tume ina uhaba mkubwa wa vitendea kazi vya ofisini kama vile vifaa vya upimaji, computers, mashine za uchapishaji n.k. Aidha kuna uhaba mkubwa wa rasilimali fedha ambao unasababisha kasi ndogo ya uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi na hivyo kuendelea kujitokeza kwa migogoro ya matumizi ya ardhi.
- 38. Mheshimiwa Spika**, katika kuonesha kuwa licha ya kuwepo kwa mpango toka mwaka 2014 wa kukabiliana na changamoto tajwa hapo awali lakini bado tatizo ni kubwa.

39. **Mheshimiwa Spika**, tarehe 7 Februari, 2019 Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi William Lukvi aliongoza kikao cha Mawaziri wenzake sita kujadili changamoto mbalimbali za matumizi ya sekta ya ardhi. Mawaziri wanaoshiriki kikao hicho ni kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Kilimo, Uvuvi na Mifugo, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Wizara ya Maji, Wizara ya Ulinzi, Wizara ya Muungano (Mazingira) pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kikao hicho cha Mawaziri kimetanguliwa na mfululizo wa vikao vyatimu ya wataalamu kutoka Wizara hizo ikiongozwa na Kamishna wa Ardhi nchini Marry Makondo kwania ya kutafuta suluhu ya migogoro ya ardhi ambayo imekuwa ikijitokeza katika maeneo mbalimbali nchini.
40. **Mheshimiwa Spika**, vikao hivi hata vikikaa kila siku au kila mwezi haviwezi kutatua changamoto tajwa ambazo zinajulikana na suluhu yake pia imetajwa kwenye NLUPP 2013-2033, hoja ya muhimu iko kwenye uwezeshaji wa kitaasisi ambao utabeba dhana nzima ya ufumbuzi kama ilivyoelezwa hapo awali. Bila uwepo wa rasilimali watu, fedha na vitendea kazi, kama mkakati wa utatuzi upo tayari, vikao si ni kuongeza matumizi yasiyokuwa na sababu?
41. **Mheshimiwa Spika**, taarifa ya utekelezaji inaonesha kuwa kwa mwaka wa fedha 2018/19 Tume ilitengewa jumla ya shilingi 7,081,926,000.00 kati ya hizo fedha za maendeleo zilikuwa ni shilingi 5,000,000,000.00 zilizopangwa kwa miradi ya maendeleo lakini hadi Januari, 2019 hakuna hata shilingi moja ambayo ilitolewa toka Hazina. Japokuwa wanasema tengeo la 2018/19 liliongezeka kwa asilimia 234 kulinganisha la lile la shilingi 2,115,371,822 la mwaka 2017/18. Lakini kama tengeo liliongezeka lakini hazikutolewa hata shilingi katika utendaji kazi wa Tume ina maana yoyote? Kambi Rasmi ya Upinzani inasema hii ni hadaa ambayo inafanywa na Serikali.

42. **Mheshimiwa Spika**, kama Serikali inasema na kujigamba kuwa kwa mwezi inakusanya kiasi ya shilingi trillioni 1.3 inakuwaje inashindwa kutoa fedha ambazo zinakuwa zimetengwa na kuidhinishwa na Bunge? Tunaomba Mheshimiwa Waziri alitolee ufanuzi suala hili.
43. **Mheshimiwa Spika**, kwa bahati nzuri sana ni kuwa wataalam wetu kwa kiwango kikubwa toka mwaka 2014 wakati taarifa ya "NATIONAL LAND USE FRAMEWORK PLAN 2013 - 2033" inatoka kulikuwa na bajeti yake ya utekelezaji, hivyo Tume ya Taifa ya Mpango wa Matumizi ya Ardhi ilitakiwa ijikite kwenye kuomba fedha kulingana na framework plan iliyokwishapitishwa hapo awali. Kwa mwaka wa fedha 2018/19 ilitakiwa kuomba na kuidhinishiwa jumla ya shillingi 60,000,000,000.00.
44. **Mheshimiwa Spika**, mwezi Februari 2019 Serikali kuptitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa (FAO) walizindua Mradi wa Msaada wa Kitaalam wa Kukuza Uwezo wa Wadau katika Kuratibu Mfumo wa Utawala wa Ardhi hapa nchini. Mradi huu unafuatia ombi la Wizara hiyo kwa ajili ya kusaidia uratibu wa mfumo wa umiliki wa ardhi kwa kutumia Miongozo ya Hiari ya Kuboresha Utawala wa Ardhi, Uvuvi na Misitu hapa nchini. Pia mradi huo unalenga kusaidia katika kuratibu sera na sekta, kukabiliiana na migogoro na kuboresha taarifa juu ya uwekezaji katika ardhi hapa Tanzania.
45. **Mheshimiwa Spika**, FAO iliandaa miongozo hii kwa muktadha wa usalama wa chakula, kama ilivyopitishwa na Kamati ya Dunia ya Usalama wa Chakula tarehe 11 mwezi Mei mwaka 2012 lengo likiwa ni kuhamasisha juu ya upatikanaji wa haki za umiliki ardhi, uvuvi na misitu kama njia ya kutokomeza njaa na umaskini, kufanikisha maendeleo endelevu na kutunza mazingira.

46. **Mheshimiwa Spika**, Uzinduzi rasmi wa mradi huu ulifanyika Wilaya ya Mvomero, mkoani Morogoro mbali ya Wilaya ya Mvomero, mradi huu pia utatekelezwa katika Wilaya za Kilombero, Malinyi, Kilosa na Ulanga ambayo ni maeneo yanayofahamika kwa migogoro ya ardhi hususan baina ya wakulima na wafugaji mara nyingine zikipelekea vifo na uharibufu wa mali na mifugo.
47. **Mheshimiwa Spika**, ni ukweli kuwa mradi huo uletaji wa suluhu katika kuboresha suala la utawala wa ardhi hapa nchini pamoja na kutatua migogoro ya ardhi hapa nchini. Kwani wananchi wanategemea upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya kilimo, ufügaji, uvuvi na misitu kwa ajili ya maisha yao. Namna rasilimali hizi zinavyopatikana na kutumika ina athari ya moja kwa moja kwenye uhakika wa chakula, maendeleo vijijini, ukuaji wa uchumi na utunzaji endelevu wa mazingira.
48. **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kufahamu ni kwa vipi mradi huu unaosimamiwa kwa ubia kati ya Serikali na Shirika la Chakula Duniani (FAO), unashirikisha Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi? Kwani majukumu ya mradi huo ndio pia madhumuni na majukumu ya Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi.

#### **F. MILKI ZA MASHAMBA NCHINI**

49. **Mheshimiwa Spika**, taarifa ya Wizara inasema kuwa Tanzania Bara ina takribani mashamba 2,653 yaliyopimwa na kumilikishwa. Hadi Oktoba, 2018 takribani mashamba 1,926 yalikuwa yamehakikiwa kwa lengo la kujua hali halisi ya maendelezo yake. Jumla ya mashamba 114 yamebatilishwa umiliki ambapo katika kipindi cha Serikali ya awamu ya tano pekee jumla ya mashamba 36 yenye ukubwa wa ekari 87,004.933 yamebatilishwa na mashamba 15 yenye ukubwa wa ekari 27,143.976 yameombewa kibali cha

ubatilisho wa milki. Aidha mashamba 238 yamewekwa rehani na mashamba 262 yamehawilishwa.

50. **Mheshimiwa Spika**, katika kutetea uamuvi huu wa Serikali taarifa hiyo imenkuu Sheria ya Ardhi Sura 113, kifungu cha 45(2) kinachompatia mamlaka Mheshimiwa Rais kubatilisha milki zote ambazo masharti yake yamekiukwa.
51. **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani haina tatizo na uamuvi wa Rais kusitisha milki za mashamba hayo, hoja yetu ya msingi ni je, utaratibu gani unatumika hadi Rais anafuta milki za awali na pia utaratibu gani unatumika kufanya "re-allocation" kwa milki zilizofutwa? Hapa kuna tatizo kubwa na hujuma kubwa zinafanyika kwani milki nyingi zimefutwa kwa sababu za kislasa au binafsi, hatuwezi kujenga uchumi ulio imara kwa maamuvi ya "personalities". Kwa mustakabali huo Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwaeleza watanzania ni utaratibu gani wa wazi unaotumika kufuta na kugawa upya mashamba yaliyotaifishwa? Aidha, tuliombe Bunge kupitia Kamati yake ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuunda kamati ndogo iweze kuangalia suala hili la kufuta milki na kugawa mashamba au kutoa milki mpya.
52. **Mheshimiwa Spika**, katika muendelezo huo huo wa kufuta milki na kufanya reallocation, kuna baadhi ya viongozi wanatumia mwanya huo kwa maslahi binafsi na rushwa kubwa iliyopitiliza. Mkoani Morogoro kuna mgogoro wa umiliki wa ekari 4000 eneo la Mkindi C kati ya wakazi na Halmashauri ya Manispaa pamoja na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa. Eneo hilo la ekari 4000 lilimegwa kutoka kwenye shamba la Tungi Sisal Estate mwaka 1984 baada ya Estate kushindwa kuliendeleza na hivyo kukabidhiwa kwa wananchi ili kuliendeleza.
53. **Mheshimiwa Spika**, mashamba yaliyofutiwa milki mwaka 1997 na kukabidhiwa kwa wananchi ni;

Kilimanjaro Sisal Estate (Mkundi B); Kihonda Sisal Estate (Mkundi A); Tungi Sisal Estate (Mkundi C), lakini wananchi walikuwa wanatumia ardhi hiyo toka mwaka 1984.

54. **Mheshimiwa Spika**, kwa masikitiko makubwa tangu mwaka 2017 alipoingia Mkuu wa Mkoa kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya wamekuwa wakitumia vyombo veya dola kutaka kuwaondoa wananchi hao kwa nguvu ilhalii wakifahamu kuwa eneo hilo la ekari 4000 tayari wananchi walikwishakabidhiwa na aliyezeka mmiliki wa mashamba hayo na Serikali ilikwisha futa milki ya eneo hilo.
55. **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri Mheshimiwa Waziri uingilie kati mgogoro huo wenye sura ya maslahi binafsi na rushwa kwani kisingizio kikubwa ni kuleta mwekezaji.
56. **Mheshimiwa Spika**, pamekuwepo na mgogoro wa miaka mingi kati ya Mkoa wa Dar Es Salaam na Mkoa wa Pwani wa mipaka katika Mitaa ya Kisopwa na Mloganzila. Wananchi wa mitaa hiyo huduma zote muhimu kwa miaka yote wamekuwa wakizipata kutoka Manispaa ya Kinondoni na sasa wanazipata katika Manispaa ya Ubungo. Hata kujianzikisha kupiga kura katika uchaguzi wa mitaa 2014 na uchaguzi mkuu 2015 wananchi hao walifanya hivyo wakiwa Manispaa ya Kinondoni na sasa wameendelea kubaki katika Manispaa ya Ubungo baada ya kuanzishwa kwa Wilaya mpya. Hata hivyo, Wilaya ya Kisarawe imekuwa ikidai kwamba mitaa hiyo ipo katika Mkoa wa Pwani.
57. **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe kauli Bungeni mitaa hiyo ipo katika Mkoa upi kati ya Dar Es Salaam na Pwani na lini itamaliza mgogoro huo wakati huu ambapo nchi inajandaa na uchaguzi wa Serikali za mitaa wa mwaka 2019?

**G. MGOGORO MPYA WA KIWANDA CHA TWIGA NA WAKAZI WA CHASIMBA**

58. **Mheshimiwa Spika**, kumbukumbu zinaonesha kuwa Mheshimiwa Waziri Lukuvi akiwa na timu yake yote ya utendaji hapa tarehe 13.06.2015 alifanikiwa kumaliza mgogoro uliokuwepo baina ya Kiwanda cha Cementi cha Twiga na wakazi wa Chasimba. Ushahidi huo upo kwenye muhtasari wa kikao kilichohusisha wananchi, uongozi wa kiwanda uliowakilishwa na Mtendaji wake Mkuu, na kiliongozwa na Mheshimiwa Waziri Lukuvi, Naibu Waziri wakati huo Mheshimiwa Angellah Kairuki, Katibu Mkuu Alphayo Kidata pamoja na timu nzima ya watendaji wake kuanzia ngazi ya Halmashauri hadi Wizarani.
59. **Mheshimiwa Spika**, katika kikao hicho katika kumaliza mgogoro ambao uliokuwa umedumu kwa miaka mingi kilitoka na maazimio saba (7) ambayo ni:
- i. Eneo ambalo limekaliwa na wananchi kwa muda mrefu libadilishwe matumizi kuanzia tarehe 13.06.2015 kutoka matumizi ya uchimbaji wa madini na kuwa eneo la makazi na manispaa ya Kinondoni ambao ni mamlaka ya upangaji kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi na Kamati ya wananchi wa Chasimba waandae mpango wa utekelezaji katika eneo hilo, hivyo litapangwa, kupimwa na kumilikishwa kwa wananchi.
  - ii. Wananchi waliotambuliwa wakati wa zoezi la uthamni ndio watakaohusika na zoezi zima, wananchi ambao hawakuwepo na walikuja baada ya zoezi la uthamni hawatahusika kabisa

na mpango huu; aidha watatakiwa kuondoa maendeleo yao na kuondoka mara moja ili kupisha zoezi la kupanga na kupima upya eneo hilo.

- iii. Wakati wa umilikishaji Wizara itoe tozo (Premium) kwa kila kiwanja itakachommilikisha kwa kila mwamanchi wa Chasimba.
- iv. Wizara imekubali kwamba sehemu ya malipo ya tozo yataenda katika kiwanda kitasaidia kujenga miundombinu na huduma za jamii kama zahanati na shule.
- v. Wananchi kwa kushirikiana na Serikali ya mtaa wataunda kamati ya utekelezaji na usimamizi ya mpango huo, na kamati itakayoundwa ifanye kazi kwa uadilifu.
- vi. Kazi za uchimbaji wa kokoto na mchanga hazitaruhusiwa katika eneo hilo kwa kuwa limekwishabadi lishwa matumizi na kuwa eneo la makazi, na mtu ye yote atakayefanya kazi hizo katika eneo hilo akamatwe na kifiki hwa katika vyombo vy ya sheria.
- vii. Kazi hii ifanyike haraka hadi nwezi Oktoba ambapo hati zitakabidhiwa kwa wananchi.

- 60. Mheshimiwa Spika**, maazimio ya kikao hicho kilichokuwa chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Waziri Lukuvi na Katibu wa kikao alikuwa Katibu Mkuu wa Wizara Ndugu Aphayo Kidata ilisainiwa tarehe 30.06.2015

61. **Mheshimiwa Spika**, katika hali ya kushangaza ni kuwa uongozi mpya wa Kiwanda cha Twiga unakuja na mambo mengine mbali na makubaliano yaliyoongozwa na Mheshimiwa Waziri baina ya wananchi na kiwanda na hivyo kuleta mtafaruku baina ya wananchi. Hii ni kutokana na barua ya tarehe 31 Januari, 2019 iliyoandikwa na Wizara kwenda kwa Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Kawe, kumueleza kuhusu suala hilo la kukiuka maazimio ya pamoja.
62. **Mheshimiwa Spika**, ni ukweli kuwa taasisi ikiwemo Serikali zinaongozwa na kuendeshwa kwa nyaraka, hivyo uongozi mpya wa Kiwanda cha Cementi cha Twiga kukataa kutambua maamuzi na makubaliano yaliyokwishafikiwa na Serikali ni "udhalilishaji" mkubwa kwa Serikali. Kama ni kweli kitendo cha Wizara kwenda kinyume kushindwa kutekeleza maazimio yaliyokwisha fikiwa chini ya Waziri na Katibu Mkuu kinaleta wasiwasi kuwa kuna mazingira ambayo yakutilia mashaka kama kweli yanatija kwa wananchi na Taifa.
63. **Mheshimiwa Spika**, ni ukweli kuwa wananchi wengi wanaimani kubwa kwa Mheshimiwa Waziri Lukuvi katika kutoa suluhu ya mogogoro na mgogoro huo wa Chasima alikwisha upatia suluhu toka mwaka 2015, lakini kitendo cha Wizara kushindwa kutekeleza maazimio ya makubaliano yaliyosimamiwa na Mheshimiwa Waziri ni kukudhalilisha wewe binafsi na kukupotezea aiba yako katika jamii hasa wananchi wa Chasimba.
64. **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutembea katika maneno yake, kwani suala hili la mgogoro baina ya wananchi wa Chasimba na Kiwanda cha Cementi cha Twiga ulikwishamalizwa na maazimio yakafikiwa, hivyo ni Serikali itekeleze maazimio yote saba (7) yaliyokubaliwa chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Waziri Lukuvi wakati

anamaliza mgogoro huo.(**KIELELEZO NA. 1-Muhtasari wa Kikao cha pamoja**)

**H. UDHAIFU KATIKA MIPANGO MIJI NA USIMAMIZI WA ARDHI**

- 65. Mheshimiwa Spika**, tafiti zinaonyesha kuwa 62.5% ya wakazi wote wa mijini wanaishi kwenye makazi yasiyokuwa rasmi<sup>3</sup> na 37.5 % pekee ndio wanaishi kwenye makazi katika maeneo ambayo yamepimwa. Sababu kubwa ya wakazi wa mijini kuishi kwenye maeneo ambayo sio rasmi inatokana na ghamama kubwa za kupanga au kujenga kwenye maeneo rasmi ambayo yamekwisha kupimwa.
- 66. Mheshimiwa Spika**, Aidha kwa mujibu wa sensa ya watu kumekuwa na ongezeko la idadi ya watu kutoka milioni 22 mwaka 1988 hadi milioni 52 kwa mwaka 2014. Ongezeko hili limekuwa kichocheo cha mahitaji na ushindani mkubwa kwenye ardhi hasa kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na makazi.
- 67. Mheshimiwa Spika**, kumekuwa pia migogoro ya muda mrefu kati ya Serikali na wananchi au kati ya wananchi na wawekezaji ambao wamepewa ardhi kwa ajili ya kuendeleza. Migogoro hii imetokana hasa na namna Serikali inavyotwaa ardhi bila kulipa fidia stahiki na kwa wakati.
- 68. Mheshimiwa Spika**, masuala yote haya sio mageni kwa Serikali kwa sababu taasisi za Serikali zenyewe pamoja na mashirika yasiyo ya Kiserikali yameshafanya utafiti wa kina juu ya changamoto ya makazi holela katika maeneo mbalimbali nchini. Katika jambo la kushangaza ni kuwa ni Serikali ya CCM ambayo imekuwa ikilea mambo haya bila ya kuyafanyia kazi kwa manufaa ya nchi yetu.

---

<sup>3</sup> Ministry of Lands, Housing and Human Settlement, Habitat III National Report, 2016

69. **Mheshimiwa Spika**, mpaka Juni mwaka 2015, takwimu zilikuwa zinaonyesha kuwa ardhi ya jumla (General Land) mbayo ilikuwa imepimwa ilikuwa na jumla viwanja milioni 1.6 na mashamba ambayo yalisajiliwa kwa hati yalikuwa 23,000 pekee na pia leseni za makazi zilikuwa ni jumla ya 379,000. Kwa maana hiyo inakisiwa kuwa ni 10% pekee ya ardhi ya jumla ambayo imepimwa<sup>4</sup>.
70. **Mheshimiwa Spika**, Kwa tafsiri ya moja kwa moja ni kuwa katika nchi yetu takribani 90% ya ardhi ya jumla haijapimwa na hivyo haijatolewa kisheria na kumilikishwa kwa wananchi. Jambo hili sio la kujivunia kwa sababu ardhi ni urithi wa wananchi na pia ikitumika vizuri ni rasilimali ambayo inaweza kuwa na tija kwa wananchi kiuchumi kuliko ilivyo sasa.
71. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na ukweli kuwa ardhi ya jumla haijapimwa kwa 90% Wizara katika randama wanaonyesha kuwa wanatekeleza mradi wa kupima ardhi ya Kijiji katika Wilaya za Ulanga na Malinyi. Ni jambo jema lakini vema Serikali ikaja na mkakati wenye mashiko na wenye kasi stahiki wa kuhakikisha kuwa ardhi ya jumla inapimwa na kumilikishwa ili kuepuka majanga yanayotokana na makazi ya wananchi hasa kwenye Miji na Majiji kutokupimwa.
72. **Mheshimiwa Spika**, Jiji la Dar es Salaam limekuwa likikumbwa na mafuriko ambayo yamekuwa yakileta majanga kwa miaka mingi sasa. Aidha Serikali haijaweka wazi kuhusu uwepo au kutokuwepo kwa mpango mkuu (master plan) wa matumizi na uendelezaji wa ardhi katika Jiji. Jambo ambalo linasababisha watu kuendelea kujenga na kuanzisha miji mingine nje ya Jiji ambayo haijapangwa wa kuratibiwa na mamlaka husika.

---

<sup>4</sup>Ripoti ya Ufanisi ya CAG kuhusu usimamizi na utoaji wa viwanja ya Machi, 2018

- 73. Mheshimiwa Spika**, Aidha Serikali imekuwa na maamuzi ya kisiasa zaidi kuliko kutegemea ushauri wa kitaalamu kuhusu namna ya kupunguza msongamano pamoja na kupanga makazi ya wakazi wa Jiji. Mathalani Serikali iliwahamisha kwa nguvu wakazi wa Mkwajuni na Jangwani na kwa kubomoa makazi yao lakini ni Serikali hiyo hiyo ambayo imewaruhusu Kampuni ya mabasi yanayokwenda kasi (UDART) kujenga kituo cha maegesho Jangwani huku wakijua ile ni sehemu ambayo maji ya Bonde la Msimbazi hukusanya pale kuelekea baharini.
- 74. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kwa Bunge kuititia Kamati yake ya Miundombinu au kuundwa kwa Kamati Teule ya Bunge illi kuhakikisha kuwa Bunge linakuwa sehemu ya kusimamia Jiji la Dar es Salaam kuepukana na majanga na kuhakikisha kunakuwa na Master Plan ya Jiji ambayo haiwaumizi wananchi na kuhakikisha tunaepukana na majanga ya mafuriko ya mara kwa mara. Tunapendekeza hili kwa sababu inaonekana Serikali imeona ni kawaida majanga kujirudia katika Jiji la Dar es Salaam ambapo mara nyingi vifo vimeripotiwa.
- 75. Mheshimiwa Spika**, Ni vema Bunge likaingilia kati jambo hili kwa sababu Serikali pamoja na kushindwa kutafuta suluhisho la kudumu, imeamua kuziua Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kuzinyang'anya vyanzo vya mapato ambavyo wangevitumia katika kutekeleza miradi mbalimbali ya mipango ya ardhi nchini. Kwa kuwa Serikali kwa makusudi wameamua kuziua halmashauri nchini na kwa kuwa Bunge ni chombo cha uwakilishi wa wananchi ni vema likachukua hatua ya kuchunguza na kuja na taarifa ambayo Serikali italazimika kutekeleza kuhusu namna ya kuhakikisha tunaepukana na majanga ya mafuriko katika Jiji la Dar es Salaam.

- 76. Mheshimiwa Spika**, Waziri atoe maelezo hapa Bungeni kuhusu mamlaka na maafisa waliohusika kutoa kibali kwa Kampuni ya UDART kuruhusiwa kujenga kituo cha maegesho katika eneo la Jangwani huku wananchi wakihamishwa kwa madai kuwa ni eneo hatari kwa makazi. Wananchi wameshuhudia hivi karibuni jinsi eneo hilo la maegesho liliyokuwa limejaa maji kama Bwawa na Serikali kuonekana kutochukua hatua yoyote kuhusu jambo hilo.
- I. SERIKALI KUSHINDWA KUTATUA CHANGAMOTO ZA UUZAJI NA UGAWAJI WA ARDHI NCHINI**
- 77. Mheshimiwa Spika**, taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Fedha za Serikali ya ufanisi katika ugawaji wa viwanja nchini ya Machi, 2018 (**CAG PERFORMANCE AUDIT REPORT ON THE MANAGEMENT OF PLOTS ALLOCATION**) imedhihirisha kuwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeshindwa kusimamia na kutatua changamoto za umilikishaji wa ardhi kwa wananchi.
- 78. Mheshimiwa Spika**, changamoto kadhaa zimewekwa bayana ikiwemo uwepo wa uhitaji mkubwa wa viwanja/ardhi kwa wananchi hasa katika Mamlaka za Miji kuliko uwezo wa Wizara au Halmashauri kuwa na idadi ya viwanja vinavyotosheleza mahitaji ya wananchi. Vilevile ilidhihirika kuwa Halmashauri hazikuwa na uwezo wa kusimamia vizuri ugawaji wa viwanja ikiwa ni pamoja na kushindwa kuwa na viwanja ambavyo vinawavutia watu kwa kupimwa kwenye maeneo ambayo huduma za kijamii zimeshapelekwa.
- 79. Mheshimiwa Spika**, CAG ameeleza pia kuwa bei za maeneo ambayo yalitangazwa kuuzwa zilikuwa kubwa kiasi cha watu wengi kushindwa kugharamia na kukidhi vigezo ili wamilikishwe viwanja. Ni dhahiri kuwa bei za viwanja kwa mita mraba katika maeneo

mbalimbali ambayo miradi hiyo inatangazwa ni kuanzia shilingi 5,000 na kuendelea, kulingana na bei hizo sio watu wote watakaokuwa na uwezo wa kumiliki viwanja na wengi wao huamua kutafuta maeneo ya mashamba au yale ambayo sio rasmi na kuamua kujenga makazi.

- 80. Mheshimiwa Spika**, mathalani kwa Jiji la Dar es Salaam maeneo ya Manzese, Tandale, Mwananyamala, Kigogo, Mburahati, Mabibo, Buguruni n.k. ni maeneo ambayo sehemu yake kubwa sio rasmi na wananchi wengi hupenda kuishi huko kutokana na urahisi wa kufika mjini kwenye shughuli zao, masoko ya bidhaa mbalimbali za kuchuuza pamoja na uhusiano wa kijamii. Kambi Rasmi ya Upinzani ingetegemea kuwa Serikali ambayo inaona mbali ingeanza kupima miji ya pembezoni mwa Jiji (Peri-Urban) ili kuepuka changamoto za makazi holela za maeneo hayo na kuhakikisha kuwa miji ya pembezoni inayochipukia inapimwa na kuwekewa miundombinu pamoja na huduma mbalimbali za kijamii. Kwa kuwa ulipaji kodi wa viwanja ambavyo humilikishwa huwa ni jambo linalochukua muda mrefu, jambo ambalo Kambi Rasmi ya Upinzani haioni sababu ya ulipaji malipo ya awali kuwa makubwa
- 81. Mheshimiwa Spika**, hilo limeshindikana kwa Serikali hii ya CCM na hasa wakati huu wa awamu inayojita ya "hapa kazi tu" huku changamoto zilezile za makazi holela zikiendelea katika miji mipy ya pembezoni mwa Jiji la Dar es Salaam.
- 82. Mheshimiwa Spika**, Miradi mingi ya ugawaji wa viwanja ilikumbwa pia na changamoto ya kukamilika kwa wakati kutokana na kukosekana kwa wataalam pamoja na Serikali au Mamlaka za Serikali za Mitaa kushindwa kulipa fidia maeneo ambayo yametwaliwa kwa ajili ya kupimwa. Hali hii pia ilishawahidi kujitokeza katika Halmashauri ya Liwale ambapo mwaka 2004 Halmashauri ilitwaa maeneo

ya wananchi kwa lengo la kuyapima na kuyarasimisha lakini mradi huo umekuwa kilio kwa wananchi wa pande zote kwa maana ya walioonyesha nia ya kununua ardhi na wale ambao ardhi yao imetwaliwa kwa ajili ya kurasimishwa.

83. **Mheshimiwa Spika**, miradi kuchukua muda mrefu bila kukamilika na wananchi kulipwa fidia inajitokeza changamoto ya kutokulipwa fidia stahiki kwa sababu mradi ukikaa muda mrefu thamani ya shilingi nayo inakuwa chini kwa hiyo inawaathiri wananchi kimaendeleo kwa sababu wanashindwa kujipangia mipango yao kulingana na thamani ya shilingi. Huko Liwale ilifikia hatua hata wale waliokuwa wamelipa fedha kwa ajili ya kupata ardhi walielekezwa waongeze fedha mara tatu zaidi ya ile ambayo ilielekezwa ili kuendana na thamani ya shillingi.
84. **Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya CAG inaonyesha pia kuwa Wizara imeshindwa kusimamia na kutoa maelekezo kuhusu miradi mbalimbali inayotekelizwa na Wizara yenewe au Halmashauri jambo ambalo linaifanya Wizara kutotoa maelekezo kwa wakati mpaka ifike hatua ya migogoro na wananchi. Tofauti na jinsi ilivyokuwa inategemewa Wizara imejikita kukusanya kodi ya pango la ardhi pekee kuliko kusimamia ugawaji na umilikaji wa ardhi kwa ufanisi ili pia kodi wanayoipigia kelele iweze kukusanywa na kuongezeka.
85. **Mheshimiwa Spika**, Halmashauri ambazo zimekuwa zikitekeleza miradi imeonekana kuwa hazina vifaa vyta kitalamu kufanya kazi hiyo. Hii inatokana gharama za vifaa hivyo kuwa kubwa huku bajeti ya kutekeleza kazi hizo ikiwa kidogo na au hata kile kidogo kimekuwa hakitolewi kwa wakati. CAG aligundua kuwa ili uwe na vifaa vizuri kwa ajili ya kupima ardhi gharama zake sio chini ya milioni 50, jambo ambalo Halmashauri nyngi nchini hazina vifaa hivyo na hivyo kushindwa kuwa na ufanisi katika

kupima ardhi kwa ajili kumilikisha. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali Kuu kuchukua jukumu hili la kuhalikisha inatoa ruzuku kwa Halmashauri kwa ajili ya kununua vifaa hivi, pendekezo hili angalau litasaidia ahadi ya CCM ya kutoa milioni 50 kila Kijiji ambayo imekuwa ahadi hewa hadi sasa.

- 86. Mheshimiwa Spika**, Wizara pamoja na Ofisi ya Rais, TAMISEMI wameonekana kushindwa kuwa na vigezo vya matokeo ya utendaji yanayotegemewa pamoja na mfumo wa kupata taarifa kutoka katika Halmashauri kuhusiana na masuala ya ardhi. Jambo hili pia limesababishwa na kutokuwa na mahusiano ya moja kwa moja na au kuwa utofauti wa taarifa kwa jambo moja. Hali hii inaonyesha udhaifu wa kiutendaji wa Serikali pamoja na kuendelea kuchochea mlgogoro katika sekta ya ardhi. Kama jambo limeamuliwa na mamlaka ya Serikali za Mitaa halafu Wizara haina taarifa, Wizara nayo inaweza kuja na maamuzi mengine kwa jambo lile lile. Kutokana na hali kuwa hivi ni wazi kuwa migogoro ya ardhi bado itaendelea katika nchi yetu.
- 87. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inamtaka Waziri kuhakikisha kuwa inasimamia na kutekeleza ushauri na mapendekezo ya CAG kuhusu changamoto za ugawaji na usimamizi wa ardhi nichini la sivyo ataendelea kuwa Waziri wa kutatua migogoro ya ardhi kila wakati kuliko kuendelea na kazi zingine za Wizara.

#### **J. URASIMISHAJI MAKAZI**

- 88. Mheshimiwa Spika**, Serikali, kwa kushirikiana na kampuni binafsi za mipangomiji na upimaji, inatekeleza Programu ya Miaka 10 ya Urasimishaji Makazi na Kuzuia Ujenzi Holela Mijini (2013-2023). Utafiti uliofanywa na Kambi Rasmi ya Upinzani umebaini kuwa pamoja na kujitokeza kwa Kampuni nydingi zinazotekeliza Programu hii maeneo mbalimbali

nchini; bado Urasimishaji Makazi unakwenda kwa kusuasua kwa sababu ya changamoto zifuatazo:

1. Kuwepo kwa urasimu mwingi katika kukagua ramani zinazowasilishwa na Kampuni katika mamlaka za upangaji miji za Halmashauri na hivyo kusababisha uchelewaji mkubwa katika kusajiliwa kwa ramani hizo.
2. Baadhi ya Halmashauri kutaka sehemu ya pesa inayolipwa na wananchi kwa ajili ya kupangiwa na kupimiwa viwanja vyao itumike kama chanzo cha mapato ya ndani ya halmashauri. Baadhi ya halmashauri hudai kupewa asilimia 10 hadi 15 ya pesa inayolipwa kwa ajili ya kupanga na kupima kila kiwanja
3. Wataalam wa baadhi ya Halmashauri, kutofanya uhamasishaji na kuziachia Kampuni zifanye kila kitu.

**89. Mheshimiwa Spika**, ili kutatua changamoto hizo, Kambi ya Upinzani, tunaishauri Serikali ifanye yafuatayo:

1. Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, izisimamie kikamilifu mamlaka za upangaji za halmashauri kwa kuhakikisha michoro yote ya mipangomiji na upimaji inakaguliwa na kutolewa maoni ya maboresho kwa wakati ili kuondoa uchelewaji mkubwa wa miradi ya Urasimishaji Makazi.
2. Wizara itoe tamko la kuzikataza Halmashauri zote nchini kuzigeuza sehemu ya pesa zinazolipwa na wananchi kwa ajili ya kurasimishiwa maeneo yao, kuwa chanzo cha mapato yao ya ndani.

3. Wizara ihakikishe watendaji wake wa Halmashauri wanashirikiana kwa karibu na Kampuni hizi ili kuwajengea wananchi imani juu ya ubia uliopo baina ya Serikali na Kampuni hizi na kuhakikisha wananchi wanahamasishwa kikamilifu kulpia gharama za Urasimishaji kwa wakati

**K. RASIMU YA MPANGO KABAMBE WA JIJI LA DAR ES SALAAM**

90. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imepokea Rasimu ya Mpango Kabambe wa Jiji la Dar Es Salaam kutoka kwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Dar Es Salaam.
91. **Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa kifungu Na. 12(1) cha sheria ya Mipangomiji Na. 8 ya mwaka 2007, wananchi na wadau wa maendeleo ya Jiji wanaalikwa kwenda Ofisi za Jiji na Manispaa zake kwenda kuwasilisha maoni na mapendekezo yawe sehemu ya taarifa ya kukamilisha mpango huo. Kambi Rasmi ya Upinzani inawahimiza wananchi kupakua mpango huo kutoka kwenye tovuti ya ***www.lands.go.tz*** na kwenda kupeleka maoni na mapendekezo kwa mamlaka zote zinazohusika.
92. **Aidha, Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imetathmini baadhi ya mijadala ya kusikiliza umma (public hearings) iliyoratibiwa na Wakurugenzi wa Manispaa za Jiji la Dar Es Salaam kwa mujibu wa kifungu Na. 12(2) cha sheria tajwa na kubaini kwamba kuna udhaifu mkubwa katika ushirikishaji na ushirikishwaji wa umma.
93. **Mheshimiwa Spika**, hivyo, kwa uzito wa Jiji la Dar Es Salaam na Manispaa zake ambazo kwa ujumla linachukua takribani asilimia kumi ya idadi ya watu nchini Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuwasilisha Bungeni Rasimu ya Mpango

Kabambe wa Jiji la Dar Es Salaam kwa ajili ya Wabunge kama wadau wa maendeleo ya Jiji kushiriki katika mchakato na kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Wabunge.

#### **L. MIGOGORO KATI YA MAMLAKA ZA HIFADHI NA WANANCHI**

- 94. Mheshimiwa Spika**, kwa miaka mingi Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu imekuwa ikieleza na kuwasilisha migogoro ya ardhi nchini ambapo inaweza kuwekwa katika makundi kulingana na jinsi inavyoshabihiana na kutokana na pande zinazohusika katika mgogoro au sababu zinazochochea migogoro hiyo.
- 95. Mheshimiwa Spika**, kumeendelea kuwepo migogoro kati ya wananchi na mamlaka za hifadhi ambapo inasemekana wananchi wamevamia hifadhi au hifadhi zimeongeza mipaka yake tofauti na jinsi ilivyokuwa awali.
- 96. Mheshimiwa Spika**, zipo sababu kadhaa zinazochangia migogoro kati ya mamlaka za hifadhi na wananchi na mojawapo ni vijiji ambavyo viro katika hifadhi lakini wakati huo vimesajiliwa na kupewa hati na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI). Taarifa ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira inaonyesha kuwa kati ya vijiji 228 ambavyo vimebainika kuwa viro katika maeneo ya hifadhi ni vijiji 157 ambavyo ni takribani 68% vimepewa hati ya usajili.
- 97. Mheshimiwa Spika**, Hifadhi zetu zinasimamiwa na Serikali na TAMISEMI ni Serikali na inaongozwa na Rais wa nchi. Kama Serikali ni moja, iweje kuwe na utofauti wa kiutendaji kati ya mamlaka mbili za Serikali ambazo zinaongozwa na Chama kile kile? Huu ni udhaifu mkubwa wa kiutendaji wa Serikali ya CCM.

98. **Mheshimiwa Spika**, imebainika pia kwamba hakuna mipango endelevu ya matumizi ya ardhi ya vijiji jambo linalosababisha ardhi yenye rutuba na maeneo ya ufugaji kupungua na kuanza kutokea kwa migogoro ya ardhi. Aidha wananchi wengi wamekuwa na tabia ya kufuga mifugo mingi jambo linalopelekea ardhi kushindwa kuhimili wingi huo.
99. **Mheshimiwa Spika**, Vilevile mamlaka nyingi za hifadhi zimeshindwa kuwa na tafsiri ya mipaka yao jambo linalopelekea kushindwa kuwa na alama za kudumu. Hali hii imepelekeea baadhi ya hifadhi kuongeza mipaka na kuingilia makazi ya wananchi. Pamoja na Waziri Mkuu kuagiza mipaka yote ya hifadhi iwekewe vizingi (beacons) jambo hilo mpaka sasa halijafanikiwa.
100. **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inalitaka Bunge kuingilia kati ili kuja na suluhisho la kudumu kuhusu migogoro ya ardhi kati ya wananchi na mamlaka za hifadhi. Hali imekuwa mbaya zaidi ambapo taarifa zinaonyesha kuwa askari wa hifadhi wamekuwa wakitumia silaha za moto kuua mifugo ya wananchi inayoingia katika hifadhi jambo ambalo linachochea chuki na uhasama na kuwa sababu ya tabia za kujichukulia sheria mkononi kuongezeka.

*[MANENO HAYA YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]*

#### **M. TAASISI ZA SERIKALI KUTOKUWA NA HATI MILIKI ZA ARDHI**

101. **Mheshimiwa Spika**, katika ripoti ya CAG ya mwezi Juni 2017, ilizitaja baadhi ya Taasisi za Serikali zisizokuwa na haki miliki ya Ardhi kinyume na maelekezo yaliyowahi kutolewa na Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ya tarehe 7 Septemba, 2016.

102. **Mheshimiwa Spika**, baadhi ya Taasisi hizo ni Wakala wa Maabara ya Mifugo, Shirika la Maabara ya Mifugo, Wakala wa Utafiti wa Miamba, Wakala wa Hifadhi ya Chakula, Taasisi ya Uhasibu, Wakala wa Ugavi na Huduma za Manunuzi, Bonde la Maji la Mto Ruvu, Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Handeni, Bonde la Maji Pwani ya Kusini Ruvuma na Bonde la Maji Rufiji, ardhi za majengo mbalimbali ikiwemo majengo ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Makamu wa Rais, Balozi mbalimbali ukiwemo Ubalozi wa New Delhi, Rome na Kampala Uganda.
103. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuwa ni aibu kwa Mamlaka za Serikali kukosa hati miliki ya ardhi, lakini pia ni muhimu mamlaka na taasisi hizi zikatambua masuala yote yanayohusu ardhi ni masuala nyeti. Usalama wa ardhi siku zote upo kwa mwenye hati ya umiliki. Ardhi ni ulinzi. Hivyo kuendelea kuwa na maeneo ya Serikali ambayo hayana hati maana yake ni kuanza kukaribisha uvamizi au migogoro baina ya Serikali na wananchi hususani katika maeneo yenye vyanzo vyaa maji na vinavyotegemewa kwa shughuli mbalimbali za kijamii.
104. **Mheshimiwa Spika**, kukosa hati za umiliki wa ardhi kunaweza kuisababisha Serikali ikaingia katika hasara kubwa endapo patajitokeza watu ambaao nao watadai kuwa wamiliki wa ardhi ya maeneo hayo kisheria. Vilevile, Serikali itashindwa kujua thamani ya ardhi inayomilikiwa na taasisi au Wakala husika na hivyo kukosa ufanisi katika kufuatilia na kusimamia mali zake
105. **Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa jambo hili limewahi kusemwa na Waziri mwenye dhamana pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara na pia Ofisi ya CAG bila kufanyiwa kazi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuanza kuzichukulia hatua mara moja

taasisi na mamlaka zote za Serikali ambazo hazijatimiza wajibu huu mkubwa wa kisheria.

#### **N. KODI YA MAJENGO NA MALALAMIKO YA WANANCHI KUHUSU THAMANI YA MAJENGO**

106. **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani kwa miaka mitatu mfululizo imepinga uamuza wa Serikali kupoka Halmashauri chanzo cha mapato kinachotokana na kodi ya majengo. Tulieleza kwa kirefu kuhusu nia ovu ya Serikali kupoka chanzo hicho kuwa ni mkakati wa kuziua Halmashauri nyingi za mijini ambazo huongozwa na Vyama vya Wapinzani.
107. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na hayo yote limeibuka sakata lingine la utaratibu mbovu wa kufanya tathmini za nyumba za wananchi kwa kuongeza thamani ya nyumba ili waweze kulipa kodi kubwa ya majengo. Jambo hili linalalamikiwa sana na wananchi kwa sababu Halmashauri nyingi ambazo zimefanya kinachoitwa tathmini ya nyumba hawajawashirikisha wananchi ambao ndio wamiliki wa majengo hayo.
108. **Mheshimiwa Spika**, Waziri wa Fedha na Mipango alilihakikishia Bunge kuwa nyumba yoyote ambayo hajafanyiwa tathmini mmiliki atalazimika kulipia shilingi 10,000 kwa nyumba ya kawaida na shilingi 50,000 kwa jengo la ghorofa.
109. **Mheshimiwa Spika**, Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini ya mwaka 2016 kifungu cha 55 kinampa Mthamini Ardhi mamlaka kuingia eneo au nyumba ya mtu kwa ajili ya uthamini isipokuwa atatakiwa kutoa taarifa kwa mmiliki au mkazi wa nyumba au eneo hilo. Aidha, kifungu cha 51 kinaweka utaratibu wa njia zitakazotumiwa na Mthamini kufanya tathimini ambapo Mthamini atatakiwa kueleza sababu za njia alizotumia.

110. **Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 7(1)(a) cha Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini inatoa mamlaka kwa Mthamini Mkuu wa Serikali kufuta tathmini yoyote ambayo anaona kuwa utaratibu haukuatuwa.
111. **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka maelezo ya Waziri wa Ardhi ya sababu zinazopelekea Serikali kufumbia macho utaratibu wa kufanya tathimini ya nyumba za wananchi bila kuzingatia utaratibu uliowekwa kwa mujibu wa sheria ambao umefanywa kwa kuwavizia wananchi. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Serikali imwelekeze Mthamini Mkuu kufuta tathmini zilizofanywa katika Halmashauri mbalimbali nchini ikiwemo Manispaa ya Bukoba Mjini ambapo tathmini ilifanyika bila kuzingatia taratibu.

## O. MAJIJI YA VIUNGANI (SATELITE TOWNS)

112. **Mheshimiwa Spika**, Mwaka 2006/07 Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ikishirikiana na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na Manispaa zake tatu(za wakati huo) ilianzisha mkakati wa kuanzisha miji midogo sita itakayokuwa na vituo vya huduma za kijamii na za kibashara. Kutokana na ukubwa wa mpango huo iliamuliwa kuwa utekelezaji uanze katika eneo la Kibamba Luguruni ambalo lilipaswa kuwa eneo la mfano ambapo uzoefu katika uendelezaji ungetumika kwa maeneo mengine ya Jiji na nchi nzima kwa ujumla.

113. **Mheshimiwa Spika**, Uanzishwaji wa Mji wa Kibamba uligawanywa katika maeneo makubwa matatu: Eneo Kitovu cha Mji cha Luguruni, eneo la makazi mbadala la Kwembe Kati na uendelezaji wa eneo linalozunguka kituo. Hata hivyo miaka zaidi ya kumi na mbili imepita bila uendelezaji huo kukamilika na hivyo sehemu kubwa ya maeneo tajwa kurejea

kuwa mapori na kuanza kurejea kwa migogoro ya ardhi katika maeneo tajwa.

114. **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza matokeo ya tathmini ya utekelezaji wa mpango huo na kueleza bayana kasoro na matatizo yaliyojitokeza sambamba na kuharakisha ujenzi wa mji husika ili kuwa mfano kwa mipango ya ujenzi wa miji mingine ambayo maandalizi yake yanaelezwa kutaka kufanyika katika mwaka wa fedha 2019/2020.

115. **Mheshimiwa Spika**, Serikali iliwahi kueleza katika Bunge la 10 wakati ikijibu swali la aliyekuwa Mbunge wa Ubungo John Mnyika ambaye sasa ni Mbunge wa Jimbo la Kibamba kwamba Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) limeteuliwa kuwa mwendelezaji wa mji huo. Aidha, Bunge lilielezwa kuwa NHC ilikuwa katika hatua za mwisho za kuipata kampuni binafsi ya kuwa mwendelezaji mwenza. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ieleze ni kampuni gani imepatikana na kazi ya uendelezaji itaanza lini? Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Wizara ieleze nini nafasi ya Serikali na wananchi katika uendelezaji wa mradi huo na lini mikataba kuhusu uendelezaji wa Mji wa Luguruni itawekwa wazi kwa wawakilishi wa wananchi na umma?

#### P. SHIRIKA LA TAIFA LA NYUMBA

116. **Mheshimiwa Spika**, Aya ya 2.1 ya Sera ya Uwekezaji wa NHC ya 2011 inataka uwekezaji wa NHC uzingatie marejesho ya mtaji uliowekezwa (Return On Investment-ROI), muda wa marejesho ya uwekezaji, pamoja na kuangalia sababu nydingine za kiuchumi na kijamii. Ukaguzi wa CAG ulibaini kuwa miradi miwili ya NHC imesimama tangu mwaka, 2017 kwa sababu ya ukosefu wa fedha.

- 117.** **Mheshimiwa Spika**, Mradi wa nyumba (711-1) uliopo Kawe wenyе Sh. Bilioni 142.55 Mradi wa Nyumba (711-1) ni mradi wa NHC uliopo katika kitalu Na 711 Kawe, Kinondoni, Dar es Salaam. Mnamo tarehe 04 Aprili 2014, NHC iliingia mkataba na Estim Construction Company Limited wenyе thamani ya Sh. bilioni 105.11 pamoja na VAT kwa ajili ya usanifu na ujenzi kupitia zabuni Na. PA/066/2011-2012/HQ/W/03 kwa muda wa wiki 156 toka siku ya kwanza ya ujenzi. Mnamo tarehe, 04 Novemba 2014, NHC na Estim Construction Company Limited waliingia mkataba wa nyongeza kwa ajili ya kuhamisha mradi huo kutoka sehemu ya awali ulipokuwa umepangwa kutekelezwa katika eneo la Ngano kitalu Na. 79-82 na kupelekwa kitalu Na.711-1 Kawe. Upembuzi yakinifu wa mradi huu ulifanywa Juni 2014; mlezi miwili baadaye baada ya kusaini mkataba. Hii inaonesha kwamba mkataba ulisainiwa kabla hata ya kufanya upembuzi yakinifu kwenye mradi huo.
- 118.** **Mheshimiwa Spika**, matoeko ya upembuzi yakinifu ni pamoja na gharama za ujenzi zilizokisiwa kuwa ni Dola za Kimarekani milioni 69.43, sawa na Sh. bilioni 114.4, muda wa ujenzi ulikadirwa kuwa ni miaka mitatu mpaka 2017, uliainisha vyanzo vya fedha za mradi, ambapo vyanzo vya ndani vitachangia asilimia 35 na mikopo itachangia asilimia 65.
- 119.** **Mheshimiwa Spika**, mnamo mwezi Septemba 2017, NHC walibadili andiko la kibashara na kuainisha kuwa, gharama za mradi zitaongezeka mpaka Sh. bilioni 142.55, mradi utaisha baada ya miaka miwili mpaka 2019 na vyanzo vya fedha za mradi vitabadilika na kuwa vyanzo vya ndani vitachangia asilimia 37 na mikopo itachangia asilimia 63.
- 120.** **Mheshimiwa Spika**, ukweli ni kuwa mradi huo wa mabilioni ya shilingi ulisimama tangu mwanzoni

mwa mwaka 2017 kutohana na ukosefu wa fedha. Mpaka wakati huo, mradi ulikuwa umekamilika kwa asilimia 20, na umetumia jumla ya Sh. bilioni 26.31 kutoka katika vyanzo vya ndani. Kwa mujibu wa upembuzi yakinifu wa CAG, NHC ilikuwa na uhakika wa kupata fedha kwa ajili ya mradi, lakini mpaka sasa imeshindwa kukopa kwa ajili ya ujenzi huo.

- 121. Mheshimiwa Spika**, mradi wa nyumba (711-2) uliopo Kawe wenye Thamani ya Shilingi Bilioni 103 Mradi wa Nyumba (711-2) ni mradi wa NHC uliopo kawe katika kitalu Na 711/2 karibu na ufukwe wa bahari, Kinondoni, Dar es Salaam. Mnamo tarehe 16 Oktoba 2013, NHC iliingia mkataba na CRJE (EA) LTD wenye thamani ya Sh. bilioni 64.37 pamoja na VAT kwa ajili ya usanifu na ujenzi kupitia zabuni Na. PA/066/2011-2012/HQ/W/38 kwa kipindi cha muda wa wiki 130 kuanza siku ya kuanza ujenzi. Mnamo tarehe 03 Novemba 2014, NHC na CRJE (EA) LTD waliiingia nyongeza ya mkataba ambapo walikubaliana bei mpya ya kazi kuwa ni Sh. bilioni 71.17 pamoja na VAT. Upembuzi yakinifu wa mradi huu ulifanywa mnamo mwezi Juni 2014 miezi tisa baada ya kusaini mkataba. Hii inaonesha kwamba mkataba ulisainiwa kabla hata ya kufanya upembuzi yakinifu wa mradi huo.

- 122. Mheshimiwa Spika**, Matokeo ya upembuzi yakinifu ni pamoja na gharama za ujenzi zilikisiwa kuwa ni Dola za Kimarekani milioni 43.61 sawa na Sh.bilioni 71.86, muda wa ujenzi ulikadiriwa kuwa ni miaka mitatu mpaka 2017, uliainisha vyanzo vya fedha za mradi, ambapo vyanzo vya ndani vitachangia asilimia 15 wakati mikopo itachangia asilimia 85. Mnamo mwezi Septemba 2017 NHC walibadili andiko la kibiashara na kuainisha kuwa, gharama za mradi zitaongezeka mpaka Sh. bilioni 103, mradi utaisha baada ya miaka miwili mpaka 2019 na vyanzo vya fedha za mradi vitabadilika na kuwa

vyanzo vya ndani vitachangia asilimia 29 na mikopo itachangia asilimia 71.

**123. Mheshimiwa Spika**, ilibainika kuwa mradi huo ulisimama tangu mwanzoni mwa mwaka 2017 kutokana na ukosefu wa fedha. Mpaka wakati huo mradi ulikuwa umekamilika kwa asilimia 30 na umetumia jumla ya Sh. bilioni 34.87; ambapo vyanzo vya ndani vilichangia kiasi cha Sh. bilioni 11.64 na mkopo kutoka Benki ya TIB ulikuwa ni Sh. bilioni 23.23. Mkopo wa TIB uliochukuliwa tarehe 6 Julai 2015 na ultakiwa uanze kulipwa baada ya miezi 36 (Julai 2018). Hii ina maana kwamba kwa sasa NHC inatumia fedha kutoka vyanzo vingine kwa ajili ya kulipa mkopo huo. Hii ni kwa kuwa wakati wa kulipwa mkopo huo tayari umeshafika huku ujenzi haujakamilika.

**124. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kuwa kwa kadri majengo yanavyozidi kukaa bila kutumika uchakavu (wear and tear) wake unakuwa ni mkubwa zaidi na hivyo kupoteza thamani yake kwa haraka sana (depreciation). Hivyo basi, Kambi inamtaka Waziri alieleze Bunge nini mustakabali wa ukamilishwaji wa miradi hiyo?

**Q. MASUALA YATOKANAYO NA HOTUBA YA UPINZANI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018**

**125. Mheshimiwa Spika**, zipo baadhi ya hoja ambazo zilibuliwa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ambazo Serikali imeshindwa kuzitekeleza kwa ujumla wake; hoja hizo ni kama ifuatavyo;

- (i) Serikali kuendelea kuchukua vyanzo vya mapato vya Halmashauri hasa kodi ya majengo ambapo imefikia hatua Mamlaka za Wilaya zimeanza kutoza kodi kwa wananchi wanyonge wa vijijini jambo ambalo Serikali imeendelea kulifumbia macho mpaka sasa na bado

inaendelea kupoka vyanzo vingine vya mapato ya Halmashauri.

- (ii) Serikali kushindwa kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa maazimio ya Kamati Teule ya Bunge kuhusu migogoro mbalimbali ya ardhi nchini. Pamoja na kuwa Serikali iliahidi kuwasilisha taarifa ya utekelezaji Bungeni.
- (iii) Serikali kushindwa kuwalipa malipo ya hisani wananchi wa Mloganzila ambao ardhi yao ilitwaliwa wa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Muhimbili Kampasi ya Mloganzila.
- (iv) Serikali kufumbia macho Wakuu wa Wilaya na Mikoa ambao wamekuwa na tabia ya kuingilia utendaji kazi wa Mabaraza ya Ardhi jambo ambalo linaathiri mfumo wa utoaji haki katika baadhi ya maeneo nchini.
- (v) Serikali kuendelea kushindwa kusimamia sekta ya milki ya nyumba pamoja na kushindwa kuunda mamlaka ya kusimamia sekta hiyo kwa miaka saba toka ushauri utolewe na Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani.

**126. Mheshimiwa Spika**, masuala haya pamoja na engine mengi bado ni changamoto ambazo Serikali haijazifanya kazi kwa ukamilifu wake. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge lako tukufu ni kwa nini mpaka sasa haijafanya kazi hoja hizi ambazo zilitolewa na baadhi yake Serikali kukubali kuzifanya kazi.

**R. MAPITIO YA BAJETI YA MWAKA 2016/2017, 2017/2018 NA MWELEKEO WA BAJETI YA MWAKA 2018/2019**

**127. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2016/17 Wizara ilitengewa jumla ya shilingi **61,873,949,000.00** kati ya fedha hizo, miradi ya maendeleo ilitengewa shilingi **20,000,000,000.00**

ambazo shilingi **10,000,000,000.00** zikiwa fedha za ndani na shilingi **10,000,000,000.00** Fedha za matumizi mengineyo zilizotengwa ni shilingi **25,531,158,000.00**

128. **Mheshimiwa Spika**, takwimu za Wizara zinaonesha kuwa hadi mwezi Februari, 2017, fedha za matumizi mengineyo (OC) zilizopokelewa ni shilingi **9,994,249,148.00** sawa na asilimia **39.2** ya bajeti iliyopitishwa na Bunge. Aidha kwa miradi ya maendeleo fedha zilizokuwa zimepokelewa ni shilingi **7,626,219,314.00** sawa na asilimia **38**, lakini katika hizo fedha za maendeleo kuna shilingi **3,301,058,684.65.00** kwa ajili ya kulipia deni la Mkandarasi aliyeanda Mipango Kabambe ya Majiji ya Arusha na Mwanza.
129. **Mheshimiwa Spika**, kwa hali hiyo ni kwamba fedha halisi zilizopokelewa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kwa kipindi cha bajeti ya mwaka 2016/17 ni shilingi **4,325,160,629.4** pekee ambapo ni sawa na asilimia **21.62** tu.
130. **Mheshimiwa Spika**, mwaka wa fedha 2017/18 Wizara iliomba na kuidhinishiwa jumla ya shilingi **68,030,880,526/-** kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali. Kati ya fedha hizo shilingi **21,470,166,074.00** ni matumizi mengineyo, ikiwa ni pungufu ya shilingi **4,060,991,926.00** kwa kulinganisha na maombi ya mwaka 2016/2017 kwa matumizi mengineyo. Fedha za maendeleo zilizokuwa zimeombwa ni jumla ya shilingi **25,400,000,000/-** ambapo shilingi **16,400,000,000.00** ni fedha za ndani na shilingi **9,000,000,000.00** ni fedha za nje.
131. **Mheshimiwa Spika**, ni dhahiri kuwa Wizara ya Ardhi bado inao uwezo wa kukusanya mapato mengi zaidi ya ndani, lakini imeshindwa kufanya hivyo kutokana na Serikali hii kushindwa kuwekeza katika kurasimisha makazi na ardhi kwa ujumla. Hii inaonekana wazi kwa kuangalia kiasi kilichotengwa mwaka 2016/2017 na kiasi kilichotolewa. Kambi Rasmi

ya Upinzani ilishauri kuwa fedha za maendeleo ziongezwe ili upimaji wa ardhi na umilikishwaji ufanyakie kwa haraka ili kodi ya ardhi ikusanywe kwa sababu haiwezani Serikali ikataka kuvuna pasipo kuwa na uwekezaji.

132. **Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia mwezi Februari, 2018 Wizara ilipokea fedha za miradi ya maendeleo kiasi cha shilingi **5,830,000,000.00** ambazo ni fedha za ndani sawa na **35%** na shilingi **6,998,186,360.00** ni fedha za nje sawa na **77.7%**. Kwa takwimu hizi za Wizara ambayo fedha za ndani zinatolewa kwa **35%** kwa ajili ya miradi ya maendeleo na wahisani kutoa **77.7%** ni ishara kuwa Serikali haina umakini na wala haina nia ya kutatua changamoto katika sekta ya ardhi nchini.
133. **Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa fedha za matumizi mengineyo fedha zilizopokelewa ni kiasi cha shilingi **12,265,022,342.92** sawa na **49.3%** ya bajeti iliyokuwa imetengwa. Katika hali ya kushangaza Serikali ilikuwa imepanga na kutenga kiasi cha shilingi **10,000,000,000.00** kwa ajili ya kuziwezesha Halmashauri nchini kusimamia sekta ya ardhi, hadi kufikia Februari mwaka, 2018 Wizara haikuwa imepokea chochote kwa ajili ya kuziwezesha Halmashauri.
134. **Mheshimiwa Spika**, Halmashauri ni wadau muhimu katika kusimamia na kuweka mipango ya ardhi nchini lakini Serikali imeona isipeleke chochote kuziwezesha Halmashauri kufanya jukumu hilo. Ni dhahiri kuwa changamoto zilizoelezwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Fedha za Serikali zitaendelea kuwepo kwa sababu Serikali haina nia ya kupeleka fedha kuziwezesha Halmashauri kwa ajili ya miradi ya kuendeleza ardhi.
135. **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2018/2019 Wizara inaomba bajeti ya jumla ya shilingi **65,989,347,638.00** ambapo fedha za maendeleo ni

kiasi cha shilingi **30,537,602,000.00** sawa na ongezeko la shilingi **5,137,602,000.00** ambapo fedha za ndani ni **20,000,000,000.00** na za nje ni shilingi **10,537,602,000.00**. Kwa upande wa matumizi mengineyo kiasi cha shilingi **35,451,745,638.00** pungufu ya **7,803,337,288.00** ambapo kwa mwaka uliopita matumizi mengineyo yalikuwa **43,255,082,926.00**.

- 136. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Februari, 2019 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi 46,119,176,931.31 sawa na asilimia 59 ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Kati ya fedha hizo fedha za maendeleo zilikuwa ni shilingi 16,858,308,152.46. Aidha kwa mwaka wa fedha 2019/20 Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 57,439,991,387.00 ikiwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya shilingi 33,155,487,000.00 na maendeleo ya shillingi 24,284,504,387.00

## S. HITIMISHO

- 137. Mheshimiwa Spika**, ardhi ni rasimali muhimu sana katika ukuaji wa uchumi wa nchi yetu, ardhi ni sehemu kubwa ya maendeleo ya wananchi. Kuporomoka kwa sekta ya miliki ya nyumba (Real Estate), udhaifu katika kusimamia ugawaji na upangaji wa ardhi, migogoro ya ardhi kati mamlaka za hifadhi na wananchi ni changamoto ambazo zinarudisha nyuma wananchi katika maendeleo yao.

- 138. Mheshimiwa Spika**, aidha Serikali kushindwa kutoa fedha za maendeleo za ndani kwa ukamilifu na pia kushindwa kabisa kupeleka fedha za marejesho kuzisaidia Halmashauri ni ishara kuwa Serikali haioni umuhimu wa kuendeleza ardhi nchini. Hali hii inapelekea wananchi walio wengi kuishi maeneo ambayo sio rasmi na hivyo kupelekea kukosa fursa ya kupata mikopo kwa ajili ya shughuli mbalimbali za maendeleo. Kambi Rasmi ya Upinzani

inaitaka Serikali kuipa kipaumbele sekta ya ardhi nchini kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

139. **Mheshimiwa Spika**, CHADEMA inaanini kuwa umiliki na matumizi ya ardhi umekuwa daima na mchango mkubwa katika kuamua mustakabali wa mchakato wa kisiasa, kiuchumi na kijamii. Ardhi hapa Tanzania imilikiwe na itumike kwa matumizi bora, kwa malengo madhuhuti, kwa uzalishaji na kwa ushirikishi pasipo kuathiri matumizi ya vizazi vijavyo.
140. **Mheshimiwa Spika**, aidha, tunaamini kwamba ardhi ndiyo msingi wa maendeleo na hivyo inahitaji kugawanywa kikamilifu mionganoni mwa wananchi na jamii kwa ujumla na pia matumizi mengine kwa namna ambayo itaongeza ufanisi wa ardhi iliyopo.
141. **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani tunaamini katika mfumo wa umiliki wa ardhi ambapo kila mwananchi atamiliiki ardhi na rasilimali zake juu na chini ya ardhi hiyo, ardhi itapatikana kutokana na ridhaa ya mnunuzi na muuzaji wa ardhi husika.
142. **Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

.....  
Wilfred M. Lwakatare (Mb)

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI-WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

31.05.2019

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, tunakushukuru sana kwa hotuba yako. Waheshimiwa tunaelekeea kwenye uchangiaji lakini kabla hatujaanza na

mchangiaji wetu wa kwanza nimekuwa nkipata maoni mbalimbali kuhusu mapendekezo ya ratiba yetu ya wiki ijayo na hasa namna ambavyo matarajio ya Idd yanavyoweza kuwa. Kwa ratiba tuliyonayo hivi sasa Wabunge, matarajio yetu ya Idd ni Jumanne au Jumatano lakini *indications* kutoka BAKWATA zinasema huenda ikawa Jumatano na Alhamis au Alhamisi.

Kwa hiyo, kuanzia Saa Kumi kwa sababu tutakuwa pamoja hapa, nitaweza kupokea mapendekezo mbalimbali kutoka kwenu Waheshimiwa Wabunge ya mnadhani ratiba yetu tunaweza tukai-*twist* namna gani ili ushiriki wenu kwenye Idd uweze kuwa mzuri lakini na mambo ya Bunge yaweze kwenda vizuri. Saa za jioni unaweza ukaniandikia kikaratasi tu, nitaratibu hapa nikiona tumefika mahali basi naweza nikahusisha Serikali na Kamati ya Uongozi tukaona tunaweza kufanya nini badala ya watu kutoroka toroka. Hakuna sababu ya kutoroka, *at least* Jumatatu tunaamka nayo na siku zinazofuata, basi mapendekezo yanaweza yakaja saa za jioni ya namna gani mnadhani tufanye.

Sasa tutapata wachangiaji kama watatu tu siyo zaidi. Tuanze na Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein upande wa CUF na atafuatiwa na Mheshimiwa Saed Kubenea dakika tano, Mheshimiwa Yussuf dakika kumi.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuwa mchangiaji wa mwanzo katika Wizara hii. Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ndiyo inayobeba maisha yetu sisi wananchi wote tulimo ndani ya Tanzania na Wizara hii inajukumu kubwa sana. Kwa hiyo, nitachangia kwa kadiri ya uwezo Mungu aliyonipa.

Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri kijukuu changu, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa namna ambavyo wanafanya kazi na sisi Kamati wanatushirikisha katika utendaji wa kazi yao. Pongezi hizi ziendane sambamba

na utendaji ambao umetukuka ambao wanao Mungu awajalie waende mbele zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ardhi haiongezeki, lakini idadi ya watanzania inaongezeka, idadi ya mifugo inaongezeka, shughuli za kibinadamu zinaongezeka, mahitaji ya vitu vilivyopo juu ya ardhi na chini ya ardhi yanaongezeka lakini ardhi yetu inabaki pale pale. Sasa ni lazima tuishauri Serikali iangalie namna bora ya kupanga matumizi bora ya ardhi kwa haraka ili tuwe na kilimo cha kisasa, tuwe na ufugaji wa kisasa lakini pia tutumie maliasili zetu kama misitu na maeneo yaliyohifadhiwa vizuri kwa sababu hayo yatabaki hivyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, hebu tujenge picha ya miaka 50 ijayo, watanzania ambapo wanaweza kufikia idadi ya milioni 100 halli itakuwaje na ardhi yetu ni lle ile. Ama Inazidi kupungua kwa sababu ya *erosion* na mambo mengine ya mabadiliko ya tabia nchi. Kwa hiyo, ni lazima Wizara iwezeshe kupewa fedha kwa ajili ya kupanga matumizi bora ya ardhi ili tuweze kukabiliana na changamoto ilinayokuja hapo mbele ya ongezeko la idadi ya watu, idadi ya wanyama, idadi ya matumizi yale tuweze kuendana na hali halisi ilivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tukiangalia miaka mitano tu au kumi tusipoangalia zaidi ya hapo tutakuja kukuta tunaachia vizazi vyetu matatizo makubwa sana ya ardhi. Kwa hiyo, tuiombe Serikali kwa heshima kubwa na taadhima kubwa na mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani, itoe fedha kumuwezesha Waziri wa Ardhi na Watendaji wake waweze kupima ardhi na kupanga matumizi ya ardhi na yasimamiwe kwa faida yetu na maisha yetu na kizazi kijacho. Vinginevyo tutajikuta katika hasara kubwa sana sana sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka nilizungumzie ni suala la migogoro ya ardhi. Hili litaendelea kuwepo lakini inaumiza kichwa kuona bado kuna migogoro ya ardhi ya wilaya na wilaya, kuna migogoro ya ardhi baina ya kata na kata, kuna migogoro ya ardhi baina ya kijiji na kijiji. Kwanini, wakati yote hayo yanasmamiwa na taasisi

moja, au vitu vyote hivyo viko chini ya Serikali. Ninavyoona na ninavyojifunza tukiwa kwenye Kamati tunapokwenda huko ni kwamba, suala la ardhi, sera na mambo mengine yako chini ya Wizara. Huko chini mmiliki wa ardhi ni halmashauri, ni kijiji, wao ndiyo wenye maamuzi, sasa hapa kutakuwa na mvutano. Waziri anasema sera inasema hivi, lakini mwenye ardhi ambaye ni kijiji au ni halmashari yeye anataka hivi. Kwa hiyo, huu mvutano tuiombe Serikali ikae pamoja ione namna bora ambavyo masuala ya ardhi yatakuwa katika sehemu moja na yataweza kufanyiwa kazi kulingana na ardhi yetu ilivyo.

Mheshimiwa Spika, lingine niombe, migogoro yote inasababishwa na kutopangwa kwa matumizi ya ardhi, ardhi kutokupimwa. Haijulikani maeneo ya mifugo, haijulikani maeneo ya kilimo, haijulikani maeneo ya hifadhi, maana yake hifadhi nazo zimevamiwa, wananchi wanagombea maeneo ya hifadhi, wananchi wanagombea maeneo ya misitu. Yatakapopimwa na hili ndiyo suala ambalo litaleta msukumo mkubwa sana wa kutatua matatizo hayo. Kwa hiyo, haya yatakapopimwa yote na matumizi yakapangiwa na hali halisi ikaenda kama ilivyopangwa, basi haya yatatatuka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuiombe Serikali, namshukuru Mheshimiwa Rais ameunda Kamati ile ya Wizara nane; Mawaziri nane, wamepita wamekwenda kuangalia hizo changamoto zilizopo huko, sasa waje hapa na hiyo taarifa baada ya kuipeleka kwa Mheshimiwa Rais ili na sisi kama kuna mvutano wa sheria na upo, kwa sababu tunaona sheria zinavyovutana. Sheria ya ardhi haioani na Sheria ya wanyamapori, kwa hiyo migongano ya sheria hizi ili tuzifanyie marekebisho kwa haraka ziweze kuendana na wakati na tuone sasa ardhi hii badala ya kuwa neema kwetu inakuwa balaa ili tatizo hili liondoke. Leo watu wanauana, watu wanapigana kwa sababu ya ardhi. Haiwezekani katika nchi ambayo watu tuko na amani na tunaweza tukakaa, tukazungumza na tukarekebisha sheria zetu kulingana na mahitaji na matumizi ya ardhi tuliyonayo.

Mheshimiwa Spika, kingine ambacho nataka nikizungumze ambacho binafsi hakinipi raha ni kuona kwamba kuna baadhi ya watu wanamiliki ardhi kubwa sana na hawaitumii. Kuna baadhi ya watu wanamiliki viwanja kumi na tano, ishirini, thelathini, wakati watu wengine hawana. Sasa haya maadam yanajulikana, ni miongoni mwa haya matatizo ambayo yanababisha watu kwa watu kupigana. Kwa hiyo, tuiombe Serikali sasa kupitia Wizara yako Mheshimiwa Waziri ili kila mtu aliyepewa ardhi aweze kuitumia, na kama haitumii basi tutumie taratibu za kisheria kuona kwamba kama ardhi huitumii basi wapewe wanaoweza kutumia ili kuondoa hii migogoro ambayo inasababisha siku hadi siku kuleta hatari katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumzie kidogo kuhusu *National Housing*. *National Housing* ilikuwa inakwenda vizuri sana na mpaka sasa Shirika hili lilikuwa linatoa picha kwamba ni shirika moja zuri ambalo linatuletea tija lakini katika kipindi cha mwaka mmoja takriban sasa au zaidi kidoho shirika hili linasua sua. Tunaomba kabisa...

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Spika, dakika moja tu nimalizie sentensi yangu. Tunaomba kabisa Serikali iruhusu ile mikopo waliyokuwa wanachukua shirika hili ili wawefe kuchukua mkopo wamalizie yale majengo waliyonayo lisipate hasara. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana, nakushukuru sana. Mheshimiwa Saed Kubenea, dakika tano atafuatiwa na Mheshimiwa Stanslaus Mabula.

**MHE. SAED A. KUBNEA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, nimshukuru pia Mheshimiwa Waziri, kwa kazi kubwa ambayo imefanyika kwenye Jimbo la Ubungo hasa kwenye eneo la urasimishaji wa maeneo ya watu amba walikuwa wanakaa kwenye maeneo yasiyo rasmi. Mheshimiwa Waziri, hongera sana kwa kazi hiyo na tunaomba ile kazi ikamilike. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia namshukuru kwa *master plan* ya Dar es Salaam ambayo sisi kama wadau tumeshirikishwa kwa sehemu kubwa. Tunaomba ile *master plan* ikamilishwe ili Dar es Salaam mpya iweze kupatikana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, suala la migogoro katika ardhi mingi inachangiwa na wafanyakazi wa Wizara ya Ardhi ambaao sio waaminifu na sio waadilifu. Hapa naomba *declare interest* kwa sababu jambo hili na mimi linanigusa kidogo kwamba kuna kiwanja katika maeneo ya viwanja 20,000 vilivypimwa Dar es Salaam kuna mmoja wa wafanyakazi wa Wizara ya Ardhi alienda kumega lile eneo na akajimilikisha na Mheshimiwa Waziri, taarifa hizi zimefika Wizarani kwake lakini kwa mshangao mkubwa ameshindwa na kigugumizi kushindwa kuchukua hatua.

Mheshimiwa Spika, nashangaa kwa sababu Mheshimiwa Waziri amekuwa jasiri kwelikweli wa kutatta migogoro ya ardhi katika maeneo mengi lakini migogoro kama hii inayomgusa kwenye Wizara yake yeye mwenyewe anashindwa kuchukua hatua. Kwa hiyo, nimkumbushe Mheshimiwa Waziri kaka yangu Mheshimiwa Lukuvu ufanye hii kazi ambayo tumekuletea na kama unataka ukumbushwe zaidi umesahau tukuletee hizo nyaraka ili uweze kuzifanya kazi haraka iwezekanavyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kuhusu *National Housing* ambalo limezungumzwa kidog na mzungumzaji aliyeppita. *National Housing* imefanya miradi mikubwa Dar es Salaam na miradi mikubwa mitatu imesimama. Mradi wa Kawe na ule mradi wa Victoria. Mradi wa Kawe ulikadiriwa kutumia shilingi bilioni 114 wakati unaanza, karibu dola za Marekani milioni 63.9. Lakini sasa hivi baada ya kusimama unakadiriwa kutumia shilingi bilioni 142. Mradi haujaenda mbele, *National Housing* imekopa kwenye taasisi za fedha. Mkopo ule unalipwa kutokana na mradi wenyewe, mradi umesimama. Matokeo yake *National Housing* wanalipa kutokana na mapato ya ndani ya kila siku ya kodi ambazo tunalipa sisi wengine. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ni muhimu sana Serikali ikachukua hatua za dharura kuruhusu *National Housing* waendelee kukopa ili kukamilisha miradi walioanzisha. Miradi kama ule wa Victoria, umekamilika kwa karibu asilimia 95 lakini *National Housing* wamezuiwa kuendelea kujenga kwa sababu wamezuiwa kukopa na baadhi ya benki zilishahamisha matawi yao kwa mfano Benki ya *NBC* ilikuwa na tawi Kinondoni pale eneo la Manyanya, wamefunga lile tawi wakitegemea watahamishia huduma zao kwenye tawi la Victoria na walishamaliza mkataba na yule mwenye jengo. Leo wamezuiwa kuendelea na Victoria *NBC* wamehamishia tawi lao pale Victoria. Kwa hiyo, wanapaswa kuhamishia hapo kwenye hilo jengo jipya, hawawezi kuhamishia kwa sababu jengo limesimama, jengo haliwezi kuendelea kwa sababu *National Housing* wamezuiwa kukopa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa jambo hili litaifanya *National Housing* isambaratike kabisa. Kwa hiyo, mikopo hii ni mikubwa kweli kweli sio mkopo wa bilioni moja au mbili, tunazungumzia mkopo wa bilioni 244, sio fedha ndogo kwa shirika kama hili! Na shirika limefika kikomo cha kukopa, limeomba ruhusa ya Serikali liruhusiwe kukopa kwa dharura. Serikali haitaki kutoa kibali. Mheshimiwa Waziri, jitahidi sana shirika hili lisije kufa mikononi mwako, utapata aibu. Limetoka mbali *National Housing* ilikuwa haijulikani kabisa, limejengwa vizuri, leo ina miradi mikubwa, ina miradi mpaka hapa Dodoma, isije ikafa mikononi mwako. Jitahidi sana.

Mheshimiwa Spika, nadhani kuna matatizo makubwa sana kwenye Bodi zetu za Wakurugenzi wa Mashirika ya Umma. Ni vizuri tunapoteua Bodi kwa sababu haiwezekani mkopo huu wote ukapita tu hivi hivi bila bodi kuangalia na kama Serikali inakuja kuona leo maana yake Bodi ilishindwa kuwajibika na ndiyo maana Serikali ilivunja Bodi ya *National Housing*. Kwa hiyo, nafikiri tunapounda Bodi zetu tuache kuingiza ushabiki wa urafiki, tuache kuingiza ushabiki wa siasa...

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. SAED A. KUBNEA:** ...tujenge Bodi imara. Nakushukuru sana. (*Makof*)

**SPIKA:** Nashukuru sana. Mheshimiwa Stanslaus S. Mabula.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi walau ya kuchangia mchana huu ili niweze kusema maneno machache ambayo nadhani yatakuwa na faraja sana kwangu na kwa wananchi wa Jimbo la Nyamagana na Taifa zima kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwa haraka naomba nianze kwanza kwa kumpongeza Waziri pamoja na Naibu Waziri na Wizara nzima kwa ujumla kwa namna ya kipekee ambavyo wamekuwa wakifanya kazi kwa ushirikiano na ushirikiano huu ndiyo ambao umetuletea ahueni ya kutatua migogoro mingi sana kwenye nchi hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nakumbuka kwenye bajeti ya mwaka jana tulilalamika sana juu ya vifa avya utendaji kazi kwenye halmashauri nyingi. Waziri aliahidi na ametekeleza hili kwa vitendo na tumeona vifaa na kwenye halmashauri zingine zimefika.

Mheshimiwa Spika, tulisema; mimi ni Mjumbe wa Kamati ya *PAC*, tulilalamika sana juu ya uwepo wa kukosekana kwa Bodi ya *NHC*, nimshukuru sana Waziri kwa kulifanya kazi na kuhakikisha Bodi inapatikana na sasa kazi inaweza kufanya vizuri na hata malalamiko mengine yale yaliyokuwa pemberi yanaweza yakaanza kufutika haraka.

Mheshimiwa Spika, nijikite kwenye suala la urasimishaji makazi. Suala hili ni ukweli kwamba ziko changamoto nyingi sana na wananchi wengi sana kwenye Taifa hili waliokuwa wamepoteza amani leo naamini wanayo amani kubwa. Waliokuwa wamepoteza matumaini leo naamini wamerejesha matumaini na wale waliokuwa wanaenda kuwa maskini wa kutupwa, leo wamerudi kuwa na uhakika wa kuendelea na utajiri wao.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengi nchi hii yalikuwa yameshachukuliwa yamejengwa na wananchi, wananchi wengi wamekaa kwenye maeneo ambayo hayakupaswa tena kuwa ni maeneo ya makazi na hii inatokana na michoro mingi nchini kutokusimamiwa vizuri pale inapokuwa imeshachorwa. Lakini nimshukuru sana Mheshimiwa Rais na Waziri Lukuvi kwa jambo moja kubwa la kuamua kurasisimisha makazi. Leo tunazungumza hapa sisi kama Nyamagana pamoja na jiji la Mwanza kwa ujumla, zaidi ya makazi 12,000 wamepata hati za makazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hili sio jambo dogo. Nitumie nafasi hii kuwashukuru sana watendaji wa mamlaka na hi ardhi kule Mwanza Jiji pamoja na Manispaa ya Illemela, kwakweli wamefanya kazi kubwa sana niendelee kuwatia moyo, hakuna kazi kubwa kama kuwatumikia wananchi wanyonge ambaao wanahitaji kupewa ahueni kila siku ili waweze kuendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala bomoabomoa. Bomoabomoa hii Mheshimiwa Waziri leo tena amesema; mwananchi ambaye yuko kwenye eneo ambalo halihitajiki kuweka barabara, eneo lilotengwa miaka iliyopita kama limetengwa kwa ajili ya ujenzi wa kitu kinachowezekujengwa eneo jingine tumuache mwananchi huyu asivunjiwe nyumba ili aendelee kuishi na tumrasimishie makazi yake.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya yote suala la mpango kabambe. Naenda haraka kwa sababu ya muda. Mheshimiwa Waziri huu mpango kabambe Mwanza umefanya vizuri sana na sisi mwanzo kama ulivyo sema nahii ni kazi kubwa inayofanywa na watendaji wa ardhi wa Jiji pamoja na Manispaa ya Illemela na kile kikosi kazi kilichotengenezwa kwa ajili ya kusimamia mpango kabambe. Yako maeneo Mheshimiwa Waziri, hayana sifa ya kupimwa kwa maana kwamba yanayo sifa lakini yako kwenye maeneo ya vilima. Mheshimiwa Waziri unajua, sisi Mwanza tuna milima mingi na wakazi wengi sana wamejenga kwenye vilima hasa vilima vya kule Isamilo, Mabatini, Igogo lakini hata maeneo ya mbugani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa jambo pekee Mheshimiwa Waziri, maeneo haya hayawezi kupewa hati za miaka 90 kama wengine lakini umezungumza suala la leseni za makazi. Nikuombe, hii 5,000 5,000 kule Mwanza ni nyingi sana. Wakazi kule milimani wanaweza kutoa fedha hii wakati wowote. Nikuombe uje Mwanza, uzungumze na wananchi wanaoishi kwenye maeneo ya milima uwapatie leseni za makazi ili na wao waweze na uhakika na maeneo yale ili mpango kabambe utakapokuja Mheshimiwa Waziri kusiwe na tatizo tena, mtu awe na uhakika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, anayekuja kwa ajili ya kutwaa lile eneo ajue anazungumza na nani ambaye atakuwa tayari kumuachia lile eneo kwa ajili ya kuendeleza mpango na wananchi hawana tatizo, wako tayari na wamekuelewa sana. Zaidi ya yote Mheshimiwa Waziri, niseme tena, umeondoa umaskini kwa Watanzania wengi, umeondoa unyonge kwa Watanzania wengi na zaidi ya yote endelea kusaidia maeneo mengi bado yanaweza kutaka kubomolewa kwa namna ambavyo unatuongoza maelekezo haya yaende mpaka kule kwenye Kata, mpaka kule kwenye halmashauri ili tuweze kuwasaidia wananchi hawa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, kujenga nyumba ni miaka 10 na mimi nawashangaa ndugu zangu wanaolalamika. Nilikuwa naona hotuba hii lakini kwa sababu Mheshimiwa Spika alishatos mwongozo mzuri na mimi nisirudie kule lakini niseme maeneo yote ambayo kwakweli yanastahili kuacha njia kwa ajili ya kuwasaidia Watanzania, leo ukienda pale kwa Mheshimiwa Kubenea pamoja na kwamba kulikuwa na majonzi lakini leo ni faraja na hata eneo linaongezeka thamani Mheshimiwa Waziri. Kwa hiyo, ni lazima tuwe tunafika sehemu nyingine wakati fulani tunaona hili ni sawa lakini tunafahamu maumivu yanaingia kwa kasi na yanatoka polepole sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, nikushukuru sana kwa kazi nzuri mnayoifanya, tunaomba muendelee kutusaidia na kulisaidia Taifa hili ili tuweze kusonga mbele. Ubarikiwe sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na Mungu akubariki na jana nimeona umefanya kazi nzuri sana ya kutoa tunzo za *Mo Awards* kwa wachezaji wa Simba. Ubarikiwe sana, hii ni kazi nzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia 100. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Stanslaus Mabula. Nadhani Mheshimiwa Hawa Ghasia unaweza ukatumia dakika zilizobaki. Karibu Mheshimiwa kwa mchango wako.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nikushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kazi kubwa sana wanayoifanya. Wote ni mashahidi, tunafahamu tulikotoka kwa kiasi gani Wizara hii ilikuwa na changamoto nyingi sana na kwa kiasi gani wameweza kuzifanyia kazi changamoto nyingi ambazo zilikuwa zinaikabili Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, kuna mageuzi makubwa sana ambayo Wizara imeyafanya. Sasa hivi karibu maeneo mengi *master plan* au mipango kabambe ya ardhi inaandaliwa mpaka katika ngazi za halmashauri kwa hiyo, napenda sana. Wamekuwa wakiandaa mipango ya makazi na vijiji, wamekuwa wakisimamia udhibiti na uendelezaji wa miji. Pia niwapongeze kwa kutwaa baadhi ya maeneo ambayo kwa kiasi kikubwa yalikuwa ni mashamba pori.

Mheshimiwa Spika, nishukuru sana kwa sababu haiwezekani mtu anachukua eneo anasema anataka kuwekeza, kufanya shamba, anachukua zaidi ya miaka 17 hajaotesha mti hata mmoja, hajaendeleza, hajafanya hilo shamba na bado tuendelee kumuangalia. Kwa kweli ninaipongeza sana hii Wizara.

Mheshimiwa Spika, pia, ninapongeza hasa ukizingatia taarifa ya Kamati, kamati wameipongeza sana Wizara yao na wamesema katika mapendekezo yale mengi ambayo waliipa Wizara yamefanyiwa kazi. Sioni kwanini Wizara hii ijadiliwe siku mbili, haki yake ilikuwa tujadili leo, ifike jioni tumalize tuangalie yajayo ambayo ni kukaribisha *Eid* na wale wanaoenda mbali waweze kwenda lakini vinginevyo kazi kubwa sana Wizara imefanya kikubwa ni kuishauri Serikali iendelee kuipatia fedha Wizara iweze kufanya kazi ambazo zinatakiwa.

Mheshimiwa Spika, jingine ambalo nilitaka kushauri. Wizara inajenga nyumba nyngi sana kupitia *National Housing* na mfuko wa watumishi wa umma lakini zile nyumba zenyewe pia waziweke kwa makundi, tusiweke tu za gharama nafuu. Kuna nyumba zingine zinajengwa karibu karibu hata ukikohoa jirani yako anakusikia. Watakapojenga nyagine basi waziweke kwa tabaka, waweke zile za bei nafuu lakini pia waweke na daraja la kati na wale wa juu pia wawafikirie kwa sababu unaweza hizi za gharama nafuu ukajenga asilimia 60, zile nyagine asilimia 20.

Mheshimiwa Spika, mwisho nirudie tena kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu ikiwezekana hii bajeti leo basi tuibariki kwa sababu kazi kubwa wameifanya na wanaendelea kuifanya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja kwamba bajeti hii tuimalize leo. (*Makofii*)

**SPIKA:** Hapana. Hoja haijaungwa mkono. Waheshimiwa wabunge, mkiamua kweli tunamaliza leo kwa sababu kwa idadi ya wachangiaji niliyonayo tunaweza kabisa kuimaliza leo, kabisa na hasa kama Mheshimiwa Waziri atanikubalia ile saa yake moja ya kujibu akatumia nusu saa, nikaiba ile nusu saa yake tukaitumia Waheshimiwa Wabunge, tunaweza kabisa kumaliza leo. (*Makofii*)

Ili ratiba yetu wiki ijayo basi iweze kukaa vizuri kama Wizara ya Fedha wanaweza wakaja Jumatatu kama

inawezekana. Kama Wizara ya Fedha inaweza ikawa Jumatatu ina maana Jumanne inaweza ikawa ni ratiba ya kamati ya bajeti n.k yaani maana yake ni kwamba Jumanne Waheshimiwa wabunge mnaweza mkaondoka, Jumatano Alhamisi, *Eid* mko kule, Ijumaa mko kule Jumamosi mko kule, Jumapili mnarudi yaani kitu cha namna hiyo lakini itategemeana na majibu kutoka kwa Mheshimiwa *Chief Whip* kama Wizara ya fedha watakuwa tayari Jumatatu. Mheshimiwa *Chief whip*.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, naomba utupe muda tufanye *consultation* ndani ya Serikali na tutakaporudi kwenye Bunge la saa 10 Jioni tunaweza tukawa tumetoa mwelekezo wa utayari wetu kwa Wizara ya Fedha kuwasilisha bajeti yao Jumatatu.

Mheshimiwa Spika, naomba utupe muda kidogo.  
(*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana, ni ushauri mzuri. Tukipata hilo jibu, mambo mengine yote yatakaa sawa, wala hakuna tatizo kabisa. Tutapata muda wa kutosha hata anayeenda Rombo atafika, anayeenda Kyerwa atafika, anayeenda Tandahimba vile vile, Pemba, kwa hiyo, tusikurupuke kurupuke kukimbia kukimbia n.k tutahakikisha ratiba zinakaa vizuri na watu wanakuwa huko na wapiga kura wao katika shughuli za Eid. (*Makofii*)

Ila Waheshimiwa Wabunge, inabidi kwenda vizuri. Inabidi ujiandae, kwenda kwenye *Eid* sio masihara. Wapiga kura wakijua Mbunge yupo basi *Eid* inakuwa nzuri kweli kweli kila mtu anapitia hapo. Kwa hiyo, tuijandae tusiende mikono mitupu tutarudi na lawama hapa.

Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyoona muda wetu ulivyo sasa basi naomba tutaendelea jioni. Mheshimiwa Dkt. Kiruswa utatuanzia na wengine wote mliopo mtapata

nafasi. Tutahitimisha leo jioni bajeti hii. Kwa hiyo, tuwahi ili tufanye kila jambo liende kwa wakati, inawezekana kabisa. (*Makof*)

Baada ya kusema hayo, basi nasitisha shughuli za Bunge hadi leo saa kumi kamili jioni.

(*Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 10.00 Jioni*)

(*Saa 10.00 Jioni Bunge lilitrudia*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae.

Katibu!

**NDG. BAKARI A. KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

### **HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama tulivyokuwa tukijadiliana asubuhi, tumeona ili ratiba yetu ya wiki ijayo iende vizuri, basi kesho kutwa siku ya jumatatu, iwe ni siku ambayo tutashughulika na Wizara ya Fedha na Mipango. (*Makof*)

Ili sasa tukishamaliza ile jumatatu, kuanzia jumanne basi tunawahiwahi saiti, na kwa maana hiyo sasa namuomba nimuite Waziri wa Fedha na Mipango ili aweze kuwasilisha hati mezani. (*Makof*)

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

### **NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:-**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Fedha na Mipango, Dkt. Ashatu Kijaji, kwa hiyo natoa nafasi sasa

kwa Kambi Rasmi ya Upinzania kuandaa hotuba yao, Kamati ya Bajeti pia nao kuandaa hotuba yao na Wizara nao kuweka mambo yao vizuri kwa ajili ya Jumatatu, tunawashukuruni sana. Katibu!

**SPIKA:** Katibu!

**NDG. BAKARI A. KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

### **HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha wa 2019/2020 – Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Majajdiliano yanaendelea, Dkt. Lemomo Kiruswa, nilishakukutaja kwamba utakuwa mchangiaji wetu wa kwanza na Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer atafuatia.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa niwezeuwa wa kwanza kuchangia alasiri hii kwenye hoja hii yetu muhimu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Spika, mimi ni mjumbe wa kamati ya Wizara hii, ninakiri na kuungana na wezangu wote wanaowapongeza watendaji wakuu wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya. Mheshimiwa William Lukuvi, Mheshimiwa Angelina Mabula, Waheshimiwa Katibu Mkuu, Doroth Mwanyika na Naibu Mathias Kagundugulu, kazi mnayoifanya pamoja na watendaji wengine wote wa idara mbalimbali, tukiwa nyuma yenu ni kazi iliyotukuka, nawapongeza sana. *(Makofii)*

Pamoja na hayo kazi yenu ni kubwa, haijafika hata nusu, bado mna kazi kubwa sana mbele yetu na nifananishe kazi mnayoifanya na uhalisia kwamba ninyi ni Wizara ya Ardhi au sisi ni Wizara ya Ardhi; na ardhi ni kitu cha kipekee sana

katika masha ya mwanadamu na uumbaji. Kwa wale wanaosoma Biblia, mnaweza mkarejea katika kitabu cha Mwanzo kwanza Mungu alioumba hii dunia, akaweka vitu vyote na mwishoni akamweka mwanadamu alimpa wajibu wa kuitunza, akamweka katika Bustani ya Edeni aitunze.

Mheshimiwa Spika, na baada ya watu kuongezeka, tukatawanyika duniani kote; na sasa nasema mwenyewe siyo kwenye Msahafu tena; tulijikuta kwamba kila sehemu ya dunia ni sehemu ya hiyo bustani na sisi Watanzania tukajikuta tuko Tanzania ndiyo bustani yetu ya edeni ambayo tuna wajibu wa kuitunza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika muda mufupi ambao nimetumikia kwenye kamati ya Wizara hii na nikiwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nimeweza kutembea maeneo mbalimbali nikashuhudia jinsi ambavyo watanzania tumejisahau katika suala zima la kutunza hii bustani yetu ya edeni, nchi yetu ya Tanzania. Mipaka yake imeingilia kuanzia mpaka wa Uganda, Rwanda, Burundi, Kenya, kila moja ina mgogoro kwa sababu imeingiliwa, na ni kwa sababu watanzania sijui tulifikiri kwamba ardhi haina ukomo, tukaachia mpaka majirani zetu wakaingilia mpaka kwenye mipaka yetu.

Mheshimiwa Spika, mimi naiomba Serikali, kwa sababu sasa tumezinduka na tumeoa Sera nzuri ya Ardhi tuliyonayo, ielekeze nguvu ya kipekee katika kuiwezesha Wizara hii kupanga, kupima na kumilikisha kila kipande cha ardhi ya nchi yetu, ipewe nguvu sana inayopewa sekta ya ukuzaji wa viwanda, uchumi wa kati. Namuomba Mheshimiwa Rais aibebbe Wizara hii, aifanye moja ya Wizara mahsusii ya kushughulikiwa ili tuweze kuipima hii ardhi yetu na tuondokana na hii migogoro ambayo itazidi kuongezeka tusipochukua jukumu. Mipaka inagombaniwa katika ngazi za vijiji, kata, tarafa, wilaya, kati ya mkoa na mkoa na sasa hata katika ngazi ya nchi na nchi.

Mheshimiwa Spika, nafikiri tukiendelea kuiona Tanzania iliyojaa migogoro isiyowahikuisha ya ardhi.

Nashukuru sana kazi nzuri aliyofanya Mheshimiwa Rais ya kuteua Wizara za kushughulika na migogoro ya ardhi. Nimeona umeshika ile *dossier* ya Mheshimiwa Waziri, likitabu ambalo umesema ni mwarobaini wa hizo kero zetu. Ninakwenda kuamini kwamba itakwenda kutumalizia kero ya migogoro tuliyonayo ya muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano sisi Longido kule wasiwasni kuna migogoro ya miaka 20, kijiji na kijiji tu, kata na kata, Matale na Gelai Lumbwa. Mipaka yetu na Mwonduli upande wa Engaruka, mipaka yetu na Arumeru upande wa Oldonyo Sambu na Engikaret, mipaka yetu na *NARCO Ranch* na kila sehemu. Hii basi ifanyike sera; ambayo hata katika bajeti hii mimi ningeomba Wizara na Serikali kwa ujumla tengeni mafungu muwape Halmashauri na ofisi za ma-*DC* ili hii migogoro ya ngazi ya wilaya waimalize wao wenye na muwape *deadline*. Wakati mwiningine wanakwama kwa sababu zinahitaji *resources* kwenda kuhakiki, kupima na kushirikisha pande zote.

Mheshimiwa Spika, naomba hilo lizingatiwe ili tuondokane na hii kero ya migogoro ya ndani, na tukiwa kuendelea kurasimisha makazi yale ambayo yalishavamiwa zamani tulipokuwa hatujui nayo iweze kuendelea. Tumejiachia mpaka mabonde yasiyofaa kuishi watu wakaishi, milima isiyofaa kuishi watu wakaishi na ndiyo maana leo tuna sera ya urasimishaji.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nielekeze kauli mbio yangu katika kuishauri Serikali. Ukienda kule katika mwisho wa Wilaya ya Longido inapopakana na Rombo, kuna kamwanya ka nchi kali mwisho wa mpaka wa Tanzania na Kenya pale na Rombo kuna watu, nina orodha yao hapa, watu 196 bao waliorodhesha mwaka 2016 ambao wameishi hapo miaka nenda miaka rudi, wamezaliana, hawana pa kwenda. Zoezi la kuhakiki mipaka lilipopita wakaonekana hawastahili kuwa pale, wameiandikia Serikali barua kuomba watafutiwe mahali pa kwenda kuishi. Walikuwa 196 mwaka 2016, sasa hivi wameendelea kuongezeka na ninaamini

watakuwa zaidi ya 200. Wengine wamezaliwa palepale, hawajuwi pa kwenda, hawana ardhi, wanaishi kwenye *strip ya no man's land*. Wanakodisha mashamba ya kulima Kenya na wakati mwингine idara ya misitu upande wa Mlima Kilimanjaro wanapovuna misitu, ndio wanakwenda kulima pale. Wananchi wale hawana ardhi na hivyo wanaililia Serikali kwamba watafutiwe mahali pa kwenda kuishi.

Mheshimiwa Spika, vilevile nipende tu kuiasa Serikali, kwamba tunapokwenda kupanga, kupima na kumilikisha kila kipande cha ardhi ya nchi yetu tuzingatia suala la kuweka benki ya ardhi; kila kijiji iwekwe benki ya ardhi kwa ajili ya matumizi ya baadaye ya vizazi vijavyo na maendeleo yatakayozidi kujitokeza. Sambamba na hilo, kwa sababu naona kama tunasubiri mpaka mazingira ya mahali paive, sijui idadi ya watu ifikie watu wangapi, ndipo tunapoingia kufanya mipango mijii; tuanze kupanga mijii yetu mpaka ile inayotarajiwa baadaye, maeneo ya wazi yasiyo na migogoro yapimwe, Serikali iwe na kazi moja tu ya kumuonyesha kila mtu sehemu iliyopimwa anapokuwa tayari kuhitaji eneo la kujidendeza na kujenga makazi yake.

Mheshimiwa Spika, kwa ajili hiyo basi niangalize kwamba sisi wafugaji wa Wilaya ya Longido, tulishabainisha mpaka nyanda zetu za malisho, zinafika 27 kwa sasa hivi. Tunaomba mkono wa Serikali katika kutusaidia kupima, kurasimisha, tuweze kusimamia kama maeneo ya malisho na benki yetu ya ardhi ya vizazi vijavyo; na kwa ajili hiyo wakati huo tutakuwa tunaingezea Serikali mapato maana najua kila ardhi iliyopimwa, tunalipia kodi. Tuko tayari, tunakata *ku-secure* ardhi yetu na Watanzania wote wanahimiza waweke benki ya ardhi, maeneo ya malisho na kilimo na makazi ya watu na tufuate sera hiyo hiyo.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa muda huu mfupi ulionipa, mawazo yangu ni hayo pamoja na kuungana na maoni yetu ya Kamati ambayo tumeyaandika na kubainisha na yamewasilishwa leo asubuhi. Naunga mkono hoja asilimia 100. (*Makof!*)

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Dkt. Lemomo Kiruswa, haya aliyokuwa anasemwa kupima ardhi na kulipia ni mabadiliko makubwa sana upande wa wananchi, hivi sasa wafugaji ikifika mahali ambapo wanawenza ku-secure ardhi, wakapimiwa, wakapata hati zao na wakalipia kodi ya Serikali; na namjua alikuwa *African Wide Life Foundation*, anachokisema anakimanisha kabisa. Ni hatua kubwa sana mbele kwa watanzania. (*Makofi*)

Niliwishamtaja Julius Kalanga Laizer, atafuatiwa na Devotha Minja.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi...

**SPIKA:** Dakika 10!

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia jioni hii, nitumie pia nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rasi wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa nia yake ya dhati ya kujaribu kusimamia rasilimali za taifa hili kwa ajili ya vizazi vya sasa na vijavyo kwa ajili ya maslahi ya taifa letu.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa dhati ya moyo wangu kabisa, nimpongeze sana Waziri pamoja na Naibu wake na watumishi wote wa Wizara ya Ardhi kwa kazi kubwa ambazo wanafanya, ndiyo maana leo ukitesha tumalize sa hivi, kila mtu anasema tumalize. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii ni historia, sisi tulikuwa tunafuutilia Bunge nje, wewe ni mzoefu katika Bunge hili, ni kwa mara ya kwanza Wizara hii inapata kupita kwa Wabunge kuchangia kwa nia njema ya kujenga na kuishauri Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na migogoro hii mingi na katika muda mfupi ambao Serikali hii imeingia madarakani, hata mauaji yale ya Kilosa na maeneo mengine ya wafugaji, si kwa kiwango hicho; kwa nini tusipongeze?

na kumpongeza mtu anapofanya vizuri ni kumtia moyo afanya vizuri zaidi; tusiwe na huruka ya kukosoa tu kila siku na kulalamika kila siku. Katika Wizara hii pamoja kwamba sisi ni wadau wazuri wa ardhi, ukianzia Kongwa, Kondoa yote mpaka Arusha na kule Kaskazini, lakini kwenye hili kwa leo sina malalamiko yoyote, naipongeza Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya na kwa kuanzia Monduli wamefanya kazi kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sisi miaka hiyo ya 1988 ardhi yote ya Monduli ilchukuliwa, wakapewa wawekezaji wakubwa, kwa hiyo hatukuwa na ardhi. Leo nikisoma hatua ya kambi ya upinzani wanalamika Rais kurejesha ardhi, mashamba makubwa ya pori, kuwarudishia Watanzani; najiliza, hawa wanawatetea watanzania wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wamefika mahali katika kurasa zao wanaeleza mpaka kuhoji mamlaka ya Rais aliopewa kwa mujibu wa Katiba, kusimamia ardhi yetu kwa niaba ya Watanzania; wanataka Bunge hili liunde kamati ikafanye nini? Na ninashangaa kama wenzetu hata utaratibu wa kufuta mashamba makubwa hawajui; wanauliza hapa, wanasema tuambwiwe ni utaratibnu gani unatumika? si inaanza kwenye halmashauri?

Mheshimiwa Spika, lakini bahati nzuri aliyesoma hotuba hii anatoka mjini, ambao wao kazi yao wakishaona ghorofa wamemaliza. Sisi ardhi ni muhimu sana kuliko vitu vyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tumtie Rais moyo kwa kuthubutu kurejesha mashamba ya watu waliyomiliki. Ukisoma Sera ya Ardhi ya Nchi yetu, inasema kugawa ardhi kwa haki na kwa usawa kwa raia wote. Ninyi wengi mnafahamu...

## **TAARIFA**

**SPIKA:** Mheshimiwa Laizer kuna taarifa, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare nimekuona.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, ningependa kumpa taarifa mzungumzaji anayezungumza hivi sasa, naomba arejee vizuri kwenye hotuba ambayo tumewasilisha hapa. Suala ambalo limezungumziwa ni kwamba ni kutaka kujua *transparence*, utaratibu unaofuata kwa sababu kuna malalamiko kwamba zoezi hili halina *transparence* lakini tumeunga mkono sheria yenyewe jinsi ilivyo tumeiunga mkono. (*Makofi*)

**SPIKA:** Taarifa hiyo Julius unapewa, unaipokea?

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, malalamiko kutoka wapi, aliyefuta mashamba ni Rais, wao wanapeleka malalamiko kwa Lwakatare, basi akawaundie tume. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sisi tunachosema, kwa mtu ambaye haridhika na uamuzi wa Serikali afuate utaratibu wa sheria uliopo kudai haki yake. Kulalamika uvunguni maana yake kitu unacholalamikia hakina haki wala hakina usawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, haya malalamiko yanayokuja kwenu tu lakini sisi hatuyaoni, tusipoteze muda, tuendelee kurejesha mashamba yale ambayo ni mapori, watanzania watumie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hatuna mashaka na uadilifu wa Mheshimiwa Rais wetu wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni Rais wa wanyonge, hawezি kuwa sehemu ya kumuonea mtu yejote, lakini na wengine wasiwaonee wengine, hili ni genge tu walianza mwaka jana, kutaka kushawishi kwamba, kwa nini watu wanyang'anya mashamba, tutaendelea kunyang'anya kwa mujibu wa utaratibu ili wote tuwe na haki ya kutumia ardhi hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunasema tunaungana na Serikali, kwamba mashamba mengi ambayo hayajaendelezwa warudishiwe watanzania wanyonge waweze kulima,

wawewe kufuga na sisi tujione hata tusio na fedha ya kumiliki makubwa Serikali inaweza ikatutetea tukapata madogo, tukaweza kutumia kwa maslahi mapana na nchi yetu. Songeni mbele, tumpongeze Rais, tunaungana Bunge hili kwa ajili ya kazi anayofanya. Amethubutu kupunguza mashamba ya wakubwa ili wanyonge tufaidi ardhi yetu ya nchi hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, labda niseme moja na ninaomba Serikali ilichukue. Mwaka 1974 aiyekuwa Mbunge wa Monduli wakati huo, Hayati Edward Molinge Sokoine, akishirikiana na Rais wa wakati huo, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere walitoa ardhi kubwa ya watu wa Monduli ili iwe chini ya jeshi iweze kutumika kwa mafunzo ya kijeshi na malisho ya mifugo ya wananchi wa Monduli, na tukaridhia jambo hilo!

Mheshimiwa Spika, mwaka 1988 baada ya kurudishwa tawala za mikoa na kuwepo Wakuu wa Mikoa, baadhi ya watu waliingilia kwenye ardhi ile na kujimilikisha kinyume na utaratibu. Mwaka 2014 wakati Mheshimiwa Jenista na Kamati yake ile mliyounda wakati ule na akina Sendeka wakaja Monduli, tukaita Mkutano Mkuu wa wananchi wa Monduli, tukasema ardhi yetu ile ni salama ikiwa chini ya jeshi kuliko kuacha ikiwa wazi. Wale watu wameendelea kuzunguka katika Wizara mbalimbali wakitafuta kulipwa fidia; na baadhi ya watumishi wasio waaminifu, wanashirikiana nao. Mheshimiwa Waziri wa Ardhi usikubali, ardhi hiyo tulitoa kwa jeshi mwaka 1974, walioingia mwaka 1988 walivamia. Sisi tunafikiri tuko salama tukiwa kwenye mikono ya jeshi letu la ulizni na usalama. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, na Monduli ni sehemu ya majimbo machache ambao sisi tunaheshimiana sana na jeshi, msitulee manyang'au na wezi wa ardhi yetu, ardhi ibaki chini ya jeshi. Leo tusingekuwa na mahali pa kulisha.

Mheshimiwa Spika, ukienda Monduli, kutoka Makuyuni, mpaka Dukabovu, upande wote wa chini, mpaka Rockdale kwenda Tarangile, ni eneo ambalo wanajeshi

wanafanya mazoezi na sisi mifugo yetu imeponea maeneo hayo wakati wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hao wanaotafuta fidia wako 42, hawawezi kuhatarisha uhai wa wananchi wa Monduli wanaozidi laki mbili, haiwezekani. Kwa hiyo, kwa sababu hatukutani nao kwenye hizo *corridor*, si maamuzi ya Monduli wala wananchi wa Monduli. Sisi tunachosema ardhi ibaki kuwa chini ya jeshi...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Julius Karanga, muda wako umeisha.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana tunakushukuru sana. Ahsante sana, kwa kweli mchango wako ni *exemplarily*. Eee, maana watu huwa wanasmama hapa jeshi limevamia, mi kila siku nawaambia jamani jeshi njoni Kongwa. (*Makofi/Kicheko*)

Ee, lakini sasa tumepata Mbunge anasema bwana ardhi ile ni ya jeshi, kabisa kabisa, ndiyo maana nikasema ni *exemplarily*, Devotha nilishakutaja, dakika tano lakini, mlivyopangiana wenyewe, atafuata Rhoda dakika tano pia, Rhoda Kunchela.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Awali ya yote nishukuru Wizara kwa kurudisha Ofisi ya Ardhi Kanda ya Kati ambayo ilikuwa Mkoa wa Morogoro; na ilikuwa haiingii akilini sana watu wanatembea kilomita zaidi ya 700 kutoka Mlimba, Malinyi, Ulanga, kuja Dodoma kufuata huduma za ardhi. Kwa

kweli kwa hilo wana wa Morogoro wameshukuru kwamba sasa tunakwenda kupata zile huduma katika Kanda yetu ya Kati.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikimfuatilia sana Mheshimiwa Waziri kwa jinsi anavyooleza, anajipambanua kwamba masuala ya migogoro ya ardhi o kwenye *fingertips* zake, na hata wakati mwingine Wabunge wanapouliza maswali anadiliki hata kusahihisha.

Mheshimiwa Spika, yako mambo mengi ya kujiuliza, kama kweli Waziri ana *mastermambo* haya ya migogoro ya ardhi, kwa nini migogoro inaendelea? Inashangaza kuona kwamba Waziri anazunguka, kila mahali yupo; na mimi ninavyoolewa, Waziri ni taasisi. Waziri unapobeba mafaili unakwenda kufanya ukaguzi wa kushtukiza katika ofisi za ardhi na *camera pamoja* na mavumbi yote wakati una watu pale ambao wangeweza wakaifanya hiyo kazi tunaona bado kuna shida mahala fulani. Haiwezekani Waziri inabebe hati mfukoni unakwedna kugawa kwa watu sijui mia ngapi ambao hawajapata ardhi kwa zaidi ya miaka 15.

Mheshimiwa Spika, hiyo kazi, ilipaswa, a-delegate kwa watu. Kwa maana kama Waziri unahangaika kufanya haya yote kushughulika na migogoro, lazima watu walioko chini yako wafanye kazi ambayo unaifanya wewe!

Mheshimiwa Spika, lingine, tumemsikia Waziri anasema, ameanzisha mpaka kipindi cha kusema a...

**SPIKA:** Kwa kweli Devotha mnapolalamika Wavunge kwa miaka kadhaa watu wangu hawajapata hati, Waziri anatoka ofisi anakuja kuhakikisha watu wenu wanapata na kuwapa ye ye mwenyewe. Hilo nalo ni kosa pia? Labda utuwekee vizuri (*Makofii*)

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Spika, ninachokizungumza, kama Waziri ameanzisha mpaka kipindi anasema cha kupambanua, watu watoe hoja zao na kero zao. Hivi migogoro ya ardhi ilivyo mingi kwa watu zaidi ya

milioni 50, kila mmoja akiamua kupambanuka kwa Waziri kueleza atatue migogoro yote ya ardhi peke yake atawea? Ninachoklamini Waziri ni taasisi, wasaidizi ni lazima katika Mikoa, kwenye Ofisi za Ardhi wafanye kazi hiyo hiyo, ndiyo ninachokimaanisha, kwamba sasa kama Waziri atakwenda kutoa hati na kuna *DC*, kuna Afisa Ardhi, hizo kazi zingine alipaswa a-delegate watu hawa...

**SPIKA:** Mtoa taarifa tafadhalii nakupa ruhusa, ni Mheshimiwa Getere.

### **TAARIFA**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Devota kwamba amekiri kwamba migogoro ya ardhi ni mingi sana katika nchi hii na Waziri kutokana na migogoro hiyo ndiyo inampa jukumu la kwenda kuangalia nini kifanyike ili migogoro ipungue. Sasa kisa cha kumwambia, kwa hiyo maana yake kwa lugha nyiningine ni kwamba Waziri aendelee kukaa ndani wakati migogoro inaharibu, anatoa maagizo kila mahali na pale inapoona inabidi kwenda, anaenda kuiona ili amalize mgogoro. Ahsante.(*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Devota unapokea taarifa hiyo dakika zako ni chache nazilinda hapa.

**MHE. DEVOTA M. MINJA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kulinda ninachomaanisha mimi kama Waziri ndiye anayefanya kazi basi kazi hiyo ionekane pia kwa wasaidizi wake, wafanye kazi kwa namna hiyo ndiyo ninachomaanisha.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ninalizungumzia ni kuhusu bomoa bomoa. Nilitegemea Waziri angeeleza jambo kuhusu bomoa bomoa ya Dar es Salaam Ubungo, Kibamba, nyumba zaidi ya 1,300. Watu hawa ambao walibomolewa nyumba zao wakiwa na hati mikononi, wengine wakiwa na *title* mikononi, mpaka watu hawa wavunjiwe tulitaka kujua Maafisa hawa waliotoa.

**SPIKA:** Taarifa Mheshimiwa Devota, nalinda muda wako usiwe na wasiwasi, Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara.

## **TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA)** Mheshimiwa Spika, nimpe taarifa Mheshimiwa Devota Minja kwamba suala la bomoa bomoa la Dar es Salam na hasa anayozungumza Kibamba kwenye maeneo ya *road reserve* ya barabara ile. Moja ni kwamba watu walilipwa fedha wengine wakaondoka, wengine hawakuondoka, waliobaki wakawauzia wageni ambaio hawakuwa na taarifa kwamba eneo limelipwa fidia. Walipoambiwa kwamba eneo litabomolewa wakaenda Mahakamani, wakaenda wakashindwa kesi na Serikali ina hukumu hapa. Katika hali ya kawaida Serikali ilitekeleza maamuzi ya Mahakama ya Juu ya Ardhi. Ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Devota, maliza dakika zako, kwa hiyo waliingizwa mkenge.

**MHE. DEVOTA M. MINJA:** Mheshimiwa Spika, ninachokisema hapa ni kwamba, kama watu walilipwa fidia na wakauza na watu wengine wakarasmishwa, lakini watu hawa hawa kuna myumba zingine zimejengwa pale na tunaamini kabisa kuna Ofisi za Mipango Miji wametoa wapi ramani, zimepitishwa na nani na ni kwa nini watu hao hawakuwajibishwa. Kuna watu wamepelekewa umeme, kuna watu wamepelekewa maji, kwa nini watu hawa hawakuwajibishwa? Kujenga nyumba si rahisi watu wanajenga nyumba kwenye ujana wao mpaka wanazeeka hawajamaliza...

**SPIKA:** Mheshimiwa Devota utakuwa unabishana na Mahakama sasa, maana yake tumeambiwa Mahakama ishahukumu hilo, utaanizisha tu kesi ambayo yaani, kwa kuwa Mahakama ilishafanya basi kanuni zetu zinasema sisi hebu hatuwezi ku-*question*, endelea Mheshimiwa Devota.

**MHE. DEVOTA M. MINJA:** Mheshimiwa Spika, hoja yangu ni kwamba suala la ubomoaji linahitaji busara pia, maendeleo yanahitajika, lakini lazima pia tuangalie kama kweli Serikali inajipambanua kwamba ni Serikali ya wanyonge, ilipaswa kuliona hilo na kuwasaidia hawa watu kuliko hasara ambayo watu hawa wameipata.

Mheshimiwa Spika, lingine baya zaidi ni pale kunapokuwa na kauli za kibaguzi kwamba watu ambaao wako Mwanza wamepiga kura kwa CCM, hao hawatabomolewa, lakini walioko maeneo mengine wanabomolewa...

**SPIKA:** Muda umeisha, dakika zako zimeisha, Mheshimiwa Devota. Nilishakutaja Mheshimiwa Rhoda Kunchela, dakika tano Mheshimiwa Devota ungeomba dakika kumi siku nytingine.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa fursa ili niweze kuchangia Wizara hii pia naunga mkono maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, katika Taifa letu asilimia 53 ya ardhi yetu ni misitu, pia asilimia 15.4 ni eneo ambalo linafaa kwa ajili ya kilimo, malisho na maeneo mengine. Sasa inashangaza kama bado tuna eneo kubwa kiasi hiki na Wizara hii ya Makazi inashindwa kutenga maeneo kwa maana ya kutenga maeneo ya makazi kwa wananchi wakapata hati zao na tukaepuka migogoro ambayo inaendelea. Hilo ni jambo la kwanza. Pia Serikali hii ikatenga maeneo kwa ajili ya malisho ili kuepuka migogoro kati ya hifadhi na Serikali.

Mheshimiwa Spika, pia kuna migogoro mingi ambayo inaendelea kwenye nchi hii inasababishwa na Wizara hii kushindwa kutatua migogoro ya ardhi, kuna masuala ya Taasisi za Serikali kukosa Hatimiliki, wananchi wanapewa hati kwa mfano kwenye Manispaa ya Mpanda kwenye Kata ya Misunkumilo, ukija Mpanda Hoteli, Milala na maeneo mengine wananchi wale wamepewa hati na wamepelekewa

huduma za kijamii kwa maana ya masanduku ya kupiga kura, umeme, maji pamoja na barabara .(*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa watu hawa wanakwenda kuwaondoa, ni Serikali hii moja ya Awamu ya Tano, imepeleka huduma hizo, pia Jeshi liko pale pia nao hawana hati. Sasa mazingira haya yanapelekea wananchi wetu kupata shida, wananchi wanajenga nyumba katika mazingira magumu sana na wananchi wetu wengi ni maskini. Kwa hiyo Wizara hii ione namna ya kuharakisha jambo hili la kutoa hati kwa wananchi haraka iwezekanavyo hususani katika maeneo ambayo wananchi wanajenga katika makazi mapya.

Mheshimiwa Spika, vile vile niongele suala la Shirika la Nyumba la Taifa, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya *PAC*, tumeweza kuzungukia maeneo mbalimbali kwa maana ya miradi ambayo iko chini ya shirika hili ikiwepo na mradi wa Dege *Eco* ambao uko Kigamboni, *TBA* na maeneo mengine. Ukiangalia nyumba hizi kuna maeneo mengine kweli shirika wamejitalidi, lakini tunaona namna ambavyo Serikali inatumia għarama kubwa kwa kutumia pesa za Serikali kujenga nyumba hizi na tukiangalia *outcome* yake ni ndogo, *outcome* yake ni ndogo kwa sababu watumishi wengi wanashindwa ku-affordkununua na kupangisha kwa sababu għarama ziko juu. Kwa hiyo kūpitit Wizara hii niombe pia Mheshimiwa Waziri kuona namna ya kuweza kupunguza għarama za upangishaji pia għarama za ununuzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ukija changamoto nyngine ni kwa nini nyumba hizi zinakosa wateja. Unakuta nyumba zimejengwa kwenye maeneo ambayo hata miundombinu hakuna, barabara nyumba inajengwa porini, sasa unategħemha mtumishi għalli anawexha kwenda kupanga au kwenda kununua eneo hilo. Kwa hiyo Serikali ione namna ya kuweza kuboresha miundombinu ya maji, umeme, barabara na huduma za afya na maeneo mengine. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, niongelee jambo la mwisho kuhusiana na suala la mipaka; narudi palepale kwamba

migogoro mingi na Mheshimiwa Waziri amesema Mkoa wetu wa Katavi pia umekuwa wa mwisho kwa kukusanya hayo makusanyo ya mapato kwenye hilo eneo. Ni kweli lazima tushindwe kwa sababu hata ukiangalia hal mashauri yetu bado haina uwezo, leo tutawalazimisha watu wapime na hakuna ushirikishwaji wa moja kwa moja na hizi Taasisi Binafsi bei imekuwa iko juu sana, watu wanashindwa kulipia tozo hizi zimekuwa ziko juu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Serikali ione namna ya moja kwa moja kuweza kushirikisha hizo kampuni binafsi, hal mashauri zetu na Serikali kwa ujumla wake kwa sababu wananchi wanashindwa kupima maeneo kwa sababu gharama ziko juu na leo tutaendelea kuweka uzembe kwenye eneo hili matokeo yake tuje kuwabomolea wananchi na ndiyo masuala ya bomoabomoa Serikali hii inashindwa kulipa pia masuala yao ya fidia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, masuala ya uwekiwa wa hizi *beacon*; kumekuwa na migogoro hii ya muda mrefu ambayo Mheshimiwa Waziri amesema na Mheshimiwa Rais ametamka kwamba kwenye eneo ambalo linahusisha mgogoro kati ya hifadhi na wananchi maana yake wananchi wapewe Kipaumbele. Sasa katika maeneo hayo ninayozungumzia katika Kata ya Sitalike ambayo iko katika Jimbo la Nsimbo Lyamgoloka, Kasekese na maeneo mengine ambayo yana migogoro hii, ni kwamba Serikali hii imeshindwa kuwashirikisha wananchi moja kwa moja kwa maana ya kuonesha hiyo mipaka. Sasa ni lengo la Serikali hii kuhakikisha linatatuwa migogoro hii...

**SPIKA:** Ahsante sana

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuweka mipaka. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rhoda nakushukuru sana. Mheshimiwa Rashid Ajali Akbar, atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Mbarouk.

**MHE. AJALI R. AKBAR:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi ili kutoa mchango wangu katika Wizara hii nyeti, Wizara ambayo kwa kweli ni Wizara mama ambayo sisi binadamu tunaitegemea. Wizara hii inatokana na unyeti wake kwamba bila ardhi maana yake hakuna dunia na bila dunia maana yake hakuna maisha, kwa hiyo Wizara hii lazima iwe makini katika kuhakikisha kwamba wanasi mamia vizuri jinsi ya kupima ardhi na jinsi ya kupanga ardhi hii.

Mheshimiwa Spika, sina shaka na utendaji wa Mheshimiwa Waziri, sina shaka juu ya utendaji wa Mheshimiwa Naibu wake, Katibu Mkuu pamoja Watendaji wote waliopo kule Wizarani. Kwa kweli wanaitendea haki Wizara hii na wanafanya kazi kama ipasavyo; *a Leader is a one who finds the way, is the one who shows the way*, Waziri yeye ni kiongozi ambaye ametafuta njia na ameonesha njia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninachotaka kuzungumza kwamba hao wanaosema kwamba yeye anatembea, nadhani kwamba yeye ndiye kiongozi ambaye anatafuta njia halafu anaonesha wale watu waliopo chini ili wajue nini wanatakiwa kukifanya nampongeza sana Mheshimiwa Waziri katika utendaji huo.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze tena Mheshimiwa Waziri au niipongeze Wizara hii kwa kupunguza viwango hivi vyta kodi ya ardhi kutoka asilimia saba hadi asilimia moja, nyingine asilimia mbili kwa maeneo ambayo yamepangwa na 150,000 kwa ajili ya gharama zile za upangaji. Viwango hivi ni vizuri, lakini sijui kama hizi huduma zote zinawafikia wananchi *properly*, kwa sababu kwa mfano halmshauri ya Wilaya ya Newala ni mji ambao ulikuwa umepangwa siku nyingi sana. Hata hivyo, kwa bahati nzuri wengine wana hati lakini wengine hawana hati. Kwa wale ambao wana hati bahati nzuri ni kwamba vile viwango vyta jinsi ya kulipia kodi ya ardhi vinakuwa vimeoneshwa kwenye hati, lakini wale watu ambao wengine *maybe* hawana hati inakuwa ni tatizo kwamba inakuwa ni majadiliano kati ya Afisa Ardhi pamoja na yule ambaye hana hati.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo watu wengine wanashindwa kwenda kujenga nyumba sababu yale maeneo wanaambiwa mpaka zile kodi ambazo ni za siku nyingi. Kwa hiyo Waziri afanye utaratibu wa kuhakikisha kwamba Wizara inatoa viwango katika Halmashauri za Wilaya zote kutegemeana na wilaya jinsi ilivyo na hivyo viwango vibandikwe sokoni, hospitali na katika majengo ya halmashauri ili kila mmoja hivi viwango avione, badala ya hizi nyaraka ambazo wanakaa nazo wale Maafisa Ardhi badala yake wawe wanakuwa na mjadala wa kujadiliana namna gani. Kwa hiyo mtu anafikia mpaka milioni tatu, aidha mtu anakimbia anashindwa kujenga au baadaye unampa kidogo inapungua mpaka kufikia 200,000 au 300,000. Kwa hiyo ninamwomba Mheshimiwa Waziri aondoe *loopholes* kama hizi, hivyo viwango viwe wazi.

Mheshimiwa Spika, la pilli ni kwamba, kuna maeneo Wizara imekiri kwamba maeneo mengi hayakupimwa. Naona sasa umefikia wakati Mheshimiwa Waziri aangalie hili jambo la kupima au kupanga miji yetu liwe ni jambo la kisheria. Kila halmashauri ihakikishe kwamba inapima hayo maeneo yake ili kupanga hiyo miji ili isiwe ni miji ambayo imekaa hovyohovyo. Katika karne ya leo tunazungumzia mambo ya *squatter*, kwa kweli nashangaa sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe kama inawezekana Mheshimiwa Waziri ahakikishe kwamba yale maeneo ambapo halmashauri wanashindwa kupima, basi wawe na utaribu hawa wapima binafsi waende katika kila halmashauri wafanye makubaliano rasmi ili kuhakikisha yale maeneo wanayapanga na hatimaye kuyapima ili kuepuka hizi *squatters*, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema maeneo mengi hayakupangwa wakati huo.

Mheshimiwa Spika, lingine, kuna huu utaratibu ambao nilikuwa nategema majiji mapya kama kwa mfano yalivyo Dodoma, tulitarajia kwamba katika miaka 30 inayokuja kusiwe tena na *squatter* katika Jijiji la Dodoma. Kwa hiyo niombe sana zile halmashauri ambazo zinazunguka Mji wa Dodoma kwa mfano Chamwino na labda Bahi na

Halmashauri ya Mji zote hizi ziingizwe katika jiji ili kuhakikisha kwamba hayo maeneo hayawi na *squatter* tena. Kama yatakuwa yameingia katika jiji maana yake kwamba kutakuwa na mpango, leo nimepita pale katika ule Mji wa City kilometra moja kuanzia pale Mheshimiwa Waziri watu bado wanaendelea kujenga bila kupanga, ni mambo ya ajabu sana. Kwa hiyo maana yake baada ya miaka 25 pale sasa Serikali itabidi iwalipe fidia wale watu wote halafu tuhakikishe tena tunaanza kupanga tena upya.

Mheshimiwa Spika, naamini kwamba katika karne hii tusirudi tena Serikali ikaingia katika gharama ya kuwalipa fidia ili tuangalie namna gani jinsi ya kupanga. Sasa ni wakati ambapo tuhakikishe kwamba kila jiji na kila mji unakuwa na *Master Plan* ambayo itakuwa ya miaka 30 au miaka 50 au miaka 100 inayokuja ili baadaye labda tupate gharama ya kubadilisha tu jinsi ya matumizi, lakini ikiwa hii miji yetu imepangwa vizuri na inakuwa inaonekana na *movement* zinazoonekana kila sehemu.

Mheshimiwa Spika, si vizuri katika miaka 30 ijayo tuwe na miji ambayo haikupangwa, maana nategemea kwamba baada ya muda fulani hakutakuwa na kila mmoja anaishi kti na nyumba yake ila tutakuwa na majumba makubwa ya Serikali kama wanavyofanya Serikali zingine duniani na kila mmoja hatapewa nyumba ya kuishi kwa wakati huo. Nasema hivyo kwa mfano ambayo kama nimezungumza kwamba hapo Buigiri hapajapima na halmashauri zingine bado wanamiliki, vilevile sisi ni kazi yetu.

Mheshimiwa Spika, lingine, nipongeze kuwa na Ofisi za Kanda, katika Mkoa wa Mtwara hiyo Ofisi ya Kanda kwa ajili ya upimaji wa kwa kweli Mheshimiwa Waziri anaitendea haki, wale wale watu kwa kweli ni watendaji wa kazi vizuri sana. Kama matatizo tunayapata ni baadhi ya halmashauri wao wenyewe wanashindwa kutengeneza zile *documents* lakini siyo Ofisi ya Kanda kwenda kule wewe ukapata hati ukaa miezi sita. Kwa kweli wale watu wanafanya kazi vizuri sana, Mheshimiwa niombe kwamba kwa kweli wale watu wanaitendea haki Wizara, ila halmashauri zingine bado

zinakuwa bado zinavuja, kwa mfano Halmashauri ya Wilaya ya Lindi ukipeleka *document* pale inakaa muda mrefu sana, kuna watendaji ambao bado wana matatizo.

Mheshimiwa Spika, ukienda Newala au Mtwara Mjini penyeewe wakishaandaa zile *documents*, zikifika katika Ofisi ya Serikali, basi inakuwa ni muda mfupi sana unapata hati yako. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri katika hili. Narudia tena *a Leader is a one who finds the way, is the one who shows the way*, Mheshimiwa Waziri anatafuta njia halafu anaonesha. Nimpongeze katika hili, aendelee katika utendaji wake.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, mchango wangu ulikuwa mfupi kiasi hicho. Ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Rashidi Ajali Akbar. Mheshimiwa Mussa Mbarouk nishakutaja, wewe una dakika kumi.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Anafuata na Mheshimiwa Suzan Kiwanga na atafuatiwa na Mheshimiwa Agness Marwa.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Spika, labda kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujalia afya njema, tukaweza kukutana na kuendelea na shughuli za Bunge letu. Pia niungane na wenzangu katika kuipongeza Wizara, pamoja na kwamba upo upungufu mchache, lakini wanapofanya vizuri lazima tuseme wamefanya vizuri, lakini pale kwenye matatizo basi hatuna budi kushauriana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema tu kwamba, ardhi ni mali, lakini kwa bahati mbaya ardhi sasa haiongezeki, lakini sisi binadamu na shughuli zetu tumekuwa tukiongezeki. Sasa tatizo linalokuja ni kwamba kwa kuwa ardhi haiongezeki na kila mmoja sasa hivi amekwishajua kwamba

ardhi ni mali ndiyo pale panapotokea migogoro ya mara kwa mara. Sasa nishauri tu kwamba Mheshimiwa Waziri aendelee kufanya kazi, lakini asiwe anafanya kazi yeye na Naibu Waziri tu, pamoja na watumishi wa Wizarani, lakini hata wale Maafisa Ardhi wa kwenye Halmashauri, Maafisa Mipango Miji na Maafisa wengine nao waige mfano wa Mawaziri wetu hawa wawili. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema hivyo? Kwenye Jimbo letu la Tanga pamekuwa na migogoro ya hapa na pale, kwa mfano ipo migogoro ambayo Mheshimiwa Waziri amekwishajaribu kuishughulikia, lakini bado haijaka vizuri sana. Nitoe mfano, labda kuna mgogoro huu wa JWTZ na maeneo ya Mwahako pamoja na wananchi. JWTZ waliwalipa pale wananchi kumi tu, lakini baada ya kulipa wananchi kumi wanasema eneo lote lililobaki ni eneo la Jeshi.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya sasa, wakati mwingine majeshi nayo yanakuwa na sheria ngumu, baada ya kuchukua umiliki wa lile eneo basi imekuwa hakuna ruhusa hata kupita kwa miguu katika maeneo hayo. Ikumbukwe baadhi ya maeneo hata kama tuna majiji lakini bado kuna vitongoji au kuna maeneo ambayo ni ukiyatazama ni maeneo ya vijiji kwa sababu kuna mashamba, kuna wafugaji na kadhalika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa namwomba kwanza Mheshimiwa Waziri, pale ambapo Jeshi liko karibu na wananchi pawe na mahusiano mazuri. Kwanza, ukilitazama jina lenyewe la Jeshi ni Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Sasa linapokuwa jeshi hapatani na mwananchi, hapo napata tabu kidogo kuelewa. Kwa hiyo naomba awaelekeze washirikiane na wananchi.

**SPIKA:** Haya Taarifa Mheshimiwa Laizer.

## **TAARIFA**

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nataka kumpa taarifa, kwamba ni Jeshi la Wananchi...

**SPIKA:** Ngoja zima kwanza, Mheshimiwa Mbarouk, endelea...

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, taarifa ninayotaka kumpa ni kwamba tulichofanya sisi Monduli, kwa sababu ni Jeshi la Wananchi tuliwapa ardhi bure, tukawa na ujirani mwema; tatizo la wananchi wengi wanataka walipwe fidia, lakini warudi kutumia ardhi hiyo hiyo ambayo alishalipwa fidia. Kwa hiyo tujenge utaratibu wa mashirikiano na jeshi.

**SPIKA:** Anakushaurini tu kwamba, ukilipwa fidia maana yake uondoke jumla.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Spika, sasa baadhi ya watu hawajalipwa, kuna wananchi 112 hawajalipwa na wamekuwa wakifuatilia malipo yao wamekuwa wanahangaishwa na wao kikubwa wanasesma kwa nini wanadai fidia? Ni kwa sababu hata kama eneo hilo limechukuliwa na Jeshi, wanasesma Sheria Na.4 ya mwaka 1999 nafikiri Waziri anajua vizuri ile inayosema: “*whether you have tittle deed or not so long you have been there for a long time, customary law recognize you as the owner of the land.*” Sasa wananchi wanapoitumia sheria hii ndiyo wanapoona kwamba ni haki yao.

**SPIKA:** Nani alikuwa anasema Mussa Mbarouk hajui Kiingereza? Si mnaona ameteremka vizuri kabisa jamani? Endelea Mheshimiwa Bwana. (*Kicheko*)

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** ...inaeleza kwamba hata kama kuna mradi wa maendeleo lakini lazima kwanza akae mwekezaji, ikae Serikali kwa maana ya Wizara ya Ardhi na wananchi; sasa wakati mwingine wananchi wanakuwa wanasumbuliwa kulipa malipo ambayo wanastahili na ni haki yao; na siyo hapo tu; kwa mfano; nashukuru kwamba Serikali Waziri Kamwelwe hapo amesema Uwanja wetu wa Ndege Tanga umepatiwa fedha takribani bilioni 36 ili ufanyiwe upanuzi na uwe wa kisasa zaidi; hususani kutookana na uwekezaji mkubwa unaokuja. Hata hivyo kuna nyumba

zimefanyiwa *evaluation* tangu mwaka 2008, wananchi wale hawajalipwa, nyumba 38. Sasa hivi ili uwanja uwe mkubwa zaidi pana nyumba 802 maeneo ya Masiwani Shamba ambayo ni kata mpya zinahitajika kuondoka. Sasa wananchi wanasema hatukatai kuondoka lakini kwa Sheria ile Namba Nne tulipwe kwanza fidia hatukatai maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mimi naishauri, Mheshimiwa Waziri, wananchi wale wa mwaka 2008 wa maeneo ya Masiwani Shamba walipwe fidia zao, lakini hata hizi nyumba 802 ambazo ni za kisasa ziondoke lakini wananchi wakabidhiwe fidia zao. Kwa sababu, mtu wa kawaida anaweza akajenga nyumba labda miaka mitatu mpaka miaka 10 lakini inapokuja shughuli za maendeleo likitolewa tu tamko ujue utaondoka; sasa hawa nao ni Watanzania wakimbilie wapi? Kwahiyo mimi naishauri, Serikali pamoja na maendeleo, maendeleo nayo yana gharama zake Wananchi wetu lazima wafidiwe.

Mheshimiwa Spika, kama hilo halitoshgi, kuna mgogoro wa eneo pia la kwa Ramsing, nafikiri Mheshimiwa Waziri hili ulilisikia. Wapo wazee amba ni wenyeji wa maeneo hayo, lakini kuna huyo Ramsing ambaye alikuwa ni Singasinga alikuwa analima miwa na kutengeneza sukari wakati huo. Baada ya kuondoka na shamba lile kutaifishwa na Serikali, kwa bahati mbaya sana lile eneo lilitrudishwa kwenye Halmashauri. Sasa baada ya Halmashauri nayo kushindwa kulisimamia vizuri pakatokea UVCCM wakasema lile eneo ni la kwao.

Mheshimiwa Spika, wale wazee hawakatai, wanasema kuna eneo la UVCCM lakini kuna eneo la wenyeji. Sasa limechukuliwa eneo lote limekuwa la UVCCM, wazee wale wanasema sisi tutakwenda kulima wapi na sisi tuna warithi wetu amba ni watoto wetu? Kwahiyo naomba pia Mheshimiwa suala hili ulishughulikie ili tuondoe migogoro isiyokuwa ya lazima; na kama wachangiaji wengi wanavyokusifu, kwamba ni kinara wa kutatua migogoro, basi nakuomba na migogoro hii iliyoko Tanga nayo uitatatue.

Mheshimiwa Spika, lakini kama hili halitoshi kuna suala la EPZ maeneo ya Mwahako vilevile; jambo hili lina karibu miaka nane watu wa maeneo ya mbugani; miaka nane imeanzishwa EPZ lakini watu bado hawajalipwa na wamezuiwa kuendeleza majengo yao. Wanasesma tunavyojua sisi sheria na taratibu za evaluation ikipita miezi sita lazima ifanyike upya kwa bei ya soko iliyokuwepo ya ardhi ya wakati huo; sasa hawa wananchi mpaka leo hawajui waende wapi. Nakuomba nalo Mheshimiwa Waziri hili ulishughulikie lipate ufanuzi.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine nikija kwenye gharama za upimaji; vifaa vya kupimia umetuambia na kupongeza kwa hili, kwamba Halmashauri zetu zikachukue vifa vya kupimia kwenye Kanda, lakini sasa kuitia Bunge hili uwatamkie wananchi kwamba gharama za kupima kiwanja kimoja ni shillingi ngapi. Kwasababu wenzetu wa kwenye Halmashauri wanatoza gharama kubwa utafikiri kile kifaa labda ni chaki kwamba ukiandikia inakwisha, kumbe kifaa kile ni kuweka *battery* kwenye *charge* ukaenda ukakitumia kinakuwa kinaendelea kudumu.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hilo, eneo la Ngamiani Kati, Ngamiani Kaskazini na Ngamiani Kusini ambayo ndiyo kioo cha Mji wa Tanga; eneo lile lilipimwa zamani enzi za wakoloni watu wakapewa offerlakini hawana hizi hati kubwa za kisasa. Sasa nilikuwa naishauri serikali, kwa gharama zake, kwasababu pale asilimia kubwa nyumba zile ni za mirathi, wengine wameuza, wengine hawaelewi taratibu; kwahiyo napo Serikali ingepima eneo la kuanzia barabara ya kwanza mpaka barabara ya 21 ili na wananchi wale wapatiwe hatu ambazo zitawasaidia katika matumizi yao ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, kama hili halitoshi, kuna mgogoro mkubwa sana sasa hivi kati ya Halmashauri na wananchi wa maeneo ya Mabokweni na Kirare na maeneo ya Amboni *Cross Z*. Tunajua kuna Kampuni ya Amboni ilikuwepo. Kamouni ya Amboni wakati huo, Waziri wa Kilimo na Mifugo...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Nilishakutaja Mheshimiwa Susan Kiwanga utafuatiwa na Mheshimiwa Agness.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichengie kwenye hii Wizara...

**SPIKA:** Dakika tano.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, mimi naanza kwa kutoa pole kwa ule mradi wa kupima vipande vyote vya radhi Wilaya ya Ulanga, Kilombero na Malinyi, natoa pole nyingi sana kwa misimamizi wa mradi huo, Kijana wetu Machabe chini ya Wizara hii ya Ardhi kwa kifo kilichotokea kwa vijana wadogo kabisa tisa; yaani huwezi kuamini. Sasa siku hiyo tulikuwa yunajipanga mimi na Lijualikali tumeitwa kwa *RCO*, lakini tukapata habari kwamba gari liliolobeba wale vijana, tena walikuwa wanakwenda kukabidhi hati za kimila, likaingia kwenye kidaraja (Korongo) yaani huwezi kuamini. Wengine baba mmoja, mama mmoja wametumbikia mule, gari sijui iliapata matatizo gani, wakafa wale vijana zile na maiti ukiangalia haki ya Mungu unaweza ukatiririka machozi mwili mzima.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo natoa pole sana kwa Wizara, kwa waru wa mradi, kwa wazazi kwa hiyo hali iliyojitokeza pale Kilombero-Ifakara. Ingawaje Mkuu wa Mkoa alifanya siasa, huyo ndiye aliyeagiza twende tukawekwa ndani (*lock up*) kwenye msiba anasema kwamba Wabunge wenu wako wapi? Jamani msifanye mambo hayo; Mkuu wa Mkoa wa Morogoro; mimi nasikitika sana kama mama.

Mheshimiwa Spika, pili, mradi upo unaendelea lakini ule mradi haukwendwa kutatua migogoro. Yaani kama aneo lenu kuna mgogoro ule mradi unawaacha unakwenda kupima ardhi nytingine, ndilo dhumuni la ule mradi. Sasa kuna maneo ambako kuna migogoro ule mradi hauwezi kwenda kutatua migogoro, labda sasa waunganishe kule kule kwenye Wizara hii na uipeleke timu ya kwenda kutatua migogoro pale migogoro inapotokea.

Mheshimiwa Spika, vilevile huo mradi tunaushukuru umekuja katika Wilaya hiyo lakini kwa hito *Stiegler's*; wenzenu *Stiegler's* imetuumiza nyie ingawa tunapenda huo umeme; kwasababu maeneo yote ya mashamba ambayo vijiji tulikuwa tunalima; maana vijijini kuna makazi, kuna maeneo wafugaji wako wengi kule kwetu na watu walikuwa wanalima lakini maeneo yale yote sasa yameingia kwenye *Stiegler* kwahiyio wafugaji hawana mahali pa kwenda. Kwahiyio kinachotokea ni nini hususan Jimbo la Mlimba ni migogoro kati ya wafugaji na wakulima, kwasababu vijiji vimebaki na maeneo machache hata kama yakipimwa hata kupanga namna gani tuweke wafugaji hamna, wakulima wenyewe wamekosa mashamba.

Mheshimiwa Spika, kwahiyio mimi ushauri wangu kwa Serikali, sasa kwa vile ule mpaka unawekwa na maliasili na nyinyi ardhi kule bonde uevu la Kilombero basi muone kwamba wale wafugaji walioko kule na wale ni binadamu jamani, wana ng'ombe kule, na wale wakulima ni binadamu. Hebu angalieni, kuna mapori mengi; kwa mfano, hapa Mkata, sijui ranchi hiyo ya Kongwa; mimi napitaga pale kila siku sijawahi kuona ng'ombe anavuka. Kwanini msiende mkawapimie wafugaji muwamilikishe yale maeneo hata kuwapangisha ili waoteshe majani waweke Ng'ombe wa kutosha wale wafugaji waliotoka kule bonde la Kilombero kuliko sasa hivi watu mpaka wanaendelea kupigana kule Kilombero hususani Mlimba?

Mheshimiwa Spika, kwahiyio, ushauri wangu; sawa mmewatoa, mmetutoa wakulima hamuwezi mkatuhamisha lakini wale wafugaji basi muwapatie maeneo kwenye hayo

mapori, hizi ranch za taifa. Kongwa hamna hata ng'ombe lakini unaambiwa hapa usipite kuna ng'ombe wanavuka. Mimi tangu nianze Bunge lile la 10, la Mama Makinda mpaka sasa sijawahi kukutana na kundi la ng'ombe likivuka pale. Kama mimi mwongo ninyi Waheshimiwa Wabunge wote bisheni. Sasa ile ranchi pale inafanyakazi gani? Hebu fanyeni mpango ili wafugaji wapate maeneo pale, na wako tayari kulipa hela, kupanga na kuotesha majani, tufuge kisasa na tuone kuna ng'ombe; Mheshimiwa Spika mwenyewe unajua.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ni kuhusu kitabu chake hiki, kizuri hiki maana alivyosema kuna mipango miji nikafurahia; nikasema Jimbo la Mlimba, Mji wa Mlimba tangu mwaka 1996 kama lilivyosema gazeti la Serikali umetangazwa kwamba unatakiwa uwe mji, lakini mpaka leo ni vijiji, Chita ni vijiji na Mngeta ni vijiji. Kuna takribani, hakuweka hapa iddai ya watu; lakini kwa sensa ya mwaka 2012 hiyo Mngeta tu yenye ilikuwa na watu karibuni 19,000 sasa hivi wako wangapi na jinsi watu walivyohamia, kengele hiyo...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** ...lakini Mlimba nayo ndiyo Makao Makuu ya Wilaya lakini mpaka leo eti ni vijiji. Nimeongea na Mheshimiwa pale wa TAMISEMI anasema hatupandishi, lakini miji kule inaanza kuwa hovyo hovyo kwanini mnatufanya hivi? Tupeni hata miji midogo ili tupange miji yetu uongo, kweli? Na hizo hela anazokusanya za ardhi hazirudi kwenye Halmashauri, kaulize Halmashauri zako hizo hela zinazokusanya kwenye ardhi zinarudi kwako? Mimi sijawahi kuona, mimi niko kwenye Kamati ya Fedha, sasa Halmashauri itapimaje? Na hao wataalam hawana magari, hawana chochote, wapo wapo tu. Kwahiyo hebu wezesheni ili tupoate mafuu katika maisha.

Mheshimiwa Spika muda umekwishaee!

**SPIKA:** Umeshakwisha Mheshimiwa

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Kicheko*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Agness Marwa dakika tano atafuata Mheshimiwa Peter Serukamba. (*Kicheko*)

**MHE. AGNESS M. MARWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze sana Mheshimiwa wangu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuunda Tume ya Mawaziri nane; Waziri wa TAMISEMI, Ardhi, Maji, Ulinzi, Kilimo, Maliasili, Ofisi ya Makamu wa Rais ambayo ni Mazingira; kwa lengo tu la kuhakikisha kwamba matatizo ya ardhi yanashughulikiwa ipasavyo. Kwa kweli Mheshimiwa Rais anafanya kazi nzuri sana na ndiyo maana imefikia hatua wananchi wamekaa kimya. Wale wanaosema wao wanataka Katiba mpya mambo yote yametendwa, mambo yote Mheshimiwa Rais anayafanya sasa yale waliyokuwa wanahitaji wao yafanywe katika Katiba mpya.

Mheshimiwa Spika, lakini haitoshi hiyo, mimi niwe kidogpo tofauti na wenzangu badala ya bomoabomoa namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa jenga jenga. Kakijenga Chama chetu Chama cha Mapinduzi, kaijenga Tanzania kwa ujumla na ndiyo maana bomoabomoa imebadilika imebomoa vyama vyapozani.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nimpongeze sana Mheshimiwa wetu Waziri Lukuvi, Mheshimiwa Waziri wetu hongera sana kwa kweli kwa kazi nzuri unayoifanya ya kutembelea wanachi na kushughulikia migogoro yao wewe pamoja na Dada yangu Mheshimiwa Angelina Mabula; na ndiyo maana badala ya kuzeeka sasa mnakuwa vijana kwa ajili ya kutembea sana na kushughulikia kero za wananchi.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni nyeti sana katika hali halisi ya uchumi wa Watanzania. Kwetu Serengeti Mkoa wa Mara kumekuwa na shida na migogoro mingi sana; katika Wilaya ya Tarime na Wilaya ya Bunda lakini yote haya Mheshimiwa Waziri na Naibu wake wameyashughulikia kwa undani zaidi na kwa uzuri; kwa kweli Mheshimiwa Waziri hongera sana. Tunawashukuru sana kwa kusababisha ile ardhi iliyokuwa inatuletea shida, sasa mmeiweka katika mipango mizuri, kwamba sasa iwe katika matumizi bora ya ardhi. Mimi niwaombe tu mfanye haraka ili wale wananchi waliokuwa wanapata shida kutokana na ugomvi au migogoro ya ardhi sasa waweze kuitumia ardhi yao. Migogoro yote iliyokuwepo sasa imekwisha hivyo tunaomba wagawiwe ili waweze kuitumia vizuri.

Mheshimiwa Spika, kule kwetu Tarime wanawake tulikuwa haturuhusiwi kumiliki ardhi; kumiliki ardhi ilikuwa ni kama kosa la jinai, lakini kutokana na utendaji mzuri na upendo wa Mheshimiwa Rais na Mawaziri wake kwa wananchi wake wa hali ya chini sasa tunaweza kumiliki ardhi ambazo wanawake pia tunakwenda kuchukua hati, tena tunachukua hati kwa muda. Kwahiyoo ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuona kwamba hata sisi watu wa hali ya chini na haswa wanawake wa Mkoa wa Mara sasa wanaweza kuimiliki hii ardhi.

Mheshimiwa Spika, niombe Wizara hii; pamoja na mambo yote kuna changamoto ambazo bado wanatakiwa wazishughulikie. Kuna baadhi ya wafanyakazi au watendaji wa Wizara hii ambao hawaoni kwamba wao wanapaswa kuendana na kasi ya Mheshimiwa Rais; bado wamekuwa ni wasumbufu sana katika Wizara hii. Wamekuwa bado wakiowaomba rushwa wananchi bila kujali kwamba wananchi wana hali mbaya au hali ngumu, lakini pia wamekuwa hawafanyi kazi ipasavyo na kwa muda; na ni wachache tu wanaosababisha hii Wizara ionekane kama vile bado ina matatizo matatizo. Mheshimiwa Waziri Lukuvi Mungu akikubariki hebu ingia sasa na kwa hao wafanyakazi warudishe tu angalau na wao vijijini wakalime ili kusudi wale

wanaoweza kufanyakazi; kuna wananchi wengi sana ambao hawana kazi; nao wapate kazi za kufanya.

Mheshimiwa Spika, katika utendaji wa Mheshimiwa Lukuvi kuna maeneo ambayo yamepakana na hifadhi ambapo ni Wilaya ya Bunda, maeneo ya Nyatwali. Ni muda mrefu sasa hilo eneo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Agness.

**MHE. AGNESS M. MARWA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

**SPIKA:** Ahsante sana. Habari ya Nyatwali ameisikia Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Peter Serukamba atafuatiwa na Mheshimiwa Rose Kamili na Mheshimiwa Timothy Mnzava ajiandae. Mheshimiwa Peter Dakika 10.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kucahngia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kabisa kabisa kumpongeza Waziri Lukuvi na Wizara nzima ya Ardhi. Waziri Lukuvi mimi nakuombea heri sana, angalau ni kati ya Mawaziri wachache ukienda ofisini kwake atakusikiliza na utaondoka na jawabu. Mimi huwa najjuliza Lukuvi aidha labda hana kazi sana ama Lukuvi anawapenda Wabunge na anapenda kutatua matatizo. Kwasababu Mawaziri wengine kwa kweli wako *busy* kweli, ukikutana naye ana haraka na hakusikilizi vizuri. Mheshimiwa Lukuvi mimi naomba niseme nakupongeza sana.

Mheshimiwa Spika, na kwa kiasi kikubwa unaweza ukaona matatizo ya ardhi mengi sana yametatuliwa kipindi hiki cha Mheshimiwa Waziri Lukuvi. Nakushukuru sana Waziri

Lukuvi, nawashukuru watendaji wote wa Wizara, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa kazi kubwa mnayofanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nina mambo mawili tu ya kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza ni suala la *National Housing*. Nimesoma hapa ndani kwenye kitabu Mheshimiwa Waziri amesema kuhusu *National Housing*. Mimi nataka nikushauri Mheshimiwa Waziri; nadhani umefika wakati *National Housing* iwe na *department* mbili. Moja ihangaike na nyumba kwa ajili ya wafanyakazi wa Tanzania ambao ni kwa ajili ya punagisha, na ndilo ilikuwa dhumuni la Shirika hili. Mbili, kuwe kuna *wing* ya biashara ya kujenga nyumba kwa ajili ya kuuza. Nina uhakika *National Housing* wakifanyakazi hizi; lakini mkataka wafanye kazi za nyumba za kuuza, nyumba za kupangisha tunawachanganya na ndio maana leo kuna miradi mikubwa sana pale Dar es Salaam imesimama.

Mheshimiwa Spika, ningewomba Mheshimiwa Waziri, ile miradi tukiachachia isimame sisi tunapata hasara kwasababu wale wakandarasi wako *site* tayari. Kama hamuwalipi wao wanapata *interest*, wanapata *idle time*; kwahiylo *at the end of the day* looser ni Serikali. Whether mikataba ilikuwa mibaya, whether mikataba ilikuwa ni mizuri lakini *it is our interest* tuhakikishe tunamaliza kazi za majumba yote ya Dar es salaam; kwasababu Shirika limekopa Benki, Shirika limeweka *collateral*. Sasa kama hatuwezi kumalizia zile nyumba maana yake hizi *collateral* zinakuaje? Na leo kinachoonekana kama vile *National Housing* imendoka na Nahemia Mcchechu, *that is the vibrancy* ya *National Housing* haionekani. *Is it true* kweli kwamba ni mtu mmoja ameondoka mabo yamebadilika?

Mheshimiwa Spika, mimi sitaki kuamini hayo, nataka kuamini kwamba ningeomba Serikalini turudi kwenye *drawing board*, kwanza tumalize yale tuliyoyaanza halafu ndipo tuje na mpango mpya; lakini tukisema tunakuja na mpango mpya yale tuliyoyaanza tunayaacha barabarani

kwa kweli tunajichoma wenyewe hatima yake *collateral/zetu zitaanza kuuzwa*; nani atalipa hii gharama? Maana *project zikisimama zina-accrue interest*, kitakachotokea ni nini? Maana yake gharama ni kubwa na Shirika letu tunaliingiza kwenye madeni makubwa. Kwahiylo niwaombe Serikali kwa umoja wenu nawaombeni tatizo la *National Housing tulitatuue*, tuipe nguvu *National Housing* ifanye kazi yake.

Mheshimiwa Spika, la pili, nataka nizungumzie suala la *mortgage financing*. Toka nimeingia kwenye Bunge hili tulitunga Sheria ya *Mortgage Financing* lakini bado *interest za benki ni kubwa sana*. Matokeo yake ndiyo maana *mortgage financing* haishamiri, nchi za wenzetu ukimaliza *university* ukipata kazi siku ya pili tu ziko nyumba za kwenda kupanga ambazo unauziwa kwa *interest* unalipa baada ya miaka 20, baada ya miaka 30, namna hiyo tutaweza kuwasadia wafanyakazi wa Tanzania. Kama *mortgage financing* hii ninayojua ambayo ni benki zimeamua yao, ambayo *interest* ni kubwa bado *mortgage financing* Tanzania safari yetu ni ndefu sana. Ningemba turudi kwenye *drawing body* tuangalie hizi *interest rate*, kama *interest rate* tuziongezee miaka mingi ya kurudisha fedha nina hakika tutakuwa tumewasaidia wafanyakazi wa Tanzania na Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho, nataka kuzungumzia suala la *Land Bank*; marehemu Mzee Mungai aliwahi kusema hapa Bungeni kwamba tunatamba sana tuna ardhi kubwa sana, Watanzania tuna ardhi yetu, Wakenya wanatuonea wivu kwa ardhi yetu, kila mtu anatuonea wivu ardhi yetu lakini ardhi isiyoleta mali ya nini. Leo tuna ardhi tunatamba nayo halafu tunakufa njaa, tuna ardhi tunatamba nayo ukiangalia kwenye *GDP growth* kutoka kwenye *agriculture* ni ndogo. Nilitarajia tumepata ardhi hii, iwe ni kichocheo kikubwa cha uchumi wa Tanzania. Kwa nini nasema hivyo? Angalia kahawa Tanzania tunazalisha tani 50,000 nchi nzima hapo Uganda tani 288,000, wana ardhi ndogo kuliko sisi tuna ardhi kubwa lakini hakuna ni kwa sababu gani tunataka kila mtu alime. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kuendelea hatuwezi kuja na *commercial farming*, kama tunataka kila mtu alime matokeo yake itakuwa ni umaskini tu, mama yangu kijijini analima miaka yote lakini hajawahi kujitosheleza kila mwaka anazo heka mbili, heka tatu zinamsaidia nini, hivyo, ningeshauri Mheshimiwa Waziri Lukuvi umefika wakati tupime ardhi yetu tuwe na maeneo ya ardhi ambayo ni kwa ajili ya *large plantations*, kwa ajili ya *commercial farming*, hili ndio itatufanya Tanzania tulishe *East Africa*, tulishe Afrika kwa sababu Mungu ametupa ardhi na ametupa maji. Hata hivyo, kama hatuna mpango miji tunadhani nia yetu ni kila mkulima, kila Mtanzania awe na kipande chake kidogo cha ardhi mwisho wa siku kukitoa *draught* tutakufa njaa.

Mheshimiwa Spika, yako mazao ambayo tulipaswa Tanzania tuwe tuna *read* kwenye hilo *continent*, kwa mfano kahawa tuna eneo kubwa sana tilitakiwa tunashinda Ethiopia. Angalia mkonge tuna uwezo wa kuzalisha tani 1,000,000 za mkonge lakini tunazalisha tani 19,000 na tuna ardhi yote hii, kwa nini? Kwa sababu hatuja-*embrace commercial farming*, hata kule ambako kuna mashamba tunaseme tuwape watu wadogo yeche si ndio atalima mahindi, kesho anaendelea kuwa masikini tu.

Mheshimiwa Spika, haya kwenye chai tuna maeneo makubwa sana ya *land* ambayo tunaweza tukalima chai, unajua tunazalisha tani ngapi za chai kwa mwaka, tani 19,000, Kenya tani 3,80,000, hivyo ikitokea bei ya chai imeanguka duniani sisi inatumiza kwa sababu hatuna *economics of scale*. Sasa mimi sielewi naomba wenzangu watusaidie.

Mheshimiwa Spika, suala la pareto, suala la korosho, korosho tuna tani 210,000, Nigeria wana tani 890,000, ukiangalia hata ugomvi wetu wote ni kwa sababu tunagombania kidogo tulichonacho, lakini tunayo ardhi ya kuweza kulima na tuka-*benefit* kwenye *economics of scale*. Hivyo ningeomba Mheshimiwa Waziri Lukuvi umefika wakati na najua hili analiweza, umefika wakati tutengeneze ardhi

hata tukiwatafuta *investors* wakatuambia nataka ardhi ya kulima kitu Fulani, unamwambiwa ardhi hii hapa.

Mheshimiwa Spika, leo akija *investor* anataka kulima kwa mfano makademia ambao ni *very higher product*, kuna Wakenya wanakuja hapa kutafuta ardhi, hawaoneshi lakini tunaimba ardhi tunayo. Kama ardhi hii haituletei maendeleo, ardhi haituletei uchumi, nadhani tunaji-*contradict* na hakuna maana ya kuwa na hii ardhi kama haiwezi kutuletea maendeleo, kwa sababu ardhi ndio maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Nilishakutaja Mheshimiwa Rose Kamil utafuatiwa na Mheshimiwa Timotheo Mzava, dakika tano, tano.

**MHE. ROSE K. SUKUM:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia kidogo kwa hizi dakika tano na nitazitumia vizuri. Wizara hii ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ina ubora wake, lakini pia kuna matatizo mengine madogo ambayo yapo, kwa hiyo naomba nichangie kwenye matatizo madogo ambayo yapo.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa kuna matatizo ambayo yako kwenye Wizara hii. Sisi Wilaya ya Hanang tulihitaji ardhi ile ambayo imerejeshwa kwa wananchi shamba la Gawal na shamba la Wareet kufuta hatimiliki ya awali ili wananchi waweze kugawiwa maeneo yao waweze kupata hatimiliki, lakini ofisini kwa Mheshimiwa Waziri naona kuna ugumu sana wa kuweza kufuta hiyo hatimiliki na tunaomba alifanyie kazi hilo kwa sababu ni muhimu sana, wananchi wanahitaji hatimiliki lakini hawawezi kupata mikopo kutokana na ugumu uliotokana na Wizara yake. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lingine la pili, napenda kuzungumzia suala la migogoro; sisi Wilaya ya Hanang tuna mashamba ya *NAFCO* ambayo kwao yamebinafishwa kwa

wawekezaji na tuna mgogoro sana na mwekezaji mmoja ambaye ni Ngano *Limited* au kwa jina lingine analitumia Rai *Group*, yeye ni wa Kenya, alibinafsishiwa mashamba matatu. Cha kushangaza huyu mwekezaji analima asilimia 30 tu tangu amepewa yale mashamba. Sasa Mheshimiwa Waziri nimesikia akinyang'anya mashamba ya watu wengine ambaao hawajayaendeleza, sasa huku Hanang kwa nini ameshindwa kufika na wakati anafika hata Babati.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri afike Hanang akatembelee hayo mashamba ambayo yanaitwa Ngano *Limited* ayaone yakoje, lakini kwa taarifa fupi napenda kumweleza kwamba Halmashauri ya Hanang inategemea cess kutokana na mazao. Sasa hivi tumekosa hiyo cess kwenye mashamba hayo matatu, tulikuwa matajiri kutokana na kupata hiyo cess, lakini mashamba hayalimwi hata kidogo na wao wenzetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nimweleze kwa kifupi Mheshimiwa Waziri aelewé kwamba shamba la Gidagamowd lina hekari 16,330 ambazo amebinafsishiwa huyo Ngano *Limited*. Yeye analima hekari 5000 tu, hekari 11,330 hajalima, hii ni miaka yote tangu amepewa hayo mashamba, yanakaa hivi hivi ni mgogoro.

Mheshimiwa Spika, shamba lingine ni shamba la Murjanda alilobinafsishiwa huyo bwana ambalo lina ekari 13,400, kwa hiyo anayolima yeye ni ekari 6000, ekari 7,400 halimi.

Mheshimiwa Spika, angalia tena shamba lingine la tatu ambalo amepewa huyo mwekezaji ni shamba la Setchet, shamba hili lina hekari 16,300, analima hekari 3,500 tu, hekari 12,800 halimi. Mheshimiwa Waziri hebu aangalie kati ya hekari hizo zote hekari 34,000 mwekezaji huyo halimi, je angeyaachia yale mashamba kwa wananchi si yangelimwa yote na tungepata cess sisi Wilaya ya Hanang? Sasa hatupati cess, wewe pia kwenye Serikali hupati kodi yoyote kwa sababu ya tatizo alilonalo. Naomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hili kwa undani na kwa huruma kwamba

Wanahanang sisi tunategemea kilimo, sasa kama halimi ya nini? Yarejeshwe kwa wananchi ili waendelee kuyalima, hatuna sababu ya kuwa na wawekezaji ambao hawafanya au hawatekelezi wajibu wao. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine la tatu napenda kuzungumzia suala la kupima viwanja. Tuna tatizo la mpango wa upimaji shirikishi, kwa sababu matatizo haya yanatokea kwa Wilaya ya Hanang kutokana na kutokuwa na majalada na headed *paper* kwa sababu inabidi Wilaya ya Hanang wakachapishe kwenye *government printers* na ni ghali. Matokeo yake upimaji unakuwa wa gharama ya juu, tunaomba Wazri atusaidie tunafanyaje ili gharama ziwe chini na Wizara yake ndio inaweza hilo. Sasa kama hawataweza kuwawezesha Wataalam wetu walioko wilayani au wale ambao ni wataalam ambao sijui ni wa upimaji shirikishi uliopatikana siku hizi, basi wawawezeshe ili gharama ziwe za chini na wananchi waweze kumudu.

Mheshimiwa Spika, ya kwangu ni hayo, sina mengi ya kuongea zaidi ya kutaka Mheshimiwa Waziri afike Wilaya ya Hanang kutatua hiyo migogoro. Haya mashamba hata sisi tuna uwezo wa kulima. Ahsante sana. (*Makof*)

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Rose Kamil, Mheshimiwa Timotheo Mnzava nilishakutaja dakika tano.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

**SPIKA:** Utafuatiwa na Mheshimiwa Selasini dakika tano.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kwanza kabisa kumshukuru Mungu lakini pia kumpungeza sana Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Naibu Waziri na Watendaji wao Wizarani wanafanya kazi kubwa, wanafanya kazi nzuri sana hongera sana kwa kazi nzuri wanayoifanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, moja kwa mujibu wa tafiti mbalimbali duniani moja ya njia bora kabisa ya kuondoa kama sio kupunguza migogoro ya ardhi ni kupima na kupanga matumizi bora ya ardhi. Hii ndio moja ya njia bora kabisa pamoja na kwamba tunakubaliana kwamba kwa mujibu wa sheria zetu *Planning Authority*ni kule kwenye Serikali za Mitaa, lakini Wizara ndio yenyen jukumu la kusimamia kutekeleza sera kwenye Sekta ya Ardhi. Naomba sana pamoja na changamoto za kifedha na za kibajeti watutafutie mkakati maalum wa kupima na kupanga maeneo yetu. Tume ya Mipango ya Ardhi inafanya kazi nzuri, lakini bado uwezo wake ni mdogo na imebaki kuwa kama waratibu tu.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kwenye mashamba yasiyoendelezwa. Nitumie nafasi hii kwa dhati kabisa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, tangu ameingia amefanya kazi ya kufuta hati za mashamba ya baadhi ya wawekezaji ambao hawayaendelezi vizuri na hata kule kwetu Korogwe, hili pia limefanyika pamoja na maboresho yaliyofanyika kwenye mashamba yale sita ambayo yalifutwa, bado alichokifanya Mheshimiwa Rais kinawasaidia sana watu wetu na sisi watu wa Korogwe tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ninayo mashamba mengine kule na nimeshamwambia Mheshimiwa Waziri zaidi ya mara moja na namwamini sana baba yangu na naikubali sana kazi yake, kama pale Wizarani kuna watu wanakwamisha yasifike kwa Mheshimiwa Waziri hebu aingie ndani aangalie kuna nini huko, kuna shamba la pale Mwakinyumbi, Hale. Nimekuja juzi kwenye Bunge lakini hii nazungumza ni mara ya tatu kama sikosei.

Mheshimiwa Spika, kuna shamba linaitwa Kwashemshi, kuna mwekezaji anasema yeze ni mwekezaji wa Mkonge, anakodisha kwa watu wengine, miaka miwili iliopita alikuwa anakodisha kwa wananchi walime mahindi kule ndani kwa sababu eneo kubwa halijalimwa mkonge. Mwaka huu ameamua mpaka na kuwafukuza wananchi

amechukua mtu binafsi amekuja analima mahindi kwenye shamba hilo, wananchi hawana maeneo.

Mheshimiwa Spika, mimi ni muumini ambaye naamini kabisa sio sawasawa kila ardhi ya mwekezaji tukaichukua tukagawa kwa wananchi, hatuwezi kuwa nchi ya namna hiyo, lakini lazima tukubaliane kama mtu amepewa ardhi haitumii kwa mujibu wa masharti aliyokabidhiwa masharti yake ya umiliki, wahukue hatua. Hili suala nimelisema muda mrefu, namwomba sana Mheshimiwa Waziri aingie, najua kwake mara naambiwa halijafika, mara limefika likarudi, sielewi kinachoendelea hapo, hebu aangalie Mheshimiwa Waziri hapo kwenye Wizara, kuna mtu atakuwa anacheza na hivi vitu, kuna shamba linaitwa shamba la Mwakinyumbi.

Mheshimiwa Spika, huu ni mwaka sijui wa ngapi tunalalamika na hili jambo. Marehemu Profesa Majimarefu amepiga kelele sana humu ndani mpaka Mwenyezi Mungu amemchukua, hatujui kinachoendelea kwenye mashamba haya. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri kwa unyenyekevu mkubwa na kwa kazi yake anayoiamini awasaide watu wa Korogwe waweze kupata maeneo, lakini pia kazi zifanyike vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri jambo lingine hasa kwa niaba ya vijana wote lakini na Watanzania kwa ujumla, sasa ni wakati muafaka wa kuwa na sera ya nyumba. Ni wakati muafaka kama Taifa kuwa na sera ya nyumba, hebu Wizara walifanyie kazi hili jambo tuweze kufikia mahali pazuri.

Mheshimiwa Spika, yamesemwa hapa na nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kazi anayoifanya, ile kazi tulioikuta inafanyika Kilombero, Ulanga na Malinyi ilikuwa ni kazi nzuri sana nimpongeze yeye lakini niipongeze na ile timu iliyokuwa inasimamia ule mradi. Mheshimiwa Waziri kwenda kugawa hati ni sehemu ya namna ya kusadia kutatua changamoto za migogoro ya ardhi kwa watu wetu, hakuna kosa. Korogwe pia tukipima tutamwita Wziri aje atugawie hati na sisi tutapokea.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri anafanya kazi nzuri, sina maneno mengi, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Timothy kwa kutumia muda wako vizuri sana. Mheshimiwa Joseph Selasini dakika tano na Mheshimiwa John Pallangyo atamalizia.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naona tofauti kubwa sana ya kazi zilizofanywa na Wizara hii katika kipindi hiki na kipindi kilichopita. Kwa hiyo si jambo baya kupongeza juhudhi na kazi kubwa iliyofanywa na Wizara hii. Pamoja na hayo ni vyema Wizara ikapokea upungufu mchache ambao tunauleta ili ufanyiwe kazi ili kazi ya Wizara iwe bora zaidi ya hapa ilipofikia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nataka niseme mambo matatu tu. Jambo la kwanza, mdogo wangu Mheshimiwa Mnzava amezungumza habari ya Sera ya Nyumba na huu Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora lazima utusaidie, ni aibu kwa Taifa kuwa na nyumba za tembe. Ukiangalia wananchi sio kwamba wanashindwa kujenga, lakini wakipewa aina fulani ya mjengo wanaweza wakaujenga taratibu wakamaliza na vilevile katika miji yetu sasa hivi kuna kujengwa holela tu.

Mheshimiwa Spika, ukienda miji ya wenzetu, najua Mheshimiwa Lukuvi ametembea sana, unakuta kuna eneo mtaa fulani ni marufuku kujenga aina fulani ya nyumba, aina hii ya nyumba ijengwe mahali Fulani. Sasa ni lazima tu miji yetu tuiboreshe vinginevyo tukiachia kila mtu ana *planramani* yake anabuni kitu chake, matokeo yake makazi yetu yatakuwa hovyo hovyo. Kwa hiyo huu Wakala ufanye kazi yake sawasawa kuishauri Serikali kuhusu nyumba ambazo kwa wananchi zinaweza kuwa *affordable* na vilevile bei na vifaa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lingine tumesema hapa na nataka nirudie Kambi Rasmi ya Upinzani haipingani na uchukua ji wa mashamba pori, yaani lazima hili lieleweke, sisi tunaunga

mkono mashamba ambayo hayajaendelezwa yachukuliwe, tunachosema Serikali sikuvi ikikutana na mwananchi mmoja anayelalamika imsikilize kwa sababu kuna baadhi ya wananchi wanalamika kwamba mashamba yetu yamechukuliwa, lakini ndani yake kuna nyumba, kuna mifugo, kuna mashine na kadhalika. Si jambo bayu Serikali ikakaa na watu hawa, ikawasikiliza wakaridhika tu, manung'uniko yakaondoka ndani ya mioyo yao.

Mheshimiwa Spika, lingine...

**SPIKA:** Mheshimiwa Selasini kwani jamaa si ameenda mahakamani au, endelea kuchangia tu.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, simjui huyo jamaa. Lingine Mheshimiwa Lukuvi akiwa Moshi alitushauri sisi watu wa Kilimanjaro tuache kuzika kwenye mashamba yetu na tulipiga kelele sana kwa sababu sisi kwa mila zetu na desturi zetu hatuwezi kuacha, lakini mimi ningesema hivi watusaidie katika yale maeneo ambayo huo utaratibu bado haujaanzishwa ili yale maeneo yabaki salama kwa sababu najua eneo ambalo limezikiwa thamani yake inapungua. Sasa kuna maeneo mengine kwa mfano kule wilayani, kwenye miji ile ambayo inakua sasa hivi watusaidie ili watu wasije wakapeleka tena huko makaburi, halafu tukapata shida. Sisi hatuna ardhi na kama nilivyosema huu Wakala wa Utafiti wa Nyumba Bora ingetusaidia sana sisi kwa maana sasa hivi hata shule tunajenga za kwenda juu maghorofa lakini tupewe ramani ili ziweze kutusaidia. Kwa hiyo Mheshimiwa Lukuvi hili zoezi sijui kama tutaliacha, lakini anaweza kuendela kuzungumza labda wazee wa kimila tutamsikia.

Mheshimiwa Spika, lingine ni hili la upimaji; upimaji umekuwa ni tatizo kubwa na hizi halmashauri sijui kama zitaweza. Zamani kulikuwa na utaratibu halmashauri zinakopa Wizarani halafu zinalipa kidogo. Nina maeneo pale Holili watu wanatafuta viwanja tumeshindwa kupima, lakini kwa nini Serikali wasirudishe ule utaratibu wa kuzikopesha halmashauri, zikafanya upimaji, zikauza viwanja halafu ile

pesa ya kuuza vile viwanja ikarejeshwa kwa kutokana na mkopo ambao watakuwa wamekopa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie tu kwa kusema Mheshimiwa Lukuvi *comment* aliyotoa mwenzangu Mheshimiwa Devota Minja...

**SPIKA:** Malizia kwa dakika moja.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** ...aliyotoa Mheshimiwa Devota Minja ilikuwa na kusudio la kusema tujenge taasisi, Mheshimiwa Waziri anafanya kazi nzuri, lakini lazima wale wa chini yake wajengwe ili hata akiondoka pale Wizarani, Wizara iendeleee na kazi ambayo tunaona anafanya ni pamoja na *restructuring* na kuhakikisha wale ambao hawafanyi kazi sawasawa wameondoka, lakini ifike mahali hata akiwa hayupo *capacity building*, Wizara iendeleee kufanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge majuzi hapa nilienda Moshi kwa sababu ambazo wote tunafahamu kuwawakilisheni. Moja ya kitu ambacho nilijifunza nikiwa kule ni kwamba wengi huwa tunaamini kwamba *affluence* inaleta hali fulani ya furaha miongoni mwa jamii ambayo ni *affluent*, jamii ambayo ina uchumi mzuri zaidi, mkubwa zaidi, inakuwa na furaha zaidi si ndio na jamii ambayo maskini zaidi wanakuwa ni wanyonge na wana masikitiko zaidi.

Sasa *of course* kwa harakaharaka ukiacha mijini Mkoa wa Kilimanjaro nadhani uko vizuri kiuchumi, lakini nikajifunza kwamba, katika mikoa inawezekana ambao unaongoza kwa *suicide*, kwa kuijuwa, kujinyonga, kunywa sumu, kufanyaje, Mkoa wa Kilimanjaro unaongoza; ndiyo, watu wanakatiza maisha yao. Sasa nimepata tabu kujua inakuwaje? Mbona tunaamini kwamba, ukiwa na uchumi mzuri unakuwa na furaha zaidi? Halafu tena, *suicide*?

Hapana wala si kuuana, wanafanya *suicide* kabisa, *including* hiyo labda kama ipo, lakini watu; tena wanaacha na maandishi wengine na nini, lakini unakuta ana nyumba ana kashamba kake, lakini ana. Kwa hiyo, nalo ni mojawapo limejitokeza, labda siku moja Mheshimiwa Selasini atatusaidia kutuambia *what is not happening in Kilimanjaro*.

Mheshimiwa Pallangyo, uwe wa mwisho dakika tano. halafu Mheshimiwa Naibu Waziri dakika 15.

**MHE. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kidogo kwenye hii hoja ambayo iko mezani. Nianze kwa kumshukuru Mungu mwinci wa rehema ambaye ndiye ametuweka hapa, lakini pia niwashukuru sana wananchi wa Arumeru Mashariki ambao waliniamini wakanichagua kwa kura nyingi na kunifanya niwepo hapa leo hii. Waungwana wanasema kwamba ukiaminika unakuwa ni mdeni; kwa hiyo niseme tu kwamba mimi ni mdeni wao kwa hiyo ninawahakikisha kwamba nitajitahidi kuwatumikia kwa kadiri Mungu atakavyoniwezesha.

Mheshimiwa Spika, kipekee sana nichukue nafasi hii kumpongeza sana Rais wetu Dkt. John Joseph Pombe Magufuli ambaye anafanya kazi nzuri sana na ya heshima kwa nchi hii. Anatekeleza ilani ya uchaguzi kwa umahiri mkubwa, na niseme kwamba anaziishi ahadi zake alizozitoa majukwaani mwaka 2015. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, niende Wizarani. Mheshimiwa Lukuvi nakupongeza sana Ndugu yangu. Nakupongeza wewe na Naibu wako, Makatibu Wakuu na watumishi wote wa Wizara hiyo, mnafanya kazi nzuri na ya heshima. Wenzangu wanakuita kinara wa kutatua migogoro, ni kweli nakubaliananao. Nilikuwa nakufuatilia kwa karibu, mara leo uko Bukoba, kesho Kilombero, kesho kwetu, Jumapili Kilimanjaro; hakika umefanya kazi nzuri unastahili pungezi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu ni Serikali makini sana, inajali Watanzania na ndio maana tuliamua kwa makusudi kutenga asilimia nne za *ecosystem* ya Selou ili tuweze kujenga kinu cha kuzalisha umeme unaotumia nguvu ya maji ili Watanzania waondokane na giza na pia wapate nyenzo muhimu ya kuzalishia bidhaa kwa kuanzisha viwanda vidogovidogo na vikubwa.

Mheshimiwa Spika, ardhi ni rasilimali muhimu sana kwa wananchi, naamini Mheshimiwa Lukuvi analijua hilo. Ninamuomba, wiki iliyopita lilzungumzwa jambo la Kata ya Ngarenanyuki, Kijiji cha Olkung'wado, kwamba kuna tatizo, lakini Waziri wa Maliasili akasema pale hakuna tatizo. Baada ya pale nilipata ujumbe kwamba kweli bado tatizo linaendelea, na nimefuatilia nikakuta wananchi kuna ardhi walikuwa wanaitumia kwa ajili ya maisha yao, ekari 960, zillikuja zikachukuliwa kihalali na *Arusha National Park*, kisheria, lakini badaye wakakaa chini wakakubaliana wakapunguza pale wakawapa wananchi ekari 360. Nilivyozungumza nao wakasema bado kuna tatizo, na watu wanateseka wamenyang'anywa uhai wao.

Mheshimiwa Spika, sasa nikuombe Mheshimiwa Waziri, nikusihi sana, tulia kidogo uzungumze na Waziri wa Maliasili na Utalii ili muone ni namna gani kwa *spirit ileile* ambayo tumetenga *four percent* ya *ecosystem* kwa ajili ya manufaa ya wananchi, uende pale Momela uzungumze na wananchi uchukue lile eneo ambalo limechukuliwa na *TANAPA*, ekari zote 960 zirudishwe kwa wananchi ili wakawage na waweze kuishi. Ardhi ni rasilimali ya msingi sana na ndio utajiri mkubwa.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa muda huu mfupi. Naunga mkono hoja *percent 100. (Makof)*.

**SPIKA:** Ahsante sana, nakushukuru sana Mheshimiwa kwa hotuba yako ya kwanza Bungeni, lakini *well calculated*. Mheshimiwa Naibu Waziri, Dkt. Angelina Mabula, dakika 15, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO**

**YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa fursa hii ambayo tumeipata kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuweza kuchangia hoja ya Wizara hii. Nianze kwa kuunga mkono hoja ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini na kuniacha katika Wizara hii kuendelea kumsaidia katika majukumu ya utawala wa ardhi na shughuli nydingine zinazohusiana na ardhi. Nimshukuru Waziri wangu kwa maongozi yake mazuri, ni *mentor* mzuri kwa kweli anaweza kusimamia watendaji walioko chini yake na kuweza kuelekeza mambo yakafanyika vizuri na kweli tunafanya vizuri. Nimshukuru Katibu Mkuu pamoja na timu nzima yote ya Wizara pamoja na taasisi zilizoko chini ya Wizara, wanafanya kazi vizuri na tunashirikiana na ndio maana pongezi hizi zinakuja kwa sababu ya ushirikiano na namna ambavyo Wizara inasimamiwa.

Mheshimiwa Spika, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia. Tumepokea michango kwa maandishi kutoka kwa Waheshimiwa Waheshimiwa Wabunge 21 na Wabunge 17 wamechangia; kwa hiyo jumla ni 38; kwa hiyo tunawashukuru sana na pongezi zenu tumezipokea kwa sababu kazi kubwa tulioifanya tumeionta.

Mheshimiwa Spika, nisiwe mchoyo wa fadhila, niendelee kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Ilemela walioniamini na kunipa fursa hii. Nishukuru na watendaji wanaosimamia sekta hii wakiongozwa na Katibu Tawala Msaidizi wa Mkoa wa Mwanza ambaye leo anashuhudia hapa, yuko na maafisa kutoka Manispaa ya Ilemela pamoja na jiji kwa namna ambavyo wanafanya kazi nzuri na ndiyo maana pia mkoa unaonekana umefanya kazi vizuri kwa sababu ya usimamizi.

Mheshimiwa Spika, niishukuru familia yangu nikimshukuru na binti yangu mpendwa, Diana, leo amekuja kushuhudia; nashukuru sana kwa hayo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru Kamati, kwa kweli ushauri walioutoa tumeuzingatia na tutaufanyia kazi. Kama ambavyo Wizara siku zote imekuwa sikivu. Kila wanapotupa ushauri ambao tunaona unajenga zaidi Wizara tunauchukua na tunaufanyia kazi; na kwa kweli kamati imekuwa ikifanya kazi kubwa ya kutoa ushauri pale ambapo tunaona kwamba tunahitaji oengine kuboresha zaidi, na wamekuwa wakifanya hivyo; na hata hotuba yao wameitoa ilikuwa pia, ina ushauri mzuri. Nimshukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti pamoja na kamati yake.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru Waziri Kivuli kwa hotuba yake nzuri, naye ametoa changamoto kadhaa na kuweza kutoa ushauri. tutayapitia yale yote ambayo ameyazungumza tuweze kuona namna bora ya kuweza kuyatumia yale yanayojenga; lakini nishukuru tu kwamba mmetambua kazi inayofanywa na Wizara na mpaka mkapongeza pia kwenye taarifa yenu. Kwa hiyo tunashukuru kwamba tunafanya kazi kwa pamoja, kwa sababu tunapojenga taifa moja tunahitaji kushikamana na kuhakikisha tunakwenda vizuri. Ardhi ni mali, ardhi ni mtaji; tuisiposimamia vizuri kila mmoja atapata shida; si mpinzani si CCM si yejote. Kwa hiyo tunashukuru sana pale ambapo tunakuwa tunazungumza lugha moja na inayoeleweka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wachangiaji wamechangia mambo mengi, lakini kwenye upande wa mipango miji zaidi ya Wabunge 10 wamechangia na wote wakiongelea habari nzima ya namna ya kuweza kujizatiti katika kupanga makazi yetu yaliyo bora. Wengi wamezungumza, Mheshimiwa Kubenea amesema, Mheshimiwa Stanslaus Mabula, Mheshimiwa Aida Khenan, Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mheshimiwa Mahmoud Jumaa, Mheshimiwa Charles Mwijage, Mheshimiwa Lwakatare, Mheshimiwa Mzava, Mheshimiwa

Kamili, Mheshimiwa Selasini, wote wamechangia upande wa mipango miji.

Mheshimiwa Spika, napenda tu niseme kwamba, Wizara siku zote inajizatiti kuhakikisha kwamba miji yetu inapangwa vizuri. Ndiyo maana kama mlisikiliza hotuba ya Mheshimiwa Waziri, tunayo miji zaidi ya 30 ambayo *Master Plan* zipo zimekamilika, kama Halmashauri 12 hivi, na nyingine ziko kwenye hatua nzuri ambayo tunakwenda; lengo ni kuhakikisha miji yetu inapangwa.

Mheshimiwa Spika, tatizo tunalokumbananalo tu ni kwamba *staff* tuliyonayo bado haitoshelezi kuweza kufanya kazi ile, na utaalam pia wa mipango miji unahitaji kuwa na timu ya wataalam inayoweza kufanya kazi ile kwa kasi kubwa na kuweza kufanya kazi inayokusudiwa; lakini lengo na dhamira ya Wizara ni kuhakikisha miji yetu imepangwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Stanslaus Mabula alizingumzia habari ya watu walioko milimani; na kama unavyojua Mji wa Mwanza una milima na kama ilivyo maeneo mengine kuna milima:-

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo ambayo yalikuwa yameachwa kwenye suala zima la urasimishaji katika kupanga ile miji yetu. sasa lile eneo lilikuwa limeachwa kwa sababu jiji lenyewe lilikuwa na mipango ambayo walisema kwamba wao ndio wanatarajia mipango hiyo. Hata hivyo kwa hoja aliyozungumza, ya kwamba tunahitaji pia kuwawezesha wale wananchi ili waweze kuwa na nguvu kiuchumi kwa kutumia rasilimali yao. Kwa sababu Halmashauri ya Jiji ina mpango wake leseni za makazi haziwezi kuzuia ule mpango kuwepo. Kwa hiyo, kwa hoja aliyoitoa kama Wizara tumeichukua, tutaona namna ya kuifanyia kazi vizuri ili wale wananchi ambao hawakupimiwa kipindi kile waweze kupimiwa.

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Selasini amezungumzia habari ya kukopesha halmashauri zetu ili

ziweze kupima na kupanga. Niseme tu, ni juzi tu hapa tumetoa mikopo ya bilioni 6.2 hivi kwenda kwenda kwenye Halmashauri 24; na Halmashauri hizo zimepewa mkopo na masharti waliyopewa ni kwamba wahakikishe wanafanya upimaji vizuri, wanaauza viwanja vyao na wanarejesha. Wakirejesha vizuri tunawapa tena; kadiri unavyokopa na kurejesha vizuri tunawapa kwa sababu tunajua hili suala la upangaji ni suala endelevu. Kwa hiyo, hiyo inafanyika na Wizara imeshalichukulia hatua vizuri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia katika suala zima la upangaji tunapokuwa tunaendelea kupima kuna maeneo ambayo halmashauri zetu pia zinazungumza na wananchi kama kawaida, pale ambapo miji inakuwa imetangazwa kuwa iko chini ya mipango miji. Kuna namna wanavyokubaliana kiasilimia, utakuta Chemba wanakubaliana 60 kwa 40, ukienda kule Mkinga nao wamekubaliana; lile nalo linaharakisha zoezi la kupima kwa sababu unakuwa umeshawashirikisha moja kwa moja. Sasa kwa sababu hawana ile pesa ya kutoa moja kwa moja wanaridhia kutoa sehemu ya ardhi yao ili iwe ni pesa ya mchango kwao kwako wewe kuweza kuwapimia na kuweka miundombinu; na hili linafanika bila tatizo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi niseme tu, tutoe rai kwa halmashauri zetu waendelee kutumia mpango huu ambaao tunaweza kusema ni *barter trade*, kwa sababu hela huna lakini ardhi unayo. Kwa hiyo unatoa kwa asilimia wanayokubaliana, wengine wana 70 kwa 30, wengine 60 kwa 40; lakini lengo letu ni kuhakikisha kuwa imepimwa. Wizara inachosema tu ni kwamba, haturuhusu kuchukua ardhi ya mwananchi bila kumlipa fidia, haturuhusu kuchukua ardhi ya mwananchi bila ridhaa na haturuhusu kuchuku ardhi ya mwananchi hlafu ukakaanayo bila kuiendeleza. Kwa hiyo hayo ndiyo maelekezo ya Wizara ambayo tunasema lazima yazingatiwe.

Mheshimiwa Spika, wamezungumzia suala la sera; kwa kweli ni jukumu la Wizara na tunakiri kwamba usimamizi wa sera na sheria katika Wizara ni jukumu letu la msingi katika

kuhakikisha kwamba tunakuwa na sera ambazo katika utendaji zinatuongoza.

Mheshimiwa Spika, kama walivyosema, ni kweli Sera Nyumba, kama alivyoiongelea, kwamba inahitaji kuwepo; ni kweli na sisi tunaliona hilo lakini tayari mchakato ulikwishaanza, *draft* za mwanzo zilishafanyika na tulishaanza pia kupokea maoni. Kwa hiyo bado iko kwenye mchakato, itakapokuwa tayari tutaitoa kwa sababu tunaona ni pengo liliopo kweli, pasipokuwa na hiyo tunasema tunaposema tunataka kuwa na makazi bora, tunataka kuwa na nyumba bora, kama huna sera ambayo ipo itakuwa ni shida. Tunayo Sera ya Makazi ya 2000 lakini inahitaji maboresho fulani.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wakati anazungumzia ameongea kwa kina sana kuhisiana na hizi sera na mpaka allongelea masuala ya *real estate*; ya kwamba tunahitaji pia kuwa na hiyo sera ambayo inasaidia sana katika kuhakikisha kwamba hawa waendelezaji milki hawajifanyii tu mambo yao jinsi wanavyojuua. Ndiyo maana tunaona wengi wanajenga halafu na ghamara na nini zinakuwa pia ni kubwa sana kulingana na hali halisi kwa sababu tu hicho chombo hakijawepo na kuweza kuwasimamia. Kwa hiyo hili kama Wizara tumelichukua na tunaendelea kulifanya kazi kwa sababu tayari liko kwenye mchakato wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, wamezungumzia migogoro ya matumizi ya ardhi. Mheshimiwa Yussuf ameongea vizuri na ni Mjumbe wa Kamati, Mheshimiwa Abdala Mtalea amezungumza, Mheshimiwa Mndolwa ameongea katika haya katika masuala ambayo yanahusiana na migogoro hii.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kumekuwepo na migogoro ya ardhi katika maeneo mengi lakini tumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa busara zake ambazo alizo nazo. Migogoro imekua ni mingi katika sekta mbalimbali, lakini Wizara zote za kisekta zimelewka katika timu moja ambayo imepitia; na wakati Mheshimiwa Waziri anatoa hotuba yake pale alionesha kitabu kimoja kikubwa sana, kina migogoro

ya kila aina mle ndani kulingana na sekta. Iko ya matatizo ya kwenye vyanzo vya maji, iko ya Jeshi la Wananchi na wananchi wenyewe, iko ya ardhi kwa wafugaji na wa kilimo, yaani iko ya aina nyingi. Kwa hiyo wamepitia mgogoro mmoja baada ya mwingine.

Mheshimiwa Spika, na hata kama hawakufika kwenye eneo lako, maana kuna baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea kwamba hawajafikiwa kwenye maeneo yao; lakini hatua iliyochukuliwa imegusa maeneo hayo, hata kama hawakufika unaweza ukakuta kwenye kitabu kipo kwa sababu wamehusishwa Wabunge. Ninyi wenyewe mlitoa migogoro pale ndani Mheshimiwa Waziri akawa anaipokea. Wakuu wa Mikoa walishakaa nao kila mkuu wa mkoa alipewa nafasi ya kuzungumzia wakatoa ile migogoro waliyonayo; lakini pia bado wananchi kwenye programu ya FUNGUKA NA WAZIRI wametoa. Kwa hiyo yale yote ambayo wameyakusanya sasa tunaangalia namna ya kuyapatia ufumbuzi kwa sababu ni jambo ambalo ni kubwa na linaingiza sekta nyingi. Kwa hiyo niwaombe tu Waheshimiwa Wabunge tujaribu kuvumiliana katika hili ili tuweze kuona ni jinsi gani ambavyo tutaweza kulimaliza.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wameongelea suala la hati kutotoka. Kuna Mbunge mmoja amechangia kwa maandishi anasema hati hazitolewi. Kwa kweli, mimi nitashangaa kama tatizo hilo lipo kwa sababu Mheshimiwa Waziri hapa wakati anatoa hotuba yake ameonesha pia hata katika picha; zaidi ya hati 6,000 ziko kwa Dar-es-Salaam peke yake. Ukienda Mwanza kuna zaidi ya 2,000; nilikwenda pia Bagamoyo kule nikakuta kuna hati ziko pale zaidi ya 100, ziko tayari na watu hwachukui, zimeshalipiwa na hazidai. Hata hivyo kuna wengine ambaao wameshapimiwa hawataki kuchukua hati kwa sababu wanaogopa watadaiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme tu hili Waheshimiwa Wabunge kwamba kuanzia Julai 1, kama tunavyosema, yejote ambaye amepimiwa ardhi yake, amelipia upimaji halafu hataki kuchukua hati kwa sababu

tu atadaiwa kodi ya ardhi, maadam tayari ukishapanga na kupima umeshaingia kwenye *system* ambayo tayari tunajua kodi yako ni kiasi kadhaa na *invoice* unayopewa inaonesha kodi yako; tutaanza kuwadai wote, watalipa kodi ya ardhi uwe una hati hauna hati, maadam umepimiwa na tunajua wewe eneo lako ni hilo basi tutajua kwamba tutakudai. Tuwaombe sana ndugu zetu, kwa sababu tunasema ukikaa bila kuwa na hati ile ardhi yako haikusaidii. Huwezi kufanya shughuli zozote za kimaendeleo ambazo unaweza ukasema pengine uende benki upate mkopo ufanyie shughuli za kuweka dhamana mahali, hauwezi. Mimi nitoe rai tu kwa wananchi wote kwamba wafanye hiyo kazi ya kuhakikisha unakamilisha hatua nzima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna Mheshimiwa mmoja amezungumzia habari ya upimaji kwenye urasimishaji kwamba watu wanalipa halafu hawapewi hati. Pia hapa kuna mambo mawili, kuna watu wanalipia upimaji halafu wanashahau kwamba hati inakuja kwa hesabu yake tofauti. Ile ya upimaji ni tofauti na ile unayolipia kwa hati. Kwa hiyo mimi niseme tunaendelea kuwaelimisha wananchi ili kwamba unapokuwa umelipia upimaji haina maana kwamba sasa unamilikishwa lazima pia gharama za kumilikishwa utapewa kwa sababu gharama za umilikishaji zinategemeana na ukubwa wa eneo, eneo mahali ilipo na matumizi ya eneo. Kwa hiyo haziwezi kuwa sawa, haziwezi kuwa *flat rate* kama hizi ambazo tunasema ni za upimaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na wakalamikia kwamba, gharama za upimaji ni kubwa. Gharama za upimaji zinaweza kushuka kutoka hata hapo 150,000 ilipo kutegemeana tu na idadi ya viwanja na makubaliano. Tumekwenda nadhani Chemba wanadai kama 90,000/= nadhani, halafu Mkinga wana 60,000/=; kwa nini wengine wana-*charge* 60 wengine 150,000/=?

Mheshimiwa Spika, 150,000/= iliwekwa kama *bench mark*, kwamba haitakiwi izidi hapo, lakini inaweza ikashuka na kushukla kwake kunategemea pia na ile *scope* ya kazi

anayokwenda kufanya. Kwa hiyo mimi niseme kuwa hayo yanawezekana; lakini pia halmashauri zinahimizwa kutumia vifaa vya ofisi ambavyo viro vya upimaji, vinatolewa bure na hivi vinaongeza kasi, na watumishi walioko kwenye kanda wanayo nafasi ya kuja kwenye halmashauri zetu kuhakikisha kwamba wanasaidia katika zoezi la upimaji. Tukutumia fursa hiyo tuliyonayo hatutakuwa na tatizo katika hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wamezungumzia habari ya matatizo kwenye mabaraza ya ardhi na utendaji wa watumishi usioridhisha; na hii si kwenye mabaraza ya ardhi tu na katika ofisi nyingine za umma ambazo zimezungumziwa kwamba, usimamizi na utumishi wa sekta lazima uimarishwe kwa sababu, kuna watu wanakwenda ndivyo sivyo.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme tu kwamba, ikama ya watumishi kunzia Wizarani mpaka na taasisi zake bado iko chini. Wizarani tulitakiwa kuwa na watumishi 1,692 lakini tulionao ni 945 tu, maana yake tuna upungufu wa 747. Ukiena kwenye mabaraza tunao 173, lakini wanahitajika 844, tuna upungufu wa 671. Halmashauri 1,546 na walitakiwa kuwa 2,957 hivyo wana upungufu wa 1,411.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo Mheshimiwa Waziri amesema kwenye hotuba yake, tunafanya upangaji upya wa watumishi katika Halmashauri zote ili kuhakikisha kwamba tunawapanga kulingana na mahitaji, tunawapanga kulingana na taaluma zao katika maeneo ambayo wanayo. Kwa hiyo niwaombe Waheshimiwa Wabunge kwamba tuwe na subira haya yanafanyiwa kazi na tutaendelea kushirikiana pale ambapo tunahitaji kuboresha kutokana na michango mnayotupa.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, naendelea kuunga mkono hoja. Ahsante. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, Dkt. Angeline Mabula. Sasa naomba nimwite mtoa hoja, Mheshimiwa

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa William Lukvi kwa muda wa nusu saa.

### **WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA**

**MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa heshima uliyoipa Wizara yetu ya kuwa kwenye kiti kuanzia asubuhi mpaka jioni na kusimamia Mkutano huu wa leo, nakushukuru sana. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa heshima kubwa waliyotupatia, nataka kuwahakikishia kwamba tutaendeleza kasi yetu ya utendaji na ushirikiano kama tulivyoanza, Mungu atusaidie.

Mheshimiwa Spika, pia namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa nguvu anayotupa maana hii nguvu yote tunapumua, tunaishi na tunafanya kazi kutokana na msimamo na nguvu anayotupa. Kama ye ye angekuwa hatupi nguvu, tusingekuwa na nguvu, kwa hiyo sisi tunapata nguvu kutokana na kiongozi wetu kwa nguvu anayotupatia na msimamo alionao, sisi tunafuata humo humo, barabara anayopita na sisi kwa sababu ya nguvu yake na imani aliyonayo kwetu ndiyo maana na sisi mnatuona tunachacharika. Kwa hiyo, nawashukuruni sana Wabunge wote kwa shukrani, wengine hawakusema lakini wamepiga makofi, tunashukuru sana, Mungu awabariki. (*Makofi!*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana wale waliopata nafasi ya kusema leo asubuhi na mpaka jioni. Labda nianze na wachache niliowaandika hapa; Mheshimiwa Yussuf namshukuru sana kwa shukrani zake, lakini amesema machache hapa, nataka kumwambia kwamba tutayazingatia na ushauri mwangi aliosema ila nataka nimhakikishie kwamba ni kweli kama alivyosema migogoro kati ya wilaya na wilaya na vijiji na vijiji, hata maelekezo ya Mheshimiwa Rais ameagiza kwamba Viongozi wa Mikoa na Wilaya lazima washughulikie kutatua migogoro hii ya mipaka ya wilaya na wilaya na vijiji na vijiji. Sisi kama Wizara tutaendelea kusimamia jukumu hili.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Saed Kubenea nashukuru kwa ushauri wake wa *National Housing*, lakini juu

ya kiwanja hicho cha 20,000 ambacho amesema binafsi nilimwalika, aje anikumbushe kidogo ili tuweze kuona kama tunaweza tukakishughulikia, tupo hapa hapa wiki nzima ijayo tuonane hapa. Si vizuri jambo lake binafsi nikalizungumza hapa ndani, tutaonana.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Mabula kwa pongezi zake na suala la urasimishaji nakubali kwamba Nyamagana wanafanya vizuri sana na ye ye amekuwa mstari wa mbele kuhakikisha kwamba watu wake wote wanamilikisha zile *squatter*. Sasa asilimia kubwa ya wananchi wa Wilaya ya Nyamagana hawaishi kwenye *squatter*, wanaishi kwenye mazingira halali na wamepata na hati za kumiliki. Sasa hilo tatizo la milimani namwahidi nitakwenda huko milimani, tutali-*solve* huko huko milimani. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia namshukuru sana Mheshimiwa Hawa Ghasia kwa shukrani alizonipa na ushirikiano wake aliotuwezesha kupanga *master plan*ya kwanza. Kwa Awamu hii ya Tano tumepanga *master plan* kule Mtwara, lakini Mheshimiwa Hawa Ghasia alitupa ushirikiano mkubwa, tumepanga *master plan* nzuri ambayo imeshirikisha Mtwara Mjini na maeneo mengine ya Mtwara Vijijini.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Kiruswa na Mheshimiwa Julius wasiwe na wasiwasi, habari ya mipaka ya Longido, Arumeru na Monduli itashughulikiwa. Bahati nzuri aliyekuwa msimamizi wa masuala ya upimaji wa mkoa nimempandisha cheo, ndiyo Mpimaji Mkuu wa Tanzania sasa na kazi anajua, atarudi kule kwenda kuhakikisha mgogoro wa mpaka kati ya Arumeru, Monduli na Longido anahuisha pamoja na mgogoro wa kijiji cha Mheshimiwa Julius lazima ataukamilisha. Kwa hiyo, nashukuru sana asiwe na wasiwasi Daktari tutakwenda kukamilisha huu mgogoro, lakini ushauri mwingine alioutoa, tutaushughulikia. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Julius namshukuru sana, naomba tu watu wa Monduli wakamilishe, tumefuta mashamba 15, watupe mapendekezo wanataka kuyatumia

namna gani, lakini nashukuru sana kwa ushirikiano. Kila nilipokwenda Monduli nimemkuta Mheshimiwa Julius tumeshirikiana naye na nashukuru kwa ushirikiano wake na tutafuatilia kuhakikisha kwamba hii ardhi ya Jeshi la Wananchi inakuwa mali ya Jeshi na hatutoi fidia kutokana na ushauri wake kwa sababu ni maoni ya Halmashauri ya Wilaya ya Monduli siyo maoni ya Mheshimiwa Julius. Halmashauri yenyewe ilishaandika kwamba wangependa hili eneo liwe mali ya Jeshi kwa sababu wananchi hawakatazwi kuchunga ndani ya eneo la Jeshi. Kwa hiyo, nawashukuru sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Devotha Minja namshukuru kwa ushauri wake. Wakati mwingine mimi shemeji yako awe ananidokeza huko nje halafu anakuja, kwa hiyo asinichukie nikienda kule, huwa nakwenda wakati mwingine ananiambia.

Mheshimiwa Spika, Morogoro nimechukua hatua wiki iliyopita nimeamua kuwaondoa watendaji wote wa ardhi wa Mkoa wa Morogoro kwa sababu mimi ni mtu mzima, siwezi kuagiza leo, nikirudi yanafanyaika yale yale. Pamoja na uhamisho ninaofanya kwa watendaji wa sekta nzima ya ardhi, lakini wa Morogoro wote lazima watoke. Hata kama sina ushahidi kwamba hawafai, nitawatafutia kazi, siwafukuzi kazi, lakini watoke kidogo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nataka nianzishe Kanda Maalum ya Morogoro, ardhi ya Morogoro ina rutuba, iko katikati ya uzalishaji, nitaweka kanda maalum lakini pia na watendaji watakuja wapya ili tuipange na tuisimamie vizuri Morogoro. Kwa hiyo, nashukuru kwa ushauri wake Mheshimiwa Devotha Minja. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, tunafanya haya tunajituma kwa sababu Mheshimiwa Rais wetu ametutuma twende kwa watu. Kwa hiyo, siwezi kukaa ofisini, lazima niende kwa watu na nitakwenda tena Morogoro nitafunua hayo mafaili machafu, ataniona tena, kwa sababu sisi lazima tutoke

twende kwa watu. Kwa hiyo, isimkere sana akiniona nakwenda kwa watu, lazima niende.

Mheshimiwa Spika, bomoabomoa ya Ubungo – Kibamba Naibu Waziri ameshaelezea na Waziri wa Ujenzi alishawahi kueleza hapa na aliwahi kuja na hukumu kwamba wakati mwingine Serikali sikuvi hii ya Awamu ya Tano lazima isikilize na itii amri ya mahakama, kama watu wameshindwa kesi mahakamani unafanye?

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rhoda namshukuru kwa ushauri wake, lakini bado narudia kwamba, pamoja na kwamba kuna matatizo kati ya maeneo ya Jeshi na wananchi huko Mpanda, lakini mara nyingi utafiti wetu umegundua, sehemu nyingi wananchi wanafuata maeneo ya Jeshi kwa sababu hiyo hiyo kwamba maeneo ya Jeshi hayana mipaka na hayana alama zinazoonekana. Mimi nimeelekeza taasisi zote za Serikali ziweke mipaka inayooonekana, wapime maeneo yao na waweke alama zinazoonekana ili kila mwananchi ajue ni ardhi ya Serikali/taasisi inaanzia wapi kwenda wapi, lakini kutokuona alama isiwe kisingizio kwa watu kuvamia ardhi za maliasili, jeshi au mali za taasisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Rhoda kama anajua kwamba watu wamekaa kwenye ardhi ya Jeshi, awashauri tu waondoke kwa sababu sisi tusingependa wafanye hivyo, ardhi ya jeshi kwanza inakuwa ni ardhi ya akiba kwa wote, Jeshi linatunza tu ardhi, lakini kuna *installation* kwa ajili ya manufaa ya Watanzania. Kwa hiyo, najua migogoro ya mwingiliano wa Jeshi na wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika Kamati yetu na Mheshimiwa Mwinyi, Waziri wa Ulinzi amejitahidi sana kupitapita katika maeneo mbalimbali. Kule ambako Jeshi limevamia ardhi ya watu, kuna mpango wa kuwalipa fidia lakini maeneo ambayo wananchi wamevamia ardhi ya jeshi hawatalipwa fidia.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rashid nashukuru sana kwa ushauri wake, hivi viwango nilivyosema vya Sh.150,000 ni vya urasimishaji ambao wanakubaliana kwenye mitaa kila mtu anachangia ili apate hati, siyo kodi ya ardhi. Kodi ya ardhi inatozwa kulingana na thamani ya ardhi kwa kila eneo la Tanzania; kodi ya ardhi ya Dodoma haiwezi kuwa sawa na Tunduru. Kwa hiyo, Sh.150,000 ni viwango vya sasa, tulianza na Sh.300,000 kwa makampuni binafsi, sasa ni Sh.150,000 na fedha hizi zinatunzwa na Kamati za Urasimishaji za maeneo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunafanya uchunguzi kwa sababu tumegundua sehemu nyingine wanarasimisha kwa Sh.100,000 na wengine chini ya Sh.100,000. Mungu akipenda Bunge Ilijalo watagundua viwango hivi vimepungua zaidi, tunataka kufanya utafiti ili tupunguze gharama ya urasimishaji kwa wananchi. Hivi karibuni tutatangaza gharama za upimaji wa mashamba maana hawa warasimishwaji ni nyumba za mijini, tutatangaza gharama za upimaji wa mashamba ili watu wajue kwa sababu gharama za mashamba za upimaji zinapaswa kuwa ndogo zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, huu ni urasimishaji, lakini kodi ya ardhi kwa ushauri wake kama alivyotuahidi, tutafanya utaratibu ili Maafisa Ardhi waweke viwango hata huko kwenye *notes board* za Wilaya kwamba ukiwa na *square meter* kadhaa, kodi ya ardhi ni kiasi fulani, wataweka. Hii ni kwa sababu kuna kodi zinatofautiana, maeneo ya biashara ni tofauti, maeneo ya makazi tofauti na maeneo ya mashamba ni tofauti na ni kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbarouk nashukuru sana kwa ushauri wake. Maeneo ya Jeshi haya nimeyasikia, nilikwenda pale nilimjibu siku ile, bahati mbaya sikuwa nimemwona, lakini Mheshimiwa Ummy alinalika kwenda pale, alinalika nilishakwenda pale na haya maneno yote ya Tanga nilishayaskia, lakini nikipata fursa siku nyingine nitarudi. Maneno mengi tulizungumza siku ile nilipokwenda, nilipoalikwa na Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Mbunge wa

Viti Maalum, Mkoa wa Tanga, tulizungumza pale na nikafanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Tanga kuna matatizo mawili, hayo anayozungumza na *airport*. Jambo la *airport* linashughulikiwa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa kwa sababu ipo tabia na iko fununu kwamba yupo Mwenyekiti wa Mtaa pale aliuza yale maeneo kwa watu, kwa hiyo, hatuwezi kuingia kichwa kichwa kulipa fidia kwa watu wakati tunajua kuna mtu nyarubanja pale alijifanya ni ardhi yake akauzuauza. Kwa hiyo, uchunguzi unafanywa na Kamati ya Ulinzi na Usalama kwanza ya Mkoa ili wahakikishe kwamba wale waliojenga ni wananchi ndiyo, lakini walipataje. Hatuwezi kuwalipa fidia wao wakati wao kuna mtu mwингine alinufaika kwa njia haramu. Kwa hiyo Kamati ya Ulinzi na Usalama inashughulikia na mengine haya tutakuja kushughulikia pamoja na hilo eneo la Ramsim.

Mheshimiwa Spika, shamba la Ramsim lote ni la Umoja wa Vijana. Nilikwenda kwenye mkutano shida yao ilikuwa wanataka kujua gharama tu za urasimishaji na nini, lakini wananchi walikiri kwamba lile ni shamba la Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Susan Kiwanga nashukuru sana kwa kutufariji kwa kufiwa kwa hawa vijana, lakini nataka nimuhakikishie kwamba nillichokisema mimi ni kwamba, kuna tofauti katika ya mipango miji, nimetumia sheria inayonipa madaraka ya kupandisha hadhi maeneo ya vijiji kuwa ya mipango yaani yapangwe kimji, lakini sina mamlaka ya kutangaza Mamlaka za Miji. Kwa hiyo, asishangae kuona kwamba Mlimba kuna vijiji vimetangazwa vipangwe kimji na watu wapewe hatimiliki lakini mamlaka ni ya kijiji.

Mheshimiwa Spika, hata maeneo yote niliyatangaza humo 455 kwenye mikoa yetu, mamlaka bado ni za vijiji ila vijiji vyenyewe vimepata hadhi vinapangwa kimji, yaani upangaji wake ni kama upangaji wa mjini siyo vijijini na wamiliki wa maeneo hayo tunawapa hatimiliki za miaka 99 siyo hati za kimila. Kwa hiyo, mwenye mamlaka ya kutoa

utawala au mamlaka ya kujitawala katika miji ni TAMISEMI lakini sisi tunatoa hadhi ya upangaji wa ardhi. Kwa hiyo, sisi tumetoa upangaji wa ardhi vijiji 455 tumevipandisha hadhi, mamlaka ni vijiji lakini ardhi inapangwa kimji.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine ya *Stiegler's* tutaoa taarifa baadaye maana haya maeneo anayosema Mheshimiwa Susan ndiyo zile *Ramsar site* ulizosema juzi. Hii miradi tumeshirikiana na Wizara ya TAMISEMI pamoja na Halmashauri zote, ni kweli waliwaondoa watu ambao walikuwa wamevamia kwenye maeneo oevu, maeneo ya TAMISEMI lakini mradi wangu huu unashughulika sana vilevile na kuondoa migogoro. Si kweli kwamba wakifika migogoro wanaiacha, hapana, Mheshimiwa Susan atakuwa hawatendei haki, wamejitätahidi sana kusuluhiha migogoro labda huo mmoja anaoujua, lakini sehemu kubwa tumetatuwa migogoro ya mipaka ya vijiji, hata mlgogoro ya mashamba kwa sababu tusingeweza kuwapimia watu hati zao bila kutatua migogoro. Kwa hiyo, sehemu nyingi tumeweza kutoa sasa hati 200,000, tusingeweza kutoa hati za kimila za mashamba 200,000 kweli bila kuwa na migogoro ya mipaka, kwa hiyo tumejitätahidi sana. Akikaa nao aendelee kuwapongeza, asiwavunje moyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Agnes namshukuru sana na kwa kweli mipaka ya hifadhi na ndiyo maana nimezungumza kwenye mambo ambayo yalikuwa yana hitilafu katika Wilaya zile za Tarime, Serengeti na Bunda, ni ule mpango wa *buffer zone* ambao kwenye Kamati yetu tumeuangalia na nafikiri wakati ukifika majibu yaktoka tutatoa taarifa, lakini nashukuru kwamba kweli migogoro imekwisha na leo tunapanga matumizi bora ya ardhi Bunda, Serengeti na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Serukamba kwa pongezi zake na ushauri wake mkubwa kuhusu *National Housing* tutauzingatia juu ya namna ya kujenga nyumba za kupangisha na za kuuza na masuala yote ya *micro financing*.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rose Kamil tutafuutilia hayo mashamba, lakini ufutaji wa mashamba yasijoendelezwa ni kazi ya Halmashauri, ndiyo inaanzaisha hiyo *process*. Fursa ya kwanza imetolewa na Halmashauri yenye we kufanya ukaguzi juu ya mashamba yaliyomilikishwa katika Halmashauri kubaini kama yamekiuka utaratibu, watu hawalipi kodi na hayaendelezwi.

Mheshimiwa Spika, pale kwenye Halmashauri ya Hanang tumewapelekea mtu anaitwa Afisa Ardhi Mteule, yule ni Kamishna pale ndiye mwenye jukumu pekee la kutoa *notice* kwa yule mwenye shamba ili aweze kujieleza hatimaye lifutwe, asipotekeleza yeye, wasipotupa jicho lao kwanza kule, mimi siwezi kuchukua hatua. Kwa hiyo, ningependa arudi na maelekezo yangu kwa Afisa Ardhi Mteule kwamba yeye amesema Bungeni, lakini nimewatupia mpira halmashauri, amwambie Mkurugenzi wayakague, wamtume Afisa Ardhi Mteule achukue hatua, hizo hatua wakichukua ndiyo zitakuja kwangu, nampelekea Mheshimiwa Rais anayafanya hayo mambo kwa mujibu wa sheria. Kwa hiyo, ningependa mambo hayo kidogo tuanzie kule Wilayani, yakifika kwangu inakuwa rahisi, mashamba haya yote aliyoorodhesha waende wakafanye ukaguzi watuandikie kisheria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Mnzava, nitapita kwenda Tanga hivi karibuni kuangalia hayo mashamba aliyoniambia. Namshukuru sana Mheshimiwa Mnzava, lazima tushirikiane. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Selasini kwa pongezi zake, tutaendelea kushirikiana. Hana matatizo sana kule kwake lakini tutakwenda kuangalia hayo matatizo. Napokea ushauri juu ya Wakala wa Nyumba ila kwa bahati mbaya mimi na Wizara yangu tumeamua kwamba tutaendelea kufanya kazi kidogo za uwakala kupitia Shirika la Nyumba kwa sababu Shirika la Nyumba nalo limeshafanya utafiti na kujua aina ya nyumba zinazoweza kujengwa vijiji na nini, lakini ile taasisi tunataka tuipeleke

Chuo Kikuu itafanya vizuri zaidi kuliko ikibaki kwetu. Nakubali kwamba *standard* za ujenzi ndivyo zinavyokuwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunaposema tunatoa kibali cha ujenzi nyumba yoyote ya mijini tunakupa kibali cha ujenzi lakini tunakutajia na aina ya nyumba, tunajua kabisa. Tunapopanga miji na *master plan* inajulikana kabisa eneo hili unatakiwa ujenge nyumba ya ghorofa moja, eneo hili nyumba ya ghorofa mbili; eneo liliopangwa kujengwa nyumba ya ghorofa moja huwezi kujenga nyumba ya ghorofa mbili hata kama una hela, hutapata kibali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni mahali ambapo wale watoa vibali wamelegea, ndiyo maana hawazingatii *standards*, lakini kwa mujibu wa ujenzi wa nyumba mijini unaenda kwa *standards* na ndiyo maana hapa Dodoma. Mjini ukijenga sasa hivi unaambiwa na batii weka rangi fulani, hizo ni *standards* za wapangaji miji lazima na *CDA* zamani walikuwa unataka kujenga mahali, ramani hii hapa nenda kajenge. Kwa hiyo, tutaendelea kuelimishana juu ya ushauri wake kwa sababu ni muhimu sana huu ushauri katika upangaji wa miji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Pallangyo karibu sana, namkaribisha sana na nampongeza sana kwa ushindi, tutafanya kazi pamoja. Tulikwenda Arumeru pale bila shaka nimemwambia juzi, yapo mashamba ambayo tumeyafuta pale kwa niaba ya wananchi, tena moja lilikuwa la Chama cha Ushirika, walikuwa hawafanyi nalo kazi, wakataka wananchi wakalime kwenye mawe halafu huku wakodishe, tumelifuta. Hata hivyo, bado wana deni hawajaniambia utaratibu wa namna ya kulitumia. Kwa hiyo, Mheshimiwa Pallangyo tunamkaribisha sana, nampa fursa kama ana mengine pengine kwa sababu ya dakika tano nipo hapa tuzungumze ili tushirikiane mambo yaende haraka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nirudie hili la watendaji wa Serikali, ni kweli nimesema asubuhi kwamba watendaji wa Serikali ni wachache lakini pia tumegundua hawakupangwa vizuri, kwa hiyo tunarudia kuwapanga upya. Kwa uchache huo huo

nataka kuahidi maeneo ambapo kulikuwa hakuna watendaji wa Serikali wa sekta ya ardhi watapatikana. Tunataka hawa watendaji watumike kama wasimamizi kwa sababu sasa kazi nydingi za sekta ya ardhi za upangaji na upimaji makampuni binafsi wanatusaidia lakini hawawezi kufanya kazi hizi ndani ya Wilaya kama hatuna mtu wa sekta ya ardhi pale wilayani. Kwa hiyo, tutawapanga vizuri na kuhakikisha kwamba wanaenea kila mahali.

Mheshimiwa Spika, masuala mengine ya *RERA* ambayo Msemaji wa Upinzani amezungumza *Real Estate Regulatory Authority*, najua kila mwaka huwa wanazungumza. Sheria hii sisi *draft* tumeshamaliza, tunakamilisha utaratibu wa Serikali, naamini ipo siku itaingia hapa. Sheria hii tunataka itusaidie kusimamia haki za wapangaji, haki za Serikali kwa kodi, lakini pia kusimamia sekta yenye ya ardhi kwa sababu tumegundua katika sekta ya ardhi inatumika sana na baadhi ya watu kwa ajili ya kutakasa fedha na kuingiza fedha haramu kwenye ardhi. Kwa hiyo, tunaifanya kazi hii sheria na Mungu akipenda itafika hapa.

Mheshimiwa Spika, suala la ulipaji wa kodi nataka kusisitiza tena, kila mtu ambaye anadaiwa kodi, wakiangalia kwenye kile kitabu mbele ya jalada safari hii sikuweka sura yangu, nimeweka maneno fulani. Ukiangalia yale yamewakumbusha Waheshimiwa Wabunge ukitaka kujua deni lako, angalia pale, ukitaka kulipa kodi ya ardhi angalia juu ya kitabu nimefanya makusudi. Kwa hiyo, waangalie huo mfano kila mtu ajue, kama anadaiwa tafadhali asisubiri nimitangaze tarehe 30 Juni kwenye gazeti maana majina yote ya wanaodaiwa nitawaabisha mwisho wa mwezi wa sita. Kwa hiyo, naomba waangalie hilo jedwali nimewatumia ili uangalie kama unadaiwa, mimi nisingefurahi sana Waheshimiwa Wabunge niwatangaze kwamba wanadaiwa kodi ya ardhi maana sheria zenyewe wametunga wenyewe.

Mheshimiwa Spika, nyuma ya jalada la kitabu nimeonesha aina mpya ya hati tunayotoa ya kielektroniki ya karatasi moja. Halafu ndani ya jalada la nyuma

nimewaonesha leseni ya makazi ya elektroniki moja ambayo tunatoa na tunataka leseni za makazi zisambae baada ya bajeti hii, mpango huu uingle mikoa yote kwa sababu ni jambo rahisi. Watanzania vijana wataalam wa Wizara yangu wametengeneza teknolojia moja, wametengeneza *app* moja ambayo tutaambukiza katika Halmashauri zote halafu watu wachangie shilingi 5,000 wapate leseni. Ni kama hati lakini ya miaka mitano, itawasaidia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo katika kitabu hicho kuna alama ambazo nimezitumia safari hii zitawasaidia Waheshimiwa Wabunge, hasa hiyo iliyopo ukurasa wa kwanza, ninaomba kila mtu ajaribu, utumbukize *plot numbers* zake zile halafu itamjulisha anadaiwa kiasi gani ili mlipe na Watanzania wote nawaomba walipe kodi ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, mwisho wa mwezi wa sita nimeagiza mabaraza yote ya ardhi, hakuna kesi nyingine isipokuwa kuwaswaga mbele ya mabaraza yale watu ambaao hawajalipa kodi ya ardhi; na Serikali, mimi Waziri asiniandikie mtu hata mmoja akiomba nimpunguzie *penalty*, hapana, sina madaraka hayo. Ukitaka sasa upunguziwe *penalty*, lipa kabda ya mwezi wa sita, ukiruka mwezi wa sita *penalty* yako iliyopo sasa inaruka kwa asilimia 300.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba Watanzania wote kuititia tangazo hili angalieni mnadaiwa kiasi gani, kila mtu anayemiliki ardhi kwa hati ahakikishe kwamba analipa kodi ya ardhi ya kila mwaka. Wenye leseni ya makazi wanalipa, wenye hatimiliki wanalipa, isipokuwa wale wananchi maskini, Serikali ya Awamu ya Tano imewaonea huruma, wale wanaomiliki kwa hati za kimila, wale hawalipi kodi ya ardhi, wale wenye vishamba vya vijiji kule wenye hati za kimila Serikali imewasamehe, hawalipi kodi za ardhi. Lakini wale wanaomiliki hatimiliki, iwe ya shamba, iwe ni kiwanja mjini au shamba la mjini, lazima walipe kodi.

Mheshimiwa Spika, lakini wale wote wanaomiliki kishamba au nyumba ambayo ina kiwanja kilichopimwa mijini lazima aingie kwenye *processya* urasimishaji apate hati

ya muda mrefu, ali pe kodi au aingie kwenye leseni za makazi ali pe kodi. Hata kama una kishamba mjini, lazima upime uchukue leseni ya makazi tukutoze hela.

Mheshimiwa Spika, kuna watu wana maeneo makubwa mjini hawataki kuyapima kwa sababu wanajua mwisho wake watalipa kodi kila mwaka lakini wakivamiwa kidogo wako kwa Waziri. Tunataka mtu mwenye shamba mjini, mwenye kiwanja mjini, mwenye nyumba mjini, hana hati achukue hati kupitia urasimishaji au leseni ya makazi ambayo gherama yake ni shilingi 5,000, shilingi 4,000 zinakwenda Halmashauri kwa kazi ya kutayarisha leseni yenye, shilingi 300 anachukua Mwenyekiti atakayemsindikiza yule kijana anayekwenda na simu kupima zile nyumba na shilingi 700 ni yule kijana mwenye simu anayekwenda kupima. Kila nyumba yule kijana atapata shilingi 700.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hii inatengeneza hata ajira kwa vijana wetu wa Wilayani kwenu; ni simu tu. Sisi tutamuwekea kifaa mule kwenye simu, akipita kwenye nyumba, uzoefu wetu unaonesha kijana anaweza kupima nyuma 20 kwa siku moja, Dar es Salaam wameweza, kwa hiyo nyumba 20 kwa siku moja na leseni zitatoka. Kwa hiyo nyumba 20 tunapata shilingi 5,000, shilingi 4,000 zinaingia kwenye Halmashauri, shilingi 300 anapewa Mwenyekiti wa Mtaa anayemtembeza huyu kijana anayepima, na 700 anapata yule kijana mwenyewe, kwa hiyo hii ni ajira. Mtakuta vijana wengi hata waliosomea masomo mbalimbali huko wenye simu za aina hii wanaweza kufanya hiyo kazi na kila siku akawa anaingiza mfukoni hata shilingi 10,000. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tuchangamkie fursa hii, nataka baada ya zoezi hili kufanikiwa Mkoa wa Dar es Salaam tutahakikisha sasa tunakwenda mikoa yote ili kila mtu awe na hatimiliki au leseni ya miaka mitano. Lakini tungependa kila Mtanzania awe na hatimiliki ya ardhi yake ili aweze kulipia kodi. Kwa hiyo ni suala la msingi na la lazima.

Mheshimiwa Spika, Naibu Waziri amesema hapa, watu wote ambao tayari tumeshawapimia halafu wamepewa *invoice* wanakaa nayo miaka mitatu, tunawatoza kodi kuanzia mwaka huu lazima walipe. Haiwezekani tumeshakupimia tumekupa na *invoice* hutaki kuchukua hati eti kwa sababu utalipa kodi, kwa hiyo lazima wote tulipe kodi.

Mheshimiwa Spika, narudia tena kukushukuru wewe, nawashukuru Wajumbe wote, Wabunge wa Bunge hili, kwa heshima mliyotupa, Mungu awabariki sana mliochangia, mlioweza kuchangia kwa kusema nawashukuru sana, mliochangia kwa maandishi nawashukuru sana, Mungu awabariki sana. Sisi majibu yetu yatakuja kwa maandishi lakini wengine nitawafuata, ambao kuna hoja ambazo zinahitaji ufanuzi zaidi, nimeshachukua majina yenu, nitawafuata tutakaa hapa tutaelewana zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini msisite kama nilivyosema, kama kuna wengine hawakupata nafasi ya kuandika na kusema, tupo na Mheshimiwa Spika ametupa chumba namba 11 hapa. Ukileta watu wako wawili kutoka Kasulu walete hapa, tutakuhudumia hapa hapa; ukileta watu wako watatu kutoka wapi, tutakuhudumia hapa hapa, mpaka Bunge liishe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ndugu zangu, kwa hiyo sisi tunafikiri kwamba tuna wajibu mkubwa wa kuwatumikia ninyi, lakini kuwatumikia na wananchi wote wa Tanzania. Hii ndio kazi tuliyopewa na Dkt. John Pombe Magufuli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Hoja imetolewa na imeungwa mkono, tunakushukuru sana kwa maelezo hayo.

Kwa kweli yaani kwa maelezo haya mtu akishika shilingi sasa ntashangaa. Itakuwa shilingi ya nini sasa maana ushauri wenu mwingi sana umechukuliwa. Kwanza kazi waliyofanya Mheshimiwa Waziri na Naibu kuzunguka nchi nzima huko kila mahali, yataka moyo ndugu zangu, siyo rahisi. Kuna wengine majimbo yenu tu hamjafika hata robo, sasa wana majimbo na bado wamezunguka kwetu kote, ni kazi kubwa sana inahitaji kuungwa mkono. (*Makofi*)

Lakini pia kwa kuchukua maoni mengi sana ya Waheshimiwa Wabunge, wala hawajabishana na ninyi, wamechukua karibu kila kitu. Lakini pia wametoa ahadi kwamba wapo hata kama kuna maeneo yana shida ya wapigakura walete, na kadhalika. Kwa hiyo mimi naamini muda uliobakia huu unatutosha kabisa kufanya kazi yetu kwa majina niliyonayo. (*Makofi*)

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 48 – Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

Kif. 1001 – *Administration and HR Mgnt.....Sh. 7,850,626,183*

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni swali dogo tu fupi. Namshukuru Mheshimiwa Selasini amelifafanua vizuri. Ninachohitaji Mheshimiwa Waziri afafanue na atuweke wazi, nimezungumza tu ni masuala mawili; kwamba hatua zinazochukuliwa za kubatilisha hatimiliki za mashamba sipingani nalo kabisa, kambi haipingani nalo na inali-support, especially kwa waliolaza mashamba. Suala tunalotaka kuzungumza ni kwamba Urais ni taasisi, si kama watu wanavyotaka kujiaminisha kwamba ni Dkt. John Magufuli, Urais ni taasisi. Kitu kinapokuwa taasisi

kuna baadhi ya watu wanaweza nyuma ya taasisi hiyo wakafanya makosa na wakavurunda kiasi kwamba yule mwenye mamlaka ya mwisho akakosea, kama ambavyo imekwa inajitokeza kwamba hata kwenye uteuzi Rais anaweza akateua mtu kumbe akaja kugundua ameingizwa chaka yule mtu hafai na akatengua, Rais wetu amekuwa *very transparent.* (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho ninahitaji kufahamu ni taratibu zinazotumika ili ifikie hatua ya *reallocation*. Lakini pia *reallocation* ya ile ardhi ambayo tayari inakuwa imebatilishwa utaratibu ni upi? Kwa sababu wanakijiji wanakuwa wachache labda zimebaki ekari 50,000, hizo utaratibu wake zinakwenda vipi? *Full stop.* Nisipotosheka na majibu ntaomba Wajumbe wenzangu waweze kuniunga mkono katika kujenga hoja ili majibu sahihi yaweze kupatikana, ahsante. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufanuzi, tafadhali.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa maelezo ya ndugu yangu, Mheshimiwa Lwakatare. Mheshimiwa Lwakatare ni jamaa yangu sana, nilipoanza ukuu wa wilaya mwaka 1994 huyu ndiye aliyenipokea, alikuwa afisa utumishi kule Bukoba, kwa hiyo tunajuana sana, ni rafiki yangu sana; na tumekuwa tunafanya kazi siku zote, ukiacha humu ndani lakini tumekuwa tunashirikiana hata kwa kazi hii. Ni miongoni mwa mawaziri vivuli wachache ambao ni waungwana, kwa hiyo naamini hata hili anauliza kwa nia njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la utwaaji wa mashamba yasiyoendelezwa linatawaliwa na sheria. Nilikuwa namwambia Mheshimiwa Rose Kamili kwamba kwa kweli wanaoanzisha jambo hili ni wilaya. Mkikuta shamba ambalo halijaendelezwa, halijalipiwa kodi, uko utaratibu, na sheria imeweka utaratibu, kwamba tunatarajia mwenye shamba kubwa aliyechukua awe ameliendeleza, angalau kila mwaka moja ya nane ya shamba lake, sheria imewekwa kuna jedwali kwenye sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mkiona ninyi wilaya kupitia afisa ardhi mteule huyu mtu haendelezi na halipi kodi, basi mnamtumia afisa ardhi mteule anampa *warning* ambayo inadumu kwa siku 30, kama onyo. Hakutekeleza mnampa ilani ambayo ni siku 90; ametoa maelezo hayakutolesheleza mnaleta kwa kamishna analeta kwangu napeleka kwa Mheshimiwa Rais, huo ndio utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama huyu mtu akiwa amefutiwa haridhiki, sheria inataka aende mahakamani. Na wapo wengi ambao wamekwenda mahakamani, uamuzi wa Mheshimiwa Rais umebatilishwa, kwa hiyo siyo jambo geni kwa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi namshauri mawili; moja, huyo mtu ambaye; mimi simjui; huyo ambaye anasema amenewa upo utaratibu wa kumuwezesha kwenda mahakamani akadai haki yake. Lakini pili, ye ye mwenyewe basi ajitokeze aseme; kama anaamini kwamba Mheshimiwa Rais ndiye aliyefanya jambo hilo si hata ajaribu kumuandikia aone kama atamjibu. Wako watu ambao hawajui kuzisoma hizi sheria, huwa wanajaribu wanaandika hata kwa Mheshimiwa Rais kama anaona labda mlolongo huu wa mahakama ni mgumu. Lakini mlolongo wa mahakama ndio wa kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lwakatare, na ninataka kukuhakikishia; akifuata utaratibu huu haki inatendeka. Ninao uzoefu na ninao ushahidi unaoonesha kwamba wapo watu ambao wamepitia mahakama, si awamu hii lakini hata awamu zilizopita, ambao amri hii ya ubatilisho imesimamishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo hili msituangalie sisi, hata kwa *level* yangu ya Waziri wala Mheshimiwa Rais. Jambo hili linaanzia wilayani kwenyewe, siyo kwetu. Hakuna Waziri mwenye mamlaka ya kufuta bila kuwa na *revocation* iliyoandikwa na afisa ardhi mteule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na Mheshimiwa Mnzava yule ni mwanasheria, siku moja alitusimulia hapa alipokuwa anazungumzia mashamba ya Korogwe. Utaratibu unaanzia wilayani, hata kama nikiliona mimi kwa macho Mheshimiwa Lwakatare, sitachukua hatua mpaka nimiradi afisa wako wa ardhi, huo ndio utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yakishafutwa sasa tunarudisha wilayani mnatupa mapendekezo ninyi mliaoamua kufuta mnataka myatumie namna gani? Sisi mkishatuletea mapendekezo tunaangalia halafu tunawasaidia kutekeleza. Ardhi ili Lukuvi hawezi kuja kuamua ardhi ya Bukoba aifanye nini, lazima ninyi halmashauri mliyoionna na mnayoohitaji mtatoa mapendekezo kwa Wizara yangu nasi tutabariki mapendekezo yenu, ndiyo utaratibu ambao tunatumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo huo ndiyo utaratibu, siyo kwamba tunafuta kwa ajili yetu. Wakati mwingine mashamba yale mnayapanga wenyewe kama maeneo ya viwanda, mnapanga wenyewe kama *land bank* kule wilayani au mnapanga kwa ajili ya makazi. Pengine kuna wannachi wamevamia mnataka tuwahalalishe, ndivyo tunachofanya. Korogwe hivi sasa tunafanya yale mashamba yaliyofungwa juzi, kuna wannachi wamevamia pale ekari 300 tunawapangia mule ndani, hatuwezi kuwavunja.

Halafu hata yule mwenyewe aliyefutiwa si kwamba ananyang'anywa kila kitu; mtu ye yeyote aliyefutiwa ardhi kwa *revocation* maendelezo yake yote analipwa fidia stahili. Kama ana nyumba, kisima, mbuzi, miti, analipwa fidia, kwamba ukifutiwa na Mheshimiwa Rais kwa amri ile, kwa sheria ile ya *revocation* unafutiwa ardhi tu, lakini maendelezo yote unapewa fidia, kwa hiyo huo ndiyo utaratibu.

**MWENYEKITI:** Ni jambo shirikishi sana, nafikiri mmeliona; shirikishi kwenda juu mpaka inafutwa, shirikishi kuteremka chini mpaka nini kifanyike. Ndiyo Mheshimiwa Lwakatare, bado una nafasi.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nishukuru kwa hoja niliyoijenga hapa, naamini watu wengi wamenufaika, wamepata *lecture* kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, ingawa katika majibu yake ameacha kakipengele kadogo tu na ambako nitaomba Waheshimiwa Wajumbe waniunge mkono katika kuchangia hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameeleza vizuri hati inafutwa na mtu anafidiwa. Na nimemwambia, je, umeshafidia? Umebatilisha, ile *reallocation* ambayo tumekuwa tunasikia mara wanakijiji wamechukua eka 50 kwenye 100,000, ile 50,000 inayobaki *transparency* yake na namna ya kuipata na kuigawa hajaieleza, malizia hapo tumalize biashara.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeombwa kwamba...

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** ahaa, unataka wachangie?

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio; na kutokana na hiyo, hako kakipengele kalikobaki ndio maana nikaomba nijenge hoja watu waniunge mkono ili waweze kuchangia.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Sasa mtakuwa mnachangia nini rafiki zangu? Haya Katibu andikeni majina ya wachangiaji, na huku pia kama wapo.

Waheshimiwa Wanakamati wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii, kama hivi vitu mnavijua ndio wakati wenu wa kutueleza vinginevyo maana yake kwenye Kamati hiyo hamuhudhuri vikao. (*Kicheko*)

Haya, tuenze na Devota, kama ulielewa; dakika mbili, tatu; kwa hiyo mwende moja kwa moja.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Lwakatare kuhusu namna hati hizi zinavyofutwa. Yapo maeneo, tunaelewa kabisa ardhi ina *direct impact* kwa wananchi...

**MWENYEKITI:** Hoja yake siyo zinavyofutwa tena...

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Hoja yake ni kwamba...

**MWENYEKITI:** Ndiyo maana nikasema mnaposimama ni vizuri muwe mmemsikiliza. Yaani kama nimemuelewa vizuri, kwenye kufuta, kwenye kufanya nini, kote ameridhika. Yeye *issue* yake ni ile ardhi inapoanza kugawanywa nyingine inaeleweka kipande kingine haieleweki vizuri, kitu kama hicho, ndiyo hoja yake. Kwa hiyo tusitoke nje tukaanza tena kujadili mambo ambayo hayapo mezani.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lipo kwenye *transparency*, wakati ardhi inavyofutwa, kibali cha ardhi kinapofutwa, sasa utoaji wa ardhi...

**MWENYEKITI:** Hapana, ni *reallocation*, kwenye *reallocation*. Kama hujalewa basi nitakukalisha chini.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, najenga hoja.

**MWENYEKITI:** Hapana, yaani kwenye kugawa pale; labda Mheshimiwa Lwakatare hebu simama tena bwana utuwekee vizuri; hoja ni nini, eleza tena.

Si nia yangu kuficha chochote, nia yangu tuelewane tunajadili nini na tunaji-*focus* hapo.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umeiweka vizuri; kwamba hoja hapa ambayo inapaswa kujadiliwa ni kwamba zimeshafutwa kama ulivyooleza hati imefutwa na huyo bwana amefidiwa, sasa katika eka 100,000, 50,000 wamepewa wanakijiji waliokuwa pale kwa utaratibu ambao utawekwa, 50,000 bado zina-*lie idle*. Ninachotaka kufahamu, na nimeomba wenzangu waweze kuchangia kuniunga mkono, hii 50,000 *mechanism* yake katika hali ya *transparency*, ikoje? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ndiyo maana nikasema mnajadili nini? Kabla ya hapo Waziri alikuwa amesema kwamba mgawanyo wa ardhi hiyo, mapendekezo yake yanatoka kwenu halmashauri. Sasa sijui kama halmashauri itakuwa imetoa mapendekezo ya 50 halafu 50 ikaacha, sasa ikiacha basi Serikali itaona nini cha kufanya, na kadhalika. Lakini kama kuna mjadala tunaendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Devotha tumnavuka, Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Lwakatare. Nitatoa mfano mdogo; Sumaye alinyang'anywa shamba, alivyonyang'anywa shamba kwa mchakato ambao pengine ulikuwa wazi au haukuwa wazi...

**MWENYEKITI:** Ngoja kidogo Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** ...kwa mujibu wa alichooangea. Natoa mfano.

**MWENYEKITI:** Kidogo tu, sekunde tu Mheshimiwa Anatropia, utaongea, sekunde tu.

Nataka kujua kutoka hukohuko kwenu; hili jambo liko mahakamani au haliko mahakamani? Hilo tu. Utatoaji mfano kitu cha mahakamani? Kama liko mahakamani *please*.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa, sitaliongelea.

**MWENYEKITI:** Siyo kwa ajili yangu, unafahamu utaratibu.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa, sitaliongelea.

**MWENYEKITI:** *Yeah*, toa mfano mwingine.

**MHE. ANATROPIA L. THEONIST:** Sawa. Maeneo yale ambayo Serikali imeyabadilisha matumizi, lakini mnakuja kuambiwa kwamba wananchi nendeni mkachukue hayo maeneo lakini katika utaratibu ambao haujulikani, imefikia maamuzi gani mpaka wananchi tena siyo wanagawiwa, wanaenda kuvamiwa wanagawa vipande vipande, sasa hapo ndiyo tunajiuliza...

**MWENYEKITI:** Nipe mfano wapi limefanyika hilo?

**MHE. ANATROPIA L. THEONIST:** Halmashauri ya Ubungo.

**MWENYEKITI:** Kuna shamba lilifanywa hivyo halafu wakavamia?

**MHE. ANATROPIA L. THEONIST:** Hilo hilo la Sumaye.

**MWENYEKITI:** Anatropia ukinichezea, *no no please*, ukinichezea ndiyo hapo huwa nafika mahali kidogo hatuelewani. Ni ustaarabu kokote duniani, jambo likishakuwa liko mahakamani, tunakiachia hicho chombo cha wenzetu, ndiyo ustaarabu wenywewe, sasa tutafanyaje na aliyeenda mahakamani si yeye huyo huyo unayemsema? Tunaacha ile iende, kwa hiyo nchi nzima mfano ndiyo hilo shamba moja tu?

Kama ni hivyo, basi hiyo ni *non-issue* katika sayansi kama huna *sample* ya kutosha, maana yake hakuna *issue*.

Vinginevyo ungetoa mifano mingi tu hivi hivi hili nalikataa kwa sababu ni jambo la mahakamani, tumbheshimu aliyeenda mahakamani na inawezekana, nasikia ni yeye, sidhani kama ameshtakiwa na Serikali, sasa kama kaenda yeye tumwachie mahakama itamaliza. Ni utaratibu wa kawaida na kanuni zetu wala si jambo geni hili.

Mheshimiwa Kubenea.

**MHE. SAED A. KUBNEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami hoja yangu ilikuwa hiyo hiyo ya Ubungo na kwa kuwa kama Mbunge wa Ubungo kwamba halmashauri ya Manispaa ya Ubungo baada ya eneo fulani hivi kutokuwa...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, nadhani tumpe Waziri halafu tumrudishie mtoa hoja ili afunge tu hoja yake kwa kweli. Mheshimiwa Waziri, hapana bado Lwakatare, umsikilize Waziri kwanza halafu ndiyo utafunga hoja yako

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuwahakikishia kwamba hakuna mtu anayeonewa katika zoezi zima la ubatilishaji wa mashamba. Yako mashamba ambayo wilaya wameamua, Kamishna ameamua, mimi nimeamua, yameenda Ofisi ya Rais yamegonga mwamba kwa sababu naye ana *Legal Office* inayomshauri, naye ana utaratibu siyo kwamba anaamua tu mara moja anatekeleza yale ninayoandika mimi. Kwa hiyo ndugu zangu tufuate utaratibu, kama kuna mtu amekosewa ni mahakamani tu ili haki yake itendeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la Mheshimiwa Lwakatare tumekuwa shirikishi sana, sana, leo kwa mfano, Mheshimiwa Devota angekuwa wa kwanza kuniunga mkono, yako mashamba yamefutwa Kilosa yeye anajua na Mvomero mengi, watu wao kule walikuwa wanataka kugawana. Wiki iliyopita anajua nimechukua timu ya Makamishna wasaidizi 15 nimewaacha Mkoa wa Morogoro ili washirikiane na viongozi namna ya kupanga yale, wale

maskini waliokuwa kwenye mashamba wamekosa haki yao, kwa sababu wenyewe kwa wenyewe wameshindwana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo uko utaratibu shirikishi, ikishindikana Mheshimiwa Lwakatare na sisi tuna macho tunaona huwa tunaingilia. Kama tukiona kwamba kuna njia ambayo si sahihi kama ya Kilosa, wako watu wanajimegea megea, sisi wenyewe tunakwenda huko tunawasoma na tunawahakiki wale watu maskini waliopo pale wanaostahili kupata ile ardhi tunawagawia ile ardhi. Kama ikibaki nyininge tunaweka *land bank* huo ndiyo utaratibu. Hata hivyo, ni kama alivyosema Mheshimiwa Mwenyekiti ni shirikishi sana sana, ugawaji wa ardhi kwa sababu hakuna ardhi inayofutwa bila kuwa na sababu, kwa hiyo sisi tunafuata ile sababu, lazima na wenyewe wafaidike.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lwakatare tafadhali

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Waziri na pia kupitia meza yako kwa sababu mwanzo kabisa ulivyoingilia kati ulieleza *one of the approach au mechanism* ambayo inapaswa kutumika kwamba ni shirikishi na ni kuanzia kule chini. Naamini kuna watu walikuwa hawajui kama hilo suala *approach* yake ni hiyo na Waziri amejazilizia kwamba kuna utaratibu na utaratibu ni shirikishi. Hii maana yake kuanzia leo kupitia Bunge hili tunaanza kufahamu kwamba wale wanaojitutumuaga wanaambia wananchi hebu kila mmoja akajigawie huko, kila mmoja akakamate kipande chake, maana yake hao ndiyo watapambana na mabaunsa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa ufanuzi wake. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Lwakatare na nyongeza tu ni kwamba mambo haya siyo kwamba ni mepesi hivyo, hata wilaya wakambiwa haya jamani sasa shamba hilo, hekta hizi wagawieni wananchi, nyinyi wote mnajua, watu wataanza kuwapa shangazi zao, wajomba zao, nani nani zao, hivi, jamani mambo haya

hatuyajui! Kwa hiyo tatizo siyo Wizara au Serikali Kuu au yaani haya mambo yanataka usimamizi wa karibu na watu waache *grid*, ulafi, utaona majina pale nini kumbe ni, kwani viwanja vinyavopimwa mijini huko si kila siku tunasema sijui mabwana ardhi wamejigawia, sijui nani nani wamejigawia, inakujaje hii, ametumwa na Serikali afanye hivyo?

Kwa hiyo ni tabia fulani ambayo ni lazima iendelee kukemewa na Serikali iendelee kuwa na macho zaidi kwenye *process*, lakini *process* yenye ukiitazama ni *process* yenye afya, ni *process* nzuri tu na Waziri bado yupo kama tuna ushauri, tunaweza kumshauri Waziri. Waziri Kivuli pia kwa hayo mengine kama una ya kuzungumza si Waziri kasema yupo, mnanong'ona kule, hayo mengine, mnanong'ona kule, mnaelewana kule, lakini ukilileta hapa kwa Ndugai hapa kesho itakuwa kesi kubwa, wamejadili jambo ambalo liko mahakamani, litakuwa halijatuweka mahali pazuri. Kwa hiyo nawashukuruni sana.

Kwa ustaarabu huo, basi sasa tunaendelea na Mheshimiwa Bashe.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza tu nimshukuru Waziri, 200 zile ameshatuletea za kupima mji wa Nzega, kwa hiyo tutaomba zingine, tunamshukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwombe Mheshimiwa Waziri atupe *commitment*, Serikali kwa kufahamu thamani ya ardhi tuna zile ardhi za vijiji ambazo zinasimamiwa na hati za mila, zinaitwa za kimila zinazosimamiwa na Sheria Na.5 ya mwaka 1999, section 23. Hata hivyo, wakati huo huo tunayo Sheria ya Na.4 ya ardhi inayosimamia zile zinazoitwa ardhi za mijini ambazo zinasajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Hati, Sura Na. 334.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni nini? Hoja yangu ni moja, hati za kimila zina *weakness*, hazikubaliwi kwenye *financial institutions* na hazitambuliki na lile jina kimila lina *negative connotation*.

**MWENYEKITI:** La kienyejienyeji.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Ndiyo, la kienyejienyeji hivi na ile hati mtu akipewa *life span* yake ni miaka mitano. Hoja yangu ni moja kwa nini Serikali isiamue kufanya *harmonization* ya hizi sheria tatu ili na zile hati za kimila zibadilishwe jina kutokana na lile neno kimila badala ya kusainiwa kule chini isainiwe na Kamishna wa Ardhi na ziwe zina muda mrefu wa uhai ili watu wetu kule vijiji wakipata zile hati waweze kuzitumia kwa ajili ya kuwa *bankable* kwa sababu sasa hivi *financial institutions* haizitambui. Haja yangu ni kuiomba Serikali na Waziri atupe *commitment* kuleta mabadiliko ya Sheria ya Vijiji Na.5, kuleta mabadiliko ya Sheria ya Ardhi Na.4 na Sheria ya Usajili, Sura Na. 334 ili kuweza ku-*accommodate* hati za kimila.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, ni hiyo tu.

**MWENYEKITI:** Ni pendekezo, Mheshimiwa Waziri pendekezo hilo.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa ushauri wake Mheshimiwa Bashe. Sisi tumeliona hilo, lakini tunataka tuanzie mbali kidogo lilikotoka. Hili jambo lilianzia kwenye Sera ya Ardhi ya mwaka 1995, kwa hiyo atupe ruhsa tuanze kwanza kwenye sera, maana sasa hivi ndiyo tunakamilisha kamilisha hivi, halafu baadaye sera ndiyo inaweza kufikiria kuja na sheria, lakini ni jambo jema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachokwaza kwa sababu niliongea naye hata jana, kinachokwaza kidogo kama wewe una hati ya kimila benki inaweza kukupa mkopo, mikopo inatolewa, lakini benki sasa wanapotaka kuuza hilo shamba lako kwa hati ya kimila sheria imewabana kwamba lazima kwanza wauzie *family members* au wale wanakijiji wa pale sasa unapataje wanakijiji ambao wana uwezo wa kununua hiyo na kurudisha hela benki kwa hati ya kimila tofauti na hizi hati za miaka 99. Wenye fursa nyingine wanaotaka ekari

zaidi ya 50, wanaomba kibali kwa Rais wanamilikishwa kwa hati za miaka 99 kwenye maeneo hayo hayo ya vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba nimwombe Mheshimiwa Bashe, tupate mawazo yake tupeleke kwenye marekebisho ya sera kwanza, halafu sera inaweza ikafikiria kwa sababu sera ni shirikishi, tupate mawazo ya Mheshimiwa Bashe na wananchi wengine.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Julius Kalanga.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika sera inazungumza habari ya utoaji wa hati na uksoma upande wa pilli wa hati unakuta kila hati ina maelezo ya matumizi yake lakini katika mashamba mengi kwenye nchi hii mengi sana ambayo yalitolewa wakati ule kwa makusudi fulani ya kilimo na bahati mbaya hali ya hewa ikabadilika watu wakaacha kulima watu wameenda benki kukopea hayo mashamba na tunasema ukikopa unaenda kuyaendeleza yale mashamba lakini watu wamekopa fedha kwa sababu ya mazingira mvua hainyeshi, wamekopa fedha wameenda kufanya kazi nyiningine, wameyatelekeza yale mashamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka ufanuzi wa Serikali inafanya nini kuhakikisha kwamba inafanya *land auditing* kwa ardhi zote za namna hiyo ili kujua yale mashamba ambayo yameshindwa kuendelezwa kwa sababu yoyote ile ili ibadilishwe hati zake na wananchi waweze kupewa, waweze kutumia kwa sababu kuna ardhi ambayo imeachwa kwa sababu watu wameenda kukopa benki na sheria inakataza kukopa halafu ukatumia kwa namna nyiningine.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. *Land auditing* yatakayopatikana wananchi wapewe, Mheshimiwa Angelina, majibu.

### **NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO**

**YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa hoja ya Mheshimiwa Kalanga na ni Mjumbe wa Kamati, Wizara ilishatoa maelekezo kwa mashamba yote ya aina hiyo ambayo yamekopewa pesa benki halafu yametelekezwa, maana yake ni kwamba wanadaiwa benki lakini pia na uendelezaji kwenye lile shamba hakuna. Kwa hiyo kinachofanyika sasa ni kuyatambua ni mangapi ambayo yamekopa pesa benki na yametelekezwa. Hata tunapokuja kusema kwamba labda imependekezwa lifutwe basi pia Wizara inafanya utaratibu wa kuwasiliana na mabenki ili yule akishafutiwa maana yake hati unaichukua, halafu yeze atafute dhamana nyingine kwa sababu tayari sisi tutakuwa tumeshachukua ardhi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo inafanyika na nitoe rai tu kwa Waheshimiwa Wabunge kule ambako wanaona kuna mashamba ambayo yamekopewa na yametelekezwa, basi *process* za kawaida za ukaguzi kama alivyosema zianzie huko zifanyike halafu hatua ziweze kufanyika. Ni wengi kweli walishafanya hivyo, kwa maana ya kukopea, halafu hawajaendeleza mashamba na sisi hatukubali hiyo iendelee, lakini naanzia kwenye halmashauri kama Waziri alipokuwa anajibu hoja ya Mheshimiwa Lwakatare.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Julius Kalanga.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa maelezo, sina tatizo na hilo, lakini hao watu ni watu wenye nguvu sana ya fedha. Kwa hiyo wame-*control* kuanzia kule chini kwenye Maafisa Ardhi na baadhi ya watu pamoja na wanasiasa na watu wengine kule chini. Kwahiyoo ukisubiri sana taarifa hizo upate chini ni ngumu sana mwananchi wa kawaida ajue kwamba eneo hili limekopewa. Kwa hiyo nataka angalau Wizara ingeweka hata kama ni *pilot areas* angalau wenyewe watafute utaratibu wa kuyafuatilia mashamba moja baada ya lingine kuangalia yaliyoendelezwa na ambayo bado, lakini ukisema tu halmashauri- kule halmashauri wametudhibiti sana kwa

hiyo unakuta wakati mwagine wataalam wale hawafanyi  
hizo kazi kwa sababu wana mahusiano nao.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Julius.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaingia kwenye  
*guillotine.*

Kif. 1001 – <i>Administration &amp; HR Mgmt</i> .....	Sh.7,850,626,183
Kif. 1002 – <i>Finance and Accounts Unit</i> .....	Sh.804,582,000
Kif. 1003 – <i>Policy and Planning Unit</i> .....	Sh.777,640,000
Kif. 1004 – <i>Mgmt Inform. System Unit</i> .....	Sh.854,422,000
Kif. 1005 – <i>Internal Audit Unit</i> .....	Sh.329,356,000
Kif. 1006 – <i>Procurement Management Unit</i> .....	Sh.303,996,000
Kif. 1007 – <i>Government Communication Unit</i> ....	Sh.380,844,000
Kif. 1008 – <i>Legal Services Division</i> .....	Sh.305,152,000
Kif. 2001 – <i>Land Admin Division</i> .....	Sh.3,836,676,000
Kif. 2002 – <i>Surveys and Mapping Division</i> .....	Sh.3,326,197,000
Kif. 2003 - <i>Registration of Titles Unit</i> .....	Sh.919,260,000
Kif. 2004 – <i>Valuation Unit</i> .....	Sh.780,436,000
Kif. 2005 – <i>Dar es Salaam Zone</i> .....	Sh.509,215,500
Kif. 2007 – <i>Central Zone</i> .....	Sh.511,140,000
Kif 2008 – <i>Western Zone</i> .....	Sh. 414,740,000
Kif. 2009 – <i>Lake Zone</i> .....	Sh.538,620,000
Kif. 2010 – <i>Northern Zone</i> .....	Sh.532,160,000
Kif. 2011- <i>Southern Zone</i> .....	Sh.429,440,000
Kif. 2012 - <i>Southern Highlands Zone</i> .....	Sh.402,610,000
Kif. 2013 – <i>Simiyu Zone</i> .....	Sh.432,450,000
Kif.3001 – Rural and Town Planning Division...Sh.4,814,743,317	
Kif. 3002 – Housing Division.....	Sh.206,728,000
Kif. 3003 – District Land and Hous. Trib. Unit.....	Sh.3,894,453,000

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 003 - National Land Use Planning Commission**

Kif. 1001 – <i>Directorate of Corporate Services</i> ...Sh.1,085,852,000
Kif. 1002 – <i>Planning Unit</i> .....Sh. 0
Kif. 1003 – <i>Procurement Management Unit</i> .....Sh.78,980,000

Kif. 1005 – <i>Internal Audit Unit</i> .....	Sh.22,480,000
Kif. 1005 – <i>Legal Services Unit</i> .....	Sh.142,422,000
Kif. 2001 – <i>Directorate of Land Use Planning and Coordination</i> .....	Sh.421,520,000
Kif. 2002 – <i>Directorate of Res. Compl. &amp; Inform</i> ....	Sh.378,938,000
Kif. 2003 – <i>Tabora Zone Office</i> .....	Sh.114,880,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **MIPANGO YA MAENDELEO**

#### **Fungu 003 – National Land Use Planning Commission**

Kif. 1001 – <i>Directorate of Corporate Services</i> ...Sh.180,000,000
Kif. 2001 – <i>Directorate of Land Use Planning Management and Coordination</i> .....Sh.2,620,000,000
Kif. 2002 – <i>Direct. of Res. Compl. &amp; Inform</i> .....Sh.200,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

#### **Fungu 48 - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

Kif. 1001 – <i>Administration and HR Mgmt</i> .....Sh.1,100,000,000
Kif. 2001 – <i>Land Administration Division</i> .....Sh.17,284,504,387
Kif. 2002 – <i>Surveys and Mapping Division</i> .....Sh.5,400,000,000
Kif.3001 – <i>Rural and Town Planning Division</i> ....Sh.500,000,000
Kif. 3002 – <i>Housing Division</i> .....Sh.0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

**SPIKA:** Bunge linarejea.

*(Bunge ilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae, Mheshimiwa Waziri taarifa, tafadhalii.

## **T A A R I F A**

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa wa Kanuni ya 104, Kifungu kidogo cha 3(a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako likikaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi zake, naomba sasa taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubalike na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa wajibu wangu ni kuwahoji Waheshimiwa Wabunge wale kuhusu hoja ya Mheshimiwa Waziri ili tuwapatie bajeti hii kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Nadhani walioafiki wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi,  
Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa Fedha  
wa 2019/2020 Yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge wote naomba nikushukuruni sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, watendaji wote wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kazi nzuri ambayo mnaifanya. Ni kazi nzuri sana, endeleeni na spidi hiyo hiyo, tunajua bajeti ya mwaka huu imepungua kidogo siyo kama ya mwaka jana hasa ya

maendeleo, lakini tunaamini mtajitahidi kwa malengo tuliyonayo ya safari hii kufanya kazi nzuri zaidi hata kuliko tunakotoka. Kama mnavyo jua tunawaaminia, mambo ya ardhi ndiyo msingi wa kila jambo, ndiyo msingi wa kila kitu, tunawapongeza sana, tunawata kia kila la kheri.

Sasa Waheshimiwa Wabunge najua muda kidogo haujaka vizuri lakini nawaombeni kwa sababu tunatengeneza mambo ya wiki ijayo yakae vizuri, nawaombeni sana, liko jambo ambalo wamekuwa wakiongeaongea Wabunge mara kwa mara humu ndani, nimekuwa nkipata vijikaratasi na wakati mwengine hata baadhi ya kutoka upande wa Upinzani, Serikali wana maelezo kidogo tu, kuna maelezo machache hayafiki hata dakika 10, lakini nimeona ni muhimu mtuvumilie tuwasikilize Serikali halafu tunaahirisha tunaelekeea kwenye mambo mengine.

Mheshimiwa Mwita Mwikabwe Waitara, hapo hapo ulipo tu au karibu, tafadhali, karibu hapa mbele, karibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Maelezo ya ufanuzi kuhusu vitambulisho vya wafanyabiashara wadogo. Utoaji wa vitambulisho vya wafanyabiashara wadogo ni utaratibu uliobuniwa na Serikali unaotambulisha biashara ndogo zinazofanywa na wajasiriamali wadogo ambao hawajasajiliwa na Mamlaka za Mapato Tanzania. Utaratibu huu unafanyika kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura Na. 438 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2017. Katika kifungu cha 22A ambacho kinampa mamlaka Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) kuwatambua na kuwasajili wafanyabiashara wadogo yaani wajasiriamali na watoa huduma wadogo ambao mauzo ghafi yao hayazidi shilingi milioni nne. Lengo ni kuhakikisha wafanyabiashara hao hawabughudhiwi wakati wa kufanya shughuli zao.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kutoa vitambulisho vya wafanyabiashara wadogo ulianzishwa rasmi tarehe 10

Desemba, 2018 na kuzinduliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Jijini Dar es Salaam alipokuwa akihutubia kikao cha Mamlaka ya Mapato Tanzania na viongozi mbalimbali wa Serikali wakiwemo Wakuu wa Mikoa kuhusu uimarishaji wa ukusanyaji wa mapato ya ndani.

Mheshimiwa Spika, katika kikao hicho Mheshimiwa Rais alitoa vitambulisho vипatavyo 650,000 kwa Wakuu wa Mikoa wote Tanzania Bara kwa awamu ya kwanza. Aidha, awamu ya pili, tulitoa vitambulisho 1,200,000 na hivyo kufanya jumla ya vitambulisho 1,850,000 vinavyoendelea kugawiwa kwa wafanyabiashara wadogo, wajasiriamali na watoa huduma wadogo. Ili kupata vitambulisho hivyo wafanyabiashara wadogo na watoa huduma wadogo wanapaswa kuchangia kiasi cha Sh.20,000 tu kwa kila kimoja. Aidha, Serikali illtoa maelekezo kwa watendaji wa Serikali kuwa vitambulisho hivyo ni maalum kwa ajili ya kuwatambua wafanyabiashara wadogo na watoa huduma wadogo ambao mauzo ghafi yao hayazidi shilingi milioni nne.

Mheshimiwa Spika, tafsiri ya mfanyabiashara mdogo au mtoa huduma mdogo kwa mujibu wa sheria ya usimamizi wa mwaka 2015 kifungu cha 22A ni kuwa mfanyabiashara mdogo na mtoa huduma mdogo ni yule ambaye mauzo ghafi yake hayazidi kiasi cha shilingi milioni nne kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maelekezo ya Serikali mfanyabiashara mdogo na anayepaswa kupewa kitambulisho anapaswa kuwa na sifa zifuatazo:-

(1) Awe na mauzo ghafi yasiyozidi milioni 4 kwa mwaka;

(2) Awe hajawahi kusajiliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania na kupewa namba ya utambulisho wa mlipakodi wa biashara yaani *T/N*; na

(3) Atambulike kama mfanyabiashara mdogo, mjasiriamali mdogo au mtoa huduma mdogo katika eneo

analofanyaia biashara kupitia Ofisi ya Afisa Mtendaji wa Mtaa au Kijiji kwa mujibu wa sheria tulizonazo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania imekuwa ikiratibu zoezi la ugawaji wa vitambulisho vya wafanyabiashara wadogo kulingana na maelekezo ya Serikali ambapo hadi kufikia tarehe 26 Mei, 2019, jumla ya vitambulisho 1,850,000 vimegawiwa kwa Wakuu wa Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara. Aidha, vitambulisho 1,176,305 vimegawiwa kwa wafanyabiashara wadogo na watoa huduma wadogo ambapo jumla ya Sh.23,566,100,000 zimekusanywa.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha mfumo wa usimamizi wa zoezi hili Serikali imekamilisha mwongozo wa kusimamia zoezi la ugawaji wa vitambulisho vya wafanyabiashara wadogo, wajasiriamali na watoa huduma wadogo ambao unatarajiwu kuanza kutumika katika mwaka wa fedha 2019/2020. Lengo la mwongozo huo ni kurahisisha usimamizi, uratibu na ufuatiliaji wa zoezi hilo.

Mheshimiwa Spika, tamko linaloendelea kuzunguka kwenye mitandao ya kijamii na vyombo vya habari na kumhusisha Mkuu wa Mkoa wa Iringa siyo maelekezo ya Serikali, hivyo natoa wito kwa Wakuu wote wa Mikoa wa Tanzania, watendaji wote wa Serikali kuzingatia maelekezo yaliyotolewa na Serikali kuhusu ugawaji wa vitambulisho vya wafanyabiashara wadogo, wajasiriamali na watoa huduma wadogo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri na naamini imewasaidia Waheshimiwa Wabunge na huo utaratibu utakapokuwa tayari ningewaombea Waheshimiwa Wabunge wangu pia wapate nakala ili wanaporudi majimboni pasiwe na lugha tofauti.

Waheshimiwa Wabunge ninalo tangazo moja tu hapa kwa haraka sana la nusu sekunde; kesho Jumamosi na keshokutwa Jumapili kutakuwa na mechii kwenye uwanja wetu zinazohusisha *Bunge Sports Club* kwa mpira wa miguu na mpira wa pete na kutakuwa na kuvuta kamba vile vile wanaume na wanawake, tunaombwa sote tuweze kushiriki pale kushangilia na kushiriki katika michezo hiyo. Kesho itakuwa Bunge na JKT Makutupora na keshokutwa Bunge na Muungano Veterans.

Kwa hiyo, shughuli zetu, Jumatatu tutakuwa na bajeti ya Wizara ya Fedha. Baada ya hapo Jumanne tutatawanyika kulia na tutaelezana siku ya Jumatatu tunakuja kuendelea vipi na mambo yetu wakati huo Kamati ya Bajeti itakuwa nayo itatupatia ratiba yake na Wizara ya Fedha katika hizi siku za *Eid* na nini nao watakakaa vipi, lakini naomba basi Jumatatu tukutane illi tumalize masuala ya Wizara ya Fedha naamini kabisa tutawahi *Eid*, kwa hiyo hakuna mashaka hata kidogo.

Baada ya hayo, basi naomba niahirishe shughuli za Bunge hadi siku ya Jumatatu, saa tatu kamili asubuhi

*(Saa 12.45 Jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu, Tarehe 3 Juni, 2019, Saa Tatu Asubuhi)*